# MAISHA BINAFSI YA AHLUL BAYT (AS)

الحياة الشخصية عند أهل البيت


**Kimeandikwa na:**
Sheikh Fawzi Aali Saif

**Kimetarjumiwa na:**
Amiri Musa Kea


08_16_Maisha_23_November_2016.indd 1 11/23/2016 12:37:26 PM

ترجمة

# الحياة الشخصية عند أهل البيت


تأليف
الشيخ فوزي آل سيف


من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
Al-Itrah Foundation

**ISBN No:** 978 - 9987 – 17 – 044 – 9

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Fawzi Aali Saif

**Kimetarjumiwa na:**
Amiri Musa Kea

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimesomwa-Prufu na:**
al-Haj Ramadhani S.K.Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**
Al-Haj Mujahid Rashid

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Aprili, 2017
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Dibaji ........................................................................ vi

Neno la Mchapishaji ........................................................................ 1

Kwa nini Tuzungumzie Maisha Binafsi? ........................................ 3

**SEHEMU YA KWANZA ........................................................ 9**

Maisha ya Maasumini baina ya ufurutu ada na kutweza ................ 9

Sababu za kuenea ufurutu ada........................................................ 12

Namna gani walikabiliana na ufurutu ada .................................... 20

Sababu za kutweza........................................................................ 31

Hitimisho........................................................................................ 45

**SEHEMU YA PILI ............................................................ 55**

Migongo safi na vizazi vilivyotakaswa.......................................... 55

Maisha ya ndoa ya Ahlul-Bayt (as)................................................ 70

Ahlul-Bayt (as) na mas'ala ya jinsia.............................................. 70

Hiyari zilizopo .............................................................................. 89

Wake wengi.................................................................................. 102

Wake vijakazi .............................................................................. 110

**SEHEMU YA TATU........................................................... 126**

Vipi na namna gani wanavaa ...................................................... 126

Kundi la kwanza .......................................................................... 127

Kundi la pili ........................................................................ 130
Mitazamo katika maadili ya jumla................................................ 138
Kutenganisha baina ya mavazi na shakhsiya ................................ 147
Mavazi yenye kulaumiwa ............................................................ 160
Mas'ala ya kivitendo na uhalisia: ................................................ 164

**SEHEMU YA NNE........................................................................ 167**

Chakula na vinywaji ...................................................................... 167
Athari za kuvimbiwa...................................................................... 175
Mifano kinzani .............................................................................. 185
Dondoo kutoka katika mafunzo ya sira ........................................ 188
Kujinyima na mahitaji ya Zama.................................................... 190
Baina ya wastani na njaa yenye kudhoofisha.............................. 193
Chakula, adabu na Sunnah............................................................ 195

**SEHEMU YA TANO .................................................................... 202**

Watumishi na watumwa katika maisha yao .................................. 202
Kuamiliana na njia ya malezi........................................................ 206
Zaydi bin Harithah al-Kalbiy ........................................................ 209
Qanbar huria wa Amirul-Mu'minin (as)...................................... 212
Na wengine ni mashahidi.............................................................. 216
Hitimisho........................................................................................ 220

08_16_Maisha_23_November_2016.indd 5 11/23/2016 12:37:26 PM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam
Al Itrah Foundation
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 6 11/23/2016 12:37:26 PM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *al-Hayatu 'sh-Shakhsiyyah 'inda Ahlu 'l-Bayt* kilichoandikwa na Sheikh Fawzi Aali Saif. Sisi tumekiita, *Maisha Binafsi ya Ahlul Bayt (a.s.).*

Maisha ni kupanga, na kupanga ni kuchagua. Kuchagua maana yake kuchukua kilicho bora na kuacha kilicho kibaya, na katika maisha maana yake ni kuishi maisha mazuri na yenye maadili mema na kuamiliana vizuri na binadamu wenzako kwa ubinadamu wenu bila kujali itikadi zenu, kabila au rangi, na kuamiliana vizuri na waumini wenzako kama ndugu zako katika imani.

Ili kuyafikia malengo haya, huna budi kupata malezi bora ya kiroho na kimwili kuanzia utotoni. Wazazi ndio chimbuko la kwanza la malezi haya, lakini kuna kufunzwa na wazazi na kufunzwa na ulimwengu. Mambo haya hayawezekani mpaka apatikane mwalimu mzuri wa kufundisha somo hili.

Allah Mwingi wa rehema kwa huruma Zake na Upole kwa viumbe Wake akawa anawatuma Wajumbe miongoni mwa viumbe Wake mara kwa mara kuanzia alipomuumba mwanadamu ili kuwafundisha maadili mema pamoja na kumjua Yeye kama Muumba wao. Kuwatoa katika hali mbaya na kuwapeleka katika hali nzuri, kuwatoa katika giza na kuwapeleka kwenye mwanga. Allah 'Azza wa Jallah ametuma takriban Wajumbe (Mitume) 124,000 wa kwanza akiwa ni Nabii Adam (a.s.) na wa Mwisho ni Nabii Muhammad (s.a.w.w.) ambaye amemtaja kwamba kuwa ni rehema kwa wal-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 1 11/23/2016 12:37:26 PM

imwengu wote. Hii ina maana kwamba si kwa wanadamu tu bali hata kwa viumbe wengine kama wanyama, n.k. Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ametajwa katika Qur'ani Tukufu kuwa ni "kiigizo chema" *(uswatun hasanah).* Mwenendo wake wote wa maisha ni somo kwa wanadamu wote. Na alipofariki akatuachia vitu viwili - Qur'ani Tukufu iliyosheheni mfumo wote wa maisha kwa mwanadamu, na watu wa nyumbani kwake – Ahlul Bayt (a.s.). Akutuusia kwamba ili tufanikiwe katika maisha yetu ya hapa duniani na Akhera, basi tushikamane na vitu hivyo vizito viwili (yaani Qur'ani na Ahlul Bayt wake watoharifu).

Mwandishi katika kitabu hiki anaonesha jinsi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul Bayt wake ambao ni Maasumina 13 (a.s.) walivyoishi ili tuige mfano wao na ili tuishi maisha bora na maadili mema.

Taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa makubwa kwao. Tunawashukuru ndugu yetu al-Haj Ustadh Amir Musa Kea kwa kufanikisha tarjuma ya kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili, pia na wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine hadi kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na Akhera pia. Amin!

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**Dar es Salaam**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# KWA NINI TUZUNGUMZIE MAISHA BINAFSI?

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu,**
**Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

Ulimwengu wa Kiislamu unashuhudia tangu miaka mingi hali ya kurejea kwenye asili na kusonga mbele kwa makundi mengi ya kijamii, wasomi wake na watu wa kawaida, vijana wake na mabarobaro wake, kuelekea kwenye kufahamu madhumuni ya kidini, na jambo hili linatuvuta kwenye kujua muundo wa maisha unaotakiwa kwa mwanadamu Mwislamu. Hiyo ni kwa sababu jambo la mwanzo linalotakiwa katika madhumuni haya hakika huonekana katika muundo wa maisha ambayo mwanadamu ameyachagua. Na huenda pia yakawa ni yale magumu zaidi. Hiyo ni kwa kuwa ni rahisi mtu kuwataka wengine kutekeleza misingi, lakini ni vigumu kwake yeye mwenyewe kutekeleza misingi hiyo katika maisha yake.

Ndio, na ingawa wengi wanaweza kujipamba kwa tabia njema katika jamii, na tukajua kuhusu wao katika maisha yao ya kivitendo, mambo mema kwa mfano, na ulinganiaji mzuri, lakini hii si dalili kamili ya kuthibitisha usalama wa utu, bali inapasa kutazama katika maisha maalumu na historia binafsi, na mwenendo wake nyumbani, muamala wake na mke wake au mume wake, kuwalea kwake watoto wake… Pale mtu anapobaki peke yake bila ya uangalizi wa nje bali, anapokuwa yeye ndiye mwenye mamlaka, inakuwaje tabia yake? Na ni muundo upi anaoufuata?



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 3 11/23/2016 12:37:26 PM

Na hapa ndipo ikawa ni lazima kurejea katika maisha ya Maasumini عليهم السلام na miongoni mwao ni kiongozi wao Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم, ambaye mke wake Bibi Aisha رضي الله عنها aliulizwa juu ya tabia yake ndani ya nyumba akajibu: "Tabia yake ilikuwa ni Qur'ani."

Maisha binafsi kwa ufafanuzi wake ambao tunaishi nao, kwa kuzingatia kuwa tuna uwezo wa kufahamu zaidi ulazima wake na mbinyo wake, na jinsi maisha hayo binafsi yatakavyotuondolea kizuizi kikubwa ambacho tumekitengeneza na kukizungusha pembeni mwa nafsi zetu kwa kule kuwa kwao عليهم السلام ni maasumu, na hatimaye kwa uwelewa wa baadhi yetu wakawatoa katika katika duara la ubinadamu na kuwapeleka katika duara la Malaika.

Hakika mwishoni mwa safari tutakuta uwiano mzuri baina ya anayoyasema ma'sum katika misingi, na uhalisia wa maisha binafsi wanayoyaishi. Pamoja na kwamba upande huu katika maisha yao matukufu haukuzungumziwa katika muundo wa nadharia kamilifu, bali naweza kusema haukupewa mazingatio ya kutosha kwa sababu ya kuangukia kwake mara nyingi katika duara la adabu na Sunnah, na haya (Sunnah na adabu) hawayazungumzii wanahistoria kwa kuzingatia kuwa sio matukio muhimu ya kihistoria, kwani yako nje ya ubobezi wao, kama ambavyo mafakihi nao wanayaacha kwa kuangalia kanuni ya kutochunguza zaidi hoja zinazothibitisha Sunnah, ukiongezea kwamba kwa kuwa ni mambo yanayoambatana na maisha binafsi hivyo Ahlul-Bayt hawakufafanua zaidi mambo hayo kama walivyoelezea na kufafanua mambo mengine.

Kwa sababu hiyo tunalazimika kudondoa nukta na kuashiria hapa na pale na kuweka wazi hadithi hii, na kujaribu kufasiri hadithi ile, ili tufikie msingi wa jumla unaokusanya fafanuzi hizi.

Hakika sisi katika maudhui haya tuko katika pande mbili za makali ya upanga zinazokata: i) Ubinadamu halisi, ii) Ghaibu halisi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 4 11/23/2016 12:37:27 PM

Na yote mawili haya yanatisha kama itatimu kushikamana nayo. Hiyo ni kwa sababu mwisho wa njia ya kwanza na ambayo wamei-fuata baadhi ya Waislamu ni kuwageuza Maasumini, na miongoni mwao ni kiongozi wa viumbe na mtu mkamilifu katika ulimwengu, kuwa ni mtu asiye na maana kiasi kwamba Mwislamu anaona aibu kuangalia katika hadithi za maisha yake binafsi.

Na hakika mimi unakaribia kutomalizika mshangao wangu kwa anayefikiria kwa sura hii kuhusiana na Mtukufu Mtume ﷺ, kwani yeye kwa mujibu wa kauli ya baadhi – *Audhubillahi* – ni mtu ali-yekuwa mshirikina kwa muda wa miaka arobaini na alikuwa katika dini ya watu wake kabla ya utume. Na anazinduka baada ya utume ili kuipamba kaumu yake au anasahau na kuongeza katika Qur'ani Aya kadhaa zinazotukuza masanamu! Ni mtu wa kucheza pamoja na wake zake na anabariki mambo ya ummah ili afanye mashindano ya kipuuzi pamoja nao. Mara anashinda na mara anashindwa na men-gineyo mengi.

Haya, na kuchupa mikapa katika mtazamo wa kibinadamu ku-natufikisha katika kuona kwamba baadhi ya maulamaa wenye ku-takasika na mabaya yaliyotajwa wana mwenendo bora zaidi kuliko mtu huyu, nayo ni kinyume kabisa na itikadi. Kama ambavyo ku-chupa mipaka katika upande wa ghaibu kwa kundi jingine miongoni mwa Waislamu kati ya waliowanyanyua Maasumini zaidi ya daraja zao, kunawafanya wadhani kwamba wao kwa hilo wanawatukuza na kuwaheshimu, nalo pia ni katika dauru ya mkanganyiko mkubwa. Hakika daraja hii sio kwa kuwa wao ni sawa na malaika na kwamba damu yao iko hivi na maumbo yao ya kimwili yako vile, bali wame-pata daraja hii kubwa kwa sababu wao walikuwa binadamu kama sisi, lakini wao wamepanda daraja kwa wahyi na elimu ya Mwe-nyezi Mungu, na kutekeleza Qur'ani kwa daraja ya juu kuliko daraja ya malaika.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 5 11/23/2016 12:37:27 PM

Hakika fahari na utukufu ambao wameupata hawa ni kwa kuwa wao waliishi katika mahitaji ya mwili na mbinyo wa uhalisia wa nje na visababishi vya kuporomoka, lakini wao pamoja na hayo walifanya ikhlasi katika ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hadi akawafanya ni makhususi na akawateua. Na Qur'an tukufu inaeleza uwiano huu kwa muhtasari kwa kukusanya baina ya hali mbili za kibinadamu na ghaibu kwa kauli yake - ikielezea kwa ulimi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ

**"Sema: Hakika mimi ni binadamu kama nyinyi tu, nimeletewa wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu mmoja." (Suratul-Kahf; 18:110)**

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّي هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَسُولا

**"…..Sema: Ametakasika Mola Wangu. Kwani mimi ni nani isipokuwa ni mwanadamu Mtume?" (Suratul-Israi; 17:93).**

Inabainika kwa mwenye kusoma maisha binafsi ya Maasumini عليهم السلام kwamba anatakiwa ashughulike katika wigo wa mipaka hii miwili: Si katika ubinadamu unaowateremsha Maasumini kwenda kwenye kilele cha mabaya, tukiachilia mbali yaliyoharamishwa kwa kumzingatia katika itikadi yetu kuwa ndio mtu mkamilifu zaidi katika zama zake – kabisa khususan Nabii Muhammad ﷺ – wala si katika ghaibu inayomuondoa katika ardhi anayoishi juu yake na kumpa nafasi mbinguni miongoni mwa malaika.

Hivyo miongoni mwa matokeo ya kutokuwa na nadharia kamilifu katika upande huu ni kuwepo tafsiri nyingi zitokanazo na kule kushikamana na ufafanuzi bila ya kuangalia misingi ya jumla na njia



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 6 11/23/2016 12:37:27 PM

za kimsingi. Ikiwa mtu ni mlala hoi basi utamuona anakusanya hadithi zilizopokewa kuhusu kujinyima kwa Amirul- Muuminina عليه السلام na kunywa kwake mtindi mchachu pamoja na vipande vya mkate mkavu ambavyo alikuwa anavivunja kwenye magoti yake kutokana na kukauka kwake. Wakati ambapo ikiwa mtu ni kati ya wale walioneemeshwa na Mwenyezi Mungu, na ni miongoni mwa wenye kujikwatua utamuona anahifadhi vizuri hadithi za vazi la Imamu as-Sadiq na Imamu Ridha عليهما السلام, hadithi za yale mavazi mazuri ya Kiyemen yenye thamani.

Na hili si jambo jipya, kwani hata katika historia sisi tunakutana na ishara zinazoashiria uelewa huu, huyu hapa Ibn al-Munkadar anakwenda ili kumnasihi Imamu al-Baqir عليه السلام, na Imam alikuwa amerejea kutoka kwenye kazi yake katika bustani yake ilihali anamiminika jasho, akaanza kumnasihi aiache dunia. Imamu akamjibu na kumfahamisha msingi mkuu wa maana ya kutafuta dunia. Na hawa hapa watu miongoni mwa masufi wanaingia kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام na wanamkataza baada ya kuona amevaa nguo nyeupe kana kwamba ni gamba jeupe.[1] Wanadai kwamba hili si katika mavazi yake wala si katika mavazi ya baba zake kama vile Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم na Amirul-Mu'minin عليه السلام. Imam عليه السلام akawaambia jinsi wakati na mazingira yanavyochangia katika kubadilika kwa ufafanuzi pamoja na kuchunga misingi.[2]

Na hapa ni lazima kutafiti mambo mengi wakati wa kueleza ufafanuzi wa maisha hayo matukufu ya Maasumini عليهم السلام. Je, vitendo vyote kwa ufafanuzi vinaingia katika wigo wa Sunnah? Mfano maasumu huyu kupendelea chakula fulani na maasumu mwingine kupendelea aina nyingine, je hali hiyo inaingia katika hali za kibinadamu na wala haina uhusiano wowote na hukumu ya kisharia? Na

[1] Kwa kufananishwa na gamba jeupe lililogandamana na weupe wa yai katika weupe wake na ulaini wake.

[2] Rejea *Tuhaful-Uquul*, uk. 256.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 7 11/23/2016 12:37:27 PM

hasa ukizingatia kwamba kwetu kunapatikana Hadithi zinazobainisha kutoafikiana kwa ufafanuzi wa kupendelea chakula hiki au kile?

Je, zama ina mchango katika kula aina hii ya chakula, na si aina ile, na kuoa mwanamke wa aina hii na si ile? Na je, nafasi aliyonayo mtu katika jamii ina mchango katika kuainisha aina ya maisha ya mtu? Kwa mfano je kiongozi anapasa kuwa na maisha ya namna hii, kama inavyofahamika katika hadithi ya Imamu Amirul-Mu'minin عليه السلام alipozungumza na Asmi bin Ziyadi, na iwapo si kiongozi awe na namna nyingine isiyokuwa hiyo?

Bali, je sehemu ina mchango katika kuainisha upande fulani wa maisha binafsi ya mtu? Ikiwa kwa mfano chakula fulani katika mji kinafaa na kinatakiwa je, inawezekana kikahitajika pia Khurasan pamoja na kutofautiana mazingira, bali pamoja na kutofautiana watu vile vile? Hii ni kwa kujengea juu ya kwamba maelekezo ya Maasumini عليهم السلام katika upande huu yanaafikiana zaidi na kanuni za afya – ikiwa tutasema kuwa maelekezo yake ni nasaha?!

Kisha nini kinatakiwa, je, ni ufafanuzi au ni misingi ya jumla? Je, kinachotakiwa ni kujinyima dunia – kwa maana yake halisi? Au kuna uhusiano maalumu pamoja na usufi kama ulivyo usufi?

Je, ni kukinai na ugumu au ni kupenda kwa dharura vipande vya shairi?

Maswali haya na mengineyo yanaweza kupata majibu katika kurasa zijazo, kama ambavyo tutajaribu na tunataraji hivyo. Na yanaweza yasipate majibu husika, lakini zikatusaidia kufungua maarifa ya akili yatakayotuwezesha kutaamali na kutafakari kwa kina katika maisha yao binafsi na huenda ukawa ndio mwanzo wa sura nyingine za watafiti.

**Fauzi Aali Saif**
**1/11/1410 Hijiria.**



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 8 11/23/2016 12:37:27 PM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# SEHEMU YA KWANZA

## MAISHA YA MAASUMINI BAINA YA KUFURUTU ADA NA KUTWEZA

Kuna njia mbili ambazo anaweza kuziona mtafiti wakati wa kuamiliana pamoja na Maasumini عليهم السلام. Licha ya kwamba zinakinzana lakini zote zinamalizikia kwenye hitimisho moja, nalo ni kuwatoa watu katika mazingira ya kufuata na kuiga. Ni njia mbili zilizotoka katika mpaka wa wastani, nje ya njia kuu na kwenda kando ya njia, nazo ni kufurutu ada na kutweza.

Na kwa kuangalia uhusiano mkubwa wa maudhui haya katika utafiti wetu tutayazungumzia kwa undani, hiyo ni kwa sababu tunasoma maisha binafsi katika nyanja zake mbalimbali katika maisha ya Maasumini عليهم السلام ili kupitia maisha hayo tupate maarifa ya muundo unaotakiwa kidini, na tujaribu kuutekeleza katika maisha yetu, kama tulivyoeleza katika utangulizi. Kazi hii inategemea kutengeneza hali ya ufuasi na kuiga kuwa uhusiano wa mwisho baina ya ummah na Maasumini عليهم السلام, na uhusiano huu hauwezi kujengeka katika kivuli cha kuenea mtazamo wa ufurutu ada na kutweza.

Hiyo ni kwa sababu mwenye kufurutu ada kama itakavyobainika baadaye hafanyi hivyo isipokuwa huwa ni mwenye kukusudia kutofuata, na hivyo hunyanyua daraja ya mtu hadi kwenye daraja ambayo mtu mwenyewe hadai, na hivyo humtoa katika hali yake ya kibinadamu kwenda kwenye mfano wa mungu au nusu mungu, na wakati huo huwa haitaki nafsi yake kumwiga mtu huyo aliyem-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 9 11/23/2016 12:37:27 PM

nyanyua. Ama mwenye kutweza ni kwa sababu haitakidi kwamba huyu mtu anatofautiana naye sana, sasa kwa nini amfuate?

Na kutokana na hadithi nyingi, inadhihirika ishara zenye kuashiria aina hizi mbili, ingawa mkazo mwingi zaidi upo katika kuwalaumu wenye kufurutu ada, na hiyo ni kutokana na hatari ya kipekee ambayo inaletwa na hawa katika itikadi, ambayo hailetwi na wenye kutweza.

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba amesema: “Ewe Ali, mfano wako katika ummah huu ni kama mfano wa Isa bin Maryam. Kuna watu walimpenda basi wakafurutu ada kwake, na kuna watu walimchukia nao wakachupa mpaka kwake, ukashuka wahyi: ‘Na mtoto wa Maryam alipopiga mfano basi ikawa watu wako kwake wanapinga.’”[3]

Na kutoka kwa Amirul-Mu’minin Ali عليه السلام amesema: “Wataangamia kwa ajili yangu watu wawili: Mwenye kupenda kwa kufurutu ada, na mwenye kuchukia kwa kutweza.” Na kutoka kwa Amirul-Mu’minin عليه السلام vilevile amesema: “Wataangamia kwa ajili yangu watu wawili: Mwenye kufurutu ada katika kunipenda, yule anayenisifia kwa nisiyokuwa nayo. Na mwenye kunichukia, ambaye chuki yake dhidi yangu inampelekea kunizulia uwongo.”[4]

Kama tulivyotaja hapo awali, hakika kufurutu ada ni ugonjwa hatari zaidi na mwingi zaidi ambao Maasumini عليهم السلام walipata mtihani kwao kutoka kwa wajinga wenye kukosea. Na tutazungumzia juu ya hawa wakati wa kuzungumzia sababu zinazosababisha mtu kufurutu ada na mambo yanayopelekea kufanya hivyo.

Alikuja mtu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia: “Amani iwe juu yako ewe Mola wangu.” Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: “Una nini; akulaani Mwenyezi Mungu, Mola

---

[3] *Biharul-An’war,* Juz. 2, uk. 283, kutoka kwa Ahmad bin Hanbal katika *Musnad* yake.

[4] Rejea iliyotangulia uk. 280.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 10 11/23/2016 12:37:27 PM

Wangu na Mola Wako ni Mwenyezi Mungu. Ama wallahi nilikwisha kukujua kuwa ni muoga katika vita na muovu katika amani."[5]

Na Amirul-Mu'minin عليه السلام amekuwa ni mlengwa wa kundi lililoshindwa kufahamu siri ya utukufu wake, na akili zao hazikuona kuwa inawezekana kuwepo utukufu huu kwa mwanadamu, hivyo wakamfanya kuwa ni Mungu. Na kwa ajili hiyo aliwachoma moto. Imepokewa kwamba Amirul-Mu'minin عليه السلام alipita kwao akawakuta wanakula katika mchana wa mwezi wa Ramadhani, akawaambia: "Nyinyi ni wasafiri au wagonjwa?" Wakasema: "Hatuna hata moja katika hayo." Akasema: "Je, nyinyi ni katika Ahlulkitabi?" Wakasema: "Hapana." Akasema: "Kwa nini mnakula mchana wa mwezi wa Ramadhani?" Wakasema: "Wewe! Wewe!"

Na hawakuzidisha katika hilo, basi akafahamu makusudio yao, akateremka juu ya farasi wake, akaweka shavu lake kwenye udongo kisha akasema: "Ole wenu hakika mimi ni mja kati ya waja wa Mwenyezi Mungu, muogopeni Mwenyezi Mungu na rejeeni kwenye Uislamu." Wakakataa, akawalingania sana lakini wakang'ang'ania jambo lao. Akanyanyuka kwao kisha akasema wafungeni na nileteeni nyasi, moto na kuni. Kisha akaamuru yachimbwe mashimo mawili, yakachimbwa, shimo moja akalifunika na jingine akaliacha wazi, na akatoboa tundu baina yake na akatupia moto kwenye kuni. Moshi ukafuka na akawa anawaambia na anawanasihi: "Rejeeni kwenye Uislamu," lakini wakakataa, basi akaamuru ziletwe kuni na moto, wakatupiwa na wakaungua, hakuacha kuwa ni mwenye kusimama kwao hadi wakawa mkaa.[6]

Na inadhihirika kwamba kundi hili hata kama lilimalizika na watu wake, isipokuwa madhumuni ya kufurutu ada yaliendelea katika nyakati tofauti, ambapo tunakuta mtu anamuuliza Imam Ridha

---

5 Rejea iliyotangulia uk. 297.

6 *Sharh Nahjul-Balaghah*; 5/6.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 11 11/23/2016 12:37:27 PM

عليه السلام kwa kutoa hoja kwa kauli inayomalizikia kwenye kufurutu ada juu ya Amirul-Mu'minin عليه السلام na Inshaallah baadaye litakuja tamko la jibu la Imam عليه السلام. Na inadhihirika kwamba Imamu as-Sadiq عليه السلام alipata mtihani vilevile kwa kundi lingine kati ya hawa wafurutu ada. Baadhi yao walisimama na kuita jina la Imam wakisema: '*Labayka*', Imam alipopewa habari ya hilo alisujudu ardhini ilihali akilia na akiuma kidole chake akisema: "Bali mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu, tunusuru na moto." Alisema hayo mara kadhaa kisha akanyanyua kichwa chake na machozi yake yanatiririka kwenye ndevu zake, Muswadifu (mmoja wa wafuasi wake) akasema: "Nikajuta kumpa habari na nikamwambia: Niwe fidia kwa ajili yako, usijali kwa hilo!" Akasema: "Ewe Muswadifu hakika Isa kama angenyamazia waliyoyasema Wakristo juu yake ingekuwa ni haki juu ya Mwenyezi Mungu kutia uziwi masikio yake na kupofusha macho yake."[7]

Na vilevile tunakuta baadhi ya waovu kati ya waliotengeneza madhehebu ya Waqifiyyah, hilo liliwalazimisha kuamini kuendelea kwa maisha ya Imam Musa bin Ja'fari عليه السلام, na hilo halikuwa isipokuwa ni mfano wa aina ya ufurutu ada wa wajinga wasioyajua maisha ya Maasumini عليهم السلام. Na ni kwao tunaanzia mazungumzo juu ya sababu za kufurutu ada na visababishi vyake.

## SABABU ZA KUENEA UFURUTU ADA

### 1. Kutokujua au Upungufu wa Maarifa:

Mwenye kufuatailia katika dhana ya maarifa ya Kiislamu atakuta kwamba maarifa sahihi yanachukua nafasi muhimu sana. Harakati za mwanadamu za kimaisha zinategemea usahihi wa maarifa yake au makosa yaliyopo katika maarifa yake, ambapo hakuna harakati isipokuwa na wewe unahitajia humo maarifa. Na kwa sababu hii

[7] *Biharul-An'war*, Juz. 20, uk. 293.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 12 11/23/2016 12:37:27 PM

mtu anapimwa kwanza katika maarifa yake kabla ya kupimwa katika kazi yake. Ni watumishi wangapi wanajitahidi katika kazi lakini anakosea mwelekeo kwa sababu ana upungufu wa maarifa; na kwa ajili hiyo anasema Amirul-Mu'minin عليه السلام: "Usimtukuze yeyote hadi ujue maarifa yake." Na kuainisha wafuasi hutimia si kwa kiwango cha vitendo vyao vya kiibada tu, bali ni kwa kiwango cha maarifa yao na yakini yao, Imam anasema: "Jueni daraja za wafuasi kwa kadri ya upokezi wao na maarifa yao." Bali hakika ibada inatofautiana kwani kwa mjuzi ni bora zaidi katika thamani yake kinyume na ibada ya mchache wa maarifa au mwenye shaka, hadi inafikia kwamba kulala ukiwa na yakini ni bora zaidi kuliko ibada katika hali ya shaka.

Na athari ya maarifa katika mwenendo na kazi inajulikana kwa kuangalia athari mbaya ya ujinga katika harakati ya mwanadamu, hiyo ni kwa sababu wewe hutomuona mjinga isipokuwa ama amefurutu ada au ametweza.[8]

Kama ambavyo maarifa sahihi yanaathiri katika harakati za mwanadamu, hakika kuathiri kwake katika itikadi yake ni kukubwa sana. Hiyo ni kwa sababu itikadi ni uzio wa jumla wa harakati ya mwanadamu bali ndio lengo la maisha yake. Na kwa kadiri inavyokuwa itikadi yake sahihi, basi maisha yake yatakuwa mazuri, na kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu ameamuru watu kuitikia wito wa Mitume Wake kwa sababu wao wanawalingania watu katika yale ambayo humo kuna kheri na mafanikio yao na maisha yao:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ ۖ

**"Enyi mlioamini mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapowaiteni katika lile litakalowapa uhai." Sura al-Anfaal 8:24**

---

[8] Hadithi zilizotajwa ni kutoka katika kitabu *al-Hayati*, Juz. 1.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 13 11/23/2016 12:37:27 PM

Na sisi tunakuta kwamba katika maombi muhimu ambayo muumini anamuomba Mola Wake ni maombi ya maarifa: "Eee Mwenyezi Mungu nifahamishe nafsi yako hakika kama hutonifahamisha nafsi yako sitomjua Nabii wako. Eee Mwenyezi Mungu nifahamishe Nabii Wako hakika kama hutonifahamisha Nabii Wako sitomjua Hujja Wako. Eee Mwenyezi Mungu nifahamishe Hujja Wako hakika kama hutonifahamisha Hujja Wako nitapotea katika dini yangu." Na huu ni mlolongo mzuri katika kumjua Mwenyezi Mungu kisha kumjua Mtume kisha kumjua Hujja na Imam.

Na hii inabainisha moja ya sababu ambazo amepotea kwa ajili yake yule aliyepotea, ambapo wao katika moja ya vipengele vya mlolongo huu hawakupata taufiki ya maarifa sahihi na kamili. Ambao hawakumjua Mwenyezi Mungu ukweli wa kumjua, hawakumheshimu ukweli wa kumheshimu, hivyo wakapotoka katika njia tangu mwanzo wake. Na hao ni ambao hawakumjua Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ukweli wa kumjua na hawakujisalimisha kwake, na kwa hiyo walitangaza vita dhidi yake. Na wale ambao hawakumjua Imam kwa maarifa sahihi waligawanyika: Mwenye kupenda kupita kiasi na mwenye kuchukia, mwenye kutweza.

Katika nyanja hii tumekuta kwamba kutojua kabisa au kuwa na maarifa pungufu kumewapelekea hawa watu kufurutu ada, hususan na wao hawakujua siri ya ubora na daraja katika shakhisiya ya Maasumini, hivyo wakawapandisha Maasumini عليهم السلام daraja ya juu zaidi ya daraja ya kibinadamu, jambo ambalo Maasumini hawakuwa wanalidai, bali wanamlaani mwenye kufanya hivyo.

Hawa hawakuweza kukusanya baina ya ubinadamu wa Manabii na Maimamu عليهم السلام, na madaraja na fadhila zao, hivyo basi wakafuata moja ya njia mbili ili kupumzisha nafsi zao na taabu ya kutafakari na kukusanya baina ya nukta hizi mbili zenye kutatiza. Baadhi wakafuata njia ya kupuuza na kutweza, wakakadhibisha yaliyopokelewa



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 14 11/23/2016 12:37:27 PM

katika haki ya hao watukufu kati ya wanadamu, wakidai kwamba yaliyopokelewa ni uongo na kwamba hakuna tofauti baina yao na wao, namna gani yeye hawezi kujinasua na minyororo ya matamanio na pingu za kimada wakati wale wanaweza kuelea katika anga la fadhila. Hivyo ndivyo alivyokuta mwenye kuchukia mwenye kutweza.

Na wengine walizipumzisha nafsi zao kwa kuleta kisingizio kinachoridhisha dhamira zao, na hiyo ni kwa kuitakidi kwamba hawa hawana sifa hizi wala hawasifiki kwa sifa hizo isipokuwa wanabeba roho nyingine ya uungu. Hakika wao si binadamu, ambapo binadamu ananyenyekea katika matamanio ya kiroho na kimwili, na ana mpaka wa zama na sehemu, na hawa hawana mpaka. Hivi ndivyo alivyoanza mwenye kupenda kwa kufurutu ada. Ambaye amesema kweli lakini hakuweza kujua na kuoanisha na kukusanya pamoja baina ya ubinadamu wa Maasumini na fadhila zao.

## 2. Hadithi za Mifano:

Katika Qur'ani Tukufu kunapatikana Aya zilizo wazi ambazo ndizo msingi wa kitabu na nyingine za mifano. Na zilizo wazi ndizo ambazo wengi wanaweza kuzifahamu na kujua makusudio yake, wakati ambapo za mifano ni zile ambazo hawezi kufahamu maana zake isipokuwa wale zilioteremshwa kwao au waliobobea katika elimu, na yote hayo ni kwa mafunzo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na kazi ya watu wa kawaida katika yanayohusiana na mifano ni kuyarejesha kwa Mwenyezi Mungu kisha kwa Mtume na Makhalifa wake. Na kuzifanyia kazi kwa Aya hizi za mifano kabla ya kurejea kwa Mwenyezi Mungu na kwa Mtume sio tu hakuongoi bali ni dhambi na ni kuangamia. Na kama ilivyo katika Qur'ani Tukufu kuwa kuna Aya zilizo wazi na nyingine ambazo kuzifahamu kwake hakuwezekani kwa wasiobobea katika elimu, vilevile katika hadithi



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 15 11/23/2016 12:37:27 PM

na athari miongoni mwazo kuna ambazo wanaweza kuzifahamu wengi kati ya wanaozisikia na miongoni mwao kuna ambazo hawawezi kuzifahamu isipokuwa maulamaa.

Kama ilivyokuwa kazi ya watu wa kawaida katika yanayohusiana na Aya za mifano katika Qur'ani ni kuzirejesha kwa Mwenyezi Mungu na kwa Mtume Wake, hakika hapa kazi ni hiyo hiyo, pamoja na kuhifadhi mnasaba baina ya Aya na hadithi katika upande wa upokezi usio na shaka kwa cha kwanza, huku cha pili kikihitajia uhakiki. Hivyo haijuzu kukataa athari na hadithi kwa kuwa tu akili zetu hazifikii au haziisadiki, bali zirejeshwe kwa wanaozijua. Na tatizo ni wasiokuwa wajuzi kuamiliana pamoja na hadithi hizi na kuzifasiri kulingana na akili zao na kuharibu, badala ya kutengeneza.

Na hali ambayo sisi tumo humo ni aina hii. Kwa mifano tuchukue mfano wa wafurutu ada wa wakati wa Amirul-Mu'minin عليه السلام. Anasema Ibu Abil-Hadid: "Ilipodhihiri kutoa kwake baadhi ya habari za ghaibu muda baada ya muda, walisema: 'Hakika hiyo haiwezekani ikawa isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, au kwa mwenye kujipamba na sifa ya uungu katika mwili wake.' Naapa kwa hakika hawezi hilo isipokuwa kwa kudra ya Mwenyezi Mungu juu yake, lakini hailazimu katika kudra zake juu yake kuwa yeye ndio Mungu au kuwa na hali ya dhati ya Mungu. Na baadhi yao wakang'ang'ania shaka dhaifu mfano wa kauli ya Umar رضي الله عنه aliyoisema wakati Ali عليه السلام alipong'oa jicho la mtu aliyemkanusha Mungu katika Eneo Takatifu: 'Nitasema nini kuhusu mkono wa Mwenyezi Mungu uliong'oa jicho katika Eneo Takatifu la Mwenyezi Mungu!' Na mfano wa kauli ya Ali: 'Wallahi sikung'oa mlango wa Khaibar kwa nguvu ya kimwili bali ni kwa nguvu za kiungu.' Na mfano wa kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: 'Hakuna Mungu isipokuwa Allah peke Yake, amesadikisha waadi Wake, amemnusuru mja Wake na ameshinda makundi peke Yake.' Na ambaye



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 16 11/23/2016 12:37:27 PM

alishinda makundi ni Ali bin Abutalib عليه السلام kwa sababu yeye aliua shujaa wao na mpiganaji wao Amru alipovuka handaki. Wakaamka asubuhi ya usiku ule wakiwa ni wenye kukimbia na wenye kushindwa bila ya kupigana baada ya kuuliwa shujaa wao."[9]

Na vile vile kauli iliyopokewa kutoka kwa Nabii ﷺ: "Ali عليه السلام amekujieni kwa *sahaab*, hawa kwa ujinga wakadhani kwamba makusudio katika maneno yake ni kwamba amekuja na mawingu, wakati ambapo Mtume ﷺ aliashiria Ali kuvaa kilemba cheusi alichopewa zawadi na Mtume na alikuwa anakiita *sahaab*.

### 3. Maslahi ya Wenye Kufurutu Ada:

Inaongezewa katika kutokuwa na maarifa, na katika hadithi za mifano, kwamba baadhi ya wafurutu ada walikuwa wanamiliki zaidi ya milki moja. Pamoja na kwamba wao katika hatua ya awali walikuwa wanakatazwa na Maasumini عليهم السلام kulingania madai yao, na katika hatua nyingine Maasumini عليهم السلام wanawalaani, wanawafukuza na wanajiepusha nao, isipokuwa wao wafurutu ada hawakuacha kung'ang'ania katika kulingania madai yao.

Hapa ni lazima kutafiti juu ya maslahi, kwani hawa kama lengo lao lingekuwa sio maslahi ya kimada au umashuhuri wa kijamii na uongozi, wangekuwa hivyo kwa hilo katazo. Bali kwa kujiepusha huko wangekuwa wanaacha ulinganiaji wao na wanaondoka. Lakini maadamu ulinganiaji huu unawaletea uwepo wa kijamii na kuzungukwa na wapumbavu na wajinga miongoni mwa watu, basi hawakuacha kuendelea! Bali ufurutu ada ulikuwa ni aina ya kukimbia kushikamana na dini. Mwenye kufurutu ada anaanza kwa kumtukuza Mtume au Imamu na kumnyanyua juu zaidi ya daraja yake kwa kumfanya kuwa ni Nabii au Mungu - *audhubillahi* - kisha anaijaalia nafsi yake kuwa ndio mlango na njia pekee ya kumfikia, na

[9] *Sharh Nahjul-Balaghah* 5/6.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 17 11/23/2016 12:37:27 PM

anafaradhisha kwa mwenye kuamini daawa yake amwamini yeye kuwa ndiye mlango wa Imamu au wa Nabii, wa huyo Mungu! Kisha anaanza kuporomosha wajibat za kidini katika nafsi yake na kwa anayemfuata, wajibat moja baada ya nyingine. Na kama tukitazama katika yaliyoandikwa na historia miongoni mwa harakati za wafurutu ada katika wakati wa Amirul-Mu'minin عليه السلام tutakuta kwamba zilimalizikia kwenye kuhalalisha haramu na madhehebu yasiyoshikamana na dini.

Wafurutu ada katika wakati wa Amirul-Mu'minin عليه السلام wanafungua katika mwezi wa Ramadhani bila ya kuwa ni wagonjwa wala kuwa safarini, kisha wananadi: "Wewe! Wewe!"

Na ni hao hao baadaye wakati wa Imamu Hasan al-Askariy عليه السلام utawakuta wanaleta tafsiri batili ya kupinga wajibu wa kidini, wao wanasema: Hakika Swala maana yake ni mtu na sio rukuu wala sijida. Vilevile Zaka maana yake ni mtu na sio idadi ya dirhamu na wala sio kutoa mali, na wanakwenda mbali katika hayo hadi wakaporomosha wajibu na wakahalalisha haramu na wakahalalisha kuoa mahramu!

Na Ahlul-Bayt عليهم السلام waliumbua lengo hili ambalo wanalipigia mbizi wafurutu ada, nalo ni kuporomosha wajibu za kidini, na walihadharisha hilo. Kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام hakika amesema: "Wahadharisheni vijana wenu, juu ya wafurutu ada, angalieni wasiwaharibu, hakika wafurutu ada ni viumbe waovu mno, wanadharau utukufu wa Mwenyezi Mungu na wanadai uungu kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu. Wallahi hakika wafurutu ada ni waovu zaidi kuliko Mayahudi, Wakristo na Majusi ambao wamemshirikisha Mungu." Kisha akasema: "Kwetu anarejea mwenye kufurutu ada na hatumkubali. Na kwetu anarejea mwenye kutweza na tunamkubali." Akaambiwa: Vipi ewe Mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: "Mwenye kufurutu ada amezoea kuacha Swala, Zaka,



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 18 11/23/2016 12:37:27 PM

Saumu na Hija, hivyo hawezi kuacha mazoea yake kamwe, lakini mwenye kutweza akitambua, anafanya amali na kutii."[10]

## 4. Sababu Nyingine:

Na kwa sababu sisi hatutaki kujikita zaidi katika utafiti wa maudhui ya ufurutu ada na sababu zake, hivyo tunaashiria sababu hizo kwa ishara ya haraka. Miongoni mwa sababu zinazosaidia kuenea ufurutu ada ni kusambaa na kupenya fikira za wageni katika itikadi za Kiislamu hadi kwenye jamii ya Kiislamu. Hiyo ni kwa sababu kazi ya kupanua mamlaka ya dola ya Kiislamu katika nchi za jirani iliwafanya watu wa sehemu hizo kuchanganyikana kwa urahisi na Waislamu na kukapatikana katika mchanganyiko huu wa kijamii hali ya kubadilishana utamaduni. Na kama ambavyo Waislamu waliwaathiri wananchi wa sehemu hizo na wakawakinaisha katika dini, hakika ndivyo itikadi ya wananchi wale ilivyopata njia ya kuchanganyika na itikadi ya Uislamu hali ya kuwa imevaa vazi jipya la Kiislamu.

Kwa kuongezea harakati za uhubiri ambazo zilichangamka wakati huo, zilikuwa na nafasi kubwa katika kupenya huku, kwani kupitia kupenya huku yalipenya mengi katika fikra za Kiyahudi kwa mikono ya Waislamu wenyewe, mfano Abdullah bin Amri bin Al-Aas, kwani imepokewa kwamba aliteka marafiki wawili kati ya vitabu vya watu wa Ahlulkitabi katika siku ya Yarmuku, hivyo alikuwa anawasimulia watu baadhi ya yaliyomo humo kwa kutegemea hadithi iliyopokelewa."[11]

Na tunaweza kufahamu kupenya huku, kwa kufuatilia kwetu kuenea kwa baadhi ya makundi. Huyu hapa Sausan mkiristo, alikuwa ni wa kwanza aliyetamka juu ya makadara na akadhihirisha Uislamu. Na kwake amechukua Maabad al-Jahaniy, na akachukua

[10] *Biharul-An'war*, Juz. 25, uk. 295.
[11] *Al-Israiliyaati Wa atharuha Fiy Kutubi Tafsiri*, Dr. Zamariy Na'ana'atu uk. 110.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 19 11/23/2016 12:37:27 PM

Ghailan al-Dimashqiy kutoka kwa Maabad. Kisha Sausan akarejea kwenye ukristo wake baada ya kupenyeza fikra yake. Na huyu hapa Ibn Kilab kutoka al-Babiyatu al-Hashawiyah, Ibaad bin Sulaiman alikuwa anasema kwamba yeye ni mkiristo. Amesema Abu Abbas al-Baghawiy: "Tuliingia kwa Fithuna, mkristo ambaye alikuwa huko Roma pande za Ulaya, yakatokea mazungumzo hadi nikamuuliza juu ya Ibn Kilab, akasema al-Fithuna: 'Mwenyezi Mungu amrehemu Abdillah (jina la Ibn Kilab), alikuwa ananijia na kukaa katika kona ile. Na kwangu amechukua kauli hii, na kama angeishi (muda mrefu) basi tungewafanya Waislamu kuwa Wakristo."[12]

Kama ambavyo sababu nyingine ilikuwa ni kulipiza kisasi ambako kulitokea kwa baadhi ya makundi ya Waislamu – au watu wao – dhidi ya kudhulumiwa kwa watu fulani katika historia. Kurundikana kwa dhulma na kuongezeka kwake kuliko kiwango kilichotarajiwa dhidi ya haki ya *Ahlul-Bayt* عليهم السلام ilipelekea baadhi ya wajinga kati ya watu kuchukua msimamo wa kinyume dhidi ya dhulma hizo kwa kupindukia katika kuwatukuza watu hawa (*Ahlul-Bayt*), kiasi kwamba walitoka katika njia ya sawa.

## NAMNA GANI WALIKABILIANA NA UFURUTU ADA:

Tunaweza kugawa juhudi za Ahlul-Bayt عليهم السلام katika kukabiliana na ufurutu ada katika sehemu mbili kufuatana na kugawanyika makundi haya. Kundi la kwanza ni lile ambalo liliamua kupita njia ya ufurutu ada. Sio kwa ajili ya kukanganyikiwa, bali ni kwa ajili ya maslahi. Hawa ambao wanajua wanafanya nini, kwa watu mfano wa hawa, Ahlul-Bayt عليهم السلام hawakuwa na msimamo isipokuwa wa

---

[12] *Al-Imamu Swadiq Wal-Madhahibu al-Arubaat*, Juz. 4, uk. 373.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 20 11/23/2016 12:37:27 PM

kuwafedhehesha, kuwalaani na kuwafukuza, pale wanapoweza, kama ilivyokuwa hali wakati wa Amirul-Mu'minin عليه السلام. Hakika wao waliteketezwa kwa kuuliwa na kuchomwa moto. Na katika zama zilizofuata Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wanaamuru wafuasi wao kuwauwa[13] - wanapoweza – na wanadhihirisha kujiepusha nao mbele ya wafuasi wao.

Ama kundi la pili na ambalo inadhihirika kwamba ndilo lilikuwa kubwa zaidi, ni lile ambalo halikuwa na uwezo wa kumjua Mtume na Maimamu عليهم السلام kwa maarifa sahihi na walikanganyikiwa na mambo, na hivyo walinasaibisha kwao mambo wanayojiepusha nayo kwa msukumo wa kuheshimu, na kutatua tatizo la kifikira ambalo linawakabili, kwa hawa tunakuta Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wanafanya:-

**Kutilia Mkazo Hali ya Ubinadamu:**

Kama ilivyotangulia kusemwa hakika baadhi ya watu kwa upungufu wao katika maarifa yao wanakimbilia katika kuwapandisha Manabii na Mawasii عليهم السلام wao kutoka katika daraja ya ubinadamu kwenda daraja ya juu zaidi. Na Qur'ani Tukufu katika kutatua tatizo hili iko wazi na dhahiri iliposema kwa kumwelekeza Mtume صلى الله عليه وآله وسلم:

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ

**"Sema: Hakika mimi ni binadamu kama nyinyi tu, nimeletewa wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu mmoja." (Suratul-Kahf; 18:110).** Kwani yeye ni kama wao kabisa katika kuumbwa kwake na kutengenezwa kwake, na matamanio ambayo wamepewa na mbinyo ambao unanasibiana naye, isipokuwa tofauti baina yake na wao ni kwamba anapata wahyi, na kwamba wahyi huu umetengeneza nafsi yake - na sio mwili - upya.

[13] Rejea *Nidhamul-Idaratu Diniyati* cha mtunzi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 21 11/23/2016 12:37:27 PM

Na katika Aya nyingine Qur'ani inazungumza juu ya Nabii Isa عليه السلام na mama yake, Maryam عليها السلام, ambapo humo wana wa Israeli walifurutu ada kuhusu Isa na mama yake عليهما السلام: "Masihi Ibn Mariyam hakuwa ila ni Mtume na walishapita kabla yake Mitume, yeye na mama yake mkweli walikuwa wanakula chakula." Maneno mawili "Mtume na Mkweli" yanaashiria kwenye upande unaofungamana na ujumbe wa Mwenyezi Mungu, wakati ambapo maneno "wanakula chakula" yanaashiria vitendo vya kibinadamu walivyokuwa wanavifanya wao. Na imepokewa katika tafsiri ya "wanakula chakula" kwamba hakika wao walikuwa wanajisaidia, ni katika mlango wa kutaja sababu ili ioneshe matokeo (kula chakula kunamfanya mtu apatwe na haja na kujisaidia), na kitendo hiki ni kitendo cha kibinadamu.

Na katika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم amesema: "Msininyanyue juu zaidi ya haki yangu, hakika Mwenyezi Mungu amenijaalia kuwa mja kabla ya kunijaalia kuwa Nabii." Na Amirul-Mu'minin عليه السلام anahadharisha juu ya ufurutu ada kwa kubainisha kwamba pamoja na fadhila zake zote bado yeye ni mja wa Mwenyezi Mungu.

Na tunakuta Imamu as-Sadiq عليه السلام anamwamuru mmoja wao, ambaye alikuwa anabeba baadhi ya fikra za ufurutu ada kwamba amwandalie maji ili aende uwani, na kwa kitendo hiki zinaporomoka fikra zote za yule mtu, na hebu sasa tusome riwaya. Imepokewa kutoka kwa Ismail bin Abdil-Aziz amesema: Aliniambia mimi Abu Abdillahi عليه السلام: "Ewe Ismail! Niwekee maji uani." Nikasimama nikamuwekea, akaingia. Nikasema katika nafsi yangu: Mimi nasema kwake kadhaa na kadhaa na anaingia uwani na anatawadha? Haukupita muda akatoka akasema: "Ewe Ismail, usinyanyue jengo zaidi ya uwezo wake litaporomoka, tujaalieni kuwa ni viumbe na kisha semeni kwetu mtakayo, hapo hamtofikia." Ismail anasema: Na ni-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 22 11/23/2016 12:37:27 PM

likuwa nasema kwamba yeye….. na nasema na nasema….. (yaani yeye ni Mola na anaruzuku na mfano wa hayo).

Ona Imamu عليه السلام katika mas'ala haya amevunja wazi fikira za kimakosa katika akili ya mtu huyu. Na utakuja utafiti ujao juu ya maisha yao ya kiroho na yanayofungamana nayo miongoni mwa matamanio ya kijinsia na juu ya mas'ala ya chakula, vinywaji na mavazi, ambayo yanaunga mkono na yanaongeza katika msisitizo wa upande huu wa kibinadamu katika kundi lile ambalo limetaka kuwaheshimu heshima kubwa hatimaye likakosea njia, lakini sisi hapa tunatosheka kwa kunukuu hadithi kutoka kwa Imamu Ridha عليه السلام na ambayo inaonyesha kwamba katika zama zake, kwa kuzingatia kwamba ilikuwa ni zama ya midahalo na mijadala, ilishuhudia mijadala mingi kuhusu nyanja hii.

Maamun alimwambia Imamu Ridha عليه السلام: Imenifikia habari kwamba watu wanafanya ufurutu ada kwenu na wanavuka mipaka kwenu. Imamu Ridha عليه السلام akasema: "Amenisimulia baba yangu Musa bin Ja'far bin Muhammad kutoka kwa baba yake Muhammad bin Ali kutoka kwa baba yake Ali bin Husein, kutoka kwa baba yake Husein bin Ali bin Abutalib عليهما السلام, amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: 'Msininyanyue juu zaidi ya haki yangu, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amenijaalia kuwa mja kabla ya kunijaalia kuwa Nabii.' Mwenyezi Mungu (swt) amesema:

مَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُؤْتِيَهُ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ثُمَّ يَقُولَ لِلنَّاسِ كُونُوا عِبَادًا لِي مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَٰكِنْ كُونُوا رَبَّانِيِّينَ بِمَا كُنْتُمْ تُعَلِّمُونَ الْكِتَابَ وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ وَلَا يَأْمُرَكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ وَالنَّبِيِّينَ أَرْبَابًا ۗ أَيَأْمُرُكُمْ بِالْكُفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 23 11/23/2016 12:37:27 PM

**"Haiwezekani kwa mtu aliyepewa na Mwenyezi Mungu Kitabu na hekima na Unabii, kisha awaambie watu: Kuweni wa kuniabudu mimi badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini (atawaambia): Kuweni wenye kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa mnafundisha Kitabu na kwa sababu mnakisoma. Wala hatawaamrisha kuwafanya Malaika na Manabii kuwa waungu. Je, atawaamrisha ukafiri baada ya kuwa nyinyi ni Waislamu.' (Al-Imran: 79-80).**

Na amesema Imam Ali عليه السلام: 'Wataangamia kwa ajili yangu watu wawili, na wala mimi sina dhambi: Mwenye kupenda kufurutu ada na mwenye kuchukia kupita kiasi.' Na sisi tunajiepusha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na mtu ambaye anafurutu ada kwetu na kutunyanyua juu zaidi ya mpaka wetu kama vile Isa bin Mariyam عليه السلام alivyojiepusha na Wakristo, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِنْ وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۖقَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ ۚ إِنْ كُنْتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ ۚ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ

مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِ أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۚ وَكُنْتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَا دُمْتُ فِيهِمْ ۖفَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

'Na pale Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe Isa bin Mariyam: Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa miungu badala ya Mwenyezi Mungu? Atasema: Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa niliyasema basi bila shaka umekwishayajua. Wewe unajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, wala mimi siyajui yaliyo katika nafsi Yako; Hakika Wewe



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 24 11/23/2016 12:37:27 PM

ndiye mjuzi zaidi wa yaliyofichikana. Sikuwaambia ila uliyoniamrisha, ya kwamba mwabuduni Mwenyezi Mungu Mola Wangu na Mola Wenu. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao, na uliponifisha ukawa Wewe ndiye Mwangalizi juu yao; na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu. (Al-Maida: 116-117).

Na Mwenyezi Mungu amesema: ‘Masihi hataona unyonge kuwa mja wa Mwenyezi Mungu wala Malaika wenye kukurubishwa.’ Na amesema (swt): ‘Masihi mwana wa Maryam hakuwa ila ni Mtume. Wamepita kabla yake mitume; na mama yake mkweli; wote wawili walikuwa wakila chakula.’ (Al-Maida; 5:75.). Na maana yake, hakika wao walikuwa wanajisaidia, hivyo mwenye kudai uungu kwa Manabii au mwenye kudai uungu kwa Maimamu au utume au kudai uimamu kwa asiyekuwa Imamu basi sisi tuko mbali naye duniani na akhera.”[14]

**Njia ya Kutweza:**

Katika mukabala wa njia ya ufurutu ada na kuchupa mpaka kwa Mitume na Mawasii kulikuwa na njia ya kutweza na kupuuza, ambapo watu wa njia hii sio tu hawakuchupa mpaka kwao bali wao walipunguza haki yao na kunasibisha kwao kauli na vitendo ambavyo havifai kwa watu wa kawaida miongoni mwa Maulamaa wanaoheshimika au wenye elimu, bali hata watukufu katika makabila. Watu wa kundi hili walichupa mpaka katika kutia mkazo juu ya ubinadamu wao kiasi kwamba waliubana upande wa ghaibu na yanayohusiana na wahyi na ujumbe katika kona finyu sana katika maisha yao.

Na tutaelezea sababu ambazo zilisaidia katika kuenea fikira za njia hii, na ambayo inadhihirika kwamba haihusiani tu na tafsiri ya maisha ya Mtume Muhammad ﷺ bali inavuka mpaka hadi katika kufasiri maisha ya Manabii عليهم السلام waliotangulia ukiachilia mbali Mawasii. Pamoja na kwamba nususi zifuatazo – na ambazo tunaitakidi

[14] *Biharul-An’war*, Juz. 20, uk. 271.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 25 11/23/2016 12:37:28 PM

kosa lake – haziafikiani na nafasi ya ujumbe na utume, isipokuwa ni kwamba kwa kuwa zilikwishapokelewa katika vitabu vya hadithi bali katika *Sahihi Sita* basi ni lazima kuashiria katika baadhi yake, ili tuone namna gani mwelekeo huu pia umetumbukia katika kuchupa mpaka kama ilivyotumbukia njia ya wafurutu ada, lakini katika upande wa mukabala. Na tunaona namna gani njia hii ilivyokuwa imesimama juu ya msingi usio sahihi, hiyo imepelekea kudai hadithi hizi juu ya Mtume ﷺ na Mitume waliotangulia, na zifuatazo ni baadhi ya hadithi hizo:

**Nabii Anajisaidia Haja Ndogo Wima:**

Kutoka kwa Abi Wail amesema: Abu Musa alikuwa mkali sana kuhusu mkojo, na alikuwa akisema kwamba hakika wana wa Israil walikuwa unapodondokea mkojo katika nguo ya mmoja wao wanaikata. Hudhaifa amesema: "Natamani kwamba mtu wenu asishadidie sana kwa ukali huu, kwani hakika mimi niliona wakati nilipokuwa natembea na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, alifika katika jalala nyuma ya ukuta akasimama kama anavyosimama mmoja wenu akajisaidia haja ndogo, nikasogea mbali naye, akaashiria kwangu, nikaenda nikasimama nyuma yake hadi akamaliza."[15]

**Na Analaani Bila Kustahili:**

Kutoka kwa Abu Huraira, amesema: Hakika Nabii ﷺ alisema: "Eee Mwenyezi Mungu, hakika Muhammad anakasirika kama anavyokasirika mwanadamu, na hakika mimi nimeshachukua Kwako ahadi, hivyo usiikhalifu kwangu, kwamba mja yeyote niliyemuudhi au niliyemtukana au niliyemlaani au niliyempiga basi jaalia hiyo iwe ni kafara yake na ukuruba unaomkurubisha Kwako."[16]

---

15 *Sahih Bukhari*, Juz. 1, kitabu cha wudhu.

16 Rejea iliyotangulia, Juz. 4, Kitabu cha daawa.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 26 11/23/2016 12:37:28 PM

**Na Anasahau Aya za Qur'ani na Anaziondoa:**

Kutoka kwa Hisham kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Aisha amesema: "Nabii ﷺ alimsikia mtu anasoma msikitini, akasema: Mwenyezi Mungu amhurumie. Amenikumbusha Aya kadhaa wa kadhaa nilizozisahau katika sura kadhaa wa kadhaa."[17]

**Na Anasikiliza Mziki Kutoka kwa Waimbaji wa Kike:**

Kutoka kwa Aisha, amesema kwamba hakika Abu Bakr aliingia kwake siku ya Iddil-Fitri au Iddil-Adhuhaa wakati Nabii yuko kwake, na walikuwepo kwake waimbaji wawili wa kike wanaimba yale ambayo Answari walitupiana siku ya ujirani, Abu Bakr akasema: "Zumari za shetani?" alisema mara mbili, Nabii ﷺ akasema: "Waache ewe Abu Bakr, hakika kila watu wana sikukuu na hakika sikukuu yetu ni siku ya leo."[18]

**Na Anawaangalia Yeye Pamoja na Wake Zake, Wanenguaji Wakinengua Msikitini:**

Kutoka kwa Aisha hakika amesema: Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ siku moja katika mlango wa chumba changu ilihali Waethiopia (wanenguaji) wananengua msikitini, na Mtume wa Mwenyezi Mungu ananisitiri kwa nguo yake ili niangalie unenguaji wao, kisha anasimama kwa ajili yangu hadi mimi nakuwa ndiye mwenye kuondoka (yaani anaondoka na kumwacha Mtume akiendelea), waheshimuni heshima ya binti mdogo wa umri anayependa mchezo."[19]

**Shavu Lake Liko Juu ya Shavu la Mke Wake:**

Vilevile Aisha katika Hadithi nyingine anasema: Siku ya Iddi Msudani alikuwa anacheza kwa panga na mkuki, ima ni mimi nilimuuli-

17 Rejea iliyotangulia, Juz. 8, Kitabu cha daawa.
18 Rejea iliyotangulia Juz. 5. Kitabu cha fadhila za Maswahaba wa Mtume.
19 Rejea iliyotangulia, Kitabu cha Swala.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 27 11/23/2016 12:37:28 PM

za Nabii au ni yeye alisema: "Je unapenda kuangalia?" Nikasema: "Ndio." Akanisimamisha nyuma yake ilihali shavu lake likiwa kwenye shavu langu, huku akisema: "Ni juu yenu enyi Bani Arfida (kwa kuwashajiisha) hadi nikachoka." Akasema: "Imetosha? Nikasema: "Ndio." Akasema: "Nenda."[20]

Na kama tungefuatilia hadithi nyingine tungerefusha sana, na sisi hapa hatutaki kujadili kila hadithi peke yake isipokuwa katika upande wa sanadi yake au katika upande wa kukhalifu kwake hadithi nyingine ambazo zimenukuliwa na vitabu hivi sahihi katika yanayohusiana na sira ya Mtume ﷺ, na amezungumzia hadithi hizo kwa namna ya pekee mwandishi wa kitabu *Fiy Rihabis-Sahihain*,[21] atakaye arejee huko.

Isipokuwa sisi katika mtazamo wa kwanza tunaweza kuona kwamba hizi hadithi hazilandani katika maana zake na muumini yeyote wa kawaida ukiachilia mbali Bwana wa viumbe na mbora wa Manabii na mkamilifu wa Mitume aliyefunzwa adabu na Mwenyezi Mungu. Kama zisingepokewa Hadithi hizi katika vitabu Sahihi Sita na tukasahau jina lililotajwa humo, kisha tukazionyesha kwa maulamaa kwamba ni matukio ya maisha ya mwanachuoni fulani kati ya wanachuoni, hakika wao bila shaka watamkimbia na watajisikia kinyaa!

Ikiwa Abu Musa ambaye ni mmoja wa Waislamu anashadidia katika mas'ala ya haja ndogo na anaona ni upungufu kwa mwenye kujisaidia wima, na hadithi nyingine zinaona – katika vitabu sahihi vilevile – kwamba miongoni mwa adhabu za kaburi ni ile inayosababishwa na kitendo cha kupuuzia haja ndogo na najisi, kisha Abu Musa anawahimiza Waislamu ambao wanamsikiliza kwamba wazingatie hilo, sasa vipi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye

[20] Rejea iliyotangulia Juz. 11, Kitabu cha Swala.

[21] Rejea iliyotangulia Juz. 4, Kitabu cha Jihadi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 28 11/23/2016 12:37:28 PM

ndio mkamilifu zaidi wa watu kwa tabia azingatie kuwa ni jambo la kawaida tu, kisha afanye kama anavyofanya mmoja wenu? Kulingana na tamko la hadithi!

Kisha sisi katika mas'ala ya kulaani hatuwezi kukubali hayo kwa mtu wa kawaida kwa sababu kulaani bila ya kustahili, kutukana na kushutumu tu bila ya sababu ni kinyume na uadilifu na tabia njema. Vipi tunakubali hilo kwa Mtukufu Mtume ﷺ naye imepokewa kutoka kwake kwamba hakuwa muovu wala mwenye kupenda uovu, hata katika kuamiliana na Mayahudi ambao walikuwa wanamtukana na wanamuombea mauti. Wala katika kuamiliana na makafiri katika vita vya Uhudi kwa sababu hakutumwa kuja kulaani bali alitumwa kuwa ni rehema kwa walimwengu, namna gani na hali ndio hii analaani watu Waislamu bila ya kustahili?[22]

Mtu analaani ovyo na anatukana, anapiga mijeledi na ananyenyekea kwenye hisia zake na matamanio yake katika yanayohusiana na kuwaadhibu watu bila ya dalili wala kosa, namna gani ataaminiwa katika maneno ya Mwenyezi Mungu na katika kutekeleza hukumu?! Jawabu la swali hili liko katika hadithi ya tatu ambayo inaona kwamba Mtume ﷺ anasahau anaondoa Aya katika Qur'ani katika Sura.

Naapa kwa Mwenyezi Mungu - ndugu yangu msomaji – je unategemea kwa mtu ambaye alikuwa anaandaa kikosi cha zaidi ya watu 80 na jeshi, na anaongoza dola na kuelekeza hukumu za Mwenyezi Mungu na kuwafundisha Waislamu n.k. Je, unatarajia kwa mtu kama huyu aache majukumu yote hayo ili atekeleze raghaba za wake zake katika kuangalia wanenguaji na mwenye kucheza kwa kutumia mkuki na watu dhaifu? Na wapi? Msikitini katika nyumba ya Mwenyezi

[22] Halifichikani lengo la kisiasa ambalo zinalenga Hadithi hizi, ambapo Mtume ﷺ aliwalaani baadhi ya wale ambao walidhihirisha Uislamu na akajiepusha nao na akawafukuza baadhi yao Madina, hivyo ili kuwatakasa hawa wamenasibisha kwa Mtume ﷺ hadithi hizi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 29 11/23/2016 12:37:28 PM

Mungu ambayo imewekwa kwa ajili ya ibada na kumtaja Mwenyezi Mungu! Jambo ambalo halikubali mwenye akili. Imepokewa katika mwisho wa hadithi hii kwamba Umar bin al-Khatwabi alipowaona hawa wanenguaji msikitini aliwakemea na akawapiga mawe wakati ambapo Mtukufu wa Manabii na Mitume ﷺ anakaa pamoja na mke wake ilihali shavu la mke wake liko juu ya shavu lake, anaangalia na anaburudika kwa mandhari haya ya kipuuzi!

Na mas'ala haya yamegeuka katika pande mbili:

**Kwanza:** Yamepanuka na kusambaa na kuwajumuisha Manabii wengine عليهم السلام waliobakia.

**Pili:** Hakika yameenea katika sura ya itikadi baada ya kuwa ni habari tu.

Amesema Ibn Abil-Hadidi kwa muhtasari: "Watu kati ya Makhawariji, na pia Ibn Fauriki miongoni mwa Maashirah, wamesema kwamba inajuzu kumpa utume mtu ambaye alikuwa ni kafiri. Na amesema Barughuth mwanatheolojia kutoka Najariyah: 'Mtume kabla ya kupewa utume hakuwa ni mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu.' Na amesema as-Sariy: 'Hakika (mtume) alikuwa katika dini ya watu wake (shirki) kwa muda wa miaka arobaini.' Na amesema Ibn Hazmi katika kitabu chake *al-Faswili Fiyl Milali Wal-Ahwai*: 'Kundi moja limesema kwamba Mitumne wa Mwenyezi Mungu عليهم السلام wanafanya maasi makubwa na madogo isipokuwa uongo katika tablighi tu, nayo ndio kauli ya kundi la al-Karamiya miongoni mwa Mamurjiah. Na ndio kauli ya Abu Twayyib al-Baqalaniy katika Maashairah na mwenye kuwafuata."

Kisha akasema: "Ama huyu al-Baqalaaniy hakika tumeona katika kitabu cha swahiba wake Abu Ja'fariy as-Samnaaniy, kadhi wa Muuswil kwamba alikuwa anasema: 'Hakika kila dhambi kubwa au ndogo inajuzu kwa Mtume isipokuwa uongo katika tablighi tu.'



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 30 11/23/2016 12:37:28 PM

Na amesema: 'Inajuzu kwao kukufuru!' Na amesema: 'Nabii akikataza kitu kisha akakifanya sio dalili juu ya kwamba katazo hilo limefutwa, kwa sababu amelifanya kwa kumwasi Mwenyezi Mungu Mtukufu, na sio haki kwa wafuasi wake kumpinga. Na inajuzu kuwepo katika ummah wa Muhammad ambaye ni mbora kuliko Muhammad ﷺ tangu alipotumwa hadi kufariki kwake.'"[23]

Na tunamzindua msomaji mpendwa kwamba hawa wasemaji: Ni miongoni mwa Waislamu, ili asikanganyikiwe na mambo. Na sisi hapa hatutaki kujadili mas'ala ya kiitikadi ili tuyabatilishe, bali tulikuwa katika maudhui ya kubainisha jambo katika muamala wa kundi la kutweza Manabii عليهم السلام na bwana wao Muhammad ﷺ, kisha itakuwa rahisi kwako kujua mtazamo wao kwa Mawasii na Maimamu عليهم السلام.

## SABABU ZA KUTWEZA

### a- Upungufu wa Maarifa:

Kama ilivyotangulia kusemwa katika utafiti wa ufurutu ada, hakika hapa pia mambo ni vivyo hivyo. Kuwa na maarifa pungufu kuhusiana na Mtume au Maasum kunawafanya hawa wenye kuchupa mipaka kuzidisha upande wa kibinadamu kiasi kwamba kunakosekana humo athari ya upande wa ujumbe (*wahyi*) katika shakhisiya ya Maasumu.

Hakika wao wanadhani kwamba utume au uimamu ni vazi analivaa mwenye vazi wakati wa kazi ili ajulikane yuko katika fungu gani! Au ni kazi anaifanya kama anavyoifanya mtu mwingine, kama angekuwa hapo mtu mwingine, na kwamba yeye hana tofauti kabisa, na kwamba "Mtume si kingine ila ni wasila tu na sio lengo. Ubo-

[23] Maelezo ya Sheikh al-Arumuwiy katika *Nahjul-Haqi* cha Allammatu al- Hilliy uk. 142.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 31 11/23/2016 12:37:28 PM

ra wake unatokana na wahyi na kuathirika kwake kwa ujumbe na utukufu wake katika jihadi. Na kigezo chake katika tabia ni mfano wa kiongozi yeyote au mkuu yeyote. Kuchaguliwa kwake kwa ajili ya ujumbe sio sifa katika shakhisiya yake, bali ni kwa sababu ujumbe ni lazima ufikishwe kupitia kwa mtume anayetimiza masharti ya kutekeleza tablighi. Na kutia mkazo juu kuchagua na kuteua sio katika wahyi kwa chochote, nayo ni karibu sana na uteuzi wa Mayahudi, na wahyi unamaanisha yanayokuja baada ya kuchaguliwa, nayo ni tablighi na sio katika kumchagua mtu binafsi."

Na anaongezea Dr. Hasan Hanafiy anasema akieleza rai ya kundi hili katika yanayohusiana na Mtume:

"Hakika kuthibitisha kwamba Mtume ﷺ ndio mwisho wa Manabii na Mitume haimaanishi vilevile kutia mkazo juu ya fadhila ya mtu au juu ya sifa pekee kwa yeyote, bali inamaanisha kwamba utume umeshamalizika na kwamba mwanadamu ameshakuwa huru."[24]

Nadharia hii inavuka ukweli mwingi wa kihistoria na misingi ya itikadi, na inadhihirika humo upungufu wa maarifa ambao unapelekea kukuza upande wa kibinadamu na kufuta upande wa wahyi na uangalizi wa Mwenyezi Mungu hatua kwa hatua.

Hakika kuchaguliwa Muhammad ﷺ kubeba ujumbe ni sifa muhimu katika shakhisiya yake kwa sababu yeye alikuwa ni kiumbe bora zaidi kubeba ujumbe huu na kuufikisha kwake. Na lau kama kungekuwepo katika viumbe vya Mwenyezi Mungu kuanzia mwanzo wa kuumba hadi kusimama Kiyama aliye bora kuliko yeye ﷺ basi huyo angekuwa ndio mwenye kubeba jukumu la kufikisha ujumbe, na kuwa kwake mwisho wa Manabii inamaanisha ukiongezea kuhitimisha kwake unabii na ujumbe pia amehitimisha fadhila.

---

[24] *Minal-Aqiydatu Ilaa Thaurati*, Juz. 1, uk. 1 -17.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 32 11/23/2016 12:37:28 PM

Hakika sisi tunakuta nafsi zetu mbele ya mantiki yenye kusifika wakati Mwenyezi Mungu anapomwambia Nabii Wake Muhammad ﷺ, huyu ni Nabii aliyefundishwa adabu na Mwenyezi Mungu hadi akafikia kiwango amesema humo: "Hakika wewe uko katika daraja la juu kabisa la tabia njema" wakati huo akampa cheo ambacho Qur'ani haijakizungumzia kwa yeyote kati ya Manabii aliposema akiwahutubia wanadamu – na hususan waislamu – "Na aliyokuleteeni Mtume yachukueni na aliyowakatazeni yaacheni." Bali amewaadabisha Waislamu kwa adabu maalumu ya kuamiliana na Mtume. Hakika yeye amewaamuru kumswalia, kwa sababu Mwenyezi Mungu na Malaika Wake wamtakia rehema: "Hakika Mwenyezi Mungu na malaika Wake wanamsalia Nabii; enyi mlioamini mswalieni na msalimieni kwa wingi." Na akaweka kanuni na adabu, Surat al-Hujurati imezizungumzia.

Na haya hayajatimia isipokuwa baada ya kujiandaa Mtume ﷺ kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kufikia daraja aliyotakiwa, tangu mwanzo alikuwa miongoni mwa wenye kusujudu.[25] Na alikuwa chini ya uangalizi wa Mwenyezi Mungu na katika utoto wake, alipokuwa ananyonya Mwenyezi Mungu alimuwekea malaika mtukufu kati ya malaika, anayemuongoza njia nzuri na tabia njema ya ulimwengu usiku na mchana.[26] Vivyo hivyo hadi Mwenyezi Mungu alipomtuma kuwa muongozaji kwa viumbe.

Manabii na Mawasii walikuwa ni wanadamu, na hii ni sahihi, lakini ni binadamu wenye sifa ya juu zaidi kiasi kwamba wanaweza kuwa ni sehemu ya kumjua Mwenyezi Mungu, na makazi ya baraka za Mwenyezi Mungu na chemchem za hekima ya Mwenyezi Mungu na wahifadhi wa siri ya Mwenyezi Mungu. Sifa yao haikuwa katika sifa za kimwili wa nje na muundo wa kimwili, na hivyo waliko-

[25] Rejea *Faswilul-Aswihabi Twahirati Wal-Arhaami Al-Mutwaharati.*

[26] *Nahjul-Balaghah*, Hotuba ya 192.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 33 11/23/2016 12:37:28 PM

sea walioishi nao – na huenda waliokuja baada yao vilevile – pale wao walipotaka kuwepo na uhusiano tofauti unaoonyesha utume wa hawa na uimamu wa wale: "Na walisema ana nini huyu Mtume anakula chakula na anatembea katika masoko." Walitaka malaika anayetembea ardhini, wakati tofauti yao ilikuwa katika sifa zao za kinafsi na katika amali yao, upole wao na uwezo wao wa kiuongozi katika kina cha imani yao kwa Mwenyezi Mungu na ikhilasi yao katika dini yake.

**b- Sababu ya Kisiasa:**

Mwenye kuangalia kwa kina anaona kwa uwazi athari za sababu za kisiasa katika kuunda mtazamo huu na kuusambaza miongoni mwa Waislamu. Hiyo ni kwa sababu kuwadhihirisha Manabii na Maasumini kwa muonekano wa watu wapuuzi na binadamu ambao wanakokotwa na matamanio yao na hisia zao, inakuwa rahisi kwa watawala ambao wanataka kuendelea katika njia ya upuuzi na kuzama katika starehe.

Na inafahamika kwamba imani ya Waislamu imesimama juu ya kwamba makosa ya kidini na kukiuka hukumu za sharia hakuendani na nafsi ya uongozi wa kidini na uongozi wa Waislamu, na kwa kuona kuwa hawa viongozi walitopea katika upotovu, hivyo ni lazima pawepo na utatuzi (wa kuficha upotofu wao), utatuzi mzuri ni kudai vitendo hivyo kwa kiasi fulani ni vya Mtume ﷺ na kutia mkazo juu yake, ili vikifanywa vitendo hivyo na khalifa na mtawala iwe ni jambo lenye kuingia akilini.

Ikiwa Mtume anasikiliza waimbaji wa kike katika nyumba yake bila ya kuwakataza, ni kipi kitazuia khalifa kunywa pombe katikati ya wapenzi wake kwa amani hadi achanganyikiwe? Na ikiwa – *Audhubillahi* – anapewa zawadi ya pombe kabla ya utume[27] sasa nini

[27] Imepokewa katika *Musnad Ahmad* Juz. 4, Hadithi ya 235, yafuatayo: Kutoka kwa Nafi'i bin Kisaani kwamba baba yake alimpa habari kwamba alikuwa anauza pombe zama za



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 34 11/23/2016 12:37:28 PM

kinawazuia makhalifa kunywa pombe asubuhi na jioni baada ya utume?

**Ni Vivyo Hivyo Katika Kanuni:**

Ikiwa mwenye nyumba anapiga ngoma basi watu wote katika nyumba ni kuicheza. Kwa kumwangalia Mtume – ukiachilia mbali maimamu – na kwa sura hii ya binadamu katika daraja za chini kabisa, inamrahisisishia mtawala kuwa kiongozi wa Waumini, na mwakilishi wa Mwenyezi Mungu katika ardhi, na mwenye kuhuisha Sunnah, lakini wakati ule ule anakunywa pombe na anaacha swala …n.k.

Hapa kadhia inafanana na Mtume kuwa mtu wa kawaida anayefanya kazi katika shirika la Mwenyezi Mungu, hivyo anawajibika katika shirika hili – na viongozi wake – kwa wajibu na majukumu, lakini yeye anapomaliza zamu hawajibiki kwa chochote katika shirika hili.

Kwa kuongezea hayo, hakika kuondoa sifa ya "Na hatamki kwa matamanio" kunamfanya Mtume ﷺ kuwa ni kiongozi aliyekuja katika kipindi, na kama ilivyo harakati yake ndivyo ilivyo misingi yake. Harakati yake ni hisia yake na utashi wake, akawa anagawa laana na huruma, kulia na kushoto na anatoa cheo na hukumu za adhabu kwa anayestahili na kwa asiyestahili. Kisha inapoenea fikra hii, inamaanisha kwamba yaliyokuja katika kushutumu Bani Ummayya na kuwa kwao ni mti uliolaniwa katika Qur'ani na yaliyopokewa katika kufukuzwa baadhi ya watu na kutangaza kumwagwa damu za baadhi yao, haikuwa katika dini bali ni katika matamanio na hivi kinatimia kitendo cha kumtakasa

Nabii ﷺ, akamwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimekuletea kinywaji kizuri." Mtume ﷺ akasema: "Ewe Kisaani hakika imeharamishwa baada yako!"



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 35 11/23/2016 12:37:28 PM

al-Hikam, Marwan, Muawaiya na Bani Ummayya ili kumtuhumu Mtume ﷺ.[28]

Kisha maneno ya Mtume ﷺ katika wakati wake hayakuwa na hoja kulingana na mtazamo huu, kwa sababu yanatokana na matamanio! Ukiachilia mbali athari ya maneno haya baada ya kufariki kwake ﷺ, wakati huo kumfuata kwake kunakuwa ni jambo lisilokuwa la kiakili, je hajasema al-Hajaji al-Thaqafiy, naye anawaangalia Waislamu wanazunguka katika kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Wana nini wanazunguka vijiti vilivyotupwa na kuharibika? Si wangezunguka kasri ya koingozi wa Waumini (yaani kasri la al-Hajaji)?"

Hakika haya ni matokeo ya kawaida ya kundi la kutweza. Je inawezekana baada yake kuwajibika kuiga na kufuta sira yake na ilihali hali ndio hii?

**c- Fikra za Nje:**

Mustashiriqina wameshajiisha mwelekeo huu katika kuandika sira na katika kueleza shakhisiya ya Mtume ﷺ, ni sawa miongoni mwao wawemo waadilifu au waovu, kwani sababu iko wazi, ama waadilifu ni kwa sababu muundo wa utamaduni ambao wametokana nao ni muundo wa kimada, hauwezi kufahamu kikamilifu sababu za ghaibu wala hawawezi kufahamu shakhsiya ya Mtume ﷺ.

Na angalizo ni kwamba wao wanaamiliana na Mtume ﷺ kutoka nje ya duara, ambalo limeweka nafsi yake humo, kwa hiyo hakika uchambuzi wao unajengwa juu ya msingi huu, husuasan na wao wanatokana na hali ya kupuuza dini ya Masihi katika maisha yao, na kufuta dauru ya Masihi (as). Pamoja na kwamba sisi tunajiepusha – mara nyingi – kunukuu kauli zao kutokana na yaliyomo humo mion-

[28] Cha ajabu ni kwamba hadithi hizi katika *Sahih Muslim* zimekuja chini ya anwani ya, ambaye amelaaniwa na Nabii na hakuwa anastahiki! Angalia Juz. 4, uk. 2007, Mlango wa aliyelaaniwa na Mtume wakati hakustahiki kulaaniwa.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 36 11/23/2016 12:37:28 PM

goni mwa ujasiri walionao dhidi ya nafsi ya ujumbe na shakhisiya ya Mtume ﷺ ila sisi hapa tutalazimika kunukuu baadhi kwa ajili ya ushahidi juu ya kundi hilo lenye chuki, ambalo lilitaka kudhihirisha shakhisiya ya Mtume ﷺ ndani ya uzio duni wa kibinadamu. Kisha tunadhihirisha kutoka katika kauli hizi au baadhi yake athari ambayo wameiacha katika mtazamo wa baadhi ya Waislamu kutoka kwa watu wa kundi la kutweza katika yale yanayofungama na shakhsiya tukufu ya Mtume ﷺ.

Katika kitabu *al-Islamu Wal-Gharbi* tunasoma yafuatayo kuhusu kitabu na makasisi wa kikristo juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: Ananasibisha mtunzi kwa mwandishi Lail kauli yake: "Alikuwa anaishi Yathiriba (Madina) na Makkah, na sehemu zote ambazo ziko pembezoni mwake ni watu wanaoamini masanamu na wanaabudu jua, mwezi, wanyama na ndege, na hawakuwa na maarifa ya Mwenyezi Mungu wala hapakupatikana kwao mfalme! Wao ni watu wenye maarifa na ufahamu duni."

"Na uzao wa Muhammad ulikuwa ni wa kawaida, ambapo mwanzo alikuwa mpagani kama walivyokuwa Waarabu waliotangulia katika zama zake! Na aliishi kibedui baina ya mabedui na mpagani baina ya wapagani."

Kisha anaendelea: "Rasi ya Uarabu ilikuwa chini ya ulimwengu wa kikristo na ilikuwa kimbilio la amani na la kawaida la wazushi walioasi kanuni, na Uislamu ulianza kama kundi kutoka katika itikadi ya Ukristo, Uyahudi na Upagani!"

Mwandishi ananasibisha kwenye rejea Raybaro Bishow kauli yake: "Mwanamke anayeitwa Maria al-Qibtwiyyah alipelekwa kwa Muhammad, basi akamfanya ni kijakazi wake. Na ilitokea alikaa naye faragha katika nyumba ya mke wake Hafsa. Na aliporejea mke wa Muhammad akawaona, akakasirika na akamsogelea huku ak-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 37 11/23/2016 12:37:28 PM

isema: 'Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, je hapatikani baina ya wake zako mwanamke duni kuliko mimi? Kwa nini umekaa naye katika nyumba yangu?' Akamjibu akijaribu kumtuliza na kumridhisha: 'Je itakufurahisha kama nitajizuia naye?' Akajibu: 'Ndio.' Akaapa kwamba hatomwingilia Maria mara nyingine na akamwambia Hafsa: 'Usimwambie yeyote jambo hili.' Na baadaye akatengua kiapo chake na ahadi yake akarejea kwa Maria na kisha ikaja katika Qur'ani yake kuhusu hilo kwa maana yake: 'Waislamu wanapoapa kisha wakataka kukitengua kiapo, basi wanaweza kufanya hivyo kwa kutoa kafara baada ya hapo juu ya kosa lao bila ya kujilazimisha na kujifunga na kiapo chao.'"

Anasema mtunzi: "Mwandishi wa kilatini amejengea (Saan Peter) rai ya maadui wa Muhammad wa kileo na hiyo ni kwa kauli yake: 'Hakika kutengeneza wahyi kwa Nabii si kingine isipokuwa ni dalili ya kudhihirisha uongo katika fadhila na dini, au hakika shetani alijichanganya na shakhsiya ya Muhammad, na naitakidi kwamba Muhammad kumpenda Aisha sio kitendo kinachofaa kwa Nabii!'"

Na mtunzi anashiriki kumkosoa Muhammad katika maudhui ya kuwa na wake wengi, anasema: "Haiwezekani kutaja orodha ya majina ya wake wa Muhammad kwani ni wengi.." Na mtunzi Saan Peter anasema: "Kwa kutoa sababu ya wanawake kumpenda Muhammad: Muhammad alikuwa anavaa mapambo na kujifukiza manukato mazuri na hivyo harufu yake ilikuwa nzuri na alikuwa anatia rangi midomo yake na kupaka wanja wa macho yake. Na alikuwa anafanya kama wanavyofanya viongozi wa Kiislamu (viongozi waliofungua Hispania miongoni mwa Waislamu) leo. Na wafuasi wa Muhammad walipomkosoa Nabii kwa vitendo vyake hivi akawajibu kwamba yeye amepewa viburudisho vitatu katika dunia hii: 'Manukato, wanawake na swala.' Ni kiasi gani mambo haya yanaaibisha kwa mtazamo wa Wakristo."



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 38 11/23/2016 12:37:28 PM

Na mtunzi anasema: "Katika mtazamo wa kikristo wa karne za kati, hakika vitendo vya Muhammad pamoja na wanawake peke yake vinatosha kumfanya Muhammad kuwa sio Nabii."[29]

Kwa kiasi ambacho ufurutu ada unaleta hatari halisi kimsingi katika usafi wa itikadi na usalama wake, hakika kutweza pia kunaleta hatari nyingine ya kimsingi katika upande wa jamhuri na watu, bali huenda ikasemwa kutweza kuna athari zaidi, kwa sababu kunafanya kazi katika medani pana zaidi kwa watu, wakati kufurutu ada kunabaki kumezingirwa katika kundi dogo lililotengwa ambalo ni rahisi kudhibiti fikira yake na kukabiliana nayo kwa sababu inakhalifu mambo ya kawaida ya Waislamu. Hakika inafanana na gonjwa lililofichikana ambalo mtu halihisi wakati linateketeza mwili. Hii ni kwa kuongozea kuwa kwake karibu na nafsi, na linapendeza kwake, kwa kuwa linamlisha mwanadamu kwa hisia za ghururi na kwamba anafanana sana na Mitume na Mawasii عليهم السلام, na anaponyenyekea chini ya kibano cha nukta za udhaifu wake na kufanya dhambi, anakuta la kumliwaza – katika mtazamo huu –, kwamba hakika Mitume vilevile walinyenyekea katika nukta za udhaifu wao.

Na kwa hiyo tunaitakidi kwamba Uislamu katika ulimi wa Mtume ﷺ na Maimamu Maasumini عليهم السلام na hasa wao wanapokabiliana na hatari ya mtazamo wa kutweza wenye kuchupa mipaka, ulifanya mikakati mingi katika kukabiliana nayo. Na tutaeleza baadhi ya hadithi katika mapambano haya:

## Hadithi za Kuteuliwa:

Tangu mwanzo ilikuwa inatiliwa mkazo juu ya mas'ala ya utume na uimamu kuwa ni kati ya mas'ala ya ghaibu ambayo yanahusiana na uteuzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa watu ambao katika

[29] *Min Majalatu al-Fikir al-Arabiy*, Tolea la 32/April 1983.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 39 11/23/2016 12:37:28 PM

elimu Yake ni viumbe wanaofaa zaidi kwa nafasi hizi, kinyume na nadharia ambayo inasema kwamba ni kwa kuchaguliwa na watu.

Kutoka kwa Saidi bin Abdillahi al-Qummiy kutoka kwa al-Qaimu عليه السلام: "Niambie ewe kiongozi wangu juu ya sababu ambayo inazuia watu kumchagua imamu kwa ajili ya nafsi zao."

Akasema: "Mwema au muovu?" (Yaani wanachagua mwema au muovu)? Nikasema: "Bali mwema." Akasema: "Je, uchaguzi wao unaweza kuangukia kwa muovu baada ya kutojua yeyote yanayozunguka katika akili ya mwingine miongoni mwa wema na uovu?"

Nikasema: "Ndio." Akasema: "Hiyo ndio sababu ambayo nakueleza kwa hoja inayokuongoza akili yako." Kisha akasema: "Niambie juu ya mitume ambao Mwenyezi Mungu amewateua na akawateremshia vitabu, na akawaunga mkono kwa wahyi na umaasum, nao ndio vielelezo vya amani, wakipewa nafasi ya kuchagua, mfano Musa na Isa عليهما السلام, je inajuzu pamoja na akili zao na ukamilifu wa elimu yao, uchaguzi wao kuanguakia kwa mnafiki na wao wanadhani kuwa ni muumini?"

Nikasema: "Hapana." Akasema: "Huyu hapa Musa عليه السلام aliyesemeshwa sana na Mwenyezi Mungu, pamoja na kutimia akili yake na ukamilifu wa elimu yake na kuteremshiwa wahyi alichagua kati ya wakuu wa kaumu yake na viongozi wa maaskari wake kwa ajili ya makutano ya Mola Wake Mtukufu, watu sabini kati ya ambao hana shaka na imani yao na ikhlasi yao, basi mbora wao akawa ni kati ya wanafiki, amesema (swt): 'Na Musa alichagua watu sabini katika watu wake kwa ajili ya makutano yetu..' Hivyo tulipokuta uchaguzi wa ambaye ameteuliwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya unabaii umeangukia juu ya muovu zaidi kinyume cha mwema, naye anadhani kwamba ni mwema zaidi na si muovu, tukajua kwamba



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 40 11/23/2016 12:37:28 PM

uchaguzi haufai isipokuwa wa ambaye anajua yanayofichikana katika nyoyo."[30]

## Hadithi za Kupenda na Uongozi:

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema: "Hatoamini mmoja wenu hadi mimi niwe napendeza zaidi kwake kuliko nafsi yake, na Ahali zangu wanapendeza kwake zaidi kuliko ahali zake, na kizazi changu kinapendeza zaidi kwake kuliko kizazi chake."[31]

Kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام, amesema: "Tazameni Ahlul-Bayt wa Nabii wenu, shikamaneni na sifa zao na fuateni nyendo zao, hawatowatoa katika uongofu na hawatowarudisheni kwenye uovu, wakikaa kaeni na wakiamka amkeni."[32]Na amesema - akiwasifu Ahlul-Bayt:- "Hakika wao ni uhai wa elimu na ni mauti ya ujinga. Wao ndio watakaowaambia hekima yao katika kitendo chao na kunyamaza kwao katika mantiki yao, na dhahiri yao juu ya undani wao. Hawakhalifu dini wala hawahitalifiani humo, kwani baina yao kuna mshuhudiaji mkweli, na mkimya mwenye kutamka."[33]

## Kuimarisha Adabu Hususan Katika Uhusiano Pamoja na Mtume ﷺ na Ahlul-Bayt Wake:

Mwenye kufuatilia nususi za Kiislamu na sira ya Waislamu pamoja na Mtume ﷺ anaona kwamba kuna adabu maalumu zimekubaliwa na Qur'ani tukufu, kama ambavyo tunakuta hayo katika Sura al-Hujurat, mfano kutonyanyua sauti zenu kuliko sauti ya Nabii wala msiseme naye kwa makelele:

[30] *Mizanul-Hikma*, Juz. 1, uk. 190.
[31] Rejea iliyotangulia Juz. 2, uk. 236.
[32] Rejea iliyotangulia.
[33] Rejea iliyotangulia.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 41 11/23/2016 12:37:28 PM

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَنْ تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ

**"Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko ya sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi viisije vitendo vyenu vikaanguka na hali hamtambui." (al-Hujurat; 49:2)**

Na chini ya vitisho vya kuanguka vitendo inakataza juu ya hilo, na inawakanya wale wasio na akili kati ya wanaomwita nyuma ya vyumba. Kisha inakataza kumbana Mtume ﷺ na kumfanya achukue misimamo asiyoitaka, kwa sababu katika hilo kuna adha kwa jamii: "Na jueini kwamba miongoni mwenu yupo Mtume kama atawatii katika mengi kati ya mambo mngepata taabu."

Na ilikuwa sira ya Waislamu wa kwanza, ambao walijua heshima ya Mtume ﷺ imesimama katika heshima kamili na heshima kubwa kwa Mtume ﷺ na Ahlul-Bayt wake, historia inanukuu sura hii kwetu juu ya upeo wa kushikamana kwao na mapenzi yao kwa Mtume ﷺ. Katika habari moja kutoka kwa Usama bin Shariki amesema: "Nilimwendea Nabii ﷺ na masahaba wake wako pembezoni kana kwamba ndege ametua juu ya vichwa vyao (yaani wamekaa kimya)."

Amesema Urwat bin Mas'ud pindi Makuraishi walipomtuma kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na akaona masahaba wake wanavyomheshimu, na kwamba hatawadhi isipokuwa wanagombania maji ya udhu wake yanayodondoka na wanakaribia kukanyagana, na hauanguki unywele isipokuwa wanaugombania, na anapowaamuru jambo wanatekeleza amri yake, na wanapozungumza sauti zao zinateremka chini, wala hawamkazii macho kwa kumheshimu kwao. Aliporejea kwa Makuraishi alisema: "Enyi Makuraishi hakika mimi nilimwendea Kisra katika ufalme wake,



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 42 11/23/2016 12:37:28 PM

Qaisari katika ufalme wake na Najashi katika ufalme wake. Wallahi hakika mimi sijaona katu mfalme katika kaumu, mfano wa Muhammad kwa masahaba wake."

Na kutoka kwa Anas amesema: "Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kinyozi anamnyoa na masahaba wake wamemzunguka na hawataki nywele zake zidondoke isipokuwa katika mkono wa mtu."[34] Na kutia nguvu upande huu, kumswalia Mtume ilikuwa ni sehemu ya swala za kila siku kwa Waislamu wote. Na katika hilo anaashiria Imamu Shafi'i ؓ katika mashairi yanayonasibishwa kwake:

**"Enyi Ahlul-Bayt wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kuwapenda kwenu, ni faradhi ya Mwenyezi Mungu ameiteremsha katika Qur'ani. Inatosha kwenu kuwa ni utukufu, kwamba asiyewaswalia nyinyi hana swala."**

Na kwa sababu hii ilipoteremka Aya ya kumswalia Nabii:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ ۚ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

**"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika Wake wanamswalia Nabii. Enyi ambao mmeamini mswalieni na mumsalimu kwa salamu."[35]** Waislamu walifahamu kwayo kuwa ni amri ya kisharia, hivyo wakamjia na kuuliza maana yake. Kaab bin Ajrah anapokea kwamba: "Ilipoteremka Aya hii tulisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tumekwishajua namna ya kukusalimia, ni namna gani tutakuswalia? Akasema ﷺ: 'Semeni: *Allahumma swali Alaa Muhammad wa Aali Muhammad kama Swalaita Alaa Ibrahim wa Aali Ibrahim Innaka Hamiydu Majiydu, Wabariki Alaa Muhammad wa Aali*

[34] *Biharul-An'war*, Juz. 17, uk. 32.
[35] Suratul-Ahzab: 56.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 43 11/23/2016 12:37:28 PM

*Muhammad kama Baarakta Alaa Ibrahim wa Aali Ibrahim Innaka Hamiydu Majiydu*.”’[36]

**Mkazo Juu ya Mas’ala ya Umaasumu:**

Wafuasi wa Ahlul-Bayt عليهم السلام wanaona kwamba Manabii عليهم السلام wamehifadhiwa kutokana na madhambi madogo na makubwa, na wametakaswa kutokana na maasi kabla ya utume na baada yake. Hawatendi maasi kwa makusudi wala kwa kusahau. Na wamehifadhiwa kutokana na kila ovu na upungufu, na kila ambalo linaashiria kasoro na udhaifu. Na hali ni hiyo hiyo kuhusiana na umaasumu wa Maimamu عليهم السلام kwa namna ile ile ya umaasumu wa Mtume, na ni vilevile ukamilifu wao. “Hakika hakuna shaka katika ukamilifu wao katika hali zote ambazo humo walikuwa ni hoja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika viumbe vyake.”

Amesema Sheikh al-Mufid (r.m): “Umaasumu utokao kwa Mwenyezi Mungu kwa Hujja Wake ni taufiki, huruma na kinga ya kuwazuia Hujja dhidi ya madhambi na kukosea katika dini ya Mwenyezi Mungu. Na umaasumu ni fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ambaye amejua kuwa anashikamana na umaasumu wake, na mshikamano ni kitendo cha mwenye kukingwa, na umaasumu hauzuii uwezo wa kufanya mabaya, wala si wenye kumlazimisha maasumu bila hiyari kufanya mema. Na wala sio kimbilio lake, bali ni kitu ambacho Mwenyezi Mungu anajua kwamba iwapo atamfanyia mja kati ya waja Wake, basi maasi hayatomwathiri mja huyo.

Na jambo hili halijulikani kutoka katika hali ya kila kiumbe, bali hujulikana kutoka kwao hao ambao ni wabora na wateule. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ‘Hakika wale ambao umetangulia wema kutoka kwetu’ (Sura al- Ambiyai: 101). Na amesema: ‘Na hakika tuliwachagua kwa ujuzi kuliko walimwengu wengine.’ Na amesema:

[36] *Biharul-An’war*, Juz. 17, uk. 19.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 44 11/23/2016 12:37:29 PM

'Hakika wao kwetu Sisi ni wateule walio bora' (Sura Swad: 47). Na Manabii na Maimamu عليهم السلام baada yao ni maasumu katika hali za utume wao na Uimamu wao kutokana na madhambi makubwa yote na madogo. Na kiakili inajuzu kwao kuacha mustahabu bila ya kukusudia kwa uzembe na uasi, na haijuzu kwao kuacha faradhi kwa sababu Nabii wetu صلى الله عليه وآله وسلم na Maimamu baada yake walikuwa wamesalimika kutokana na kuacha Sunnah na faradhi kabla ya uimamu wao na baada yake."[37]

## HITIMISHO:

Baada ya kufanya mzunguko huu katika makundi mawili yaliyokosea, yenye kuchupa mpaka na baada ya kuashiria katika kasoro zake wakati wa kuyazungumzia, sasa tunaweza kufaidika na hitimisho lifuatalo katika muhtasari wa utafiti:

### 1. Si Ruhusa Kuhalalisha Ufurutu Ada kwa Sababu tu Upande Mwingine Umefurutu Ada:

Hakika moja ya makosa ambayo humo zimetumbukia pande mbili katika kutazama shakhsiya za Manabii na Mawasii عليهم السلام, ni kuwa na mtazamo wa kulipiza kisasi dhidi ya upande mwingine. Na huenda hili ni kosa na bado lingali linaendelea katika yale wanayoyafanya baadhi wenye kukosea katika kufurutu ada katika shakhsiya hii au ile, kwa mtazamo wa dhana yao kwamba imedhulumiwa na haikupewa haki yake kama inavyopasa. Hivyo wanalipiza kisasi kwa dhulma hiyo, kwa kuongeza sifa za kuzidisha na kuchupa mpaka.

Mfano unapoona kwamba Maimamu عليهم السلام wakati wa maisha yao walikuwa wanakabiliwa na aina mbalimbali za machungu na adha kutoka kwa watawala hadi maisha yao yamemalizikia kwa kuuliwa

[37] *Taswihihu al-Itiqad* cha Sheikh al-Mufid, uk. 106.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 45 11/23/2016 12:37:29 PM

na kupewa sumu, baadhi ya wafuasi wanakuja baadaye na wanafanya – kwa madai yao – kulipiza dhulma hii kwa kuwaheshimu na kuwatukuza, na wanawaongezea sifa hizo. Wakati ambapo ilikuwa ni jambo la kawaida kulingana na kanuni ya kihistoria, ambapo warekebishaji na watu wema hawapokelewi kwa maua na manukato bali kwa taabu na kibano katika kazi yao ya kurekebisha hadi wafikie kwenye malengo yao makuu.

Ambapo Mwenyezi Mungu kama angetaka kwa Manabii Wake alipowatuma kuwafungulia hazina ya dhahabu, madini ya thamani na miti ya peponi, na kuwakusanyia ndege wa mbinguni na wanyama wa ardhini angefanya hivyo. Na kama angefanya hivyo basi mtihani ungeondoka, malipo yangebatilika na habari zingemalizika na isingekuwa ni wajibu kwa watahini ujira wa mtahiniwa, na waumini wasingestahiki malipo ya wema na wala majina yasingelazimiana na maana zake. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia Mitume Wake عليهم السلام kuwa ni wenye nguvu katika azima zao na akadhoofisha ambayo macho yanayaona miongoni mwa hali zao pamoja na kutosheka kunakojaza nyoyo na macho kukinai, hususan kunajaza macho na masikio adhaa.

Na kama Manabii عليهم السلام wangekuwa ni wenye nguvu zisizoshindwa, na uwezo usiowezekana, na ufalme wenye kutanuka unaotamaniwa na watu, na kwao wanafunga safari kuuendea, hilo lingekuwa ni jepesi zaidi kwa viumbe katika mazingatio na lingewaondolea wao kiburi na wangesalimika na kitisho chenye kuwakandamiza au raghba yenye kuwaelemea, basi nia zingekuwa ni zenye kushirikiana na mema yangekuwa ni yenye kugawanwa. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka kufuata Mitume Wake عليهم السلام na kusadikisha vitabu Vyake na kunyenyekea kwa ajili Yake, na kutii amri Zake na kujisalimisha katika twaa Yake, yawe ni mambo maalumu yasiyokuwa na mkanganyiko wowote. Na kila mtihani na



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 46 11/23/2016 12:37:29 PM

balaa unapokuwa mzito zaidi malipo na thawabu zinakuwa nyingi zaidi.[38]

Kama anavyosema Amirul-Mu'minin عليه السلام: "Isipokuwa hawa kutofahamu desturi hii imewapelekea wao kwenye mwelekeo huo wa kufurutu ada na kupetuka."

Na katika upande mwingine kulikuwa na kupetuka kwingine ambako kulichukua sura ya ghadhabu wakati mwingine, na kisasi kwa mara nyingine. Ambapo kutukuza huko na kupetuka kumepelekea kupinga na kuzembea katika upande huu hivyo wakaharibu ambapo walitaka kutengeneza, huku wakisahau kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na wala kusiwazuie uovu wa watu kufanya uadilifu, fanyeni uadilifu kwani hilo liko karibu zaidi na uchamungu." Vivyo hivyo kama walivyopata hasara Mayahudi kwa kosa la kumfanyia uadui Masihi kwa chuki kutoka kwao kwa kutukuzwa Masihi juu yao. Hapa jambo limejirudia, wamepatikana baina ya Waislamu wenye kuwadharau Manabii عليهم السلام na hususan wa mwisho wao Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم na Ahlul-Bayt wake عليهم السلام baada yake, na tumeshatangulia kunukuu maneno ya baadhi yao.

Hakika sisi kama tunavyoshutumu uchupaji mipaka wa wafurutu ada, na tunaitakidi kuwa ni njia ya kimakosa hasa ukizingatia kwamba inawatoa watu katika uwezekano wa kufuata shakhsiya hii ambayo imeletwa ili kumwendeleza mwanadamu, vilevile tunashutumu uchupaji mipaka wa kutweza, wa kupinga fadhila na daraja maalum kwake, na tunaitakidi kwamba ni njia ya kimakosa, kwa sababu inaiondoa shakhsiya hii katika daraja na nafasi ya kuwa kigezo chema.

Hakika njia ya kati baina ya njia mbili hizi za uchupaji mipaka ndio tunayoichagua, ambapo sisi wakati tunapoitakidi kwamba

[38] *Nahjul-Balaghah*, Hotuba ya 192.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 47 11/23/2016 12:37:29 PM

Manabii na Mawasii ni binadamu na ni watu kama sisi katika upande wa kimaumbile ya kimwili, ila ni kwamba wao wanataofautiana na sisi katika ukubwa wa majukumu yao na katika kiwango cha sifa zao na katika mawasiliano yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## 2. Kutenganisha Baina ya Aina Mbili Katika Maisha ya Maasumini عليهم السلام:

Hakika sisi tunaitakidi kwamba riwaya ambazo zinazungumzia maisha ya Maasumini عليهم السلام inapasa kuzigawanya katika aina mbili kufuatana na kwamba maisha yao yanagawanyika katika sehemu mbili:

**Sehemu ya kwanza:** Maisha yanayofungamana na mambo ya kidini, kwa yale anayoyafanya maasum katika dauru ya tablighi katika dini ya Mwenyezi Mungu, kwa kuwa kwake ni mfikishaji wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu katika jamii hii, na katika maisha haya inakuwa ni Sunnah ya maasum, na hivyo kauli zao, vitendo vyao na kukubali kwao ni hoja kamili, kwa sababu katika maisha haya anaamiliana katika msingi wa sifa yake ambayo amepewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na jamii inaangalia katika vitendo vyake na kuvitathimini ndani ya lengo hili, naye katika maisha haya anaamiliana ndani ya uzio wa umaasumu, hivyo kila neno kutoka kwake linazingatiwa kuwa ni sharia au ni mwongozo katika sharia.

Inadhihirika kwamba Waislamu walifahamu uwiano huu - aghlabu – na hivyo walikuwa wananukuu sira ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم na wanaizingatia kwa mazingatio makubwa, na wafuasi wa Ahlul-Bayt عليهم السلام wamekuwa mahususi katika kufuatilia sira ya Maimamu, ukiongezea na sira ya Mtume kwa kuzingatia kwao kwamba sira hii inatengeneza msisitizo wa kujua mengi kati ya hukumu za Mwenyezi Mungu katika maisha na dini.

**Sehemu ya pili:** Ambayo yanafungamana na mambo binafsi yanayohusiana na Maasumini عليهم السلام kwa kuzingatia kuwa wao ni bin-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 48 11/23/2016 12:37:29 PM

adamu, wanaishi ndani ya mkusanyiko wa watu, ukiongezea katika kuwa kwao wanyenyekevu katika matakwa yake na mahitaji yake ambayo yanahusiana na mambo binafsi. Licha ya kwamba sisi hatupati katika Hadithi kitenganishi hiki kwa uwazi, ila ni kawaida kila sehemu katika maisha kuhitajia jambo hili. Na katika aina ya pili sisi hatulazimiki kwa ulazima kupitisha kanuni ya umaasumu, wala haiangukii pia kwa katika duara la sharia. Kwa mfano yale ambayo yanahusiana na chakula, maasum kupendelea chakula hiki au kile, na kula kwake aina hii au ile haiingii kwa dharura ndani ya duara la hukumu za ulazima au za kuhitajia, bali inaweza kuingia ndani ya duara la mambo binafsi na utashi halali.

Hakika ufahamu huu halisi wa maisha ya Maasumini, unaziba njia baina ya njia ya kufurutu ada na kutweza, wakati huo huo unaweka mguu wa mtafiti katika njia ya muamala sahihi pamoja na sira hii. Hakika sisi tunapoitakidi kwamba Maasumini عليهم السلام ni binadamu na kwamba Mtume ﷺ ni binadamu kama nyinyi, anateremshiwa wahyi, hakika hii inamaanisha kwamba yeye atathibitisha ukweli huu kwa vitendo vyake vya kibinadamu, na sehemu ya vitendo hivyo inaingia katika uzio wa maelekezo katika hukumu ya kisharia, wakati ambapo sehemu nyingine haielekei katika mwelekeo huu, bali inatekeleza haja maalum kwa Nabii ﷺ.

Na inapasa isifahamike kwamba kuna utengenisho na mgongano baina ya sehemu mbili, bali uhusiano, ni uhusiano wa kushirikiana na kukamilishana. Lakini tunapinga katika sehemu ya pili dharura ya kuwa ni sharia, inaweza kuwa na inaweza isiwe, lakini haitoki katika uzio wa shakhsiya iliyokamilika ambayo anaiwakilisha Maasum, hivyo haiwezekani kufaradhisha katika sehemu hii kuwepo kitendo au shughuli zinazokiuka misingi mikuu ya shakhsiya ya Maasum عليه السلام.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 49 11/23/2016 12:37:29 PM

## 3. Kutafuta Utukufu wa Maasumina عليهم السلام Katika Sifa Zao na Majukumu yao:

Mwenye kufuatilia matamko ya Hadithi na riwaya zilizopokelewa kuhusu Ahlul-Bayt عليهم السلام anaona kwamba riwaya hizo hazidhihirishi juu ya sifa ya nje, bali zinaainisha sifa za kitabia na zinabainisha maneno ya jukumu la msingi ambalo walikuwa wanalifanya.

Na kuna tofauti kubwa baina ya maneno ya jukumu la kidini, kijamii na kisiasa, na maneno ya mtu na hali zake za pembezoni zinazohusiana naye kama mtu binafsi, wakati ambapo unatokea mjadala na unakuwa mkali baina ya makundi mawili: La wafurutu ada na wenye kutweza, kuhusu mambo ya mtu. Je, anaingia chooni kama sisi? Au je, damu yake ni ya bluu au nyekundu? Je, damu hii ni twahara au ni najisi? Je, sehemu yake ya kibinadamu ni kubwa zaidi au ya kiungu? Hadi mwisho wa orodha ya mjadala unaozunguka. Na hatimaye unasahauliwa upande muhimu zaidi na ambao unawataka watu kumfuata, ambao ni sifa za nafsi yake na jukumu lake.

Na tusome moja ya mifano hii ambayo inazungumzia juu ya sifa za jukumu walilonalo Maasumini عليهم السلام, mfano unapokewa kutoka kwa Imamu Ali al-Hadi عليه السلام, nao unapata umuhimu wa kipekee, na tunaweza kuona kwamba kutokea kwake ilikuwa ni kutoka kwa Imamu Ali al-Hadi ambaye alipata mtihani katika siku za uimamu wake, wa wafurutu ada, ambapo walipanua shughuli zao na kuwa kubwa, na kwa hiyo kulikuwa na haja ya tamko la wazi katika yanayohusiana na sifa halisi walizonazo Ahlul-Bayt عليهم السلام mbali na ufurutu ada na kutweza.

Na tutaona ushahidi kupitia baadhi ya vipengele vyake, na hatutovitaja vyote kutokana na urefu wake, na kutofahamika baadhi ya vipengele vyake kwa kuhitajia kwake kufafanuliwa na kufasiriwa, jambo ambalo litatutoa katika asili ya utafiti. Pengine tutaweza ku-

pata taufiki kuliangalia na kufafanua katika wakati ujao juu ya tamko hili linaloitwa *Ziyaratul-Jamiah*:

اَلسَّلامُ عَلَيْكُمْ يا اَهْلَ بَيْتِ النُّبُوَّةِ، وَمَوْضِعَ الرِّسالَةِ، وَمُخْتَلَفَ الْمَلائِكَةِ، وَمَهْبِطَ الْوَحْيِ، وَمَعْدِنَ الرَّحْمَةِ، وَخُزّانَ الْعِلْمِ، وَمُنْتَهَى الْحِلْمِ، وَاُصُولَ الْكَرَمِ، وَقادَةَ الامَمِ، وَاَوْلِياءَ النِّعَمِ، وَعَناصِرَ الابْرارِ، وَدَعائِمَ الاخْيارِ، وَساسَةَ الْعِبادِ، وَاَرْكانَ الْبِلادِ، وَاَبْوابَ الأيْمانِ، وَاُمَناءَ الرَّحْمنِ، وَسُلالَةَ النَّبِيّينَ، وَصَفْوَةَ الْمُرْسَلينَ، وَعِتْرَةَ خِيَرَةِ رَبِّ الْعالَمينَ

**"Asalamu alaykumu ya Ahlul-Bayt nubuwati wa maudhi'i risaalati wa mukhitalafil-malaaikati wamahbatwi al-wahayi wama'adin rahamati wa khuzaanil-i'limi wa muntahal-hulumi wa usulil-karami wa qaadatil-umami wa auliyaai ni'ami wa a'anaaswir al-abraari wa da'aimi al-khiyaari wa saasatil-ibaadi wa arkaanil-bilaadi wa abuwabil-imaani waabnaai rahamaan wa salaalatu nabiyyiina wa swafuwatu al-mursaliina wa itiratu khirati rabil-alamiina."**

**"Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya unabii, maweko ya ujumbe, mapishano ya Malaika, mashukio ya Wahyi, makazi ya rehema, hazina ya elimu, kilele cha upole, misingi ya heshima, viongozi wa mataifa, mawalii wa neema, nguzo na mihimili ya watu wema, viongozi wa waja, nguzo za nchi, milango ya imani, waaminifu kwa Rahmani, asili ya Manabii, wateule wa Mitume, kizazi cha chaguo bora la Mola wa walimwengu."**

Hakika sisi katika tamko hili tunakuta baada ya kuwaainishia watu sehemu ya uhusiano na kuwa kwao Ahlul-Bayt wa Mtume na sehemu ya ujumbe, tunakutana na baadhi ya maneno, ambayo namuomba msomaji mpendwa ayatafakari. Hakika sisi tuko mbele ya "viongozi" na "mawalii" na "nguzo" na "misingi" na "mihimili" na "waaminifu", vivyo hivyo tamko linaendelea katika sifa hizi "Maim-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 51 11/23/2016 12:37:29 PM

amu" na "taa" na "wajuzi" na "vigezo" na "ulingano" na "Hoja" na "wahifadhi" na "wabeba kitabu."

اَلسَّلامُ عَلى اَئِمَّةِ الْهُدى، وَمَصابيحِ الدُّجى، وَاَعْلامِ التُّقى، وَذَوِى النُّهى، وَاُولِى الْحِجى، وَكَهْفِ الْوَرى، وَوَرَثَةِ الانْبِياءِ، وَالْمَثَلِ الاعْلى، وَالدَّعْوَةِ الْحُسْنى، وَحُجَجِ اللهِ عَلى اَهْلِ الدُّنْيا وَالآخِرَةِ وَالاولى وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكاتُهُ، اَلسَّلامُ عَلى مَحالِّ مَعْرِفَةِ اللهِ، وَمَساكِنِ بَرَكَةِ اللهِ، وَمَعادِنِ حِكْمَةِ اللهِ، وَحَفَظَةِ سِرِّ اللهِ، وَحَمَلَةِ كِتابِ اللهِ، وَاَوْصِياءِ نَبِيِّ اللهِ، وَذُرِّيَّةِ رَسُولِ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكاتُهُ

**"Amani iwe juu ya viongozi wa uongofu na taa katika giza, na vielelezo vya uchamumgu, na wenye akili na wenye hoja, na ngome ya kujinyima, na warithi wa Manabii na kigezo cha hali ya juu, na ulingano mwema, na Hujja wa Mwenyezi Mungu kwa watu wa duniani na akhera, na rehema na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao. Amani iwe juu ya sehemu za kumjua Mwenyezi Mungu, na makazi ya baraka za Mwenyezi Mungu, na chimbuko la hekima ya Mwenyezi Mungu, na wahifadhi wa siri ya Mwenyezi Mungu, na wabeba Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na Mawasii wa Nabii wa Mwenyezi Mungu na kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ"**

Kisha naatazame msomaji mtukufu katika umakini wa maneno, ambapo hakika hawa uwepo wao haupo isipokuwa katika kuwazingatia kuwa wao ni waja na watumishi na walinganiaji kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na haiwezekani wakawekwa katika nafasi ya waungu kama wanavyofanya wafurutu ada. Hakika wao wanamtii Mwenyezi Mungu, na ni wasimamizi wa amri Zake na ni watekelezaji, lakini kwa matakwa Yake. Ila tamko linaendelea. Kama ambavyo linapinga kundi la wafurutu ada, hakika pia linapinga kundi la kutweza. Kipengele kinakamilisha ubainifu huo sehemu za



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 52 11/23/2016 12:37:29 PM

uteuzi wa Mwenyezi Mungu kwao, wao ni waja na ni watiifu, lakini wakati uleule "amewateua" kwa elimu Yake na "amewaridhia" katika ghaibu Yake na "amewateua" kwa ajili ya siri Yake na "amewachagua" kwa uwezo Wake.

اَلسَّلامُ عَلَى الدُّعاةِ اِلَى اللهِ، وَالادِلاّءِ عَلى مَرْضاة اللهِ، وَالْمُسْتَقِرّينَ فى اَمْرِ اللهِ، وَالتّامّينَ فى مَحَبَّةِ اللهِ، وَالمخْلِصينَ فـى تَوْحيدِ اللهِ، وَالْمُظْهِرينَ لاِمْرِ اللهِ وَنَهْيِهِ، وَعِبادِهِ الْمُكْرَمينَ

**"Amani iwe juu ya walinganiaji kwa Mwenyezi Mungu na waelekezaji katika radhi za Mwenyezi Mungu, na wenye kutulizana katika amri ya Mwenyezi Mungu na usalama katika mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na wenye ikhlas katika tauhidi ya Mwenyezi Mungu, na wenye kudhihirisha amri ya Mwenyezi Mungu na katazo lake na ni waja wake wenye kukirimiwa."**

وَاَشْهَدُ اَنَّكُمُ الائِمَّةُ الرّاشِدُونَ الْـمَهْدِيُّونَ الْمَعْصُومُونَ الْمُكَرَّمُونَ الْمُقَرَّبُونَ الْمُتَّقُونَ الصّادِقُونَ الْمُصْطَفَوْنَ الْمُطيعُونَ للهِ، الْقَوّامُونَ بِاَمْرِهِ، الْعامِلُونَ بِارادَتِهِ، الْفائِزُونَ بِكَرامَتِهِ، اصْطَفاكُمْ بِعِلْمِهِ، وَارْتَضاكُمْ لِغَيْبِهِ، وَاخْتارَكُمْ لِسِرِّهِ، وَاجْتَباكُمْ بِقُدْرَتِهِ، وَاَعَزَّكُمْ بِهُداهُ، وَخَصَّكُمْ بِبُرْهانِهِ، وَانْتَجَبَكُمْ لِنُورِهِ،

**"Na nashuhudia kwamba nyinyi ni maimamu, wenye kumtii Mwenyezi Mungu, wenye kusimamia amri Yake wenye kutenda kwa matakwa yake wenye kufaulu kwa karama zake amewateua kwa elimu yake na amewaridhia katika ghaibu yake na amewachagua kwa siri yake na amewateua kwa uwezo wake na amewatukuza kwa uongofu wake na amewafanya mahususi kwa huja zake na amewateu kwa nuru yake."**

Isipokuwa uteuzi huu na uchaguzi huu haukumalizikia kwenye ghururi au kupinga, bali baada ya yote hayo wameufanya kuwa ni njia ya uchamungu na kumtukuza Muumba:

فَعَظَّمْتُمْ جَلالَهُ، وَاَكْبَرْتُمْ شَأْنَهُ، وَمَجَّدْتُمْ كَرَمَهُ، وَاَدَمْتُمْ ذِكْرَهُ، وَوَكَّدْتُمْ ميثاقَهُ،
وَاَحْكَمْتُمْ عَقْدَ طاعَتِهِ، وَنَصَحْتُمْ لَهُ فِى السِّرِّ وَالْعَلانِيَةِ، وَدَعَوْتُمْ اِلى سَبيلِهِ
بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ، وَبَذَلْتُمْ اَنْفُسَكُمْ فى مَرْضاتِهِ، وَصَبَرْتُمْ عَلى ما
اَصابَكُمْ فى جَنْبِهِ، وَاَقَمْتُمُ الصَّلاةَ، وَآتَيْتُمُ الزَّكاةَ، وَاَمَرْتُمْ بِالْمَعْرُوفِ، وَنَهَيْتُمْ
عَنِ الْمُنْكَر

**"Mkatukuza uungu Wake na mkakuza jambo Lake na mkaheshimu ukarimu Wake, na mkadumisha utajo Wake, na mkatilia mkazo ahadi Yake, na mkaimarisha mafungamano ya utii Wake, na mkatoa nasaha kwa ajili Yake kwa siri na kwa dhahiri, na mkalingania katika njia Yake kwa mawaidha mazuri na mkajitolea nafsi zenu katika radhi Zake, na mkasubiri katika yaliyowasibu katika upande Wake, na mkasimamisha Swala na mkatoa Zaka na mkaamrisha mema na mkakataza maovu."[39]**

[39] *Mafatihul-Jinan* cha Sheikh Abbasi al-Qummiy.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 54 11/23/2016 12:37:29 PM

# SEHEMU YA PILI:

## MIGONGO SAFI NA VIZAZI VILIVYOTWAHARISHWA

Wakati wa kuzungumzia maisha ya mtu, hususani ya ndoa inatusimamisha anwani pana nayo ni "migongo safi na vizazi vilivyotoharishwa."

Hiyo ni kwa sababu sisi tunaitakidi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anachukia uchafu kwa waja Wake waongofu na viongozi, hivyo amewateua na amewachagua hawa tangu zamani, na amehukumu hawa wawe katika kizazi chema, na wakue katika familia njema. Na kwa kuangalia umuhimu wa maudhui, tunaeleza maneno humo kupitia nukta zifuatazo:

Kutokana na jukumu ambalo linawasubiri Manabii na Mawasii عليهم السلام katika kuongoza binadamu, na kuwaelekeza kwenye ibada ya Mwenyezi Mungu, jukumu hilo kubwa ambalo linabeba lengo la kuumbwa viumbe, majini na wanadamu: "Sijaumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu," hakika watu wenye kipaji cha kusimamia jukumu hili ni lazima wawe ni katika aina maalumu. Wanaumbwa na wanatengenezwa[40] chini ya uangalizi wa Mwenyezi Mungu. Na hii inamaanisha kwamba wao wanateuliwa tangu mwanzo kutoka katika familia bora na wanachaguliwa kutoka vizazi bora kati ya vizazi vya binadamu, ambapo hawabebi katika nafsi zao uchafu bali walitumwa kuwatakasa wanadamu.

[40] Katika kisa cha Nabii Musa عليه السلام: **"Na nimekutilia mapenzi kutoka Kwangu na ili ulelewe machoni Mwangu." (Surat-Twaha; 20:39).**



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 55 11/23/2016 12:37:29 PM

Hapa tunakuta kazi inatimia ndani ya uzio wa uteuzi ambapo haitokei ghafla au kwa mchezo tu, bali uteuzi wa Muumba unafanyika ili isiingie humo raghaba ya huyu Nabii au kutopenda kwake kuwa hivyo. Na wala uchaguzi wa watu na ridhaa yao kwake usiwe na nafasi ndani ya uchaguzi wa kidemokrasia.

Hakika kazi hii ya ghaibu na ni ya jumla na ni ya kiungu kabisa, na vyovyote mwanadamu atakavyojaribu kuifasiri hakika wao hawatofikia isipokuwa kwenye maana ya nje tu. Na kwa hiyo tunakuta katika Qur'ani tukufu kitendo chote cha uteuzi ni cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, wakati ambapo Manabii wanasimama katika msimamo wa utekelezaji wa jumla:

إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

**"Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adamu na Nuhu na watoto wa Ibrahimu na watoto wa Imrani juu ya walimwengu wote. Ni kizazi cha wao kwa wao na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua." (al-Imraan; 3:33-34).**

Na kwa sababu uwiano huu ni wa ghaibu na ni wa kiungu, na wala hauingiliwi na vipimo vya kibinadamu ambavyo tunavizoea, kwa hiyo hakika Mwenyezi Mungu kuna wakati anamchagua na kumteua mtu, na mara nyingine anamchagua mwanamke, pamoja na kwamba mantiki ya kibinadamu ya kawaida haitegemei hilo: **"Akasema: Mola Wangu! hakika mimi nimezaa mtoto wa kike."** Isipokuwa Qur'ani inasema:

وَإِذْ قَالَتِ الْمَلَائِكَةُ يَا مَرْيَمُ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاكِ وَطَهَّرَكِ وَاصْطَفَاكِ عَلَىٰ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 56 11/23/2016 12:37:29 PM

**"Na Malaika waliposema: Ewe Mariam! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteua na akakutakasa na akakuteuwa juu ya wanawake wa ulimwenguni." (al-Imraan; 3:42).**

Na huenda sababu ya uteuzi huu ambao umekuja kwa kukaririwa katika Aya ni kwa kuwa Mariamu atambeba mmoja wa Manabii watukufu wa Mwenyezi Mungu, naye ni Isa bin Mariyamu عليه السلام.

Bali wakati watu wanapopinga uteuzi wa mtu fulani, hoja ya mwisho kwa waumini inakuwa: **"Hakika Mwenyezi Mungu amemteua juu yenu."** Ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu ndio Mwenye kheri na wala hawezi mwingine asiyekuwa Yeye:

**"Na Mola Wako huumba na huteua atakavyo; hawana hiyari. Mwenyezi Mungu ametakasika na hao wanaowashirikisha Naye." (al-Qasas; 28:68).**[41]

Uteuzi huu maalumu katika jukumu kubwa unafanya ulazima wa kuendelea uangalizi na huruma ya kiungu kuhusu jambo la mtu mteule tangu mwanzo, kuanzia hatua ya awali katika mlolongo mrefu ambao atatengenezeka humo, hiyo ni kwa sababu sisi tunaitakidi kwamba huyu mteule mwokozi ni wajibu awe ni mkamilifu na mbora katika zama zake katika baadhi ya mambo, na katika mambo yote kwa Nabii wetu Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم.

Na kwa kuangalia kwamba kurithiana kuna mchango muhimu katika kizazi hiki kupata hatua zinazofuata kutoka kwenye sifa za hatua iliyotangulia (baba, na mababu) kwa hiyo ni lazima kila mlolongo wa unabii uwe safi ili abebe mtoto huyu – ambaye atakuwa nabii mwenye kutumwa au Imamu kiongozi – sifa safi, vinginevyo hakika wewe hutosalimika na mwiba wa mzabibu!

[41] Suratul-Qasas; 28:68, na kwa kujengea tafsiri ya Aya hii imepokewa kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Mwenyezi Mungu Mtukufu anawachagulia Imamu na wao hawana haki ya kuchagua." Kutoka katika *Nuru Thaqalain,* Juz. 4.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 57 11/23/2016 12:37:29 PM

Hakika wataalamu wa urithi wa tabia wanakubali kwamba mwanadamu anaathiriwa kwa kiasi fulani na watangulizi wake, sawa iwe katika utengenezaji wake wa kimwili na umbo lake la nje au katika matamanio yake ya kinafsi na sifa zake za kitabia: "Mwanadamu katika wakati ni kama anavyoendelea katika faragha mpaka baada ya mipaka ya mwili wake, na mipaka yake ya wakati haina umakini sana wala si thabiti kuliko mipaka yake ya upanuzi. Yeye anafungamana na yaliyopita na yajayo pamoja na kwamba dhati yake haiendelei nje ya wakati uliopo. Na unakuja upekee wetu kama tunavyojua kwenye uwepo wakati mimba inapotunga katika yai. Lakini chembechembe zake zinakuwepo kabla ya muda huu, na zinatapakaa katika mishipa ya baba zetu na babu zetu na watangulizi wetu wa mbali sana.

Kwa sababu sisi tumetengenezwa kutokana na chembechembe za baba zetu na mama zetu, chembechembe zinategemea yaliyopita katika hali ya kiungo kisichomalizika, na tunabeba ndani ya nafsi zetu chembechembe ndogo zisizohesabika kutoka katika miili ya watangulizi wetu, na sifa zetu na upungufu wetu  si kingine ila ni mwendelezo wa upungufu wao na sifa zao.

Hakika msingi wa kuumba umbo la mwanadamu ni mas'ala ambayo yanatawaliwa na kutofahamika, ambapo sisi hatujui namna gani zimekusanywa chembechembe za wazazi wake, baba zake na babu wa babu zake katika mayai ambayo humo ametokana nayo, kama ambavyo hatujui chochote ikiwa  chembechembe fulani kutoka kwa mmoja wa watangulizi walio mbali waliosahaulika hazimo humo, au ikiwa mabadiliko ya hiyari katika chembechembe yanaweza yasisababishe kudhihirika kwa baadhi ya sifa bila kutarajia, kwani inaweza kutokea wakati mwingine  mmoja wa watoto ambao imejulikana kuelemea kwa watangulizi wake kwa vizazi vingi akaanza kuonesha mwelekeo mpya usiotarajiwa.[42]

[42] A*l-Twiflu Bainal-Warithari Wataribiyati*, cha Sheikh al-Falsafiy, Juz. 1, uk. 64, kutoka *al-Insaanu Dhalika al-Majuhulu*.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 58 11/23/2016 12:37:29 PM

Na pamoja na kwamba sisi hatuitakidi ulazima wa kuathiri na kurithiana kitabia kwa maana ya kuwa mwanadamu ni mwenye kupokonywa matakwa kabisa katika upande wake ila ni kwamba: "Hakika kanuni ya jumla ya kurithiana inapelekea mababa waumini na mama wenye heshima kuzaa watoto wema, hawa inawezekana wakapata furaha katika vizazi vya mama zao hivyo zisipatikane katika nyendo zao sababu za upotovu wa kurithi. Ila sisi hatuwezi kuhukumu juu ya hawa moja kwa moja kwamba watakua na kuishi milele hivyo hivyo, ambapo wanaweza kukutana na mazingira mabaya yanayofanya kazi ya kuwapotosha na kubadilisha nyendo zao na sifa zao za kurithi na kuzigeuza juu chini."

Na vivyo hivyo mtoto anayezaliwa kutoka kwa baba na mama wasiojua chochote katika imani, hakika anazingatiwa kuwa ni muovu katika kizazi cha mama yake kulingana na kanuni ya kurithi, lakini anaweza kupata mazingira mazuri na malezi ya kimsingi yanayofanya kazi ya kung'oa visababishi vya uovu toka ndani ya nafsi yake na hatimaye anakuwa miongoni mwa waumini wema na watu wema katika jamii.[43]

Na huenda sisi tunaweza kufasiri hadithi ya Imamu as-Sadiq عليه السلام katika maudhui haya ambapo anasema: "Mwenyezi Mungu anapotaka kuumba kiumbe anakusanya sura zote baina yake na baina ya Adamu kisha anamuumba katika sura ya mmoja wao." Athari hizi ambazo urithi unaziacha kwa watu ni jambo linalokubalika baina ya wenye akili na kwa hiyo tunakuta Amirul-Muumina عليه السلام alipotaka kuoa baada ya kufariki Fatmah Zahrah عليها السلام anamwambia ndugu yake Aqil – naye alikuwa anajua nasaba za Waarabu – "nichgulie mwanamke aliyezaliwa na mashujaa miongoni mwa Waarabu ili ananizalie kijana atakayekuwa ni mwenye kumnusuru mwanangu Husein." Na anamwambia Maliki al-Ashtari katika waraka wake

[43] Rejea iliyotangulia Juz. 1, uk. 79.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 59 11/23/2016 12:37:29 PM

mashuhuri: "Kisha anaandamana na wenye utu na heshima, na wenye nyumba njema, na waliotangulia katika wema, kisha watu wenye jitihada na ushujaa, wema na upole, hakika wao ni wakusanya utukufu na wakusanya umaarufu."[44]

Yeye anaamiliana pamoja na kadhia kana kwamba ni mas'ala ya kawaida. Katika hadithi ya kwanza hataki mwanamke mzuri au kutoka katika kabila maarufu au tajiri, bali kutoka katika familia shujaa ili azae shujaa, na vivyo hivyo katika tamko la pili ambapo anaona kwamba watu wa nyumba njema na viashiria vya ukarimu humo zinakusanyika sifa nzuri na humo unajikita umaarufu.

Na kama ambavyo athari nzuri zinahama kutoka kwa babu kwenda kwa baba hadi kwa mtoto, vilevile athari mbaya zinahama, aliyezaliwa na mzinifu ana uwezekano mkubwa zaidi kuliko mwingine wa kufanya zinaa na kosa, na kama tukitazama katika maisha ya wauaji na waovu katika historia tungekuta athari za kurithi ziko wazi. Huyu hapa Ibn Nabagha, yule pale mtoto wa wala maini, na zaidi ya hao ni yule kule Ibn Zaraqau n.k.

Kwa kuangalia hayo hakika sisi tunaitakidi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu, naye Ndiye Mwenye kuendesha mambo kwa hekima yake, amewajaalia Manabii na Maimamu kuwa ni wasafi, kizazi bora kuanzia kwa Adamu hadi wakafika katika dunia hii. Na ili tusirefushe utafiti tunaacha Hadithi zizungumze:

**Katika tafsiri ya Aya Tukufu katika Sura Shuaraa:**

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ الَّذِي يَرَاكَ حِينَ تَقُومُ
وَتَقَلُّبَكَ فِي السَّاجِدِينَ

[44] *Nahjul-Balaghah*, Barua ya 53.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 60 11/23/2016 12:37:29 PM

**"Na mtegemee Mwenye nguvu Mwenye kurehemu. Ambaye anakuona unaposimama. Na mageuko yako katika wale wanaosujudu."**
**(Sura Shuaraa; 26: 217 - 219).**

Kutoka kwa Jabir bin Abdillah al-Answariy رضي الله عنه amesema: Aliulizwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: Ulikuwa wapi Adamu alipokuwa peponi? Akasema صلى الله عليه وآله وسلم: "Nilikuwa katika mgongo wake, aliteremka ardhini na mimi nipo katika mgongo wake na nilipanda safina katika mgongo wa Nuhu, na nilitupiwa katika moto katika mgongo wa Ibrahim, na hawajakutana wazazi wawili katu katika uchafu, Mwenyezi Mungu hakuacha kunihamisha kutoka migongo mizuri hadi kwenye matumbo mema ya uzazi, ongofu hadi Mwenyezi Mungu alipochukua ahadi yangu kwa unabii na mafungamano yangu kwa Uislamu."

☞ Na kutoka kwa al-Baqir Muhammad bin Ali عليه السلام katika tafsiri ya Aya iliyotajwa amesema: "Anaona kugeuka kwake katika migongo ya manabii kutoka kwa Nabii hadi kwa Nabii, hadi Mwenyezi Mungu akamtoa katika mgongo wa baba yake kwa ndoa na sio kwa zinaa tangu kwa Adamu عليه السلام."

☞ Na kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: "Nimetolewa kutokea kwa Adamu عليه السلام kwa ndoa na sio kwa zinaa."

☞ Na kutoka kwake رضي الله عنه vilevile: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: "Hawajakutana wazazi wangu katu katika zinaa, na Mwenyezi Mungu hakuacha kunihamisha kutoka katika migongo mizuri hadi kwenye vizazi vyema safi vilivyotakaswa, na hazigawanyiki sehemu mbili ila nitakuwa katika iliyo bora.[45] Vivyo hivyo hawakugawanyika watu makundi mawili ila Mwenyezi Mungu ananijalia katika lililo bora zaidi, hivyo nimezaliwa ku-

[45] Hadithi kutoka katika *Nahjul-Haqi wa Kashifu Swidiq*, cha al- Allammah al-Hilliy uk. 157.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 61 11/23/2016 12:37:29 PM

toka kwa wazazi wawili na hakikunipata chochote kutoka katika zama za ujahiliya, na nimetokana na ndoa, na wala sijatokana na zinaa kuanzia kwa Adamu عليه السلام hadi nikafikia kwa mama yangu na baba yangu, na mimi ni mbora wenu kwa nafsi na ni mbora wenu kwa baba."[46]

Na Amirul-Mu'minin عليه السلام anazungumza juu ya mas'ala haya katika hotuba nyingi kwa kuzingatia kuwa ni moja ya mambo ya kawaida ya kiitikadi, anasema عليه السلام kwa kuwasifia Manabii عليهم السلام: "Akawaweka katika sehemu nzuri zaidi na akawatuliza katika makazi yenye kutulia migongo mitukufu hadi kwenye matumbo ya uzazi matwaharifu. Kila anapoondoa mtangulizi wao anakuja katika dini ya Mwenyezi Mungu anayefuatia, ikafikia karama ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم, akamtoa katika madini bora zaidi na maoteo matukufu zaidi, na katika shamba lenye kumea kutoka katika mti ambao kwawo kumetoka Manabii Wake. Na akateua miongoni mwao waaminifu, kizazi chake ni kizazi bora na familia yake ni familia bora na mti wake ni mti bora, umemea katika utukufu na umechanua katika ukarimu, una matawi marefu na matunda yasiyofikiwa….."[47]

Na anasema عليه السلام vilevile katika kumtaja Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: "Amemchagua kutoka kwenye mti wa Manabii na taa yenye kuangaza, na hazina ya maulamaa, ngome ya mashujaa na taa za giza na chemchem ya hekima." Na anasema katika sehemu nyingine: "Na nashuhudia kwamba Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم ni mja Wake na Mtume Wake na Bwana wa waja Wake. Kila viumbe vinapogawanyika makundi mawili, anamjalia katika lililo bora zaidi na haukuingia humo uzinzi wala hajaingia humo muovu."[48]

---

[46] *Al-Bidaya* cha Ibnu Kathir, Juz. 2, uk. 255.
[47] Mkazo hapa ni juu ya baba na mababu wa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم kwa sababu ni asili ya mti ule.
[48] *Nahjul-Balaghah*, Hotuba ya 94, 108 na 214.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 62 11/23/2016 12:37:29 PM

Haya, na historia inatusimulia juu ya wazazi wa Nabii ﷺ. Na baba zake katika utekelezaji wa majukumu yao, ni kilele cha wema, utukufu na watu wenye sharafu na utukufu, watetezi wa wenye kudhulumiwa na wenye kukataza maovu.[49] Na tunanukuu katika historia baadhi ya yanayotajwa kuhusu utukufu wa Abdullah mzazi wa Nabii ﷺ na ambaye alifariki wakati Nabii akiwa katika tumbo la mama yake Amina.

Amepokea Ibnu Is'haqa: Hakika Abdul-Mutwalib alipoondoka baada ya kumtoa fidia mtoto wake, mwanamke wa Bani Asad bin Abdul-Uza bin Quswai naye ni Ummu Qataal, dada yake na Waraqa bin Naufal bin Asad Abdul-Uza, alipita kwa Abdillahi, wakati huo alikuwa kwenye Kaaba, akaangalia uso wake na akasema: Unakwenda wapi ewe Abdillahi? Akasema: Niko pamoja na baba yangu. Akasema: Unao mfano wa ngamia ambao walichinjwa kwa ajli yako naomba unioe. Akasema: Mimi niko pamoja na baba yangu na wala siwezi kumkhalifu wala kumwacha.

Abdul-Mutwalib akatoka naye hadi akaenda kwa Wahab bin Abdu Manafi bin Zahara, na Wahab huyu alikuwa ni mkuu wa Bani Zahara kwa umri na utukufu, ndipo akamuoza binti yake Amina binti Wahab, naye siku hizo alikuwa ni Bibi wa wanawake wa kaumu yake.

Na baada ya Abdillahi kumchukua bibi harusi Amina, ulikuja ujumbe wa kundi la Makuraishi na humo kuna mwanamke ambaye alitaka aolewe naye, Abdillahi akamwambia kwa nini hunitamkii leo yale uliyokuwa ukiniambia jana?

Mwanamke akasema: "Imekuondoka nuru uliyokuwa nayo jana, hivyo mimi sina haja na wewe." Na alikuwa anasikia kutoka kwa kaka yake Waraqa bin Naufal – na alikuwa ni mnaswara na akifuata

[49] Katika fadhila unaweza kurejea Ufafanuzi wa *Nahjul-Balaghah* wa Ibnu Abil-Hadidi al-Ghazaliy, Juz. 10, uk. 200.

vitabu – kwamba itatokea katika ummah huu Nabii hivyo akatamani awe ni miongoni mwao, na pengine Ummu Qataal binti Naufal alisoma baadhi ya mashairi akisikitika katika yaliyompita kati ya jambo ambalo alilitamani, na hiyo ni katika aliyoyapokea al-Bayhaqiy:

> "Shikamana na Aali Zahara popote walipo,
> Na Amina ambaye alibeba kijana,
> Anamuona mwongofu alipomwingilia,
> Na nuru imeshamtangulia mbele."

**Hadi aliposema:**

> "Viumbe vyote vinamtarajia,
> anaongoza watu imamu mwongofu,
> Mwenyezi Mungu anamuona kwa nuru ya usafi wake,
> Nuru yake imetuondolea giza,
> Na hayo ni maamuzi ya Mola Wako pale alipomchagua,
> Atakapokwenda siku moja au akikaa,
> Ataongoza watu wa Makkah baada ya ukafiri,
> Na atafaradhishiwa baada yenu Swaumu."

Na amepokea Abu Bakri al-Kharaitwiy: Hakika kuhani wa kiyahudi katika watu Tabalah na ambaye alikuwa amekwishasoma vitabu, aliyekuwa akiitwa Fatimah binti Mur al-Khathia'miyah aliona katika uso wa Abdillahi nuru ya utume akamtamani katika nafsi yake kwa kumpa ngamia mia moja, lakini Abdillahi akamjibu:

> "Ama, haramu ni bora nife,
> Na ufumbuzi, hakuna hila nitaubainisha,
> Sasa itakuwaje, kwa jambo ambalo unalitaka?
> Mtukufu analinda heshima yake na dini yake."[50]

[50] *Suwaru Min Hayati Swahabiyaati Rasuli* ﷺ, cha Khalidi Abdurahamani al- Aka, uk. 51, kwa kunukuu kutoka kwenye *al-Bidayati* cha Ibn Kathir.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 64 11/23/2016 12:37:29 PM

Na katika mashairi haya ambayo yananasibishwa kwa mzazi wa Mtume ﷺ unadhihiri utukufu na kulazimiana na usafi, ambapo jambo haliepukani na kuwa ama ni haramu au halali, ama haramu hakika anatanguliza mauti kabla ya kufanya haramu, na wala haibainiki humo halali akaikwepa kwa hali yoyote, hii ni katika siku za ujahilia wa Waarabu ambapo wengi walikuwa hawaogopi haya mambo, bali unamuona mtu wa heshima miongoni mwao anakwenda kwenye madanguro na kufanya zinaa na makahaba, na baadaye anazaliwa mtoto asiyejulikana nasaba yake kwa kushiriki baba zake na kuchanganyika kwao.

Na yaliyopokewa katika kisa cha kwanza pamoja na Ummu Qataal yanatunufaisha katika sehemu hii, ambapo yanatia mkazo wazi kuhusu habari ambazo zinamaanisha kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa ni nuru katika mgongo safi hadi kwenye tumbo la uzazi safi. Na mwanamke kumtaka Abdillahi siku ya kwanza ilikuwa ni kwa kuona nuru hii, alipooa na nuru hii kuhamia kwa Amina binti Wahabi, mzazi wa Mtume, ili iumbike katika kizazi chake kitukufu, akaikosa katika uso wake. Na ambapo inadhihirika kwamba jambo hili lilikuwa ni katika mambo mashuhuri, na kwa hiyo Abutalib alipokuwa anahutubia watu kwa kubainisha sifa hizi katika minasaba mbalimbali, hakupingwa na yeyote. Alikwishasema katika hotuba ya ndoa ya Fatmah binti Asad, ambaye ni mke wake: “Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola mlezi wa viumbe, Mola wa Arshi tukufu na Maqamu tukufu na Mash’ari na Hatwim (Jahannam), ambaye ametuteua kuwa vielelezo, na watumishi mashuhuri wenye ikhilasi na ngome za viongozi mashujaa, watwaharifu kutokana na maovu na shaka, adha na aibu. Na akasimamisha kwetu mipaka na akatufadhilisha kwa makabila, wateule wa kizazi cha Ibrahimu na wabora wake, zao la Ismaili….” Hadi mwisho wa hotuba yake. Yeye anatia mkazo utakaso kutokana na maovu na shaka, yaani zinaa na



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 65 11/23/2016 12:37:30 PM

haramu bali na yenye mkanganyiko, adha na aibu. Ishara ya usafi wa kimaanawi katika tabia na sifa. Kama unavyobainisha hili mwendelezo ambao unawaunganisha kwa Ibrahimu na Ismail عليهما السلام.

**Mwendelezo wa Uangalizi wa Kiungu:**

Kama ulivyoanza uangalizi huu wa kiungu kwake صلى الله عليه وآله وسلم uliendelea pamoja naye na pamoja na Mawasii wake عليهم السلام, ambapo utangulizi uleule ambao tumekwisha kuuzungumzia katika yanayohusiana na dharura ya kuhifadhiwa wazazi wa Mtume na babu zake kutokana na kila dosari za kitabia na ufisadi wa kimaanawi unaojitokeza hapa katika dharura ya kuhifadhiwa Mawasii baada yake.

Ama katika yanayohusiana na Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم ambapo anakuwa mzazi wa familia hii kupitia kwa Zahra Fatimah عليها السلام yameshatangulia mazungumzo. Ama kwa yanayohusiana na Amirul-Mu'minin عليه السلام ambaye yeye ni mzazi wa familia hii tukufu moja kwa moja, na anashirikiana katika nasaba pamoja na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم katika babu yao Abdul-Mutwalib amesema عليه السلام:

"Wallahi hakuabudia baba yangu wala babu yangu Abdul-Mutwalib, wala Hashim, wala Abdu Manafi sanamu katu."[51] Na wanayoyaona baadhi ya waandishi juu ya shirki ya Abutalib mzazi wa Amirul-Mu'minin عليه السلام tukijaalia kuwa rai hii imeepukana na kasumba maarufu katika historia, yanafasiriwa na hadithi iliyopokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq عليه السلام kwamba Abutalib alipewa malipo yake mara mbili kwa sababu aliamini mwanzo na pili akaficha imani yake.[52] Na ni vivyo hivyo mama wa Amirul-Mu'minin عليه السلام Fatimah binti Asad bin Hashim, nasaba hii iliyotakaswa inapoungana kwa babu yake Hashimu.

---

[51] *Biharul-An'war*, Juz. 35, uk. 98.
[52] *Biharul-An'war*, Juz. 10, uk. 144.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 66 11/23/2016 12:37:30 PM

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anapokuwa na wake wengi basi mbora wao na aliyeandaliwa kubeba nasaba hii takatifu ni Khadija binti Khuwaylid, ambaye anaungana na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika nasaba yao katika babu wa nne (Quswai bin Kilaab). Na hata katika ujahiliya alikuwa na lakabu ya Twahira, pamoja na kuwepo wanawake wengine, baadhi yao ni wazuri kuliko Khadija na wengi wao ni wadogo kwa umri miongoni mwao, na hii inamaanisha kwamba wao wana uwezekano mkubwa zaidi wa kubeba mimba na kumzalia Mtume, lakini anabakia yeye Khadija ndio mteule kwa ajili ya utukufu huu. Na vipi isiwe hivyo wakati mbora wa wanawake wa peponi ni Khadija binti Khuwaylid, Fatima binti Muhammad, Mariyam binti Imrani na Asia binti Mazahim mke wa Firaun?!

Na vivyo hivyo inapofikia dauru kwa Bibi wa wanawake wa ulimwenguni Fatimah Zahara عليها السلام ambaye alikuwa ni chombo cha uimam na uongozi, naye ndio mama wa Hasan na Husein عليهما السلام na ni kiunganishi baina ya utume na uimamu. Na unadhania nini kwa mtoto anayetokana na mbora wa viumbe vya Mwenyezi Mungu tangu wa mwanzo na wa mwisho, Bwana wa Manabii Muhammad ﷺ na baina ya mbora wa wanawake wa peponi mtwaharifu Khadijah binti Khuwaylid?

Kwa hiyo kwa kutilia mkazo ukweli huu tunasoma ziyara ya Imamu Husein عليه السلام maarufu kwa jina la *Ziyaratul-Warithah* iliyopokewa kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام kwa sanadi sahihi:

اَشهَدُ اَنّك كُنتَ نوُرا في الأصلابِ الشّامِخَةِ وَالأرحـامِ المُطَهَرَةِ لم تـُنَجِسـكَ الجـاهِلِيَّةُ بـاَنِجـاسِها وَلَم تـُلبِسكَ مِن مُدلَهِمّاتِ ثِيابـِها

**"Nashuhudia kwamba hakika wewe ulikuwa ni nuru katika migongo mitakatifu na vizazi vitwaharifu. Ujahili haujakutia dosari kwa uchafu wake, na wala haujakugusa kwa uovu wake."[53]**

---

[53] Na yaliyo baada yake *Mafatihul-Jinani* cha Sheikh Abbasi al-Qummiy.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 67 11/23/2016 12:37:30 PM

Na kwa kuangalia kuwa mas'ala hii ni sehemu katika utamaduni wa kiitikadi ambao anashikamana nao muumini, tunakuta mkazo juu yake katika matamko ya Ziyara zilizopokewa kutoka kwa Maimamu عليهم السلام, na kwa kuongezea katika yaliyotangulia tunakuta maana ileile inajirudia katika ziyara ya mwezi wa Rajabu. Vilevile maana inajirudia katika Ziyara yake عليه السلام, katika ziyara ya Iddi mbili na ziyara ya arubaini, na hayo si kingine isipokuwa ni kufahamisha umuhimu maalum ambao wanao Maasumini katika kutilia mkazo juu ya maana hii.

Kama ambavyo Imamu Ali bin Husein Zainul-Abidin عليه السلام anatilia mkazo juu ya ukweli huu katika hotuba yake katika baraza la Yazidi bin Muawiya, wakati alipopelekwa Sham pamoja na msafara wa mateka miongoni mwa wanawake na watoto, pamoja na kuwepo ishara za upinzani katika utawala wa Yazidi, na uovu wa kizazi chake, isipokuwa inatilia mkazo maana ambayo sisi tunaielezea na hiyo ni katika kauli yake عليه السلام:

"Mimi ni mtoto wa wasio na dosari, mimi ni mtoto wa watakatifu wasio na kasoro."

## Hata Mama Watoto (vijakazi):[54]

Na tutazungumzia katika kurasa zinazokuja maudhui ya kuoa kwa Ahlul-Bayt عليهم السلام vijakazi na undani wa hayo, lakini sisi sasa hivi tunazungumzia juu ya Mwenyezi Mungu kuhifadhi na kulinda usafi wa kizazi ambacho kimechaguliwa kwa ajili ya kuongoza binadamu, ambapo ni maarufu kwamba vijakazi walikuwa wanauzwa na wananunuliwa kutoka kwa mtu hadi kwa mwingine. Na mara nyingi hasalimiki mmoja kati yao isipokuwa kwa nadra. Lakini matakwa ya Mwenyezi Mungu yanapokuwa ni kumhifadhi mmoja wao, mmoja wa sehemu ya mlo-

[54] Hilo ni jina la kijakazi ambaye yuko chini ya miliki ya mwanaume na amemzalia, wakati huo huitwa Mama Watoto, na anakuwa huru kwa kifo cha Mume wake.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 68 11/23/2016 12:37:30 PM

longo huu mtukufu, hakika mambo yote yanaandaliwa ndani ya uzio wa kuhifadhi utwahara na usafi. Natusome yanayoandikwa na historia kutoka kwa Hamida al-Muswafatu al-Barbariya mke wa Imamu as-Sadiqi na mzazi wa Imamu al-Kadhim عليهما السلام.

Aliingia Ukashah bin Muhaswan al-Asadiy kwa Abu Ja'far al-Baqir عليه السلام, wakati huo Abu Abdillahi as-Sadiq عليه السلام alikuwa amesimama kwake. Ibn Ukashah akamuuliza Imamu al-Baqir عليه السلام juu ya sababu ya Imamu as-Sadiq عليه السلام kuchelewa kuoa akamjibu kwamba: "Atakuja muuza watumwa kutoka Barbar na atafikia katika nyumba ya Maamun, tutamnunulia kwa hela hii kijakazi." Na zikapita siku, kisha mpokezi aliingia kwa Imamu al-Baqir عليه السلام kwa mara nyingine, Imam akasema: "Je, niwaambie kuhusu muuza watumwa ambaye niliwaambia? Amekwishafika, nendeni na kanunueni kwa hela hii kijakazi." Tukamwendea muuza watumwa akasema: "Nimekwishauza niliokuwa nao isipokuwa vijakazi wawili wagonjwa, mmoja wapo ni mzuri kuliko mwingine." Tukasema: Watoe ili tuwaone, na tukasema: Ni kiasi gani unamuuza kijakazi huyu mzuri? Akasema: "Dinari 70." Tukasema: Punguza. Akasema: "Sipunguzi chini ya dinari 70." Tukasema: Tutamnunua kwako kwa bei hii uliyofikia. Na baada ya kutimia maafikiano na kijakazi akaletwa kwa Imamu al-Baqir عليه السلام, akamuuliza jina lake, akasema: "Hamida" Imam akasema: "Mwenye kushukuru duniani, ni mwenye kushukuriwa akhera. Niambie kuhusu hali yako: Ni bikira au mtu mzima?" Akasema: "Ni bikira." Imam akasema: "Vipi na ambapo haangukii mjakazi kwa wauza watumwa isipokuwa wanamharibu?" Kana kwamba Imamu عليه السلام alikuwa anataka kudhihirisha kwa waliohudhuria, namna Mwenyezi Mungu alivyomhifadhi kijakazi kutokana na uchafu. Na anatarajia jawabu lake kwa hilo, vinginevyo kama angetarajia yasiyokuwa hayo asingemuuliza mbele ya waliohudhuria. Akamjibu kwamba alikuwa anakuja lakini Mwenyezi Mungu alikuwa anamkinga na hilo.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 69 11/23/2016 12:37:30 PM

Na kwa kutukuza jambo la huyu kijakazi ambaye Mwenyezi Mungu amemjalia ili awe mbebaji wa moja ya nuru kati ya waongozaji, amesema juu yake Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Hamida ametakaswa kutokana na uchafu, kama vile kiini cha dhahabu, maadamu mamlaka yamemlinda hadi akafikishwa kwangu kwa karama ya Mwenyezi Mungu kwangu na kwa Hoja baada yangu."[55]

Haya pamoja na kujua kwamba Imamu as-Sadiq عليه السلام alikuwa na wake wengi, mmojawapo ni mjukuu wa Imamu Hasan عليه السلام, isipokuwa matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yalitaka kijakazi huyu atukuke kwa kumbeba walii wa Mwenyezi Mungu. Na kisha je, hatujatanguliza katika kurasa zilizotangulia kwa msomaji mtukufu kwamba ni mas'ala ya kazi ya ghaibu kabisa!

# MAISHA YA NDOA YA AHLUL-BAYT عليهم السلام

## 1. Ahlul-Bayt na Mas'ala ya Jinsia:

Mas'ala ya jinsia yanachukua sehemu kubwa katika fikira za mwanadamu kwa kutokana na yale yanayoyatengeneza miongoni mwa vibano na yale yanayoyawakilisha katika haja inayoendelea. Na kwa kuangalia hilo, hakika katika rai ya binadamu, kwa ajili ya kutatua tatizo hilo kuna njia mbili: Kukandamiza na kuhalalisha jumla. Wakati ambapo wahyi una njia ya tatu.

### a. Kukandamiza: ni mtazamo wa watawa na masufi:

Tangu mwanzo ambapo mwanadamu alikuwa anatafuta peke yake njia ya kumfikisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliona kuna mgongano baina ya dunia na akhera, na baina ya matamanio na utakaso, kwa hiyo alichukua njia ya kupinga cha kwanza. Hivyo akakataa chakula kitamu, pamoja na kwamba ni neema ya Mwe-

[55] *Biharul-An'war*, Juz. 48, uk. 6.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 70 11/23/2016 12:37:30 PM

nyezi Mungu, ili afike Akhera, naye anaacha vazi safi na laini, kwa kubadilisha na vazi la sufi na gumu, kwa kuwa la kwanza linamzuia kwenda kwa Mwenyezi Mungu. Na anaacha kuoa vilevile, kwa sababu kuingiliana kijinsia ni dalili ya kushikamana na dunia.

Na katika yanayohusiana na mas'ala ya jinsia yametiwa nguvu na yaliyoyafahamika kwa baadhi ya watu wa dini kwamba mwanamke ni kielelezo cha makosa, kupitia tafsiri yao katika kisa cha Adamu na Hawa kutoka peponi. Na kwamba Masihi Isa bin Mariyamu عليه السلام aliishi maisha ya ukapera na kujizuia na wanawake. Hakika msingi wa mtazamo huu unasimama juu ya mambo mawili:

**1.** Hakika kuacha maingiliano ya kijinsia na kukandamiza matamanio ya kijinsia katika nafsi kunatoa fursa kwa nguvu za kiakili na za kiuvumbuzi ili kupevuka na kustawi, kama ambavyo kufanya mazoezi ya michezo kunanufaisha mwili katika kuondoa mafuta ya ziada yenye kudhuru na katika kustawisha misuli na nguvu. Hakika ukandamizaji huu katika matamanio ya kijinsia kupitia uasi wa wito wake na kutoyajali, kunazingatiwa kuwa ni mazoezi ya kiroho yanayonufaisha kudhihirisha vipaji vilivyofichikana na nguvu ya kinafsi, wakati ambapo kuyatii kwake – katika rai yao – na kuitikia matakwa yake kunamfanya mwanadamu kuwa ni mateka wa matamanio na mtumwa wa utashi, na hivyo kuzimika taa za hekima katika moyo wake.

**2.** Hakika kujitenga kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu na kutaka yaliyopo Kwake miongoni mwa fadhila inahitajia ikhilasi ya kuelekea Kwake kimwili na kiroho, na hivyo moyo hautashikamana na mapenzi ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu, wala mwili hautoshughulishwa na siri ya ibada yake. Na uitikiaji wa matamanio yoyote miongoni mwa matamanio unazingatiwa kuwa ni ibada kwa mwenye kushikamana na matamanio



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 71 11/23/2016 12:37:30 PM

hayo, kwa hiyo, hakika ikhilasi katika ibada - katika rai yao - inahitajia kuepukana na matamanio haya na kuyaacha.

Na mitazamo hii imepatikana katika zama za zamani na imekhalifu msingi wa jinsia, na kwamba fikira hii ilikuwa inapata uungwaji mkono na kusambazwa, hususani katika sehemu ambazo kumeenea dini za Ukristo na Ubudha, na kwamba "siri ya mwenye kuacha" anatutajia mifano ya fikira hii yenye kushangaza inayosema kwamba uovu na upotevu ni mambo mawili yote yanalazimiana na uhusiano wa kijinsia.

Na katika sehemu ambazo zimeishi mbali na athari za dini mbili hizo za Ubudha na Ukristo ilidhihiri mitazamo na wakapatikana watawa waliolingania utawa na kutokuoa. Na kama inavyodhihirika, hakika fikira ovu "uhusiano na maingiliano ya kijinsia" ilienezwa kwa Wakristo kwa kiasi hiki kwa sababu ya tafsiri ya upande wa kanisa mwanzoni mwa kuasisiwa kwake. Kuhusu maisha ya ukapera ambayo aliishi Isa Masihi عليه السلام, ilikwishasemwa kwamba Masihi aliishi ukapera kwa sababu ya uovu halisi uliopo katika uhusiano wa kijinsia na kwa hiyo hakika viongozi wa dini ya Kikristo walijua kupanda daraja hadi daraja za kiroho za juu kwa kutochanganyikana na wanawake muda wote wa maisha binafsi, kama ambavyo mapapa ni wajibu wachaguliwe baina ya ambao hawajatangamana kabisa na wanawake, na viongozi wa kanisa wanaitakidi kwamba uchamungu wa mtu ni kuwa mbali na kuoa.[56]

Na fikira hii haikuishia tu katika Ubudha na Ukristo, bali ilipatikana pia baina ya Waislamu pamoja na kwamba mafunzo ya Uislamu yako wazi na yanajali dunia na akhera. Alikuja mke wa Athmani bin Madhuuni hali ameacha kujipamba, akaulizwa na mmoja wa wake za Mtume ﷺ juu ya sababu ya hilo, akampa habari kwamba

[56] *Al-Dhawaabitu al-Khilaqiya Lilisuluki al-Jinsiy* cha Sheikh Murtadhaa Mutahhariy kuhusu kitabu *Aziwaaju wal-Akhilaaq* cha Bartaraa nid Raasil

mume wake anafunga mchana na anakesha usiku kwa ibada na wala hamwingilii. Akamwambia Mtume ﷺ juu ya hilo. Mtume akatoka mbele ya Maswahaba wake akasema: "Je, mnawachukia wanawake? Hakika mimi nawaendea wanawake na ninakula mchana na ninalala usiku, basi mwenye kuchukia sunna yangu basi hayuko pamoja na mimi, na Mwenyezi Mungu amekwishateremsha:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُحَرِّمُوا طَيِّبَاتِ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ وَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنْتُمْ بِهِ مُؤْمِنُونَ

**"Enyi mlioamini! Msiharamishe vizuri alivyowahalalishia Mwenyezi Mungu. Wala msipetuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaopetuka mipaka. Na kuleni katika vile alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu vilivyo halali na vizuri; na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye nyinyi mnamwamini." (Surat al-Maidah: 87- 88).**

Wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika sisi tumeapa katika hilo! Mwenyezi Mungu akateremsha: "Mwenyezi Mungu hatopatiliza kwa sababu ya kuapa kwenu kwa upuuzi."

Na vilevile tunakuta mwanamke anaacha kuolewa kwa kupenda fadhila na kujikurubisha kwa hilo kwa Mwenyezi Mungu. Alikuja mwanamke kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام akasema: "Mwenyezi Mungu akutengenezee mambo yako, hakika mimi ni mtawa." Akamwambia na utawa una maana gani kwako? Akasema: "Sitaki kuolewa kamwe." Akasema: Kwa nini? Akasema: "Nataka fadhila katika hilo." Akasema: "Ondoka, kama hilo lingekuwa na fadhila basi Fatimah عليها السلام alikuwa na haki zaidi kuliko wewe, hakika hakuna yeyote anayemshinda katika fadhila."



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 73 11/23/2016 12:37:30 PM

Hii ndio njia ya kwanza aliyoichagua mwanadamu ili kutatua mas'ala ya kijinsia. Na inafupishwa katika dharura ya kukandamiza matamanio yake kwa kuacha kuyaitikia, na kusahau wito wake kwa ajili ya kuacha nguvu za kiakili zilizofichikana katika upande mmoja na kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu – katika rai yao – kwa upande mwingine.

**b. Uhuru kamili: Mwanya wa ustaarabu wa kisasa:**

Baada ya mzunguko huo mrefu ambao mwanadamu ameupitia (au baadhi yao) katika kukandamiza mas'ala ya kijinsia, wamekuja upya ili watafute njia kinyume na waliyokuwa nayo hapo kabla. Na hiyo ni kwa kufungua mlango mbele yake katika kuabudu matamanio, na kuyatekeleza matamanio haya.

Na utekelezaji huu unaanzia katika nukta tatu:

Kulichukulia tendo la jinsia kuwa ni kitendo cha kawaidia kinachofanywa na baadhi ya viungo vya mwanadamu kwa namna ya kawaida tu. Ni sawa sawa kabisa na kula, kunywa na kulala. Na kama ambavyo vitendo hivi ni vya kimazoea na vya kawaida kwa mwanadamu, hakika kufanya kitendo cha kijinsia – kulingana na mtazamo huu – ni wajibu uwe vivyo hivyo. Kwa kukitenda kwa wingi na katika mazingira mbalimbali, bila ya kikwazo wala mpaka, na pindi itakavyokuwa hivyo: Kwa wingi na bila ya kikwazo, basi tatizo litakuwa limekwisha kumalizika.

Kuchukulia kitendo cha jinsia kuwa ni jambo binafsi linalopangwa na raghaba ya pande mbili humo, bila ya kuingiliwa na kanuni au hata ada za kijamii katika kuliratibu, sawa iwe katika idadi au katika njia ya kulitekeleza. Kulingana na watu wa nadharia hii, maadamu mas'ala hayapingani na uhuru wa wengine, hakika jambo linaachiwa pande hizi mbili zinazolifanya. Na pindi linapovunja uhuru wa



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 74 11/23/2016 12:37:30 PM

wengine, basi hakika mpaka ni kwa kiasi hicho tu. Na kisha hakuna kuingia kanuni wala ada katika kuratibu njia yake au kiasi chake kabisa. Kwa sababu ni jambo binafsi, ni sawasawa kabisa kama ambavyo kanuni haiwezi kupanga idadi ya saa za kulala kwa mtu, au kiasi anachokula.

Na kwa sababu vitendo hivi ni vya kawaida na vya kimazoea kama vile kula, na kwa sababu katika upande mwingine ni jambo binafsi, hivyo basi hakupatikani sehemu inayokataza humo kuvifanya kulingana na raghaba ya mtu, ni sawa iwe anavifanyia katika bustani ya umma au katika nyumba. Hii ni ukiachilia mbali vikwazo vingine vya kidini au kisharia, hii inasihi na ile haijuzu!

Na matokeo ya nadharia hii, leo tunaona katika nchi za Magharibi kuporomoka haraka kwa mpangilio wa familia na kulipuka matamanio yenye kuangamiza, na ongezeko la nasaba katika kupatikana watoto wasio wa kisharia na orodha nyingine.

**Uislamu na Jinsia:**

Na kabla ya kuanza mazungumzo kuhusu mtazamo wa Uislamu kupitia utekelezaji wa Maasumini عليهم السلام, tunarejesha kwenye akili yale yaliyotangulia kutafitiwa kuhusu upande wa kibinadamu na wa ghaibu wa Ahlul-Bayt, na tunamrejesha msomaji katika sehemu hiyo kabla ya kuanza kusoma mistari ifuatayo:

Baada ya kumaliza umuhimu wa kuoa, tunaitakidi kwamba Mwenyezi Mungu hakuumba kwa mwanadamu kiungo wala utashi isipokuwa kwa lengo, na lengo tukufu vilevile, kama itatimia kuelekeza kiungo hicho na utashi huo mwelekeo sahihi. Na hawa masufi au watawa wanaitakidi bila ya kusita kwamba wao wanajua kuliko Mwenyezi Mungu? Na wanafahamu kuliko Yeye njia ya ibada yake? *Audhubillahi*, na kwamba kuumba utashi huu kumetimia katika



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 75 11/23/2016 12:37:30 PM

kughafilika na bila ya kupangilia, na kwa hiyo wao wanakalifishwa kudhibiti kosa hili kwa kukandamiza na kulimaliza! Njia hii sio tu haimkurubishi mja kwa Mwenyezi Mungu, bali inaweza kumfikisha kwenye mpaka wa kumkufuru Mwenyezi Mungu kupitia kumjua Mwenyezi Mungu kimakosa.

Ama yanayohusiana na kustawi vipaji vilivyofichikana tumekwishakuta kwamba wengi wa Manabii kwa ujumla, na miongoni mwao ni mbora wao, Nabii wetu Muhammad ﷺ naye ndio akili kamilifu zaidi na tabia njema zaidi katika ulimwengu, wote walikuwa wameshatangaza kwamba sunna yao ni kuoa, bali tunakuta Mtume huyu mtukufu ﷺ ana wake tisa, na hilo halikuathiri katika vipaji vyake na vipawa vyake isipokuwa ukali na uimara na (Mwenye kuchukia sunna yangu basi sio katika mimi), na katika mukabala tumekuta wengi wa wale wenye upungufu na wenye cheche ni wale wasiooa.

Ama nadharia ya pili matokeo ambayo imeyaleta katika muda huu mchache katika utekelezaji wake katika nchi za kimagharibi ni jibu zuri zaidi, na kwa kuwa kwake hivyo hatukalifishi nafsi zetu na taabu ya kuijadili. Ama kuhusu mas'ala ya jinsia katika Uislamu, sisi tunaitakidi kwamba inapambanuka katika mambo yafuatayo:

**1. Kazi yenye kulenga kuendelea aina:**

Mwanzo inapasa kuweka wazi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomuumba huyu mwanadamu katika umbo zuri alipanga kila sehemu humo na kila chembe na kiungo humo kwa ajili ya lengo, na wala akili ya binadamu haiwezi kufikiria mfano kamilifu zaidi kuliko mfano huu ambao ameuumba Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na ikiwa kila aina katika viumbe ni aina maalumu katika kuongezeka na kuzaliana, hakika njia bora zaidi za kuendelea kuumba ni ambayo tunaikuta kwa mwanadamu kupitia kazi ya jinsia na inayoifuatia kati ya mas'ala ya mimba, kuzaa na kunyonyesha.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 76 11/23/2016 12:37:30 PM

## 2. Maelezo ya hisia juu ya mapenzi ya moyo

Tunapotafakari katika nususi ambazo zinazungumzia kadhia hii, tunazikuta ziko mbali na hali ya zana (chomo) tupu na kuzigeuza kwenda kwenye hali ya kibinadamu na kutoka kwenye kazi ya viungo na kwenda kwenye hisia za nyoyo, na hivyo tunasoma katika Aya tukufu:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

**"Na katika ishara zake ni kuwaumbia wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao, na akajaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya kuna ishara kwa watu wanaofikiri." (ar-Rum; 30:21).**

Hakika sisi tunakuta katika Aya tukufu ambayo imekuja katika mtirirko wa Aya zinazoelezea ishara kubwa za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu, kuanzia ishara ya kumuumba mwanadamu kutokana na udongo, kisha ishara yake katika kuumba mbingu na ardhi na kutofautiana ndimi, lugha, tofauti za rangi na muundo. Hivyo Aya hii nayo imekuja katika mtiririko wa kubainisha ishara kubwa za Mwenyezi Mungu. Ni kweli kwamba mabadiliko ambayo yanatokea katika maisha ya wawili waliokuwa wageni kabisa katika muda uliopita, lakini inapatikana huruma, mapenzi na utulivu wa ndoa baina yao, katika haya mabadiliko kuna ishara tosha kwa mwenye kutaka kutafakari.

## 3. Upande wa kiroho katika mas'ala ya jinsia:

Dini haitosheki kwa kulipa zoezi hili lengo linaloungana na kuzaliana, wala kwa kulisifia kwa huruma, mapenzi na upendo tu, hakika pia inalipa wigo mtukufu wa kiroho, ambapo inalibadili-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 77 11/23/2016 12:37:30 PM

sha hadi kuwa moja ya ibada na inaliwekea kanuni, sunna na nyuradi.

Kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام amesema: "Mmoja wenu anapoanza kujamiiana basi aseme: 'Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Eee Mwenyezi Mungu, niepushe na shetani na umwepushe na shetani utakayeturuzuku."' Amesema عليه السلام: "Kama Mwenyezi Mungu atakadiria baina yao mtoto basi shetani katu hatomdhuru kwa chochote."[57]

Imepokewa vilevile: "Inapokaribia muda wa bibi harusi kuingia kwa bwana harusi ni sunna kumwamuru aswali rakaa mbili na awe na udhu anapoletwa kwako, na wewe vilevile uswali kama alivyoswali.Mhimidi Mwenyezi Mungu, mswalie Nabii na Ahali zake na useme: 'Eee Mwenyezi Mungu, niruzuku upole wake, mapenzi yake na ridhaa yake kwangu, na uniridhishe kwake na utukusanye mkusanyiko mzuri, na ufanye wepesi mazoea yetu, hakika wewe unapenda halali na unachukia haramu.'"[58]

Na umuhimu wa upande huu unadhihirika katika kubadilika kitendo na kuwa ni njia ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia mwanadamu kuihifadhi nafsi yake kutokana na haramu, kulazimiana kwake kukidhi matamanio yake kwa njia ya Mwenyezi Mungu.

Na msimamo huu wa kulazimiana na sharia ya Mwenyezi Mungu kutoka kwa muumini hautofautiani kulingana na maamrisho yake, kama vile swala au saumu au jihadi au ndoa, hakuna tofauti ya msimamo kutokana na maamrisho hayo, ambapo kinachotakiwa kwa muumini ni asili ya kulazimiana na kuleta hali ya unyenyekevu na kujisalimisha katika amri ya Mwenyezi Mungu katika nafsi yake. Na kwa hiyo hakika sisi tunakuta kwamba hadithi nyingi zinalinganisha baina ya maamrisho na vitendo hivi, pamoja na kwamba sisi

---

[57] *Wasailu Shi'ah* Juz. 7, uk. 96.
[58] *Makarimul-Akhlaq*, uk. 208.

tunajua kwamba kwa nje kuna ikhitilafu na tofauti baina yake. Na usawa huo si kingine isipokuwa ni ishara ya msingi wa kujisalimisha na unyenyekevu unaotakiwa kutoka kwa mja mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliingia katika nyumba ya Ummu Salama akakutana na harufu ya manukato mazuri, akasema: "Amekujieni Haulau." Ummu Salama akasema: "Ndivyo hivyo, yeye ana mashtaka juu ya mume wake." Na mara Haulau akajitokeza mbele ya Mtume akasema: "Naapa kwa baba yangu na mama yangu, hakika mume wangu ananichukia." Mtume akasema: "Mzidishie ewe Haulau." Akasema: "Siachi kitu kizuri cha kujipamba ila hujipamba nacho kwa ajili yake, lakini yeye hanitaki." Mtume akasema: "Laiti angejua anayoyapata kwa kitendo cha kuja kwake kwako!" Haulau akasema: "Na vipi atakuja kwangu?" Akasema ﷺ: "Ama anapokujia anapambwa na malaika wawili na anakuwa kama yule aliyechomoa upanga wake katika njia ya Mwenyezi Mungu, na anapojamiiana yanapukutishwa madhambi kama yanavyopukutika majani ya mti, na anapooga anaondokana kabisa na madhambi."[59]

Na Imamu as-Sadiq عليه السلام anafasiri jambo lililotangulia kwa kunukuu kwake kauli ya Mtume ﷺ kwa Abu Dhari: "Mwendee mke wako utapata malipo." Abu Dhari akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nawaendea na nalipwa?" Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Kama ambavyo unavyofanya haramu unapata dhambi, vivyo hivyo unapofanya halali unalipwa."[60] Na anazingatia tendo la ndoa maadamu ni katika njia ya halali ni sadaka. Kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimwambia mwanaume kati ya Maswahaba wake siku ya Ijumaa: 'Je, umefunga leo?' Akasema: 'Hapana', akasema ﷺ:

---

[59] *Wasailu Shia*, Juz. 7, uk. 75.
[60] *Wasailu Shia*, Juz. 7, uk. 76.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 79 11/23/2016 12:37:30 PM

'Je, umetoa sadaka kwa chochote?' Akasema: 'Hapana.' Akasema ﷺ: 'Simama mwendee mke wako, hakika ni sadaka yako kwake.'"[61]

## 4. Uhalisia:

Japokuwa upande wa mas'ala ya jinsia umejumuisha kiasi fulani cha dhana, kiasi kwamba kinayafanya kuwa matamu zaidi, isipokuwa ni kwamba kuchupa mipaka katika upande huu kunampokonya kijana anayeinukia nguvu ya kazi na uchangamfu, wakati anapogeuka kila mmoja wao na kuwa kichaa wa usiku mwenye kutahayari na kukanganyikiwa pamoja na fikira zake na mawazo ya mapenzi yake, na kushughulika kwake na hisia za mapenzi na matamanio. Nao ni mwanzo wa tatizo lenye kuhamia kwa watu wawili, na hakika hawezi kutatua tatizo lake, kwa sababu yeye anaishi katika ulimwengu mwingine usiokuwa ulimwengu huu, na vivyo hivyo anaendelea hadi kwenye moja ya miishilio miwili, ama atapata mwenye kumuongoza kwenye njia halisi na kumuokoa kutokana na kudumu kwenye mawazo haya, kupitia ndoa au kwa kujishughulisha na nyanja nyingine miongoni mwa harakati zinazochukua mazingatio yake.

Na ima mwishilio wa umajinuni kama ataendelea na mwenendo huu, hali ya kusimamisha nguvu ya akili yake, na kukosa lengo la maisha yake na anaweza kumalizikia katika hali hii. Hivyo haubakii kwake utajo, na sisi tunasoma katika vitabu vya fasihi na historia kisa cha "Aliyeshikwa na ashki, akajizuia na hatimaye akafariki." Katika kisa hicho kuna mchanganyiko wa uongo wa wasimulizi wa visa kwa kueleza visa vya uongo. Lakini muhtasari wake unatoa habari juu ya kwamba kuna mtu au watu hawafuati uhalisia katika kutatua tatizo la moyo hadi jambo lake linamalizikia katika kubomoa maisha yake.

[61] *Wasailu Shia*, Juz. 7, uk. 76.

Na sisi tunakuta hali hii imeenea kwa kiasi kikubwa katika safu za vijana na mabarobaro wa kiume na wa kike ambao hawawezi na wakati mwingine hawajaribu kudhibiti hisia zao na hivyo huchagua njia ya dhana na kukimbia kukabiliana na matatizo halisi katika njia nyingine. Na uchaguzi huu hauzidishi isipokuwa ukali wa tatizo.

Tunapoangalia jinsi Uislamu ulivyoamiliana na kadhia hii, hususan kupitia riwaya za Ahlul-Bayt عليهم السلام tunakuta kwamba wao walikuwa wanakwenda mbio kwa ajili ya kuepusha mas'ala haya kadiri iwezekanavyo, na kuyatatua kupitia uhalisia, kwa kujua kwamba kama yataepushwa na makadirio ya uongo yaliyoongezwa na yakabakia katika mipaka yake halisi inawezekana kuyatatua bila ya ugumu. Na dalili dhahiri katika hilo ni ambayo tunayakuta katika uhalisia wa nje, ambapo hapatikani kijana aliyebaleghe isipokuwa anatarajia kuwa ni mwenye kupenda, mwenye huzuni, mwenye tahayari katika ulimwengu wa mawazo, kwa kuangalia kufunguka hisia zake za kijinsia, na kumwekekeza kwenye jinsia nyingine, sawa iwe katika sura maalumu na finyu au katika sura ya jumla. Isipokuwa wengi wanaamiliana pamoja na mas'ala haya kwa uhalisia na kumalizika, na baadhi wanabakia katika tatizo hili hadi linawafikisha katika mauti yao, na cha kwanza tunachokabiliana nacho katika habari hizi ni:

## Kupinga kukokotwa na matamanio:

Hakika sisi tunapoangalia katika hadithi ambazo zimezungumzia nyanja hii tunazikuta zinazungumzia juu ya athari za kupenda na matamanio ambayo yanamfanya mwanadamu asifikiri kwa njia nzuri, tukiachilia mbali mwenye kung'ang'ania na matamanio yake na hawaa zake, ambayo ni katika matokeo ya kawaida ya aina hii ya mapenzi ya ubabe, hakika yanampokonya mwenye kuwa nayo uzani wa uwiano katika kupima mambo.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 81 11/23/2016 12:37:30 PM

Na wakati mwingine zinazungumzia juu ya upuuzi wa kazi hii, wakati ambapo inapasa mtu aelekeze mazingatio yake, hima yake na mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye amemneemesha kwa aina za neema. Na katika daraja ya pili ni kwa wenye neema juu yake, kama vile wazazi wake, na watu wa nyumba yake. Anakabiliana na yote hayo hadi kumalizikia mambo katika matamanio na kutukuza jinsi, na laiti angefuata njia halisi, ambayo wanaifuata watu wote. Kutoka kwa al-Mufadhal amesema: "Nilimuuliza Abu Abdillahi عليه السلام juu ya kupenda akasema: 'Ni nyoyo zilizoepukana na utajo wa Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu akazionjesha mapenzi ya mwingine asiyekuwa Yeye.'"[62]

Na kutoka kwa Imamu Musa bin Ja'far, kutoka kwa baba zake عليهم السلام amesema: "Amesema Nabii صلى الله عليه وآله وسلم: 'Hakika ninachokiogopa zaidi kwa ummah wangu baada yangu ni haya machumo ya haramu, matamanio yaliyofichikana na riba.'"[63] Kutoka kwa Imamu Ali bin Musa Ridha عليه السلام, kutoka kwa baba zake amesema: "Amesema Nabii صلى الله عليه وآله وسلم: 'Jikingeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kupenda huzuni.'"[64]

Na riwaya nyingi zimezungumzia juu ya athari ya kupenda vitu juu ya uwezo wa akili ya mwanadamu, ambapo njia ya kwanza inajumuisha hawaa na matamanio. Kutoka kwa Amirul-Mu'minina عليه السلام: "Mwenye kupenda kitu anapofusha macho yake na anatia ugonjwa moyo wake, kwani anaangalia kwa jicho lisilo sahihi, na anasikia kwa sikio lisilosikia. Matamanio yake yamekwishavuka akili yake, na dunia imekwishafisha moyo wake." Na anahadharisha kutokana na matokeo yenye kuangamiza yanayofuatia kwa kutoa fursa kwa matamanio katika maisha ya mwanadamu, anasema: "Hakika wewe kama utatii matamanio yako yatakutia uziwi na yatakupofusha na

---

[62] *Biharul-An'war* Juz. 70. uk. 158, na wamekwishafasiri mapenzi ya huzuni na matamanio yaliyojificha kuwa ni shauku.

[63] Rejea iliyotangulia.

[64] *Nahjul-Balaghah*, Hotuba ya 109.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 82 11/23/2016 12:37:30 PM

kuharibu hatima yako na kukurudisha nyuma."[65] Bali hakika: "Matamanio ni mshirika wa upofu."[66]

Na cha ajabu hakika sisi pamoja na kuangalia kwetu hadithi za kupenda wanawake, nayo ni katika sifa za Manabii, Maimamu na waumini isipokuwa sisi hatupati maelezo ya aina moja juu ya kupenda wanawake, na ambalo linadhihirika ni kwamba kuna istilahi tatu, na kila istilahi inawakilisha aina maalum katika uhusiano pamoja na wanawake: Mapenzi, kupenda na jimai.

Ya kwanza imezama katika upuuzi na ya mwisho imezama katika kiwiliwili, na ya katikati inakusanya baina ya hayo mawili, wakati ambapo haupati maelezo ya istilahi ya kwanza katika maneno ya Maasumini عليهم السلام unakuta istilahi ya pili kwa wingi, na ya tatu wakati mwingine kwa sababu ambayo tutaizungumzia baadaye. Na hebu tuelezee baadhi ya hadithi katika nyanja hii kisha tuangalie kwa mtazamo wa udadisi:

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: "Sipendi katika dunia yenu isipokuwa wanawake na manukato." Na kutoka kwake vilevile: "Nimejaaliwa kiburudisho cha macho yangu ni Swala na kupenda wanawake." Na kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Miongoni mwa tabia njema za Manabii ni kupenda wanawake." Na kutoka kwake vilevile عليه السلام: "Sidhani kama mtu atazidisha katika imani kheri isipokuwa atazidi kupenda wanawake."[67] Na kutoka kwake عليه السلام vilevile: "Mja kila anapozidi kupenda wanawake anazidi kupata ubora katika imani."[68]

## Hadithi Hizi Zinamaanisha Nini?

Mwanzo inapasa kuashiria kwamba huku kupenda wanawake haimaanishi kuchupa na kufurutu kawaida, ambapo hakika hilo liko nje ya

[65] *Mizanul-Hikima*.
[66] Rejea iliyotangulia.
[67] *Wasailu Shia* 7.
[68] *Makarimul-Akhilaq* 197.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 83 11/23/2016 12:37:30 PM

ushahidi wa riwaya hizi, kwa sababu kufurutu ada na kawaida hakupendezi kabisa hata katika ibada,[69] bali riwaya zinaweza kubeba lawama ya kupenda wanawanake, hali inayojulikana kama upanga wa shetani, na kwamba ni katika mambo ambayo humo ameasiwa Mwenyezi Mungu.

Ama maana ya upendo, hii inaweza kuwa kwa maana ya kupenda wanawake kwa jumla, mkabala wa chuki ya Waarabu kwao, na kuwadhalilisha kabla ya Uislamu. Na hapa inafasiriwa na baadhi ya hadithi ambazo zinausia kuwahurumia wanawake, na kuwafanyia upole kwa udhaifu wao, kwani hadhi ya mwanamke katika zama za kabla ya Uislamu ilikuwa ni kuzikwa hai, na hali iliyo afadhali kwake ilikuwa ni kuonekana nuksi kwa wazazi wawili kwa ujio wake, kama Qur'ani isemavyo:

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ بِالْأُنْثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ
يَتَوَارَىٰ مِنَ الْقَوْمِ مِنْ سُوءِ مَا بُشِّرَ بِهِ ۚ أَيُمْسِكُهُ عَلَىٰ هُونٍ أَمْ يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ

**"Na mmoja wao akibashiriwa msichana uso wake unasawajika naye amejaa chuki. Anajificha na watu kwa ubaya wa aliyobashiriwa. Je akae naye juu ya fedheha au amfukie mchangani….."**
**(Sura Nahli; 16:58 – 59).**

Hivyo alipokuja Mtume ﷺ akibeba pamoja naye mafunzo ya ujumbe. Ilikuwa kati ya mambo ya awali ambayo aliyafanya, ni kwamba alimrejeshea mwanamke thamani yake na akawausia Waislamu kuwapenda na kuwahurumia. Naye anausia maradufu kwa yatima na mwanamke, ambapo mwanamke ni mtu laini na sio mtu wa ubabe. Na maana hii ingawa nayo pia ni sahihi na inaungwa mkono na yaliyopokewa katika riwaya katika kuwahurumia wanawake, isipokuwa mtiririko wa hadithi za kupenda wanawake na yaliyopo katika maana yake hayaungi mkono juu yake.

[69] *Kitabu Nikaahi* katika Mausuatu ya Ayatullahi Shiraziy Juz. 1, uk. 16.

Na maana ya pili: Ambayo inakaribia ni ule uhusiano ambao ameuumba Mwenyezi Mungu Mtukufu na akauweka kwa mwanadamu: Wanaume kwa wanawake[70] na kinyume chake, uhusiano huo ambao unaanza kwa kupenda na kumalizikia kwa matamanio.

Upendo huu wenye nguvu ni jambo la kawaida, watu walio sawa wanaukuta katika maisha yao, na wala hawaupingi isipokuwa wenye kiburi. Umeumbwa pamoja na mwanadamu na unaendelea kuwa naye hadi azeeke na kukoma kufanya kazi. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu ameumba uzuri, amemuumba mwanadamu katika kupenda uzuri na kushikamana nao. Bali imekuwa ni tabia ya wanadamu katika nyanja zao mbalimbali kuamiliana na ukweli huu ulio wazi na kumzingatia mwenye kuupuuza kwamba yuko nje ya kawaida ya kibinadamu.

Na yaliyopokewa ya kwamba Nabii wa Mwenyezi Mungu Isa na Yahya عليهما السلام hawakuoa na kwamba Yahya amesifiwa kwamba ni kapera, hiyo ni kwa ajili ya kuwa kwao ni wenye kufukuzwa na utawala wa kiyahudi na maisha ya ndoa kwa kawaida yanahitajia utulivu, na yanakinzana na maisha ya kufukuzwa na kutishwa. Kisha inafahamika kwamba mwenye kuibana nafsi yake na kutokuoa kwa ajili ya jambo muhimu zaidi, hakuna shaka anakuwa ni mwenye kusifiwa kwa kitendo hicho.[71]

Na maana hii huenda hadithi zinaelekeza kuwa ndoa na kuoa ni jambo la kimaumbile, kwa kujengea juu ya kwamba maumbile yanaashiria kwenye upande wa uumbaji na utengenezaji.[72] Na kati

---

[70] Makusudio ya Hadithi: Katika mwanzo wa kuumba ambapo Mwenyezi Mungu amemuumba Adamu na akamuumba Hawa na akamuwekea matamanio na akamuoza Hawa kwake. *Wasailu Shia*, Juz. 7.

[71] *Kitabu Nikaahi* Juz. 1, uk. 8.

[72] Maumbile ya Mwenyezi Mungu: Ni kuleta kitu na kukianzisha kwake katika umbo kwa kupendekeza kitendo kati ya vitendo akasema (Maumbile ya Mwenyezi Mungu ambayo



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 85 11/23/2016 12:37:31 PM

ya yanayounga mkono rai hii, ni hadithi zenye uwazi zaidi ambazo zinazungumzia juu ya kupenda utamu[73] na kwamba ni katika tabia ya Manabii na sifa zao, na kisha waumini ni wengi wa wanawake.

Kutoka kwa Imamu Ridha (a.s) amesema: "Mambo matatu ni katika Sunnah za Mitume: Manukato, kuchana nywele na wingi wa wanawake." Kutoka kwake (a.s) amesema: "Katika jogoo mweupe kuna sifa tano kati ya sifa za Manabii (a.s): Kujua kwake wakati wa swala, ghera, ukarimu, ushujaa, na wingi wa wanawake."[74]

Ama namna gani Maasumini (a.s) wanazungumza kwa uwazi huu juu ya kadhia, lakini tunaamiliana pamoja nayo kwa kawaida kwa wingi wa aibu na haya? Hakika jambo linaonekana ni gumu kulibeba kwa baadhi, hususan wale wenye kujitakasa, ambao wanawatazama Maasumini (a.s) kinyume na hali yao ilivyo. Na tutakuta kwamba Maasumini (a.s) walikuwa wako wazi sana katika yanayohusiana na mas'ala haya kama ilivyo katika mas'ala mengine, sawa iwe katika mazungumzo juu ya asili au katika ufafanuzi.

Kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s) amesema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alimuona mwanamke akamvutia akaingia kwa Ummu Salama, na ilikuwa ni zamu yake akamwingilia na akatoka kwa watu na kichwa chake kinadondoka maji, akasema: 'Enyi watu hakika kuangalia kunatoka na shetani, atakayepata katika hilo jambo basi na amwendee mke wake.'"[75]

---

amewaumbia watu juu yake) ishara itokayo kwake (swt) kwa ambayo ameumba, yaani ameanzisha na akasisitiza kwa watu miongoni mwa kumjua Mwenyezi Mungu. *Mufuradati Raaghibu*: 3820,

[73] Raghibu amegawa katika Mufuradaati wake matumizi ya (*al-hubu*) katika aya katika migawanyo, kwanza ni kupenda ladha nayo ni mwanaume kumpenda mwanamke.

[74] *Wasailu Shia*, Juz. 7, uk. 179.

[75] Baadhi ya Maulamaa wameidhoofisha sanadi ya riwaya iliyotajwa, na ambacho kinanidhihirikia mimi ni kwamba kudhoofisha huku kumetokana na uelewa wa hoja kuwa hoja yake ni ya dhahiri haiafikiani na yale ambayo tunayaitakidi katika hadhi ya Mtume (s.a.w.w).



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 86 11/23/2016 12:37:31 PM

Na mfano wa hayo ni ambayo yananukuliwa kutoka kwa Amir-ul-Mu'minin عليه السلام, alikuwa amekaa pamoja na wafuasi wake anazungumza nao, akapita mwanamke mzuri kwa watu, watu wakamwangalia na akawazuia kusikiliza mazungumzo ya Imamu, akasema عليه السلام: "Hakika macho ya mafahali hawa yana tamaa, na hakika hilo linasababisha mchemko wake, basi anapoangalia mmoja wenu mwanamke akamvutia, basi na amwendee mke wake. Hakika yeye ni mwanamke kama mke wake.'"[76]

Na tunakuta katika hadithi zao عليهم السلام maelezo "Nilimwingilia jana" na mfano wake. Na wao wanazungumza juu ya huu uhusiano maalumu, na katika ufafanuzi ni kwamba wakati Mtume صلى الله عليه وآله وسلم anapotuma mposaji kuposa kwa ajili yake, hajizuii kujizuia kwa mfano wa wenye kujitakasa au kujizuia kwa wenye kujinyima bali anasema nusa shingo yake. Shingo yake ikiwa nzuri basi harufu yake itakuwa nzuri, na tazama kongo zake, kama kongo zake zimejaa basi magoti yake yatakuwa makubwa, yaani maungo yake yatakuwa ni mapana."[77]

**Moja ya njia za kujifunza hukumu za kidini:**

Ni wazi kwamba Maasumini عليهم السلام wanabeba jukumu la kufikisha hukumu na maarifa ya kidini katika mambo mbalimbali ya maisha ya mtu binafsi na ya watu wote. Na ilipokuwa mambo ya ndoa na jinsia ni miongoni mwa yaliyomo ndani ya duara lililopuuzwa, kwa sababu nyanja yake ni nyumba na maisha maalumu ambayo mara nyingi zinafichikana sehemu zake kwa kuzingatia kuwa ni mambo ya haya na aibu, wanaogopa watu kuyaulizia, kwa hiyo ilikuwa ni jukumu la Maasumini عليهم السلام kufanya baadhi ya vitendo, kama ilivyo katika hadithi ya kwanza. Inaweza isiwe ndio makusudio hasa, ambapo

[76] *Nahjul-Balaghah*, Hekima ya 420.
[77] *Al-Wasaili*, Juz. 7, uk. 36.

tungali tunaitakidi umaasumu wa Mtume ﷺ na ukamilifu wake, hivyo haiwezekani kufikiria pamoja na hayo, kutokea mchemko wa kijinsia kwake kwa kumwangalia tu mwanamke mzuri, jambo ambalo halitokei kwa asiyekuwa Mtume ﷺ miongoni mwa waumini wa kawaida, sasa itakuwaje kwake ﷺ. Hakika hadithi hii inafasiriwa na ya baada yake kwamba makusudio ya Mtume yalikuwa ni kuwaelekeza Maswahaba wake sawa kabisa na alivyofanya Amirul-Mu'minin عليه السلام, na hivyo tunakuta kusudio la hadithi mbili ni moja.

**Kudhihirisha upande wa kibinadamu wa Maasumini:**

Kudhihirisha upande wa kibinadamu wa Maasumini عليهم السلام ni muhimu, kwa kuondoa ufurutu ada na itikadi potovu ambayo inawezekana kuwa umejengeka kwa baadhi ya wafuasi wasio na uelewa sahihi katika kudhihirisha upande huu unaozama katika ubinadamu, na yanayofungamana nao miongoni mwa matamanio na ladha ya kuoa n.k, bila hivyo watakuwa wanasimama katika kudhihirisha mwelekeo huo wa kimakosa na wa kuchupa mipaka katika kufahamu ukweli wao.

**Kushutumu mkanganyiko na unafiki:**

Kushutumu mkanganyiko na unafiki wanaoufanya wale wanaodai kujinyima na wanaodhihirisha kujitakasa. Kama wanavyodhihirisha kujinyima katika mavazi na chakula watu waongo, vilevile wamepatikana watu waliodai kujitakasa na kuacha wanawake, na kuwa mbali na jinsia, kwa madai yao kwamba hayo yanawakaribisha kwa Mwenyezi Mungu na kwamba wao wanatafuta fadhila kwa hilo. Na kumepatikana miongoni mwa hawa, wakweli wenye kukosea, kama ambavyo walipatikana waongo wenye kukusudia kwa nje, wanaojitakasa na wanajizuia kufanya halali, wakati ambapo katika uhalisia



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 88 11/23/2016 12:37:31 PM

wa jambo lao wanafanya haramu. Na huenda katika kisa cha mchamungu wa Bani Israili kuna mfano ulio wazi kuhusu hili. Na katika visa vya wanaodai usufi na kupetuka kwao katika jinsia ni miongoni mwa yanayotilia mkazo ukweli huu.

**Ubainifu wa ukamilisho wa kidini:**

Inawezekana mtu kuwa katika daraja za juu za kumkurubia Mwenyezi Mungu na kumtii, lakini pamoja na hivyo anaburudika na mazuri katika maisha ya kidunia kati ya aliyohalalishiwa. Na hii ndio sifa ya kidini ya Kiislamu. Na huenda tunayoyaona katika ghadhabu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ miongoni mwa wale ambao walitaka utawa hakika ilikuwa ni kwa ajili ya kosa lao katika kufahamu ukamilisho wa kidini, na kutumia mfano wa kimakosa wa wanadamu wenye dini mfano watawa wenye kujitenga, kwa sababu hiyo amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa kubainisha hali yake, naye ndio mbora wa viumbe vya Mwenyezi Mungu na aliye karibu mno naye, katika kula kwake chakula na kuwaendea wanawake, na kisha kutahadharisha kwamba mwenye kukhalifu mfumo huu atakuwa nje ya sunnah yake na njia yake, katika kumwambia Uthman bin Madh'un:

"Ewe Uthman hajanituma Mwenyezi Mungu kwa utawa, lakini amenituma kwa unyoofu mwepesi rahisi, nafunga, naswali na namwendea mke wangu. Anayependa dini yangu, basi na afuate sunnah yangu, na miongoni mwa sunnah yangu ni kuoa."[78]

# HIYARI ZILIZOPO:

Uislamu unapomwelekeza mtu katika uhalisia katika uhusiano wake pamoja na jinsia nyingine unaweka mbele yake utatuzi unaoweze-

---
[78] *Safinatul-Bihar*, Juz. 2, uk. 611.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 89 11/23/2016 12:37:31 PM

kana mara nyingi, kisha unamtaka kushikamana na kanuni na kutovuka mpaka. Na jambo hili ni moja ya sifa ya sharia hii nzuri wakati ambapo baadhi ya madhehebu yanafanya kazi katika njia:

"Alimtupia baharini huku amekunja mikono na akamwambia,

Tahadhari, tahadhari usilowe kwa maji."

Uislamu unafanya kazi kwa kutayarisha hiyari nyingi mbele ya mtu na kumsaidia katika baadhi yake, kwani mwanzo unamuonyesha njia ya kushikamana nayo na kushinda matamanio kupitia kuzipa nguvu pande za kiroho na kudhoofisha mwili na matamanio yake kwa funga.

Alikuja mtu kwa Nabii ﷺ akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, sina wasaa (uwezo wa kimali) wa kuoa mke, nashtakia kwako ukapera, akasema ﷺ: "Tayarisha hisia za mwili wako na dumisha Swaumu." Akafanya hivyo na akaondokewa na aliyokuwa nayo miongoni mwa matamanio.[79]

Na kutoka kwake ﷺ: "Enyi vijana atakayeweza miongoni mwenu kupata mahari, basi aoe, hakika, kufanya hivyo kunasaidia kuinamisha macho zaidi na kunasitiri utupu, na asiyeweza basi adumu katika Swaumu hakika ni kinga kwake."[80]

Na kwa sababu utatuzi huu ni wa muda tu na haiwezekani kama tulivyotanguliza kughafilika na upande huu milele, kwa hiyo Mtume anageukia Sunnah ya kawaida katika kutatua kadhia hii nayo ni kuoa, na anahamasisha na kutia shauku juu ya jambo hilo.

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Mwenye kutaka kukutana na Mwenyezi Mungu akiwa twahara ametakasika, basi akutane naye akiwa na mke." Na kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام:

[79] *Al-Wasailu*, Juz. 7, uk. 178.
[80] *Makarimul-Akhlaq*, uk. 197.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 90 11/23/2016 12:37:31 PM

"Oeni! Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema: 'Mwenye kutaka kufuata sunnah yangu basi naajue hakika katika sunnah yangu ni kuoa.'"

Na kutoka kwake ﷺ: "Mwenye kuoa amehifadhi nusu ya dini yake, basi naamuogope Mwenyezi Mungu katika nusu nyingine." Na kwa kiasi kile kile alichohamasisha na kupendekeza kuoa alichukia pia ukapera, akasema: "Rakaa mbili anazoziswali mwenye kuoa ni bora kuliko rakaa sabini anazoziswali kapera." Na kwa kuangalia ukapera kuwa ni kama aina iliyo karibu zaidi na maasi, hususan katika yanayohusiana na mas'ala ya jinsia, na kwa hiyo imekuwa: "Wengi wa watu wa motoni ni makapera."

Bali hakika wanandoa wao ni sehemu muhimu sana inayotegemewa na Uislamu kama msingi wa kujenga jamii, na ndio nguvu ya familia, na kwa lengo hili Uislamu unalingania kupunguza vikwazo na kurahisisha mambo katika ndoa, na unaona kwamba katika baraka ya mwanamke ni uchache wa mahari, na wanawake bora ni wale wenye mahari chache. Na unaona hakika kutia ugumu katika mambo haya kunapelekea kuchelewesha kuoa, na humo kuna fitina na ufisadi mkubwa.

Na ilipokuwa jambo hili kwa nafasi yake sio jepesi kwa watu wote, ambapo katika uhalisia inapasa kuangalia mazingira ya vijana kwa mazingatio. Kuna mwanafunzi huyu ambaye anakaribia kutopata matumizi ya masomo yake ila baada ya taabu na adha, ni namna gani anaweza kupata mali inayohitajika kwa ajili ya gharama ya kuoa, nyumba na mengineyo? Na vyovyote tutakavyofikia katika kurahisisha, kinabakia kikwazo kingine: Kuna huyu ambaye mazingira ya masomo yake hayaruhusu kuoa, na kuna yule ambaye inalazimu kusafiri kwenda mbali kwa ajili ya kazi yake n.k.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 91 11/23/2016 12:37:31 PM

Na tunayoyasema sio makisio ya kifikira tu, bali huenda msomaji mpendwa, ni mmoja kati ya tunaowazungumzia, au anajua kati ya marafiki zake wengi yule anayeguswa na mazingira haya. Na kwa sababu funga si kingine isipokuwa ni utatuzi wa muda na wala wote hawauwezi, kama ambavyo athari yake inabaki katika duara la wenye kujilazimisha sana. Kwa hiyo hakika mas'ala ya Mut'ah (ndoa ya muda) yanaleta athari inayotakiwa katika utatuzi wa tatizo la jinsia kwa idadi kubwa miongoni mwa vijana.

Kutoka kwa Jabir bin Abdillahi, amesema kwamba hakika wao walikwenda vitani pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, basi akawahalalishia Muta na hakuwaharamishia, na Ali عليه السلام alikuwa anasema: "Kama asingenitangulia kwayo Ibn Khattabi (Umar) asingezini isipokuwa muovu." Na kutoka kwa Abu Ja'far al-Baqir عليه السلام amesema: "Mut'ah imeteremka katika Aya hii:

فَمَا اسْتَمْتَعْتُم بِهِ مِنْهُنَّ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيضَةً ۚ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَاضَيْتُم بِهِ مِن بَعْدِ الْفَرِيضَةِ ۚ

**'Ambao mmestarehe nao katika wao, basi wapeni mahari yao yaliyo lazimu. Wala si vibaya kwenu katika yale mliyoridhiana baada ya (kutoa) kile kilichowalazimu.' (Sura Nisaa: 24), hakuna ubaya kuongeza muda unapomalizika baina yao. Atasema: Nimekuhalalishia kwa muda mwingine kwa ridhaa yangu. Na wala hawi halali kwa mwinginewe hadi eda yake imalizike."[81]**

Na kutoka kwa al-Mufadhal bin Umar katika hadithi ndefu, ni kwamba alimuuliza Imam as-Sadiq عليه السلام baadhi ya mas'ala hadi akamuuliza: Je, vipi kuhusu Mut'ah ewe kiongozi wangu? Akasema عليه السلام: "Ni halali kabisa na ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Wala si vibaya kwenu kuonyesha ishara ya kuwaposa wanawake

[81] *Biharul-An'war*, Juz. 100, uk. 314.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 92 11/23/2016 12:37:31 PM

au kutia azma katika nyoyo zenu Mwenyezi Mungu anajua kwamba mtawakumbuka. Lakini msifanye nao ahadi kwa siri; isipokuwa mseme maneno yaliyoruhusiwa na sharia.' Yaani iwe na mashahidi. Na maneno yaliyoruhusiwa na sharia ni yaliyo mashuhuri kwa walii na mashahidi, na imehitajia walii na mashahidi katika nikahi ili kizazi kithibitike na astahiki mirathi. Na kauli ya Mwenyezi Mungu: 'Wapeni wanawake mahari yao, ni zawadi kama wakiwafanyia kitu kizuri basi kuleni kwa uzuri na furaha.'"[82]

Na kutoka kwa al-Fatihu bin Yazid amesema: Nilimuuliza Abu Hasan عليه السلام juu ya Mut'ah, akasema: "Ni halali mubaha kabisa, kama Mwenyezi Mungu hajamtosheleza kwa kuoa basi ajisaidie kwa Mut'ah, na akijitosheleza kwa kuoa basi ni halali kwake anapokuwa mbali naye."[83]

Na katika neno la Amirul-Mu'minin عليه السلام linaloashiria kwamba kama sio kuharamishwa Mut'ah na khalifa Umar bin al-Khatabi asingezini isipokuwa muovu, kuna maarifa kamili juu ya haja za watu na tabia ya uchaguzi wa mwanadamu wakati zinapofungwa mbele yake njia za halali, na huenda ambayo tunayakuta leo katika jamii zetu za Kiislamu – na katika jamii nyinginezo – ikiwa ni pamoja na kuenea ufisadi na uhusiano ulioharamishwa, kiasi kwamba inakuwa ni kanuni kwa vijana wengi, bila shaka yanaunga mkono neno la Amirul-Mu'minin عليه السلام.

Na ndoa ya muda ina masharti yake na nguzo zake zinazoifanya kuwa katika daraja lile lile la ndoa ya daima kwa kuondoa baadhi ya athari. Na katika hiyari hizi ambazo tumezitoa, Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wanabainisha hukumu zake za kisharia katika upande mmoja, na wanasaidia kadri iwezekanavyo katika kuzitekeleza, na inakuwa ni sehemu ya matumizi ya Khumsi na haki za kisharia kumuozesha asiyekuwa na uwezo.

82 *Biharul-An'war*, Juz. 100, uk. 304.
83 *Al-Wasail*, Juz. 14, uk. 450.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 93 11/23/2016 12:37:31 PM

Kutoka kwa Ibn Qudahi, kutoka kwa Abu Abdillahi عليه السلام amesema:

"Alikuja mtu kwa baba yangu (al-Baqir) akamwambia: 'Je, una mke?' Akasema: 'Hapana.' Baba yangu akasema: 'Sipendi mimi kuwa na dunia na yaliyomo, kuliko mimi kulala usiku mmoja hali ya kuwa sina mke.' Kisha akasema: 'Rakaa mbili anazoziswali mwenye kuoa ni bora zaidi kuliko mtu asiyeoa kusimama usiku kucha na kufunga mchana wake.' Kisha baba yangu akampa dinari saba na akamwambia: 'Oa kwazo.'"[84]

Na vilevile tunakuta mmoja wa wafuasi wa Imamu al-Kadhim عليه السلام alikuwa ameazimia kufanya Mut'ah na mwanamke, na kwa kuwa hamiliki mali alibakia amekaa katika nyumba ya Imamu عليه السلام. Imamu alipojua kutoka kwake hilo akampa mali na akamruhusu kuolea Mut'ah kwazo.[85]

**Kutukuza Jengo na Kurahisisha Ufafanuzi:**

Katika hadithi za Ahlul-Bayt عليهم السلام tunakuta nadharia ya kuoa inakamilika kwa kutukuza jengo la ndoa na kujenga familia kama asili, na kurahisisha utukufu na namna, wakati ambapo watu wengi wanafanya kinyume cha nadharia hii kabisa. Wao wanazidisha katika mahari na wanapamba nje na wanatoa katika mwonekano wa kijuu juu ili watimize kwa madai yao furaha, wakati ambapo unabakia msingi na asili ni dhaifu.

Na tofauti baina ya hali mbili ni sawa na tofauti baina ya mhandisi anayejenga ghorofa na kuimarisha msingi wake na anakuwa makini sana katika kuchagua vifaa, na anachimba ardhi kwa kina kizuri kwa ajili ya kuimarisha nguzo, na anazingatia mambo haya kuliko

---

[84] *Kitabu Nikahi Min Fiqhi* cha Ayatullahi Shiraziy – Juzuu ya kwanza uk. 7.

[85] *Biharul-An'war*, Juz. 48, uk. 62.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 94 11/23/2016 12:37:31 PM

anavyozingatia rangi ya jengo, na katika kupamba dari. Na mwingine anaweka nguzo atakavyo na wala hajali kiwango kinachotakiwa katika vifaa vya jengo, bali anatumia mali baada ya kukamilisha jengo katika kuchagua milango mizuri na kuchagua rangi nzuri zaidi na samani za ghali zaidi.

Hakika la pili linakabiliwa na kuporomoka kabisa, wakati ambapo la kwanza pengine linakosa baadhi ya vikamilisho, lakini mtu anaweza kuishi katika jengo hilo kwa miaka mingi. Na kwa sababu hii sisi tunakuta kwamba ndoa inageuka kuwa ni tatizo kati ya matatizo makubwa kwa baadhi, na ikitimia basi inazingatiwa kuwa ni mwanzo wa matatizo mengine. Mpigana jihadi mwanaharakati anahisi kibano cha maisha ya ndoa, hivyo analazimika kupunguza kazi yake, na wakati mwingine kuacha! Na mfanyakazi anahisi mzigo wa gharama za kimali katika ndoa yake mwanzoni na inaendelea hali hiyo, wakati ambapo anasikia kwamba ndoa inaleta riziki!

Vivyo hivyo sisi hatuwezi mbele ya hali hizi za uhalisia kwa nje kusadiki kwamba Mtume ﷺ kwa mfano alikuwa ameoa wake kumi na tano na alifariki akiwa na wake tisa! Na Imamu Amirul-Mu'minin عليه السلام alioa wake kumi na Imamu Hasan wanahistoria wanahitalifiana juu ya idadi ya wake zake, na kiasi ambacho kina yakini kati ya yaliyosemwa ni wake kumi, na Imamu Husein عليه السلام naye ni mwanamapinduzi mpiganaji katika ufahamu wa watu alioa wake watano, na ni vivyo hivyo kama utafiti utakavyokuja baadaye.

## Inawezekanaje Kufanya Hivyo?

Namna gani Maasumini عليهم السلام walikuwa wanaoanisha baina ya kazi zao za kidini, kijamii na kisiasa katika upande mmoja, na majukumu ya idadi hii kubwa ya wanawake kwa upande wa pili? Hakika mmoja katika wanajamii na katika wafanyakazi pia anazingatia mke



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 95 11/23/2016 12:37:31 PM

mmoja kuwa ni mzigo mkubwa kwake, na hivyo kazi yake inapungua, harakati zake zinabanwa, na sifa zake za kimaanawi kama vile ushujaa na kujitolea zinapungua kuliko alivyokuwa kabla ya kuoa, haya yote naye hajashughulishwa isipokuwa na mmoja tu, hali itakuwaje kwa Maasumini عليهم السلام?

Hakika mimi naitakidi kwamba mas'ala yanarejea katika yaliyotangulia kutajwa kwamba sisi katika jamii tumepata mtihani katika mas'ala ya ndoa kwa mambo mengi:

**Kugeuza mas'ala ya jinsia kuwa kikwazo:** Pamoja na kwamba wote watayapinga ila kwa hakika yanakuja kwa mtazamo wa kikwazo na aibu, na kwa hiyo mmoja anajidhihirisha mbele ya watu kwa asiyokuwa nayo katika upande huu, na huenda kama angeachwa na mambo yake njia yake isingekuwa ni njia hii.

**Kukuza maandalizi na masharti:** Ndoa imefungamanishwa na kuandaa kiasi kikubwa cha maandalizi ya kimali ambayo hayapatikani isipokuwa baada ya taabu kubwa, jambo ambalo linachangia kutia ugumu katika jambo, na inaturejesha katika jambo lililotangulia.

Vilevile hakika masharti ambayo anayaweka mshirika au watu wake au mazingira ya kijamii - na mengi kati yake sio sahihi kisharia – yanamwingiza mume – na mke vilevile – katika ulimwengu wa vikwazo na kutengua harakati zake na kuathiri katika maanawiya yake,  na kuona udhuru wake baada ya hayo ni kwa sababu ameoa! Wakati ambapo tunakuta ni kinyume kabisa kwa Maasumini عليهم السلام, kwani wanazungumza juu ya maudhui ya kuoa kana kwamba ni kitendo cha kawaida tu walichokimaliza jana.

Imamu as-Sajad عليه السلام anasikia kuhusu mwanamke anayevutia katika baadhi ya pande za Makkah, anatuma ujumbe kwake na anamposa kwa ajili yake, na kumuoa. Na anakuwa na kijakazi, ambaye



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 96 11/23/2016 12:37:31 PM

anamwacha huru kisha analala kwake hali ya kuwa ni mume katika hali nyepesi kabisa. Na lilikuwa ni jambo lisilokuwa na vikwazo lakini halijazoeleka kwa baadhi ya watu, na kwa sababu hiyo basi, Abdul Maliki bin Mar'wan anatuma kwake barua akimlaumu juu ya hilo, kwani kitendo hiki katika mtazamo wa Mar'wani kinashusha hadhi ya Imamu kijamii. Na yeye anamjibu kwa barua yenye kukinaisha na kushinda, hiyo tutaielezea katika kurasa zijazo. Na anazungumzia juu ya kijakazi aliyepewa zawadi: "Wakamwandaa na akalala kwake akiwa bwana harusi, na akashika mimba ya kijana huyu -Zaydi".[86] Na inanukuliwa kutoka kwa Abu Abdillahi as-Sadiq عليه السلام kwamba: "Ali bin Husein عليه السلام alikuwa anaoa ilihali anamiminika jasho, anakula na hazidishi isipokuwa kusema Alhamdulillahi Waswalallahu Alaa Muhammad Waalihi, na anamtaka Mwenyezi Mungu Mtukufu maghofira, na anasema: Hakika tumekuoa kwa masharti ya Mwenyezi Mungu."[87]

Na alipoingia mmoja wao kwa Imamu al-Baqir عليه السلام anamuona amevaa nguo zilizopambwa, na amekaa juu ya mto ambao hakuwa nao jana, basi anashangaa kwa hilo, na Imamu anamfafanulia jambo hilo kwa kusema: "Nyumba ni nyumba ya mwanamke na mimi niko katika harusi." Kisha anaongeza kumwambia kwamba ni wajibu wake ajipambe kwa ajili ya bibi harusi, kama ambavyo yeye amejipamba kwa ajili hiyo." Na alipovaa nguo zilizopakwa rangi nyekundu katika siku ya yule mwanamke walimuuliza baadhi ya wafuasi wake juu ya hilo, akajibu: "Athaqafiya amenilazimisha kuzivaa na mimi nampenda, na sisi hatuswali nazo." Na vivyo hivyo alibakia pamoja naye isipokuwa alipojua kwamba yeye anamchukia Amirul-Mu'minin, hapo alijaribu kumkinaisha, naye hakukubali, basi akamtaliki kwa sababu hataki kuweka katika shingo yake kaa

[86] *Biharul-An'war* Juz. 46, uk. 184.
[87] *Awaalimul-Ulumi/al-Imamu Ali bin al-Husein* 151.

la moto wa Jahannam, pamoja na kwamba haifichikani kwamba anampenda.[88]

Na mmoja wao anamuuliza Imamu Ridha عليه السلام kwa kusema: "Niwe fidia kwa ajili yako, umepaka hina?" Akasema: "Ndio, hakika maandalizi yanachochea wanawake kujiheshimu, na wanawake wameacha kujiheshimu kwa sababu waume zao wameacha maandalizi." Kisha akasema: "Je, inakufurahisha kumuona akiwa katika hali uliyonayo wewe, ukiwa huna maandalizi?" Akasema: "Hapana." Akasema عليه السلام: "Basi ndio hivyo." Kisha akasema: "Katika tabia za Manabii ni usafi, kufukiza manukato, kunyoa nywele na kuwa na wake wengi."

Wakati ambapo katika mukabala tunawakuta wanatia mkazo katika asili ya jengo la ndoa na dharura ya kulilinda kutokana na hatari za talaka: Kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: "Halijajengwa katika Uislamu jengo linalopendeza zaidi na tukufu zaidi kuliko ndoa."[89]Na imepokewa hadithi kutoka kwa Maimamu kwa matamko yanayofanana.

Na kutoka kwake صلى الله عليه وآله وسلم: "Jengeni ndoa na itangazeni."[90] Na kwa kiasi ambacho hadithi zimetia mkazo juu ya utukufu wa msingi wa ndoa, na kusimamisha jengo hili, zimerahisisha pia upande wa maandalizi na kusisitiza kwamba ni wajibu yasiwe ni kikwazo mbele ya kusimamisha jengo hili muhimu.

**Yamesahaulika mazingatio ya kijamii:**

Nacho ni kikwazo kwa watu ambacho hawakivuki mashujaa wenye kuruka sana! Uislamu umezingatia muumini mwanaume kuwa anafaa kwa muumini mwanamke, wakati ambapo watu kwa kawaida wanaangalia nafasi ya kijamii na kazi ambayo anayo mwenye

[88] *Biharul-An'war* Juz. 46, uk. 293.
[89] *Wasailus-Shi'ah*, Juz. 14, uk. 183.
[90] *Mizanul-Hikma*, Juz. 4, uk. 271.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 98 11/23/2016 12:37:31 PM

kutaka kuoa au kuolewa. Hivyo anakataliwa au anakubaliwa kulingana na nafasi hii aliyonayo katika familia au kazi au mengine yasiyokuwa hayo. Hakika Mtume ﷺ katika kukataa vipimo hivi alimuoza Dhiba'ah binti Zuberi bin Abdul- Mutwalib, naye ni binti wa ami yake, na ni kutoka katika nyumba tukufu zaidi kati ya nyumba za Makuraishi (Bani Hashim). Alimuoza kwa Miqdad bin al-Asiwad naye si Kuraishi, bali inapokewa kuwa alikuwa ni mtumwa, basi al-Asiwad al-Kindiy akamfanya kuwa ni mwanae na hivyo akanasibishwa kwake. Na amesema ﷺ: "Waumini baadhi yao wanafaa kwa baadhi," na akaongezea baada ya kumuoza Dhiba'ah kwa Miqidad: "Enyi watu hakika nimemuozesha binti ya Ami yangu kwa Miqidad ili kuikomboa ndoa."[91] Na imepokewa kwamba Zainul-Abidin عليه السلام alimuona mwanamke katika baadhi ya sehemu za Makkah akamposa kwa ajili yake na akamuoa na akawa kwake, na alikuwa na rafiki katika Answar akachukia kwa kumuoa kwake yule mwanamke. Akaulizia kuhusiana na mwanamke huyo, akaambiwa kwamba anatoka katika familia ya Dhil-Jadain katika Bani Shaiban, katika nyumba ya Ali aliye mtukufu kwa watu wake. Basi rafiki yule akamwendea Ali bin Husein akasema: "Mwenyezi Mungu anijaalie niwe fidia kwa ajili yako! kumuoa kwako huyu mwanamke bado kungali katika nafsi yangu, na nilisema: Ali bin Husein amemuoa mwanamke asiyejulikana kwa watu, na watu pia wanasema hivyo, sikuacha kuwa namuulizia hadi nikamjua na nikamkuta katika nyumba ya watu wa Shaiban." Imamu عليه السلام akamwambia: "Nilikuwa nakuhesabu miongoni mwa wenye rai nzuri miongoni mwa niwaonao! Hakika Mwenyezi Mungu ameleta Uislamu ukamnyanyua aliye duni na ukakamilisha upungufu, na akatukuka kwayo mtu duni, hivyo hakuna uduni kwa Mwislamu. Hakika uduni ni uduni wa Kijahiliya."

[91] Rejea iliyotangulia.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 99 11/23/2016 12:37:31 PM

**Kufurutu ada katika gharama za kimali katika mahari, zawadi na gharama za kuoa**:

Na ikawa kufurutu ada katika mazingatio ya kijamii ni moja ya vikwazo ambavyo vinazuia kusimamisha jengo la ndoa. Hakika kufurutu ada katika gharama za kimali katika mahari, zawadi na gharama za kuoa sio tu kunapelekea kuzuia wengi kuoa, bali mara nyingi kunapelekea kubomoa jengo hili baada ya kukamilika, au kulitia uzito. Uislamu umeelekeza kupunguza masharti haya. Ukaona kwamba "Mahari bora ni yale machache zaidi" na amesema Mtume ﷺ: "Punguzeni mahari, hakika mwanaume anampa mwanamke mahari nyingi hadi hilo linabakia katika nafsi yake kuwa ni fundo la uadui." - Na huenda tutakuta katika kisa kifuatacho mengi miongoni mwa maana hizo:

Kutoka kwa Abu Ja'far عليه السلام amesema: Mwanamke alikuja kwa Nabii ﷺ akamwambia: Nioe. Mtume ﷺ akasema: "Nani atamuoa huyu mwanamke?" Akasimama mwanaume akasema: Mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ niozeshe, akasema: "Utampa nini?" Akasema: Sina kitu, akasema ﷺ "Hapana." Mwanamke akarudia tena, na Mtume ﷺ akarudia maneno, na hakusimama yeyote isipokuwa yule mwanaume, kisha mwanamke akarudia, Mtume ﷺ akasema katika mara ya tatu: "Unajua chochote katika Qur'ani?" Akasema: Ndio. Akasema: "Nimeshakuozesha kwa kile unachokijua katika Qur'ani, umfundishe."

**Cha kwanza ambacho tunajifunza katika riwaya iliyotangulia:**

Cha kwanza ambacho tunajifunza katika riwaya iliyotangulia ni kwamba wengi kati ya Waislamu hawakuwa wanatia kikwazo katika mas'ala ya kuoa, na kwamba mwanamke alikuwa anaeleza shida yake halisi na anaipata bila ya kujificha chini na kufanya haramu,

na kwamba Mtume ﷺ hakukataa hilo kwake, bali alikubali maneno yake na akamuozesha. Na kama tukijaalia kwamba hili tukio lingetokea katika wakati wetu katika moja ya mikusanyiko, wote wangepinga kauli ya mwanamke na kusema: “Aibu! *Astaghafirullahi*, ni uchache wa haya ulioje?” Hadi mwisho. Pamoja na kwamba baina yake na nafsi anakubali hilo, na huenda angesimama kama alivyosimama mwanaume  aliyetaka kuoa, lakini mazingira ya jamii yamefikia katika daraja ya mkanganyiko na unafiki wa kijamii kiasi kwamba wote wanafichana yale  anayoyahisi kila mmoja kati yao.

Hakika mwanamke huyu anaeleza – ndani ya uzio wa kimaumbile na wa kawaida – kuhusu haja yake ya kuolewa bila ya kuangalia kikwazo cha kutengeneza. Kisha Mtume ﷺ hakumkatalia na wala hakumkemea kama wanavyofanya baadhi ya wanadini kwetu, ambao wanawakemea watoto wao wa kiume na wa kike kuzungumzia jambo la kuoa. Na wanazingatia mazungumzo ya mvulana katika mambo haya ni aina ya uchache wa haya. Ama mazungumzo ya binti kwamba anataka kuolewa inazingatiwa kuwa ni balaa kubwa! Na wote wanalazimika kuficha raghba zao mbele ya wazazi lakini, je, inamalizika raghba hiyo?

Vilevile hakika mwisho wa mambo ilikuwa ni kuozeshwa kwa kile anachoweza kukisoma vizuri katika Qur’ani ili amfundishe, hivi ndivyo Mtume ﷺ alijenga jengo la ndoa kwa Waislamu bila ya kujali vikwazo vya kutengeneza wala uchache wa mahari.

Na baada ya Uislamu kuamuru kurahisisha utangulizi, kupunguza masharti na kupinga vikwazo, ulijaribu kufunga njia kujitoa katika ndoa, na hiyo ni kwa kuchukia talaka ambapo imekuwa hakuna kitu kinachomchukiza Mwenyezi Mungu kuliko nyumba inayoharibika katika Uislamu kwa kufarakana, kama ambavyo hakika Mwenyezi Mungu anapenda nyumba ambayo humo kuna harusi. Hakika



08_16_Maisha_23_November_2016.indd   101		11/23/2016   12:37:31 PM

Yeye anachukia nyumba ambayo humo kuna talaka na hakuna kitu kinachomchukiza Mwenyezi Mungu kama talaka.[92]

## WAKE WENGI:

Katika yaliyotangulia tumeona namna gani mas'ala ya ndoa ni ya msingi, na kisha wake wengi kwa Maasumini عليهم السلام lilikuwa ni jambo la kawaida. Na tunayoyakuta leo katika jamii yetu miongoni mwa kugeuka ndoa kuwa ni jengo gumu, na kifungo chenye kukwaza, hakika ni matokeo ya mikono yetu na mila zetu. Na tutupie macho katika nyanja hii ya maisha yao binafsi.

Ni wazi kwamba wake wengi ni jambo linaloonekana katika maisha yao ya ndoa, sawa iwe ilikuwa kwa kuoa ndoa ya daima au kwa kuoa vijakazi waliowamiliki au kwa ndoa ya muda katika hali chache. Mtume ﷺ alioa wake kumi na watano, na aliowaingilia ni kumi na mbili miongoni mwao, na alifariki akiwa na wake tisa kama ilivyo mashuhuri.

- Ama wale ambao hakuwaingilia ni Umratu, Sanaa na Baidhwau.
- Na wanawake aliowaingilia wa kwanza wao na mbora wao ni Ummul-Muuminina Khadija binti Khuwailid, Sauda, Zam'ah, Ummu Salama, (Hindu binti Abi Ummaya), Aisha binti Abu Bakri, Hafsa binti Umar, Zainabu binti Khuzaymah binti Harithi (Ummul-Masakiin), Zainabu binti Jahshi, na Ummu Habiba (Ramla binti Abi Sufiyan), Maimuna binti al-Harithi, na Ummu Shariki (ambaye alitoa nafsi yake zawadi kwa Nabii ﷺ, Juwayriyyah binti al-Harithi al-Mustwalaqiya na Sofia binti Hayyi bin Akhitwabi.

[92] *Al-Wasaili,* Juz. 15, uk. 266.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 102 11/23/2016 12:37:31 PM

— Hawa wawili wa mwisho walikuwa ni vijakazi wa Mtume ﷺ akawaacha huru kisha akawaoa.[93] Na Maria al-Qibtwiya alikuwa kwake kwa anuani ya suria, ukiongezea na vijakazi wengine wawili.

Na Amirul-Mu'minin عليه السلام alioa wanawake saba, ukiongezea na mama wa watoto mbalimbali aliowamiliki, na ananukuu al-Huru al-Amiliy katika *Wasailus-Shia*, kwamba Imamu alimuoa ndoa ya muda mwanamke wa Bani Nahashi.[94] Ama wake zake wa kwanza wao ni Fatima Zahra عليها السلام binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Bibi mbora kuliko wanawake wote wa ulimwenguni, Ummul-Banin ambaye ni Fatima binti Hizam bin Darim al-Kilabiyyah, Khaula binti Ja'far bin Qais al-Hanafiyyah (Mama yake na Muhammad al-Hanafiyyah.[95] Na Ummu Habiba binti Rabi'ah, Laila binti Masuud Daramiyyah, Asmai binti Umais al- Khathia'miya, Ummu Said binti Uruwa bin Thaqafiyyah, na waliobaki walikuwa ni mama wa watoto wake (vijakazi).

Na Imamu Hasan عليه السلام japo kuna mengi yamesemwa juu ya wingi wa wake zake hadi baadhi yao wamesema idadi yao ni mia tatu, lakini rejea namba kwa uzuri uone kutothibiti kwake. Na aliyezua fikra hii (ya 300) ni huyu Abutalibu al-Makkiy, naye ni kati ya wanaojulikana kwa kutokuwa mwaminifu na kukosa umakinifu. Hata hivyo rai iliyo karibu zaidi inaashiria kuwa idadi yake ni 10. Wanaojulikana kati yao ni Ummu Bashir binti Abi Masuudi al-Khazariyyah, Khaula binti Mandhur al-Fazaraniyyah, Ummu Is'haq binti Twalha bin Ubaudullahi Tamimiy, Ju'dah binti al-Ashiathi bin Qais al-Kindiy (naye ndiye aliyempa sumu baadaye), Hafswa binti Ab-

[93] *Biharul-An'war*, Juz. 22, uk. 202.
[94] *Al-Wasailu*, Juz. 14
[95] Tumemhesabu katika walio huru pamoja na kwamba alikuwa ni mateka wa Bani Hanafiya kwa sababu yeye عليه السلام alimwacha huru na akamuoa baada ya kaka yake kuhudhuria ndoa.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 103 11/23/2016 12:37:31 PM

durahman bin Abu Bakri. Na wakati ambapo haikuwezekana kuwa na wake zaidi ya wanne kwa wakati mmoja, alikuwa anaacha baadhi kulingana na kuchunga hukumu hii. Ama aliowamiliki (vijakazi) hawahesabiwi katika kanuni ya wake wanne.

Imamu Husein عليه السلام alioa wanawake watano, nao ni: Shahribanu binti Yazdegerd,[96] Laila binti Abi Murrah bin Masuud Athaqafiyyah, Rababu binti Imri al-Qais al-Kalibiyyah, Ummu Is'haq binti Twalha bin Ubaydullahi Tamimiy na Ummu Ja'far[97] naye ni Qadhwaiyyah.

Ama Imamu as-Sajjad عليه السلام alioa wanawake saba, wa kwanza wao ni Ummul-Hasan binti wa Imamu Hasan عليه السلام, naye ni mama wa Imamu al-Baqir عليه السلام na sita waliobaki ni mama wa watoto wake (vijakazi).

Na Imamu al-Baqir عليه السلام yeye alioa wake wanne, na walio mashuhuri ni: Ummu Faruwah binti al-Qasim bin Muhammad bin Abu Bakri, naye ndio mama wa Imamu as-Sadiq عليه السلام, na wa pili ni Ummu Hakim (au Ummu Ali) Thaqafiyyah ambaye alimwaacha baada ya muda mfupi kama itakavyokuja, na wengine wawili ni katika mama wa watoto wake (vijakazi).

Ama Imamu as-Sadiq عليه السلام yeye alimuoa Fatima binti wa Husein bin Imamu Hasan mjukuu wa Mtume عليه السلام, na waliobakia ni mama wa watoto wake (vijakazi). Wa kwanza wao ni Hamidah al-Muswafatu mama wa Imam al-Kadhim عليه السلام. Na haijapokewa kutoka kwa Imamu al-Kadhim عليه السلام ambaye alikuwa na watoto 37 kwamba alioa, zaidi ya kuwa na mama wa watoto (vijakazi)

[96] Tumesema kwamba ni huru kwa sababu Amirul-Mu'minin عليه السلام alikuwa ameshaacha huru hisa yake na hisa ya Bani Hashim katika mateka wa Kiajemi, na Waislamu wakaacha huru baada ya hapo mateka wao, na Shahrubau akaachwa huru kisha Imamu Husein عليه السلام akamuoa. Kutoka katika *Biharu* Juz. 45, uk. 33.

[97] Imeshatangulia kwamba Ummul-Waladi (Mama Watoto) ni jina analopewa kijakazi ambaye anakuwa katika himaya ya mwanaume katika miliki ya mkono wa kuume na kumzalia, na anakuwa huru baada ya kifo cha mmiliki wake.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 104 11/23/2016 12:37:32 PM

isipokuwa ni kwamba mbora wao alikuwa ni Sakan au Takatum, mama wa Imamu Ridha عليه السلام.

Na Imamu Ridha عليه السلام alikuwa na vijakazi, akiwemo Khayzaran al-Marsiyyah kutoka katika nyumba ya Mariya al-Qibtwiya mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم, naye ndio mama wa Imamu al-Jawad عليه السلام.

Imamu al-Jawad عليه السلام alioa katika waungwana, nao ni Ummul-Fadhil binti Maamun al-Abbasiy, na miongoni mwa vijakazi ni Samaanah al-Maghribiyyah (Mmoroko) mama wa Imamu al-Hadi عليه السلام. Ama Imamu al-Hadi yeye hakuoa isipokuwa mke mmoja tu, naye ni Mama wa mtoto (kijakazi), jina lake ni Hadiythah au Saliyli, aliyemzalia Imamu al-Askariy عليه السلام na watoto wake wengine wanne.

Na ni hivyo hivyo kwa Imamu Hasan al-Askariy عليه السلام, hakuwa isipokuwa na mama wa mtoto (kijakazi), naye ni Narjis, Mama wa Imamu Mahdi عليه السلام.

Ni kipi kinachopelekea Maasumini عليهم السلام kuwa na wake wengi ambapo haondolewi katika jambo hili isipokuwa Imamu al-Hadi عليه السلام, na ambapo hali yao inavuka ada inayojulikana katika zama zetu ya idadi isiyovuka wake watatu kwa kawaida, pamoja na angalizo la kutowezekana kuoa kwa suria?

Hakika sisi tunaitakidi kwamba mas'ala yana pande tatu:

1. Upande wa kisiasa
2. Upande wa kijamii
3. Upande wa binafsi

**Katika Upande wa Kisiasa:**

Ni maarufu kwamba moja ya pande za ushirikiano wa kisiasa ulikuwa unapatikana kupitia kuoa. Na jambo hili halikuwa tu katika



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 105 11/23/2016 12:37:32 PM

upande wa Ahlul-Bayt عليهم السلام bali hakika wengi miongoni mwa watu katika zama hizo walikuwa wanaitakidi uhusiano wa kupitia kuoana na nasaba. Na ukaribu wa nasaba na uhusiano wa kuoana wakati huo ulikuwa ni uhusiano muhimu sana. Hakika mtu kuoa kutoka kabila fulani ilikuwa inazingatiwa kuwa amekuwa mmoja ya watu wa kabila lile, na anakuwa analindwa na nguvu yake na kabila linahisi kwa namna ya kawaida kwamba ni wajibu wake kumnusuru na kushirikiana pamoja naye.

Na kwa hiyo tunakuta Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ananufaika na uwiano huu, na aliweza kupitia kuoa kwake wake wengi kutoka katika makabila mbalimbali kujihakikishia upendo wa makabila hayo au kwa uchache kuzuia shari zao kwake na kwa daawa yake. Kama ambavyo alilainisha nyoyo za wengine kwa kuoa kutoka kwao, hakika kwa kumuoa kwake Safia binti Akhitwabi alifanya kundi kutoka katika watu wake miongoni mwa Mayahudi kuingia katika Uislamu. Na imeelezwa kwamba kumuoa kwake ﷺ Aisha wakati hakuwa amefikia umri wa kuolewa, kwani alikuwa ni binti wa miaka saba, na hakumwingilia ila baada ya miaka miwili na miezi kumi katika mji wa Madina, ilikuwa ni ili kumuweka baba yake (Abu Bakri) karibu na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Na wakati mwingine mambo yanakuwa ni kinyume kabisa ambapo kunakuwa na maslahi ya kisiasa yanayopelekea kukubali kumuoa mwanamke asiyekuwa katika hadhi ya Maasumu. Anakubali ndoa hii kwa kuangalia maslahi hayo kama tunavyokuta katika tukio la ndoa ya Imamu al-Jawadi عليه السلام kumuoa binti wa Maamun, Ummul-Fadhil, ambapo kukataa ukwe huu ambao aliulazimisha Maamun kunahesabiwa kuwa ni msimamo mbaya, na hiyo ni kinyume na maslahi, na ni jambo lisilofichikana.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 106 11/23/2016 12:37:32 PM

Na Ahlul-Bayt عليهم السلام wanakubali ndoa hii ya kisiasa kwa kadiri yake na nafasi yake ndani ya lengo la kisiasa. Na sisi tunajua sababu ya kutozaa kutoka kwa hawa wake wa kisiasa: je ilikuwa ni kwa sababu ya ghaibu au kwa sababu ya matakwa ya Maasumini عليهم السلام, pamoja na kuwa wanawake hao walikuwa na uwezo wa kuzaa kulingana na vipimo vya dhahiri vya kuzaa? Isipokuwa sisi tunajua nafasi ya ndoa hii ya kisiasa inasimama katika mpaka maalumu, na kwamba mke huyo maadamu haijathibiti kufaa kwake kuwa mke wa Maasumu عليهم السلام hakika anabaki kando ya maisha yake ya uhalisia haya kama atanufaika kwa mazingatio ya ndoa, na tumeshaashiria katika kurasa zilizopita katika maudhui haya na hivyo hatuyarudii.

**Upande wa Kijamii:**

Katika upande huu inaonekana kwamba Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wanalenga kukuza kizazi chao kitukufu kwa kuangalia yale ambayo kitayafanya kizazi hiki miongoni mwa majukumu makubwa katika kurekebisha hali ya ummah, na pamoja na kwamba Uimamu ulikuwa umezingirwa kwa watu maalumu katika kizazi cha Imamu Husain عليه السلام isipokuwa hakika kuwepo idadi hii ya watoto ilikuwa inasaidia katika kusabambaza elimu ya Ahlul-Bayt, na katika kubeba haya majukumu ya mageuzi na mapinduzi mmoja baada ya mwingine.

Na kama tutaangalia katika idadi ya watoto wa Maimamu عليهم السلام kisha tukafuatilia nafasi yao ya kihistoria itatudhihirikia mambo yaliyotajwa. Amirul-Mu'minin عليه السلام alikuwa na watoto 27, kumi na mbili kati yao ni wanaume. Na Imam Hasan عليه السلام alikuwa na watoto 15, kumi na watatu kati yao ni wanaume, na ni maarufu kwamba watoto na wajukuu wa Imamu Hasan عليه السلام ndio walikuwa wabeba bendera ya mapinduzi ya mapambano katika historia yao. Na Imamu Husein عليه السلام alikuwa na watoto 6, wanne kati yao ni wanaume. Na Imamu as-Sajjadi عليه السلام alikuwa na watoto 15, kumi kati yao ni wanaume.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 107 11/23/2016 12:37:32 PM

Na Imamu al-Baqir عليه السلام alikuwa na watoto 7, watano kati yao ni wanaume. Na Imamu as-Sadiq عليه السلام alikuwa na watoto 10, saba kati yao ni wanaume. Na Imamu al-Kadhimu عليه السلام pamoja na kurefuka muda wa kufungwa kwake jela ila alipata watoto 37, kumi na nane kati yao ni watoto wa kiume. Na sisi tunakuta hadi leo wengi wa Massayidi wa Alawiya nasaba yao inamalizikia kwa Imamu Musa bin Ja'far al-Kadhim عليه السلام. Na Imamu Ridha عليه السلام alikuwa na watoto 6, watano kati yao ni wanaume, baada ya wapinzani wake kuwa na shaka juu ya uimamu wake, ambapo hakupata watoto wa kiume ila kwa kuchelewa kama itakavyokuja. Na Imamu al-Jawadi عليه السلام alipata watoto 5, wawili kati yao ni wanaume. Na Imamu al-Hadi عليه السلام alikuwa na watoto 5, wanne kati yao ni wanaume. Na Imamu Hasan al-Askariy عليه السلام hakupata mtoto isipokuwa Mahdi عليه السلام anayesubiriwa.

Hakika ni jambo la kawaida Ahlul-Bayt عليهم السلام kujitahidi kukuza kizazi chao na watoto wao, na hiyo ni kwa ajili ya kukabiliana na shambulio la kuwaangamiza ambalo litawapata katika mustakabali, na kwa ajili ya kufidia ambayo yanaendana pamoja na majukumu makubwa katika mapigano, mapinduzi na yale yanayofuatia miongoni mwa jela na kufukuzwa, na kwamba hakuna kati yao ila alipewa sumu au aliuliwa kwa upanga.

Na mara nyingi walikuwa wanalingania kuongeza kizazi cha waumini. Ikiwa hivyo ndivyo basi wao ndio wa kwanza kutekeleza wito huu katika nafsi zao. Kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام: "Sikumuomba Mola Wangu watoto wenye nyuso nzuri wala sikuomba watoto wenye maumbo mazuri lakini nilimuomba anipe watoto wenye kumtii Mwenyezi Mungu, wenye kumuogopa Mwenyezi Mungu ili ninapowatazama, jicho langu liburudike."[98]

Na kwa hiyo tunakuta kwamba alipofariki Fatma Zahra عليها السلام alimwambia ndugu yake Aqil, naye alikuwa anajua nasaba za Waara-

[98] *Biharul-An'war,* Juz. 101, uk. 98.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 108 11/23/2016 12:37:32 PM

bu: "Niposee mwanamke aliyezaliwa na mashujaa ili anizalie kijana atakayekuwa ni mwenye kumnusuru mtoto wangu Husein." Ndipo akamuonyesha Ummul-Banina, Fatmah binti Hizam al-Kilabiyyaa, na huyu baba zake na babu zake walikuwa ni kati ya mashujaa wa kiarabu wenye kujulikana kwa ushujaa.

Na kutoka kwa Imamu Zainul-Abidin عليه السلام amesema: "Katika furaha ya mtu ni kuwa na kizazi kitakachomsaidia." Na kutoka kwa Imamu Ridha عليه السلام amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu anapotaka kheri kwa mja hamfishi hadi amuonyesha watoto."[99] Na amepokea Isa bin Sheikh, amesema: Aliingia Hasan al-Askariy عليه السلام kwetu wakati tukiwa mahabusu, na nilikuwa namjua hapo kabla, akaniambia: "Una miaka 65," na ilikuwa kama alivyosema, kisha akasema: "Je umeruzukiwa watoto?" Nikasema: Hapana, akasema: "Eee Mwenyezi Mungu mruzuku mtoto atakayekuwa msaada kwake, hakika msaada bora ni mtoto."

Kisha akasoma beti kwa kusema: "Mwenye kuwa na msaada anadiriki alichodhulumiwa. Hakika dhalili ni yule asiye na msaada." Nikamwambia: Je, una mtoto? Akasema: "Ndio, naapa kwa Mwenyezi nitakuwa na mtoto ataijaza ardhi usawa na uadilifu. Ama kwa sasa hivi sina." Kisha akasema: "Huenda siku moja utaniona kana kwamba, watoto wangu ni wengi kama nywele nyeusi. Hakika Tamimi kabla ya kuzaa watoto wengi, alikaa muda mrefu naye akiwa mpweke baina ya watu."

Hakika kuwa na wake wengi kunatoa fursa kubwa ya kuzaa watoto wengi na uzuri wa uangalizi wao, hiyo ni kwa sababu kuzaa kwa wingi na mfululizo kwa mke mmoja kunamzeesha na hakumwezeshi kuwa na uangalizi na malezi mazuri.

[99] *Al Wasaeel,* Juz. 15, uk. 96.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 109 11/23/2016 12:37:32 PM

**Upande Binafsi:**

Imeshatangulia kuzungumzwa kwamba Maasumini عليهم السلام kwa kuzingatia upande wao wa kibinadamu, na kwamba kuoa ni katika utamu ambao ameuhalalisha Mwenyezi Mungu, bali ameuumba kwa ajili ya mawalii wake waumini katika njia ya kipaumbele ukilinganisha na watu wengine, nayo ni miongoni mwa udhihirisho wa ukweli au utamu katika yasiyokuwa haramu. Na Ahlul-Bayt عليهم السلام na wao wanaishi baina ya watu kama binadamu, wana raghaba na matamanio kama waliyonayo watu wa kawaida, kinyume na anayeona kwamba wao ni sawa na waungu au mfano wa malaika. Walikuwa wanatumia raghaba na matamanio haya katika sehemu zake zililizohalalishwa na wala hilo halidhuru utukufu wao au umuhimu wa nafasi zao, bali ni moja ya vielelezo vya utu uliotukuka kwao katika maisha yao.

## WAKE VIJAKAZI:

Kisha muonekano unaotusimamisha katika maisha ya ndoa ya Ahlul-Bayt عليهم السلام ni wanawake vijakazi au kulingana na istilahi (mama wa watoto). Hiyo ni kwa sababu sisi tunakuta kwamba wake wa Maimamu عليهم السلام, kuanzia na Imamu as-Sadiq عليه السلام, kati ya wale waliokadiriwa wawe ni mama wa Maimamu, walikuwa ni vijakazi waliomilikiwa.

Mama wa Imamu al-Kadhim عليه السلام Hamida al-Muswafatu ni kijakazi aliyenunuliwa na Imamu as-Sadiq عليه السلام, na alikuwa kwake kwa kumilikiwa na akamzalia idadi kadhaa ya watoto, mbora wao ni Imamu Musa bin Ja'far عليه السلام. Na mke wa Imamu al-Kadhim عليه السلام alikuwa ni kijakazi anayeitwa Takatum. Alimzaa Imamu Ali bin Musa Ridha عليه السلام. Na hali ni hiyo hiyo kwa Imamu Ridha عليه السلام. Alimuoa kijakazi anayeitwa Khayrazan al-Marsiyyah, akamzaa Imamu Muhammad bin Ali al-Jawadi عليه السلام, kisha Imam al-Jawadi عليه السلام alimuoa Samaana al-Maghiribiyyah, na akamzaa Imamu Ali al-Hadi عليه السلام, na



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 110 11/23/2016 12:37:32 PM

ambaye kwa nafasi yake alimuoa Saliyli au Hadithah, ambaye alimzaa Imamu Hasan al-Askari عليه السلام. Na mwisho, hakika mama wa Imamu Mahdi عليه السلام na mke wa Imamu al-Askariy عليه السلام vilevile ni kijakazi anayeitwa Narjisi. Yaani sisi tunakuta kwamba, sita katika Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wameoa vijakazi waliowamiliki kwa kuwanunua. Na jambo linaweza kuwa jepesi kama ingeishia kwa kuoa tu kwa ajili ya kujiburudisha, jambo hili wanalifanya wengi. Lakini ndoa hii kuwa ni kwa lengo la kuzaa, na kuzaliwa sita kati ya Maimamu عليهم السلام katika vizazi vya wanawake hawa ni jambo linalopelekea kujiuliza, na angalizo, hususani tunaporejea kwenye mwanzo wa sehemu hii na tukarejea katika akili na athari ya kurithi, na rai ambayo tumeichagua katika twahara wa baba za Maasumini عليهم السلام na mama zao vilevile, na kwa kuongezea katika ambayo tunayajua katika maelekezo ya Maimamu wenyewe kwa ulazima wa uchaguzi unaofaa kwa mke, hakika mjomba ni mmoja wa mahusiano ya pande mbili. Ukiongezea na mkusanyiko wa mazingatio ambayo yanaangaliwa mara nyingi katika mfano wa haya.

Haionyeshi kwamba jambo lilikuwa linatokea kwa sadifa (ghafla) na bila ya angalizo, ambapo inaweza kutokea hilo katika hali au hali mbili. Ama katika sura hii ambayo tunaiona jambo linaonyesha limekusudiwa au kwa uchache kuna uangalifu juu yake, hivyo basi ni zipi sababu zilizopo nyuma ya mwonekano huu? Tunapotafakari katika riwaya ambazo zinaelezea maudhui haya tunakuta mambo yafuatayo yanaambatana nazo:

### 1- Kuondoa mazingatio ya kimakosa katika jamii:

Hakika neno "ili kuinyanyua ndoa" linatukabili katika zaidi ya sehemu moja, nalo linabainisha falsafa ya kazi hii ambayo wanaifanya Maasumini عليهم السلام. Hiyo ni kwa sababu Uislamu ulipokuja katika jamii ya Kiarabu, jamii hii ilikuwa imekusanya mkusanyiko wa ada mbal-

imbali na mazoea kadhaa, ambayo ni kanuni zilizokuwa zikifuatwa na kuheshimiwa na jamii na kizazi baada ya kizazi. Mazoea yanayohusiana na watumwa na vijakazi, ikiwa ni pamoja na watu hao kufanyiwa dhulma na kuondoa ubinadamu wao, yalikuwa yamegeuka kuwa kanuni ambayo haivunji isipokuwa kwa yule anayesifika kwa kwenda kinyume na ada. Na tofauti zilizothibiti baina ya makabila, kwa kuwa kabila hili liko juu na lile liko chini, kupitia kujifakharisha kwa washairi, ilikuwa imegeuka kuwa ni aya zenye kutukuzwa ambazo hana shaka nazo yeyote. Na sio ajabu kukuta mtu asiye na uwezo wa kuidhibiti nafsi yake, na mwenye tabia mbaya katika mwenendo wake, lakini anabakia kuwa bora kwa sababu tu ni kutoka ukoo huu wa Makuraishi!

Uislamu ulipokuja kwa mafunzo yake matukufu ukaweka mpaka katika upande wa nadharia kwa mazingatio na mila hizi, ukaziondoa sawa iwe kwa maelekezo kuhusu usawa wa binadamu katika asili ya kuumbwa, na kwamba utumwa ni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, au kwa kuweka vipimo vipya vya ubora visivyotegemea jinsia, rangi na kabila, bali vinategemea uwezo na juhudi za binadamu mahususi kwa mtu. Isipokuwa siasa za kimakosa zilizotokea baada ya Mtume ﷺ kufariki na hasa Bani Ummayya walipokamata hatamu za utawala wa kisiasa katika ummah, zilirejesha mas'ala upya kwa kurejesha yaliyopo kwenye historia ya Ujahiliya, na mara ukazuka moto wenye mwamko mkubwa wa kasumba, huku mashairi ya mizozo na kujifakharisha ikichomoza mpaka katika kilele chake, na ikawa mila na ada hizo za kijahiliya zimerejea upya!

Ikawa Mwislamu mwenye tauhidi, mwenye uwezo, na mwenye ikhilasi kwa ajili ya kuinua neno la dini, anafukuzwa katika medani, si kwa jingine lolote isipokuwa ni kwa sababu tu ni huria au si mwarabu, hadi alisema msemaji wao kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام: "Ametushinda huyu mwanamke mwekundu dhidi yako ewe Amir-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 112 11/23/2016 12:37:32 PM

ul-Mu'minin, wafukuze!" Na hadi walizuiwa wasiokuwa Waraabu kuingia Madina! Na hadi kukawa na tabaka jipya linaloitwa huria, *al-Hamrau* na mengineyo!!

"Ilikuwa inatakiwa hawa huria katika daraja la kijamii wawe sawa na Waarabu katika nafasi, na hiyo ni kulingana na misingi ya kidemokrasia ambayo ililetwa na Uislamu na akaitangaza Mtume ﷺ katika hotuba mashuhuri ya Kuaga, nayo ndio ile misingi ambayo inafanya ubora wa watu usiwe kwa msingi wa asili au ukoo, bali ni kwa msingi wa uchamungu. Lakini ubora ni kitu kimoja na uhalisia ni kitu kingine. Zilipomalizika tu zama za Makhalifa waongofu na jamii ya Kiislamu kumwaga Ali bin Abutalibi عليه السلام ambaye inapokewa kwamba alikuwa akisema: "Hakuna ubora wa muungwana juu ya mtwana, wala mwarabu juu ya asiyekuwa mwarabu," walianza Waarabu katika zama ya Bani Ummayya kuwatazama huria kwa mtazamo wa bwana na mtumwa. Na wakawa wanaamiliana nao kwa muamala usiokuwa na upole ambao amewaamrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bali kwa muamala duni ambao unaelezewa kuwa uko mbali na moyo wa Kiislamu na ulioepukana na misingi yake mitukufu ya kibinadamu.

Walikuwa wanawaona ni jinsia duni isiyotofautiana na watumwa isipokuwa kidogo tu, au kama anavyosema Shabathi bin Rabii, mmoja wa vigogo mashuhuri vya udikteta vya huko Kufah: "Wao ni ngawira aliyowapa Mwenyezi Mungu." Na mambo yalifikia katika daraja kwamba baadhi ya Waarabu walikuwa wanaona kuswali nyuma yao si unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu. Bali mambo yalifikia kwa Shaabi Kadhi wa mji wa Kufah katika ukhalifa wa Umar bin Abdul-Azizi kueleza wazi kwamba huria waliuchukia msikiti hadi wakauacha. Wakauona ni mbaya zaidi kuliko kanisa. Na kwa sababu hii hatupatwi na mshangao wakati tunaposikia kwamba katikati ya karne ya pili kulikuwa na msikiti huko Kufah unaitwa 'Msikiti wa



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 113 11/23/2016 12:37:32 PM

Huria', ambao Khudaa Bakhish anapouelezea anaelemea kwenye dhana kwamba wao walilazimika kuswali Swala zao humo baada ya kuona kasumba za Waarabu dhidi yao. Hawakuwa wanawaruhusu wao hata kufanya ibada katika msikiti mmoja."[100]

Uislamu ulitiwa doa kwa njia ya nyuma, kiasi kwamba ikawa mwenye kujipamba kwa vazi la dini, bali mwenye kuvaa vazi la ukhalifa anaukhalifu katika kanuni ndogo kabisa za usawa. Na jibu la mageuzi haya linahitajia kitendo, ukiongezea na maelekezo, kama alivyofanya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika suala la kumuozesha Zayd bin Harithi, aliyekuwa huria wake kwa Zainab binti Jahshi mtoto wa shangazi yake, na Zayd alikuwa ni kijana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na huria wake, wakati ambapo Zainab binti Jahshi alikuwa ameshapata utukufu wa kifamilia katika pande zake, kwani yeye ni Asadiyyah kwa upande wa baba na ni Hashimiyyah katika upande wa mama. Pamoja na hivyo Mtume ﷺ alimuozesha ili kuinyanyua ndoa, yaani ili mazingatio haya ya kijamii yasiwe ni kikwazo kwa watu kiasi cha watu kukataa kuozesha kutokana na vigezo hivyo.

Na sisi tunakuta maelezo ya maana hii katika tamko ambalo limepokewa kutoka kwa Imamu as-Sajad عليه السلام. Hiyo ni kwa sababu Imamu as-Sajad aliacha huru kijakazi wake na kisha akamuoa. Na kwa kuona kwamba Khalifa wa Bani Ummayya Abdul-Maliki bin Mar'wan bado angali anaishi katika hali ya mazingatio ambayo tumeshayazungumzia, alipata fursa ya kumkosoa Imamu عليه السلام.

Kutoka kwa Zayd bin Hatimu amesema: Abdul-Maliki bin Mar'wan alikuwa na mpelelezi huko Madina anayemwandikia matukio yanayotokea humo, na kwamba Ali bin Husein عليه السلام alimwacha huru kijakazi wake kisha akamuoa. Mpelelezi akamwandikia hayo Abdul-Maliki, na Abdul-Maliki akamwandikia ujumbe Ali عليه السلام: "Ama baada, imenifikia habari ya kumuoa kwako huria wako,

---

[100] *Hayatu Shiiri Fiyl-Kufah* 169 / Dr. Yusufu Khalifa.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 114 11/23/2016 12:37:32 PM

na nimeshajua kwamba kulikuwa na anayekufaa katika Makuraishi ambaye utatukuka kwaye katika ukwe na kumzalisha watoto. Hujaangalia katika nafsi yako wala hujabakisha kwa ajili ya kizazi chako, wasalaam."

Ali bin Husein ﷺ akamwandikia kumjibu: "Ama baada, imenifikia barua yako unanikemea kwa kumuoa huria wangu na unadai kwamba kulikuwa na wanawake wa kikuraishi ambao ningeweza kutukuka kwao kwa ukwe na kunizalia watoto. Hakika hakuna mwenye daraja kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ wala mwenye kumzidi katika ukarimu. Hakika (huria) alikuwa ni katika miliki yangu, ametoka kwangu – Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaka - katika jambo ambalo kwalo nimetaka thawabu Zake, kisha nikamrejesha kwa mujibu wa Sunnah yake ﷺ. Na yeyote ambaye ni mtukufu katika dini ya Mwenyezi Mungu hapunguzi lolote katika amri Zake. Na Mwenyezi Mungu amemnyanyua kwa Uislamu yule aliyekuwa duni na amekamilisha kwake upungufu na akaondoa uduni, hivyo hakuna uduni kwa mtu Mwislamu. Hakika uduni ni uduni wa kijahiliya, wasalamu."

Aliposoma barua akamtupia mwanawe Sulaiman, naye akaisoma, akasema: "Ewe kiongozi ni utukufu ulioje aliojifakharisha kwako Ali bin Husein!" Akamwambia: "Ewe mwanangu usiseme hayo hakika ni ndimi za Bani Hashim ambazo zinapasua majabali na zinachota katika bahari yake, hakika Ali bin Husein ewe mwanangu ananyanyuka mahala ambapo wanateremka hadhi watu wengine."[101] – Tazama tofauti baina ya mantiki ya ubaguzi wa kijahiliya na mantiki ya usawa wa kiujumbe.

**2- Kuwa tayari kushikamana na Maimamu:**

Ambayo yamethibiti katika historia ni kwamba hawa vijakazi walikuwa wasafi na wameteuliwa. Imeshatangulia kwamba tumebaini-

[101] *Biharul-An'war*, Juz. 46, uk. 164.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 115 11/23/2016 12:37:32 PM

sha katika sehemu ya wake wengi, kwamba Maasumini عليهم السلام walikuwa na wake wengi kati ya vijakazi na waungwana, isipokuwa sisi tunaona kwamba kuanzia kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام wanawake wenye utukufu, wazuri na wateule kwa Maimamu walikuwa ni vijakazi pamoja na kuwepo waungwana ambao baadhi yao ni kati ya wenye utukufu wa kifamilia wenye kusifika – kulingana na vipimo vilivyoenea wakati huo – isipokuwa ni kwamba hawa vijakazi ndio ambao walikuwa ni mahususi kwa kubeba Maimamu Maasumini عليهم السلام.

Inaongezewa katika hilo kwamba ni juu yetu tuelewe vizuri maana ya vijakazi. Hakika kinachofahamika kwao kutoka kwa watu kinawakilisha maana halisi ya neno hili. Hiyo ni kwa sababu kinachofahamika katika akili kuhusu kijakazi ni wale vijakazi weusi wanaotumikishwa katika kazi na shughuli ambazo hazina heshima nzuri kwao, au wale wanawake ambao wanahama kutoka kwa mwanaume kwenda kwa mwingine kwa ajili ya starehe na jimai. Na ufahamu huu ingawa unawezekana isipokuwa ni katika upande ulioenea katika vitabu vya fasihi, sio kwamba vijakazi wote walikuwa katika aina hii, hakika sisi tunakuta wengi kati ya hawa wanawake walikuwa ni kutoka katika nyumba tukufu katika jamii zao, lakini kufuatana na mazingira ya vita na yanayojiri miongoni mwa kuteka wanawake, utekaji huu haukutofautisha baina ya wanaotoka katika nyumba tukufu na wasiokuwa hao, bali huenda wanawake wanaotoka katika nyumba tukufu kijamii walikuwa wako karibu zaidi na kutekwa na ngawira kuliko wasiokuwa wao, kwa kuangalia kuwa wanaume wa nyumba hizi walikuwa ni viongozi wa kisiasa au wa kijeshi katika jamii ambazo zilifunguliwa na Waislamu. Hivyo wanaume hawa walikuwa wanauliwa au wanashindwa katika vita hivi, wakati ambapo wake zao na mabinti zao wanachukuliwa mateka, na wanachukuliwa kama ngawira na vijakazi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 116 11/23/2016 12:37:32 PM

Na huenda sisi tunakuta katika kisa cha mabinti wawili wa Yazdegerd ukweli ulio wazi katika maana hii. Hiyo ni kwa sababu jeshi la Waislamu lilipolishinda jeshi la Kiajemi na kuiteka tawala ya Uajemi lilichukua ngawira ya vitu vingi, na miongoni mwa hayo ni wale wanawake ambao walitekwa. Na kulingana na ada inayofuatwa, hakika wao wanakuwa watumwa na wanaingia katika miliki ya Waislamu. Isipokuwa Amirul-Mu'minin عليه السلام kama ilivyotangulia, alibainisha kwamba hawa mabinti wawili ni mabinti wa Mfalme. Na kulingana na mafunzo ya Kiislamu ya kuwakirimu watu watukufu ambao zama imewafanyia hiyana,[102] aliwaacha huru wale wa fungu lake na fungu la Bani Hashim, na Waislam wakawaacha huru kufuatana na mafungu yao. Imamu عليه السلام akawapa hiyari ya kuchagua, mmoja wao akamchagua Imamu Husein عليه السلام na baadaye akawa ndio mama wa Imamu as-Sajadi عليه السلام, na alifariki siku chache baada ya kujifungua akiwa katika damu ya uzazi. Na mwingine alimchagua Muhammad bin Abu Bakr, na akamzaa Qasim bin Muhammad bin Abu Bakr. Na wanahistoria wanasema hakika watu walikuwa wanachukia kuwazalisha vijakazi kwa kuogopa kizazi chao kutokuwa safi hadi alipozaliwa Zainul-Abidin عليه السلام na Qasim bin Muhammad bin Abu Bakri. Watu wakaona kuwa wa kwanza kuwa ni mbora wa watu baada ya baba yake kwa elimu, maarifa na uchamungu, na wakaona kwa huyu wa pili mwanachuoni wa fikihi kati ya mafakihi wakubwa. Basi wakapenda kuwazalisha.

Bali pengine ikasemwa kwamba sababu za kurithiana zitakuwa katika kutumikia mtoto huyu ambaye anatokana na watu wawili, ambapo maulamaa wamethibitisha kwamba ada ni mtoto kubeba muhtasari wa mazuri na nukta za nguvu kutoka pande mbili. Na huenda Hadithi ambazo zinaelekeza kuoa nje ya familia moja na kuchagua kutoka katika familia nyingine kwa kuzingatia kuwa hali

[102] Imekuja katika Hadithi: Wakirimuni watu watatu: Tajiri aliyefilisika, mtukufu wa watu aliyedhalilika, na mwanachuoni aliyepotea baina ya majahili.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 117 11/23/2016 12:37:32 PM

hiyo inapelekea kuzaa watoto zaidi na inasaidia zaidi katika afya ya mwili, na upevu wa kiakili, huenda hadithi hizi zinajumuisha pia kuoana pamoja na watu wengine kwa muunganiko wa madhumuni, na hivyo kuunga mkono tuliyoyataja mwanzo.

Na tunaona jambo hili wazi tunapoona kwamba Maasumini miongoni mwa Ahlul-Bayt عليهم السلام ni kati ya ambao mama zao ni vijakazi na walikuwa katika daraja ya juu zaidi ya elimu na maarifa katika upande wa kiakili, uchamungu na utulivu, na katika mwenendo, bali walikuwa katika zama zao ni Maimamu kwa maana zote za neno, na wala hatuwezi kupata kwa mmoja wao kuteleza katika kauli au kosa katika kitendo. Na hii ni kwa kuongezea umaasumu ambao tunautarajia kwao عليهم السلام. Hiyo inatuongoza kwamba hakika hazikuwepo athari mbaya katika maisha yao kutokana na kurithi kutoka kwa mama zao, na hiyo ni miongoni mwa yanayoonyesha kwamba mama zao walikuwa katika kiwango cha juu katika dini na tabia njema.

Na umekwishapita utafiti wa upande huu katika utangulizi wa sehemu hii. Na tuchukue mfano mmoja naye ni Narjisi, mama wa Imamu Mahdi عليه السلام, na ni maarufu na dhahiri kwamba yeye ni kijakazi aliyenunuliwa kwa ajili ya Imamu Hasan al-Askariy عليه السلام, isipokuwa uhalisia unaonyesha kwamba alikuwa ni katika familia ya Yushua bin Nun, na kutoka katika familia kongwe na tukufu huko Roma, isipokuwa yeye alitekwa na Waislamu na akauzwa kama kijakazi.[103]

**3- Sio sharti mke kuwiana na mume:**

Kama tukiangalia katika Hadithi ambazo zinabainisha sifa za mke anayetakiwa kisharia, tungekuta kwamba hazishurutishi kuwiana mke na mume na kuwa kwake ni kutoka katika tabaka moja pamoja naye, na hili ni tawi la yaliyotangulia, na kwamba tumelisema katika kuondoa mazingatio ya kijamii. Na hii inamaanisha kuwa yal-

[103] *Biharul-An'war*, Juz. 51, uk. 6.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 118 11/23/2016 12:37:32 PM

iyosemwa kuwa wake wa Nabii ﷺ na mama wa waumini ni wanawake bora zaidi na kwamba hapakuwepo katika uso wa ardhi aliye bora kuliko wao, kama ilivyo kwa al-Fakhru Razi, hilo halijathibiti si kwa kuanza wala si kwa historia, halijathibiti hilo katika sira yao.

Na ikiwa Khadija binti Khuwaylid عليها السلام ni kati ya Mabibi wanne wa peponi  kama ilivyotangulia katika hadithi iliyotangulia, hiyo imethibiti kwa kupokewa tamko juu ya utukufu wake na haivuki kwa mwinginewe isipokuwa kwa dalili na hakuna dalili hapa. Na hii ni kwa kuongezea katika ambayo yatakuja utajo wake katika Qur'ani tukufu ya kuwatuhumu wao kwamba baadhi yao nyoyo zao zilielemea upande usio wa haki na wakasaidiana dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, na kwamba walitishiwa kupewa talaka na walitengwa kwa muda fulani. Yatakuja hayo chini ya anwani ya 'wanawake wenye kukhalifu.'

Na hadithi mashuhuri: "Muumini mwanaume anamfaa muumini mwanake," sio tu kwamba haionyeshi juu ya ulazima wa kulingana bali inaonyesha juu ya kutolingana, kwani inafuta mazingatio mengine na inaona kwamba imani yenyewe ni kigezo tosha cha kumuoa muumini mwanamke, kama ambavyo inathibitisha kufaa kwa muumini mwanaume kabla ya kuzungumza juu ya kufaa kwa muumini mwanamke.

Na hii hata kama haiko wazi kuhusu yaliyo baina ya watu wa kawaida, lakini iko wazi kuliko jua katika yanayohusiana na Manabii عليهم السلام na Mawasii. Nabii Muhammad ﷺ alioa wanawake kumi na watano, miongoni mwao ni Khadija binti Khuwaylid, isipokuwa hakuna hata mmoja miongoni mwao anayedai kuwiana kwake na Mtume ﷺ. Itawezekana vipi naye ndio kiumbe bora zaidi? Cha juu kabisa ambacho kinaweza kusemwa katika nyanja hii ni ukaribu wao na chanzo kikuu cha tabia njema. Na mwema miongoni mwao



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 119 11/23/2016 12:37:32 PM

ni mwenye kufuata nuru katika nuru yake. Ila haiwezekani kuwiana mmoja wao na Mtume ﷺ. Na hali ni hiyo hiyo kuhusiana na Maimamu عليهم السلام.[104]

Na hii huenda inafasiri maneno ya Imamu al-Hadi عليه السلام yaliyopokewa kutoka kwake: "Kama asingetuozesha ila kwa wenye kuwiana na sisi tu, basi asingetuozesha yeyote."[105] Na kwa kujengea juu ya hayo, hivyo hakuna vijakazi wala waungwana wanaowiana na Maasumini عليهم السلام, kwa sababu sisi tunaitakidi juu ya ubora wa hawa juu ya wale. Na hivyo hakuna tofauti katika kuwa mke ni kijakazi au ni muungwana kuhusiana na Ma'asumu kwa sababu wote hawawiani naye isipokuwa mwenye kuvuliwa kama ilivyotangulia haya na kwa kuongezea yaliyotangulia katika maana ambayo tumeichagua katika kuwaelezea vijakazi.

**Wanawake Waasi na Wapinzani:**

Hapa kuna muonekano mwingine anaouona mwanahistoria mwenye kufuatilia maisha ya Ahlul-Bayt عليهم السلام, nao ni kuwepo wanawake wenye kuwakhalifu katika itikadi na utamaduni. Sisi tunamuona Juudah binti al-Ash'athi mke wa Imamu Hasan عليه السلام, naye si kwamba hakuwa ni mwenye kumuafiki tu, bali hakika yeye alimpa sumu na kumuuwa kwa kukubali njama ya Muawiya bin Abu Sufiyan. Na inatosha kujua kiwango cha uasi ambacho kilikuwepo kwa huyu mwanamke kwa Imamu, kiasi kwamba alimpa sumu.

Kama ambavyo tunakuta katika maisha ya Imamu as-Sajad na Imamu al-Baqir عليهما السلام,[106] kwamba walikuwa na wake kutoka kwa

[104] Haya kwa kumuondoa Fatmah Zahra عليها السلام ambaye imepokewa kuhusiana na utukufu wake hadithi maalum ambapo imepokewa kwamba kama si Ali عليه السلام Fatima عليها السلام asingepata anayewiana naye.

[105] *BiharulAn'war*, Juz. 50, uk. 178.

[106] *Wasailu Shia*, Juz. 14, uk. 435.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 120 11/23/2016 12:37:32 PM

Shaybaniyyah na Thaqafiyyah,[107] na Imamu al-Baqir alikuwa anampenda mke wake wa Thaqafiyyah kama ilivyotangulia katika kurasa zilizotangulia, isipokuwa wao Shaybaniyyah na Thaqafiyyah walikuwa na rai ya Makhawariji, na walikuwa wanamchukia Amirul-Mu'minin عليه السلام hivyo wakawataliki. Na jambo lile lile tunalikuta katika maisha ya Imamu al-Jawadi عليه السلام ambapo Ummul-Fadhil binti al-Maamun mke wa Imamu al-Jawadi alikuwa na ghera sana kwa Ummu Ridha عليها السلام, naye ni kijakazi, na alikuwa hafichi chuki yake kwa mume wake kutoka kwa baba yake Maamun.

Na ambacho kinadhihiri ni kwamba jambo hili halikuwa mahususi tu kwa Maimamu Maasumini عليهم السلام bali lilikuwa ni balaa kwa Manabii عليهم السلام pia, ambapo sisi tunasoma katika Qur'ani Aya zinazoashiria kwenye mas'ala haya katika Sura Tahrim:

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِلَّذِينَ كَفَرُوا امْرَأَتَ نُوحٍ وَامْرَأَتَ لُوطٍ ۖ كَانَتَا تَحْتَ عَبْدَيْنِ مِنْ عِبَادِنَا صَالِحَيْنِ فَخَانَتَاهُمَا فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهُمَا مِنَ اللَّهِ شَيْئًا وَقِيلَ ادْخُلَا النَّارَ مَعَ الدَّاخِلِينَ

**"Mwenyezi Mungu amewapigia mfano waliokufuru mke wa Nuhu na mke wa Luti. Walikuwa chini ya waja Wetu wema wawili miongoni mwa waja Wetu. Lakini wakawafanyia hiyana, nao wasiwafae kitu. Na ikasemwa: Ingieni Motoni pamoja na wanaoingia."**
**(at-Tahriim; 66:10)**

Na kauli ya wakawafanyia hiyana haimaanishi hiyana ya ndoa kama ambavyo inaweza kufahamika katika akili za baadhi, hilo ni suala ambalo Mwenyezi Mungu amewaepusha Manabii wake kupata balaa kwalo katika wake zao, bali inamaanisha waliwakhalifu katika itikadi na dini. Imepokewa kwamba hiyana yao ilikuwa ni unafiki na

[107] Vilevile inapokewa kwamba Imamu Hasan عليه السلام alikuwa na mke vilevile aliyekuwa anajiepusha na Amirul-Muuimina عليه السلام akamtaliki.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 121 11/23/2016 12:37:32 PM

kuficha kwao ukafiri na kusaidia kwao dhidi ya Mitume wawili. Mke wa Nuhu aliiambia kaumu yake kwamba Nuhu ni kichaa, na mke wa Luti alikuwa akiwafahamisha kuwasili kwa mgeni Ibrahim, na wala haijuzu hiyana yao kuwa ni katika kufanya uchafu. Kutoka kwa Ibn Abbasi: "Hakika hajafanya zinaa mke wa Nabii katu, na imesemwa hiyana yao ni katika dini.[108] Na vile vile inayoyaashiria Aya tukufu katika Sura Tahrim:

وَإِذْ أَسَرَّ النَّبِيُّ إِلَىٰ بَعْضِ أَزْوَاجِهِ حَدِيثًا فَلَمَّا نَبَّأَتْ بِهِ وَأَظْهَرَهُ اللَّهُ عَلَيْهِ عَرَّفَ بَعْضَهُ وَأَعْرَضَ عَنْ بَعْضٍ ۖ فَلَمَّا نَبَّأَهَا بِهِ قَالَتْ مَنْ أَنْبَأَكَ هَٰذَا ۖ قَالَ نَبَّأَنِيَ الْعَلِيمُ الْخَبِيرُ

إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا ۖ وَإِنْ تَظَاهَرَا عَلَيْهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَوْلَاهُ وَجِبْرِيلُ وَصَالِحُ الْمُؤْمِنِينَ ۖ وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَٰلِكَ ظَهِير

عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبْدِلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِنْكُنَّ مُسْلِمَاتٍ مُؤْمِنَاتٍ قَانِتَاتٍ تَائِبَاتٍ عَابِدَاتٍ سَائِحَاتٍ ثَيِّبَاتٍ وَأَبْكَارًا

**"Na Nabii alipomwambia mmoja wa wake zake jambo la siri. Basi alipolitangaza yule mke, na Mwenyezi Mungu akamdhihirishia Mtume, akamjulisha sehemu na akaacha sehemu nyingine. Alipomwambia hayo, huyo mke akasema: Nani aliyekwambia haya? Mtume akasema: Kaniambia Mjuzi Mwenye habari. Kama nyinyi wawili mtatubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwishaelekea kwenye haki. Na mkisaidiana dhidi yake Mtume, basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye kiongozi wake na Jibril na waumini wema, na zaidi ya hayo malaika pia watasaidia. Akiwapa talaka asaa Mola Wake akampa wake wengine badala yenu ninyi, walio bora kuliko nyinyi wanyenyekevu, waumini, watiifu, waliotubu, wenye kushika ibada wafanyao kheri, wajane na wanawali." (66: 3 – 5).**

[108] *Tafsiri al-Kabiir* ya Raziy, Juz. 30, uk. 50.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 122 11/23/2016 12:37:32 PM

Hakika Aya zinaashiria katika kutumbukia wake wawili wa Mtume ﷺ Aisha na Hafsa kwa Maria al-Qibtwiya, Mama wa Ibrahimu katika kadhia ya asali, au Mtume kuwa naye katika siku ya mmoja wao, kulingana na ikhitilafu za riwaya. Hakika zinaonesha kwamba wao walikuwa katika hali ya kusaidiana kutoa siri kati ya siri zake, na pia zinaonesha hatua ya Mtume ﷺ baada ya kukasirika katika hali hiyo, na kuwahama kwake wake zake na kuwatishia kuwapa talaka. Bali na uchochezi wao kwa kufananishwa msimamo wao na msimamo wa wanawake wawili wa Nuhu na Luti.[109]

Na katika maudhui haya vilevile tunarejesha katika akili yale ambayo tumekwishayachambua katika mas'ala ya wake wengi, kuwa sababu ya kisiasa ni moja ya sababu ambazo zimepelekea jambo hili, ndoa kwa lengo hili inabakia inakabiliwa na kutoafikiana, ambapo mume anaangalia katika maslahi hayo kabla ya kumwangalia mke. Na makusudio ya kabla yake ndio msingi wa mahusiano katika upande huu kupitia ndoa kabla ya kuangalia nani atakuwa mke. Na umekwishapita utafiti wa nyanja hii hapo awali, ukiongezea kwamba mke katika mfano wa ndoa ya aina hii haijuwi thamani halisi ya mume, tumepata kwamba heshima ya baadhi ya wake wa Mtume ﷺ ni duni kuliko heshima ya wengi miongoni mwa wanaume na wanawake kati ya Waislamu. Na hali ni hiyo hiyo kuhusiana na Maasumini عليهم السلام, vinginevyo namna gani inawezakana kufasiri malalamiko ya baadhi ya wake zake ﷺ kwa baba zao? Na Mtume ﷺ ndio kiumbe bora zaidi na mtukufu zaidi na kiumbe mkarimu mno?

Hakika hayo hayakuwa ni yenye kutokea kwa mke anayejua hadhi ya Mtume au Imamu, na kwa hiyo tumekuta kwamba alipopatikana mwanamke huyo, ni namna gani alimheshimu Mtume ﷺ hadi akawa ni bibi mbora wa wanawake wa kaumu yake? Na vilevile hakika kukutana wanawake hawa kwa Mtume ﷺ na Maasumini عليهم السلام

[109] Surat-Tahrim: 3.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 123 11/23/2016 12:37:32 PM

na mahusiano yao nao kwa mafungamano ya ndoa haimaanishi kupewa teketi ya wema wa mwisho kwao, bali hiyo inamaanisha kuwepo uwezekano kwao wa kuwa watukufu na wenye hadhi kubwa. Hiyo ni kwa sababu mwanadamu kwa kiwango anachokaribia katika chanzo cha nuru ndivyo anavyopata mwanga wa kuangazia katika njia ikiwa ana uwezo na moyo wenye kuelewa, vinginevyo kuwa mwanaume au mwanamke aliye karibu na Mtume haimaanishi kuwa mwema, achilia mbali kuwa mbora wa viumbe.

Hakika kama tulivyokuta katika Maswahaba zake ﷺ kuna watu kama vile Ali عليه السلام Salman, Miqdad, na mfano wao رضي الله عنهم, pia tumekuta wanafiki ambao Qur’ani tukufu imeashiria kwao kwa kauli yake: “Na miongoni mwa mabedui walio pembezoni mwenu wamo wanafiki na katika wenyeji wa Madina wako waliobobea katika unafiki”, haya ni licha ya kwamba wao wanasikia maneno ya Mtume na wanatangama naye na wanaona vitendo vyake na Sunnah zake.

Na sisi tunafaradhisha umaasumu wa Maasumini عليهم السلام na sio umaasumu wa anayefungamana nao miongoni mwa wanawake. Na kama tukitafakari katika sira ya wanawake hao tunakuta baina yao kuna hali za ghera za kukhalifu, kama inavyonukuu historia. Baina ya Ummul-Muuminina Aisha na Ummul-Habiba رضي الله عنهما kulikuwa na ugomvi kiasi cha mtu kufurahia msiba wa adui yake. Ummul-Habiba binti Abu Sufiyani mke wa Mtume alituma kwa Aisha kondoo aliyechomwa baada ya kuuliwa Muhammad bin Abu Bakri huko Misri, na alimchoma katika ngozi ya punda. Hiyo ni kwa sababu Ummul-Habiba aliitakidi kwamba Muhammad alishiriki katika kuuliwa Uthman رضي الله عنه. Aisha akasema: “Mwenyezi Mungu amlaani mtoto wa malaya, wallahi sintokula nyama ya kuchoma abadani.”

Na historia imenukuu kwamba baadhi ya wake zake ﷺ walimuonea wivu Maria alipomzaa Ibrahim kwa Mtume ﷺ, bali na kuliku-

wa na vita baina yao! Katika kitabu *al-Ijabah* imeandikwa kwamba: "Hakika Aisha alishika kichwa cha Sauda binti Zam'ah baada ya kumsikia anasoma mashairi aliyofahamu kwayo kuwa ni uchochezi kwake na kwa Hafsa. Hafsa akamsaidia, akaja Ummu Salama naye akamsaidia Sauda."

Na katika wake wa Imamu as-Sadiq عليه السلام tunakuta kwamba Ummu Is'haq alinyoa nywele za kijakazi wa Imamu عليه السلام kwa kumuonea gere, na hiyo ni katika Hijja, kwa kuwa Imamu alimpenda. Na tunakuta Ummul-Fadhil mke wa Imamu al-Jawad عليه السلام daima alikuwa na ghera (wivu) na malalamiko kwa mama wa Imamu al-Hadi عليه السلام naye ni kijakazi, na kulingana na mawazo yake kijakazi ni wa daraja la chini kijamii kuliko yeye, hivyo ni vipi yeye anapendwa zaidi na Imamu عليه السلام?

Na huu ni upande mmoja tu wa sura, vinginevyo kuna pande zenye kuchanua zaidi za wake zao عليهم السلام, zinaashiriwa na hadithi zilizopita katika fadhila za Khadija عليها السلام na za mke wa Imamu as-Sajad na ambaye alikuwa mkweli hajapatikana katika familia ya Hasan mwanamke mfano wake, kama alivyomuelezea Imamu as-Sadiq عليه السلام au Ummu Faruwah[110] mjuzi ambaye alikuwa anatufu Kaaba, mmoja wao akataka kumsahihisha akasema: "Hakika sisi hatuhitajii elimu yako."

Na kama tukifuatilia nyanja hii basi tungerefusha kwa sababu ndio asili, bali tumetaja utafiti uliotangulia kwa sababu ni wa pekee katika upande mmoja, na katika upande mwingine ili tubainishe kwamba Maasumini عليهم السلام walikuwa wanaamiliana pamoja na uhalisia, wanakabiliana na aina hii katika mambo, na mambo yao yote hayakuwa ndani ya uzio wa ghaibu.

---

[110] Ummu Faruwah binti al-Qasim bin Muhammad bin Abu Bakri mama wa Imamu as-Sadiq عليه السلام na nafasi yake imepokewa kutoka kwa as-Sadiq عليه السلام aliposema: "Abu Bakri amenizaa mara mbili." Ambapo nasaba yake kwa baba yake inamalizikia kwa Abu Bakri رضي الله عنه, na vilevile nasaba yake kwa mama yake ambapo mama yake ni Asmai binti Abdur-Rahmani bin Abu Bakri.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 125 11/23/2016 12:37:33 PM

# SEHEMU YA TATU

## VIPI NA NAMNA GANI WANAVAA?

Ni msingi upi unaofuatwa katika yanayohusiana na sira ya Ahl-ul-Bayt عليهم السلام katika mas'ala ya mavazi, kama njia kati ya njia za maingiliano ya kijamii? Je, asili ni kujikwatua na kujipamba, isipokuwa katika hali chache zinazolazimishwa na mazingira maalumu yanayopelekea dhiki kudhihirisha hali ya kujinyima? Au asili kwao ni kujinyima na kuidhihirisha, na hadithi za kujikwatua zinachukuliwa katika hali chache za dharura?

Hakuna shaka kwamba kuna aina mbili za riwaya ambazo zinaelezea sira yao, na tunaweza kukuta riwaya zinazoelezea njia mbili katika maisha ya baadhi yao. Inapokewa kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kwamba alikuwa anavaa nguo za kawaida na wakati mwingine zinakuja riwaya kwamba alikuwa anapenda kujikwatua, ni sawa iwe katika mavazi au katika mwonekano binafsi, na hali ni hiyo hiyo kwa Amirul-Muuiminina عليه السلام. Asili ni ipi katika mas'ala haya, na ni riwaya zipi zinatawala nyingine?

Hakika sisi tunarejesha katika akili zetu ambayo yametajwa katika utangulizi kwamba kutokuwa wazi njia ya msingi ya maisha ya Ahlul-Bayt عليهم السلام, na misingi ya jumla ya sira yao kwa baadhi ya Waislamu, jambo hili limefanya kadhia kuwa katika wepesi mkubwa kiasi kwamba mtu anaweza kufuata njia ambayo anaipendelea katika maisha yake na wala hakosi njia katika kutoa dalili juu yake kupitia riwaya na historia. Ikiwa ni katika watu watanashati na wa kujikwatua hakika atategemea rundo hilo la riwaya zinazotia mkazo juu ya upande huu. Na baadhi ya wengine miongoni mwa watu wa kujinyima wanataka msaada kutoka katika rundo jingine, kwa hiyo



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 126 11/23/2016 12:37:33 PM

inapasa tujue msingi katika riwaya hizi ni upi na nadra chache ni ipi. Kabla ya hayo inapasa kueleza makundi yote mawili ya riwaya:

## KUNDI LA KWANZA:

Kutoka kwa Mtume ﷺ: "Hakika mimi navaa nguo ngumu na nakaa juu ya ardhi, nalamba vidole vyangu na napanda punda bila ya tandiko na nabeba abiria, hivyo mwenye kuchukia Sunnah yangu basi sio katika mimi." Na amesema ﷺ akimwambia Abu Dharr رضي الله عنه: "Ewe Abu Dhari! Vaa nguo ngumu katika mavazi na zilizochakaa miongoni mwa nguo ili kujifakharisha kusipate njia kwako."

Na Amirul-Mu'minin عليه السلام anazungumzia juu yake: "Na alikuwa ﷺ anakula juu ya ardhi na anakaa mkao wa watumwa, na anashona viatu vyake kwa mikono yake na anatia viraka nguo zake kwa mikono yake."[111]

Na ama Amirul-Mu'minin عليه السلام alionekana amejifunga shuka chakavu lenye viraka akaambiwa kuhusu hilo, akasema: "Kwalo moyo unanyenyekea na kwalo nafsi inakuwa dhalili na kwalo wanaiga waumini."[112]

Ama Zainul-Abidin عليه السلام alikwishatoka na nguo nzuri akarejea haraka akasema: "Ewe kijakazi rejesha nguo zangu, hakika nimetembea na nguo zangu kana kwamba mimi sio Ali bin Husein." Na kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام alionwa na Muhammad bin Husein bin Kathir amevaa joho la sufi baina ya mashati mawili mazito, akamuuliza kuhusu hilo, akasema عليه السلام: "Hakika mimi nilimuona baba yangu anavaa hivi na hakika sisi tunapotaka kuswali tunavaa nguo zetu zilizo ngumu zaidi."[113]

---

[111] *Mizanul-Hikmah*, Juz. 8, uk. 474.
[112] Hadithi kutoka katika *Mizanul-Hikmah*, Juz. 8, uk. 474.
[113] *Biharul-An'war*, Juz. 76, uk. 314.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 127 11/23/2016 12:37:33 PM

Na kutoka kwa Abu Ubaad رضي الله عنه amesema: "Hakika Ridha عليه السلام ilikuwa kukaa kwake wakati wa kiangazi ni juu ya hariri na katika masika ni juu ya ardhi, na vazi lake ni nguo ngumu, na anapotoka kwa watu anajipamba kwa ajili yao."[114]

Na sisi mbele ya hadithi za kundi hili tunakuta kwamba Mtume صلى الله عليه وآله وسلم anavaa nguo nzito na anafanya hiyo ni Sunnah yake na mwenye kuchukia Sunnah yake basi sio katika yeye, na wala sio katika ummah wake. Na anamuusia Abu Dharr رضي الله عنه kuvaa nguo nzito ili ajikinge na kujifaharisha na kiburi, na Amirul-Mu'minina عليه السلام anatia mkazo juu ya maana hii katika maisha ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم wakati anapobainisha kwamba alikuwa anatia nguo zake viraka kwa mikono yake, na anaona kama hatovaa nguo ngumu anahofia kutounganishwa na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ukiongezea na hadithi ambazo amezisoma kwamba yeye anavaa nguo zilizotiwa viraka, pamoja na kuangalia athari zake katika kiwango cha mtu binafsi "kwayo moyo unanyenyekea na nafsi inadhalilika" na katika kiwango cha jamii "na waige kwayo waumini."

Na Imamu Zainul-Abidin عليه السلام anataka kutoa angalizo katika athari mbaya ambazo zinaambatana na nguo nzuri, laini na maridadi kwamba zinamkosesha mwanadamu utu wake wa kawaida na kumletea utu wa bandia hadi akaihesabu nafsi yake kwamba yeye sio Ali bin Husein!

Na Imamu as-Sadiq عليه السلام anatilia mkazo kwa kumfuata kwake baba yake al-Baqir عليه السلام kwa kuvaa kwake nguo ngumu na nzito katika wakati wa Swala. Na mwisho hakika Imamu Ridha عليه السلام anachukulia uzito na ugumu kama ndio vazi la kudumu pamoja naye, maadamu yuko peke yake. Anapotoka kwenye jamii anajipamba kwa ajili yao, na kundi hili la hadithi ambazo tumezieleza si kingine isipokuwa ni idadi ndogo katika hadithi nyingi zinazomalizikia katika ulazima

[114] Rejea iliyotangulia, Juz. 76, uk. 321.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 128 11/23/2016 12:37:33 PM

wa kujinyima na dhiki. Inawezekana kuhitimisha madhumuni yake kama ifuatavyo:

Hakika dunia kwa uduni wake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu aghlabu imejaaliwa kwa wasiokuwa mawalii wa Mwenyezi Mungu, ambao Qur'ani tukufu inazungumzia juu yao: "Na siku wataingizwa motoni; mmepoteza mazuri yenu katika maisha yenu ya duniani na mmestarehe humo." Ama Mawalii wake nao ni ambao amewaandalia makazi ya akhera, mahususi kwa neema zake na malipo yake na aliyoumba humo ambapo jicho halijawahi kuona, sikio halijawahi kusikia wala moyo wa mwanadamu haujawahi kuwaza. Lau kama dunia ingekuwa sawa na uzani wa ubawa wa mbu basi kafiri asingekunywa humo maji. Na haya ni madhumuni ya hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoingia kwake Umar bin al-Khatab رضي الله عنه naye amewaacha wake zake kwenye vyumba, na katika nyumba kuna ngozi za ngamia, naye ﷺ amelala juu ya mkeka na mkeka umeacha alama katika mbavu za Mtume. Umar akanusa harufu ya ngozi, Mtume ﷺ alipoketi. Umar akaona alama za mkeka katika ubavu wa Mtume ﷺ akasema: "Ama mimi nashuhudia kwamba wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na wewe ni mtukufu zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko Kisra na Kaisari na wao wamo katika waliyonayo miongoni mwa dunia, na wewe unalala juu ya mkeka, nao mkeka umeshaathiri katika mbavu zako!" Mtume ﷺ akasema: "Je huridhiki wao kuwa na dunia na sisi kuwa na akhera."[115]

Na hakika hii ni moja ya ukweli wa kuipa nyongo dunia, na ndio inatakiwa kwa waumini kujizuia kujikwatua na kujipamba. Hiyo ni kwa sababu waumini dunia imewataka na wao hawakuitaka, na imewafurahisha basi wakazitoa nafsi zao fidia kwayo. Kama ambavyo malengo ambayo yanamsubiri muumini ili kuyatekeleza hayawapi fursa ya kufikiria sana katika mas'ala haya ya ukamilisho miongoni

[115] *Biharul-An'war*, Juz. 16, uk. 257.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 129 11/23/2016 12:37:33 PM

mwa kuboresha chakula, kujikwatua kwa mavazi na mengineyo, hakika wao wanaposubiria katika dunia hii juu ya hali hizi za dhiki na kujinyima, hakika wao wanakuwa wepesi ili wafike, na kama anavyosema Amirul-Mu'minin ﷺ: "Wallahi alishaniambia msemaji: Je, huipuuzi? Nikamwambia: Kuwa mbali na mimi kwani asubuhi watu watashuruku usiku." Kwa kiasi hiki tunatosheka na hadithi za kundi la kwanza katika hadithi za kujinyima na kujidhiki.

## KUNDI LA PILI:

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Mwenyezi Mungu akikupa mali basi ionekane athari ya neema za Mwenyezi Mungu na utukufu Wake kwako." Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Pambeni vizuri mavazi yenu na vipando vyenu ili muwe ni kielelezo kwa watu."

Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri na nadhifu na anapenda unadhifu."[116]

**Na katika sira yake ﷺ tunakuta Hadithi:**

Hakika yeye alikuwa anapenda kujipaka mafuta na anachukia uchafu,[117] na alikuwa anajiangalia katika kioo na anajitengeneza vizuri na kuchana nywele zake. Na wakati mwingine anajiangalia kwenye maji na kujiweka vizuri humo. Na alikuwa anajipamba kwa ajili ya Maswahaba wake ukiachilia mbali kwa ahali zake na anasema: "Hakika Mwenyezi Mungu anampenda mja Wake anapotoka kwa ndugu zake ajitayarishe kwa ajili yao na ajipambe." Na alikuwa anavaa kilemba na anajitanda kwacho, na alikuwa anajifunga shuka na anajitanda kwayo, na anapendeza sana katika weusi wake na weupe, ambao unaonekana katika miundi yake na miguu yake. Na in-

[116] Hadithi kutoka katika *Nahjul-Faswaha*, Maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.
[117] *Biharul-An'war*, Juz. 16, uk. 247.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 130 11/23/2016 12:37:33 PM

asemekana alifariki akiwa anashonewa shuka lenye miraba mieupe na mieusi na Ban al-Ashihali ili aje alivae. Na Aisha amesema juu yake ﷺ kwamba alivaa joho la sufi na kilemba kisha akatoka na akahutubia watu juu ya mimbari: “Sijaona katika aliyoumba Mwenyezi Mungu mzuri aliyependeza kwalo kama yeye.”

Na kutoka kwa Amirul-Mu’minin عليه السلام hakika amesema: “Na ajipambe mmoja wenu kwa ajili ya ndugu yake Mwislamu kama anavyojipamba kwa ajili ya mgeni ambaye anapenda amuone katika hali nzuri zaidi.”[118]

Na imenukuliwa kutoka kwa Imamu Hasan عليه السلام kwamba alioga na akatoka katika nyumba yake kwa pambo zuri la fahari, nguo safi, mapambo mazuri na uso wake unang’ara kwa uzuri na umbo lake limekamilika kwa sura na maana. Na kuja kwake kunanukia kwa manukato na muonekano mzuri unajulikana kati ya sehemu zake. Na kadari imeshahukumu kwamba wema ni katika sifa zake. Kisha akapanda nyumbu wake akiwa na bashasha na si mwenye chuki na akaenda akiwa amezungukwa na wapambe wake na akapambwa na safu. Akakutana na mtu miongoni mwa Mayahudi na mafakiri akiwa katika hali chakavu (nguo chakavu zenye viraka) amechoshwa na njaa na amepigwa na udhalili na amehilikishwa na ukosefu. Ngozi yake imefunika mifupa (amekonda sana) na udhaifu wake unamzuia kusonga mbele. Akamsimamisha Hasan عليه السلام na akasema: “Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, nifanyie insafu!”

Imam akasema: “Kwa kitu gani?”

Akasema: “Babu yako anasema: Dunia ni jela ya muumini na ni pepo ya kafiri, na wewe ni muumini na mimi ni kafiri. Sioni ila dunia ni pepo kwako, unaneemeka kwayo, na sioni ila ni jela kwangu. Yamenihilikisha madhara yake na umenimaliza ufakiri wake.”

[118] *Al-Adabu Was-Sunanu* cha Ayatullah Shiraziy, uk. 233.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 131 11/23/2016 12:37:33 PM

Imamu عليه السلام akamjibu: "Kama ungeangalia aliyoniandalia Mwenyezi Mungu mimi na waumini akhera katika ambayo jicho halijaona wala sikio halijasikia, ungejua kwamba mimi kabla sijayaendea hayo katika dunia hii niko katika jela mbaya. Na kama ungeangalia aliyokuandalia Mwenyezi Mungu na kila kafiri akhera katika adhabu ya moto wa Jahanamu na mateso yake, basi ungeona kwamba wewe kabla ya kuyaendea, sasa hivi uko katika pepo pana na neema nyingi."[119]

Isipokuwa hakika hadithi zinapokea mengi zaidi kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام na mjukuu wake Imamu Ridha عليه السلام kiasi kwamba zinageuza kuwa ni kadhia ya kijamii, wengi wanauliza juu yake. Huyu hapa ni Ubaad anamuuliza Imamu as-Sadiq عليه السلام kuhusu vazi lake zuri laini, pamoja na kwamba babu yake Amirul-Mu'minin عليه السلام alikuwa anavaa nguo ngumu, na Sufiyan Thauriy anauliza vilevile, na linaingia kwake kundi la masufi wanamuuliza, na hali ni hiyo hiyo kwa Sufiyan bin Uyainah, na vilevile Imamu Ridha عليه السلام ambapo anaashiria katika hadithi iliyopokewa kutoka kwake, kwamba raghba ya baadhi ya wafuasi wake ni aache kujikwatua ili avae nguo ngumu, ili udhihiri kwake Uimamu zaidi.

Kutoka kwa as-Sadiq عليه السلام: "Hakika Mwenyezi Mungu anapenda uzuri na kujipamba na anachukia uchafu na kujichafua. Hakika Mwenyezi Mungu anapomneemesha mtu yeyote kwa neema, basi anapenda aone kwake athari zake." Akaambiwa: Vipi? Akasema عليه السلام: "Asafishe nguo zake, ajifukize ili harufu yake iwe nzuri, na afanye vizuri (au atengeneze) nyumba yake vizuri. Asafishe eneo lake, na kwamba kuwasha taa kabla ya kuzama jua kunazuia ufakiri na kunaongeza riziki."[120]

---

[119] *Aawalimul-Ulumi/Imamu Hasan* 106.
[120] *Biharul-An'war*, Juz. 76, uk. 300.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 132 11/23/2016 12:37:33 PM

Na amesema عليه السلام katika jibu lake kwa Sufiyan Thauriy baada ya kumwambia Imamu: "Wewe unapokea kwamba Ali bin Abutalib عليه السلام alikuwa anavaa nguo ngumu, na wewe unavaa nguo za fahari na za kuvutia?" Imam as-Sadiq عليه السلام akasema: "Ole wako, hakika Ali bin Abutalib alikuwa katika zama ya dhiki. Zama inapokunjuka basi kudhihirisha zama inafaa zaidi kwake."[121] Na anabainisha kanuni ya zama katika kupanga vazi linalofaa maadamu haipelekei katika yaliyoharamishwa kwa kauli yake عليه السلام: "Vazi bora la kila zama ni vazi la watu wake." Na itakuja hadithi kuhusu upande huu katika kurasa zijazo.

Na linalodhihirika ni kwamba kulikuwa na tatizo la ufahamu kwa baadhi ya Waislamu, sawa iwe katika wafuasi wa Maimamu au kwa wasiokuwa wao, ufahamu unaomalizikia kwamba mwenye kutaka kushikamana na dini na wema ni juu yake ajidhihirishe kwa kuvaa sufi na nguo nzito, na kwamba mwenye kuvaa nguo nzuri hafai katika nafasi ya uongozi wa kidini. Na nadhani tatizo hili limeletwa na watangazaji wa soko la usufi katika zama hizo, na kwa hiyo wakati Imam as-Sadiq عليه السلام alipokuwa anafanya tawafu basi, Ubaad bin Kathir al-Baswariy akawa anavuta nguo yake na anasema:

"Ewe Ja'fari bin Muhammad, unavaa mfano wa nguo hizi (nzuri) na wewe uko sehemu hii pamoja na kwamba sehemu ambayo uko humo ni kutoka kwa Ali عليه السلام." Akamwambia: "Ole wako hii nguo ya fahari nimeinunua kwa dinari na senti kadhaa, na Ali عليه السلام alikuwa katika zama inayokubali kwake aliyovaa. Na kama ningevaa mfano wa vazi hilo katika zama zetu hizi watu wangesema: Hii ni kujionyesha mfano wa watumwa."[122]

Na tunakuta hawa watu katika kutatua tatizo la ufahamu wao wanakimbilia katika kumkinaisha Imam avae vazi la kisufi na ajidhi-

---

[121] *Biharul-An'war*, Juz. 76, uk. 307.
[122] *Biharul-An'war*, Juz. 76, uk. 316.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 133 11/23/2016 12:37:33 PM

hirishe kwa hali ya kujinyima. Kutoka kwa Imam Ridha عليه السلام kwamba amesema: "Hakika watu dhaifu miongoni mwa huria wanapenda nikae chini ardhini na nivae nguo ngumu, na zama haikubali hayo."[123]

Na wanakuja watu kutoka Khurasan wanaingia kwa Imamu Ridha عليه السلام huku wakisema: "Hakika watu wamekupinga juu ya vazi hili ambalo unalivaa." Imamu عليه السلام akawaambia: "Hakika Yusufu bin Yaaqub alikuwa Nabii mtoto wa Nabii, na alikuwa anavaa vazi zuri na anajipamba kwa dhahabu na anakaa katika majilisi za watu wa Firaun. Hilo halikumshusha bali analaumiwa kama ingetolewa hoja katika uadilifu wake. Hakika ni juu ya Imamu anapohukumu afanye uadilifu na anapoahidi atimize na anapozungumza aseme kweli. Hakika Mwenyezi Mungu ameharamisha haramu yenyewe, iwe chache au nyingi, na Mwenyezi Mungu amehalalisha halali yenyewe, iwe chache au nyingi."

Lakini mazungumzo yanakuwa na ikhitilafu kubwa wakati tunapozungumza juu ya wingi wa mavazi yanayohitajika na kwamba haihesabiki kuwa ni israfu. Kutoka kwa Is'haq bin Ammar amesema: "Nilimwambia Abu Abdillahi عليه السلام: Muumini anakuwa na nguo kumi?" Akasema: "Ndio." Nikasema: Ishirini? Akasema: "Ndio, na hiyo sio katika ubadhirifu, bali ubadhirifu ni kuifanya nguo ya heshima yako kuwa nguo ya uchafu wako."[124]

Na kutoka kwake vilevile amesema: "Nilimwambia Abu Ibrahim (al-Kadhim) عليه السلام: Mtu anakuwa na nguo kumi; je, hiyo inakuwa ni ubadhirifu? Akasema: "Hapana. Lakini hiyo inasaidia nguo zake kudumu zaidi, lakini israfu ni kuvaa nguo ya heshima yako katika sehemu chafu."

---

[123] Rejea iliyotangulia, uk. 309.

[124] Rejea iliyotangulia, uk. 308. Na huenda kumfananisha Yusufu katika kuvaa taji na dhahabu ni katika kujengea juu ya kuwa kwake haikuwa haramu wakati huo au kwa anwani ya dharura au ni kwa ajili ya jambo muhimu zaidi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 134 11/23/2016 12:37:33 PM

**Rai Yenye Kuchaguliwa:**

Tutakuwa na utangulizi kadhaa ili tufikie katika kuchagua rai iliyo karibu zaidi:

**Kwanza:** Kujinyima ni nini? Kujinyima kuna pande mbili: Uhalisia wake na dhahiri yake. Ama dhahiri yake ni maarufu, ni kuvaa nguo za hadhi ya chini na kukaa katika sehemu duni, na kutozingatia mandhari ya nje. Na hili watu wote wanaweza kulifanya sawa mtu awe mkweli katika kujinyima au ni mwenye kujionesha kuwa anajinyima.

Na kujinyima kuna uhalisia ambao umeelezwa na hadithi tukufu, na huku hakupatikani isipokuwa kwa wanazuhudi halisi, na kunakosekana kwa wengineo. Imekuja kwamba kujinyima sio kupoteza mali wala sio kuharamisha halali, bali kujinyima katika dunia ni isije ikawa yaliyoko mikononi mwako yana thamani zaidi kuliko yaliyoko katika mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Na kwa maana hii hakika mpaka wa kujinyima umekuja katika Qur'ani tukufu ndani ya Aya katika maneno mbalimbali **"ili msihuzunike kwa yaliyowapita wala msifurahi kwa mliyopewa,"** kwa sababu kuamini yaliyopo kwa Mwenyezi Mungu na kutoamini yaliyopo katika mkono wa mwanadamu ni kazi ya moyo, na kutofurahi katika kupewa na kusikitika juu ya yaliyopita vilevile. Hivyo kujinyima kuliko bora zaidi ni kuficha hali ya kujinyima, sawa iwe katika yale ambayo yanafungamana na moyo kama tulivyotanguliza, au yale ambayo yanafungamana na mandhari, jambo ambalo zinaashiria kwalo baadhi ya hadithi zinazozungumzia hali zao maasumin عليهم السلام, ambapo walikuwa wanajidhihirisha kwa watu kwa mavazi mazuri "hii ni kwa ajili yenu" na wanaficha mavazi magumu "na hii ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu", kinyume na wengi kati ya wanaojidai kuwa wanajinyima ambao wanapindua uwiano. Mbele ya watu wanavaa nguo ngumu lakini wanakula vinono wanapokuwa peke yao, hakika wanapindua Aya.

Katika mwisho wa hadithi iliyopokelewa katika kujaribu kwa Sufiyan Thauriy kumkemea Imamu as-Sadiq عليه السلام baada ya kumuona amevaa nguo za thamani ya ghali na nzuri, baada ya Imamu kumjibu aliongeza: “Isipokuwa mimi ewe Thauriy pamoja na kuona nguo nilizonazo, hakika nimezivaa kwa ajili ya watu.” Kisha akashika mkono wa Sufiyan na akauvuta kwake kisha akanyanyua nguo ya juu na akatoa nguo ngumu katika ngozi yake chini ya hiyo, akasema: “Hii ngumu nimevaa kwa ajili ya nafsi yangu, na uliyoiona (yaani laini) ni kwa ajili ya watu.” Kisha akavuta nguo ya Sufiyan, akakuta ya juu yake ni ngumu na iliyo chini ya hiyo ni nguo laini, akasema: “Umevaa hii ya juu (yaani ngumu) kwa ajili ya watu na umevaa hii (yaani laini) kwa ajili ya nafsi yako ili uifurahishe.” [125]

Na kwa maana hii halisi vazi halikukanganyi wala hakuna shaka kwamba Maasumini عليهم السلام walikuwa ni watu wakubwa katika kujinyima bali ndio waalimu wao. Lengo lao halikuwa ni dunia kwa kutaka utawala wala chochote katika fadhila zenye kuondoka, na wala hawakuwa wanafurahia wanapopewa wala hawasikitiki wanaponyimwa. Na hii huenda ndio maana ambayo anaashiria kwayo Imamu as-Sadiq عليه السلام kwa kauli yake kwa mmoja wa wafuasi wake: “Ewe Hafsi! Sikuipa dunia katika nafsi yangu isipokuwa daraja ya mzoga, kwamba unapokuwa na dharura unaula.”[126]

**Pili:** Inadhihirika kwamba kuna tofauti katika maisha ya Maasumini عليهم السلام baina ya hali binafsi, raghaba binafsi na mazingira ya hadhira ya kijamii yanayotokana na nafasi yao ya kuwa kigezo kwa watu, na kugeuza kitendo wanachokifanya kuwa ni Sunnah.

Na sisi tunaweza kusema kwamba Maasumini عليهم السلام wangekuwa wanafanya kwa kipimo cha maisha binafsi tu, basi kungekuwa na minong’ono baina ya wanayoyamiliki miongoni mwa uhalisia wa

[125] *Furuul-Kafiy*, Juz. 2, uk. 203.
[126] *Safinatul-Bihar*, Juz. 1, uk. 572.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 136 11/23/2016 12:37:33 PM

kujinyima – kama ilivyotangulia – na wanayoyaficha miongoni mwa mwonekano wa kujinyima. Na haya ndio makusudio ya hadithi nyingi. Imamu Ridha عليه السلام wakati wa kiangazi alikuwa anakaa katika mkeka na masika anakaa juu ya ardhi na anavaa nguo ngumu. Hii ni katika maisha yake binafsi, na anapotoka kwa watu (katika maisha yake ya kijamii) anajipamba kwa ajili yao.

Na huenda sababu ya hilo ni kuziba njia ya fikira za kimakosa za jamaa wa kisufi ambao walitaka kuugeuza Uislamu kwa mafunzo yake ya kimaisha na misingi yake ya kimaendeleo katika elimu, ustawi, maendeleo na neema, kwenda kwenye nguo fupi yenye viraka na nywele chafu, na kusahau misingi ya asili. Wao wanatilia mkazo juu ya nguo kuukuu na wala hawaangalii kupasuka kwa hukumu za kidini katika mikono ya madhalimu na waovu. Wao wanasimamisha mandhari ya kuchukia uhalisia. Katika nyanja hii hakika Maasumini عليهم السلام walikuwa wanaelekeza kwamba kinachotakiwa kwa Imamu na mtawala sio nguo yake, bali kinachotakiwa ni uadilifu wake. Na hayatakiwi mandhari yake ya kujinyima bali vitendo vyake kuendana na nadharia yake, hisia zake kuendana na nyendo zake.

**Tatu:** Hakika baadhi ya vitendo ambavyo walikuwa wanavifanya Maasumini عليهم السلام hakika vilikuwa katika lengo la mafunzo na malezi kwa anayeshuhudia tukio pamoja nao au kwa anayesikia kutoka kwao na baada yao, vinginevyo inawezekanaje kufikiri kwamba Imamu Zainul-Abidin عليه السلام inatokea kwake ghururi na kiburi hadi atoke katika shakhisiya yake kwenda kwenye shakhisiya nyingine kama jambo lisingekuwa ni kwa ajili ya kufundisha, hususan na yeye alikuwa anavaa joho la hariri la dirhamu 500, na koti la hariri la dinari 500 wakati wa masika. Unapotoweka msimu wa masika analiuza na kutoa sadaka thamani yake na kusoma: "Nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amelitoa kwa waja Wake



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 137 11/23/2016 12:37:33 PM

na mazuri miongoni mwa riziki."[127] Vipi unaweza kuoanisha baina ya hili na lile kama haikuwa ni kwa ajili ya mafunzo.

Na inaaminika kuwa vingi kati ya vitendo vya Amirul-Mu'minin عليه السلام vilikuwa ni kwa ajili ya kurekebisha mpetuko ambao ulitokea katika siku za watangulizi wake miongoni mwa ufisadi wa kimali na uharibifu uliozidi. Na ilikuwa ni kushutumu madhumuni ya kila siasa za kimakosa za kimali ambazo zilikuwa zimetawala. Na kama Imamu عليه السلام asingefanya hayo ingegeuka kuwa kanuni madhubuti katika dini. Na huenda hii ni moja ya maana walizozieleza Maimamu عليهم السلام kwamba kipengele cha wakati katika zama za Amirul-Mu'minin عليه السلام kilikuwa ni sababu iliyofanya vazi lake na nguo yake viwe katika sura hiyo.

Na hapa tunaashiria katika angalizo muhimu, nalo ni kwamba kuna kundi kubwa ambalo wakati mwingine hutofautiana na misingi, na jukumu la Imamu ni kuainisha msingi unaofaa katika zama. Kwa kujengea katika hilo hakika sisi tunaitakidi kwamba asili kwao عليهم السلام katika maisha yao mahususi na ya kiibada, ndio mantiki halisi ya kujinyima (katika nyoyo zao) pamoja na muonekano (wa nje). Ama katika maisha ya kijamii asili humo ni kujipamba na kujikwatua – katika wastani – Mwenyezi Mungu anapenda uzuri na kujipamba na anachukia uchafu na ubaya. Na Mwenyezi Mungu amekwishaumba pambo kwa ajili ya waja Wake, na watu wema ndio wanaostahiki zaidi kuliko wasiokuwa wao.

## MITAZAMO KATIKA MAADILI KWA JUMLA

### Utangulizi:

Mwanzo wa binadamu kutumia mavazi unazungumziwa katika Aya tukufu katika Sura al-Aaraf, hivyo basi mazungumzo juu yake yawe

[127] *Biharul-An'war*, Juz. 76, uk. 298.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 138 11/23/2016 12:37:33 PM

ndio utangulizi katika baadhi ya dhana zinazohusu upande huu wa maisha ya Maasumini عليهم السلام.

يَا بَنِي آدَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُوَارِي سَوْآتِكُمْ وَرِيشًا ۖ وَلِبَاسُ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ۚ ذَٰلِكَ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ

يَا بَنِي آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْآتِهِمَا ۗ إِنَّهُ يَرَاكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ

وَإِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا وَاللَّهُ أَمَرَنَا بِهَا ۗ قُلْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ ۖ أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

قُلْ أَمَرَ رَبِّي بِالْقِسْطِ ۖ وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ۚ كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ

فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ ۗ إِنَّهُمُ اتَّخَذُوا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُهْتَدُونَ

يَا بَنِي آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ الرِّزْقِ ۚ قُلْ هِيَ لِلَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا خَالِصَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ كَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَنْ تُشْرِكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 139 11/23/2016 12:37:33 PM

**"Enyi wanadamu! Hakika tumewateremshia vazi lifichalo tupu zenu na vazi la pambo. Na vazi la takua ndio bora zaidi. Hiyo ni katika ishara za Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka. Enyi wanadamu! Shetani asiwatie katika fitina kama alivyowatoa wazazi wenu katika bustani (pepo), akawavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye na kabila lake anawaona, na nyinyi hamuwaoni. Hakika tumewajaalia mashetani kuwa watawala wa wale ambao hawaamini. Na wanapofanya machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi machafu: Je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua? Sema Mola Wangu ameamrisha uadilifu. Na elekezeni nyuso zenu katika kila msikiti, na muombeni Yeye tu kwa ikhlasi. Kama alivyowaumba kwanza ndivyo mtarudi. Kundi moja ameliongoa, na kundi jingine limethibitikiwa na upotofu. Hakika wao wamefanya mashetani kuwa ni watawala wao badala ya Mwenyezi Mungu. Na wanadhani kwamba wao wameongoka. Enyi wanadamu! Chukueni mapambo yenu katika kila msikiti na kuleni na kunyweni wala msifanye ufujaji (israf), hakika Yeye hawapendi wafanyao ufujaji (israf). Sema: Ni nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amewatolea waja Wake, na vilivyo vizuri katika riziki? Sema: Hivyo ni kwa wale walioamini katika maisha ya dunia, ni vyao tu Siku ya Kiyama. Namna hii tunazieleza ishara kwa watu wajuao. Hakika Mola Wangu ameharamisha mambo machafu yaliyodhihirika na yaliyofichika. Na dhambi na dhulma bila ya haki. Na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambacho hakukiteremshia dalili. Na kusema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua."**
**(Surat al-Aaraf: 26 – 33.)**

Ni wazi kwamba Aya zinazungumzia juu ya kisa cha Nabii Adamu عليه السلام na mke wake Hawa baada ya (kuwafitinisha) shetani na kuwatoa peponi, hali ya kuwa wameshakuwa uchi bila ya vazi, Qur'ani tukufu imetoa darasa katika kisa katika pande mbili: upande wa neema ya Mwenyezi Mungu juu ya waja Wake kwamba Yeye ameteremsha kwa waja Wake vazi na pambo, na ilikuwa inawezekana kuwabakisha kwa muda mrefu – au milele – wakiwa uchi na



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 140 11/23/2016 12:37:33 PM

kuonekana aibu zao, kama tunavyoona leo katika makabila yaliyo mbali na ustaarabu. Na somo jingine ni kuelekea kwenye uchamungu na unyenyekevu kwa kuzingatia kuwa ni vazi la ndani baada ya kuneemeshwa vazi la nje. Vazi la uchamungu lenye kuzuia maasi na maovu ni bora kuliko kila vazi.

Na vazi ni kila kinachofaa kuvaa na kusitiri mwili, na pambo ni ambacho humo kuna uzuri. Na ameeleza vazi katika Aya tukufu kwa kauli yake **"linasitiri aibu zenu,"** ili kubainisha lengo lake la msingi. Lengo hilo ndio kufuata haja ya mwanadamu ambayo imemlazimisha kutafuta vazi ili kuficha ubaya ambao unamchukiza kuonekana mbele ya watu. Ama pambo analichukua kwa uzuri wa ziada baada ya haja ya asili. Na katika aya kuna neema ya kuongozwa mwanadamu kwenye vazi na pambo, na humo ni kama ilivyosemwa – kuna dalili ya uhalali wa vazi la pambo.[128]

Kisha Qur'ani tukufu inazungumza juu ya uovu wa Waarabu kabla ya kuslimu kwao, kule kutufu kwao na mikuki wakiwa uchi, na imekiita kitendo hicho kuwa ni uovu, ambapo Waarabu katika zama za kabla ya Uislamu walikuwa katika wanaosema: "Tunafanya tawafu kama tulivyozaliwa na mama zetu na wala hatutufu na nguo ambazo tumechuma nazo madhambi!" Sawa awe mwanaume au mwanamke. Hadi ilipokombolewa Makkah na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, akamtuma Ali عليه السلام na Aya ya Baraa kwenda Makkah, akawazuia kufanya tawafu uchi katika Kaaba.

La muhimu ni kwamba Aya ambazo zinazungumzia juu ya vazi na pambo ambalo linakuja baadaye, zinaamrisha kuchukua pambo wakati wa kwenda misikitini. Ni sawa pambo hilo liwe ni kuchana nywele kama ilivyopokelewa kutoka kwa Imamu Ridha عليه السلام au kuvaa nguo nzuri zaidi kama ilivyopokelewa kutoka kwa Imamu Hasan عليه السلام, ambapo alikuwa anaposimama kwenda kuswali anavaa

[128] *al-Mizanu Fiy Tafsiril-Qur'an*, Juz. 8, uk. 67.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 141 11/23/2016 12:37:33 PM

nguo zake zilizo nzuri zaidi, akaambiwa: Kwa nini unavaa nguo zako zilizo nzuri zaidi? Akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri anapenda mazuri, hivyo najipamba kwa ajili ya Mola Wangu naye anasema: Chukueni mapambo yenu wakati wa kwenda msikitini, hivyo napenda kuvaa nguo zangu zilizo nzuri zaidi."[129]

Na hapa tunanukuu aliyoyasema Allamma Tabatabai katika tafsiri yake kuhusu Aya hizo: "Kauli yake (swt): 'Sema nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amelitoa kwa ajili ya waja Wake na mazuri katika riziki' hii ni kuengua hukumu maalumu – kwa umma huu – kutoka katika hukumu ya jumla iliyotangulia. Ni kama mfano wa yaliyotangulia katika kauli yake: 'Hiyo ni katika dalili za Mwenyezi Mungu, huenda watakumbuka.' Na kauli yake: 'Wanapofanya ovu ….'

Na ni swali la kujiuliza la kupinga. Pambo mkabala wake ni uchafu, nao ni kile ambacho anaaibishwa nacho mwanadamu. Hivyo pambo ni kile ambacho huondoa aibu na kuondosha kukwepana kwa nafsi. Na kutoa ni kinaya ya kudhihiri, na kuazima mawazo yake, kana kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ilhamu Yake na kwa kumuongoza Kwake mwanadamu kwa njia ya maumbile katika kuleta aina za mambo ambayo jamii yake inayapendelea na kupelekea kuzivutia nafsi zao kwayo na kuondoa chukizo na kinyaa kwao, ni kana kwamba anawatolea pambo, na lilikuwa limefichikana halionekani akalidhihirisha kwa ajili ya jamaa zao.

Na kama mwanadamu angekuwa anaishi katika dunia peke yake bila ya kuwepo jamii ya mfano wake, basi asingehitajia pambo la kujipamba katu, wala kuzinduka juu ya ulazima wa kulitafuta, kwani sababu ya kuzinduka ni haja. Lakini ilipokuwa hakuna njia isipokuwa kuishi katika jamii ya watu, na wao wanaishi kwa matakwa na karaha, kupenda, kuchukia, ridhaa, ghadhabu basi hakuna nafasi

[129] *al-Mizan*, Juz. 8, uk. 92.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 142 11/23/2016 12:37:33 PM

kwao ya kupata wanayoyapenda na wanayoyachukia katika miundo na mitindo, hivyo basi mwalimu asiyeonekana akawafahamisha kupitia maumbile yao, yale yanayotengeneza yaliyoharibika miongoni mwao, na yanayopamba yale yanayowatia doa miongoni mwao, nayo ni pambo kwa aina zake zote. Huenda hii ndio nukta hususani katika maelezo ya kauli yake: ‘Kwa ajili ya waja Wake.’

Na hiki kinachoitwa pambo ni kati ya mambo yaliyo muhimu ambayo jamii ya kibinadamu inayahitajia. Nayo ni miongoni mwa adabu kongwe ambazo zinalazimiana na jamii, na zinapanda na kuteremka kulingana na maendeleo ya kijamii na ustaarabu. Na kama itaondoka asili hiyo kutoka katika jamii yoyote kati ya jamii, basi utavunjika mkusanyiko wake na kusambaratika sehemu zake wakati huo huo, kwa sababu maana ya kubatilika kwake ni kuondoka uzuri na ubaya, upendo na chuki, matakwa na kuchukia na mfano wake baina yao, na wakati huo hakutakuwa na uhalisia wa mkusanyiko wa kibinadamu.

Kisha mazuri kati ya riziki – kizuri ni kinachofaa katika mazingira – ni aina mbalimbali za riziki anayoitafuta mwanadamu ili kujipatia chakula kwayo. Au yote ambayo anayahitajia katika maisha yake na kubakia kwake, kama vile aina za chakula na vinywaji, ndoa, malazi na mfano wa hayo. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amekwishamwandalia mwanadamu yale anayohisi kuyahitaji katika aina za riziki, na yale anayohitajia katika kula kwake miongoni mwa aina za matamanio yenye kuchemka katika tumbo lake, miongoni mwa yale yanayofaa katika kukidhi haja yake, na haya ndio mazuri na yanayofaa kwa kawaida.

Na kujenga maisha ya mwanadamu mwenye furaha katika riziki nzuri haihitajii maelezo. Mwanadamu hastawi katika maisha yake kwa riziki isipokuwa kwa ile ambayo inaoana na hali ya nguvu zake na viungo vyake alivyoumbiwa, na inayomsaidia katika kubakia



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 143 11/23/2016 12:37:33 PM

ule muundo wake ambao ameumbiwa. Na hakuandaliwa kitu wala hakuumbiwa kiungo isipokuwa kwa kuwa ana haja nacho. Hivyo kama atavuka mpaka katika jambo kutoka katika yale yanayooana na maumbile yake hadi kwenda katika yale yasiooana na hali yake, basi atalazimika kukamilisha upungufu uliojitokeza kwake katika nguvu inayofungamana nayo kwa kuondoa kitu katika nguvu nyingine. Kama vile mlafi mroho ambaye anavuka mpaka katika kula na kupatwa na matatizo ya kumeng'enya, ambapo hulazimika kutumia dawa za kutibu mfumo wa umeng'enyaji na raghba ya tumbo, na hatoacha kutumia na kupita mpaka hadi atazoea na hivyo dawa hizo kutomsaidia tena. Na hapo mwanadamu anakuwa mgonjwa anayeshughulishwa na afya katika jumla ya wajibu wa kimaisha. Na lililo muhimu zaidi ni fikra salama na huru katika kipimo hiki.

Na kuvuka mpaka wa mazuri katika riziki kunampeleka mwanadamu katika kitu kingine ambacho hakijaumbwa kwa ajili ya ulimwengu huu, wala ulimwengu huu haujaumbwa kwa ajili yake hicho Na ni kheri gani ipi inayotarajiwa kwa mwanadamu anayetarajia kuishi katika mazingira yasiyokuwa mazingira yake ambayo ulimwengu umemwandalia. Na anafuata njia ambayo maumbile hayajamwandalia, na anapata lengo lisilokuwa lile lengo lake. Naye anajitanua katika kufurahia kwa kila kinachompambia matamanio yake na uroho wake, na kumpa mawazo ya kufikiri mambo mengine yaliyo juu zaidi au chini ya kadiri iwezekanayo.

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anakumbusha katika Aya kwamba kuna pambo alilolitoa kwa waja Wake na amelidhihirisha na amelibainisha kwao kwa njia ya ilhamu ya kimaumbile. Na maumbile hayatoi ilhamu isipokuwa kwa kitu ambacho kuna haja ya mwanadamu humo. Na hakuna dalili yenye nguvu juu ya uhalali wa kitendo kati ya vitendo na kufuata njia kati ya njia, kushinda uhitaji unaolingana na uwepo wa kimazingira na ambao unasema kwamba



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 144 11/23/2016 12:37:33 PM

Mwenyezi Mungu ndio kiunganishi baina ya mwanadamu mwenye kuhitajia na yale anayoyahitajia, ambayo yamefunuliwa katika nafsi yake miongoni mwa nguvu na viungo vinavyomsukuma kwayo kulingana na maumbile na uumbwaji.

Kisha anakumbusha kwa kuunganisha mazuri miongoni mwa riziki katika pambo kwa mfumo wa swali lenye kupinga, kwamba kuna vigawanyo vya riziki nzuri inayoafikiana na maumbile ya mwanadamu, ambayo anahisi uzuri wake kwa njia ya nguvu zake zilizowekwa katika uwepo wake. Na wala haihisi wala hazinduki isipokuwa kwa kuwa ana haja nayo katika maisha yake, na anahitaji kuitumia humo kwa matumizi anayoyategemea katika kubakia kwake. Na hakuna dalili yenye nguvu juu ya uhalali wa kitu kushinda haja ya kimazingira na ufakiri wa kimaumbile alionao, kama ulivyosikia.

Kisha anakumbusha kwa swali la kupinga, kwamba uhalali wa pambo la Mwenyezi Mungu na mazuri katika riziki ni kati ya mambo ambayo hapaswi mtu kuwa na shaka nayo. Ni katika mfumo wa sheria kupitisha hukumu ya kiakili na hukumu ya kimaumbile. Na kuhalalisha pambo na mazuri katika riziki haimaanishi kuvuka mpaka wa uadilifu humo na wastani wa uadilifu uliyopo baina ya kufurutu na kuzembea. Hakika wastani ni miongoni mwa yale yanayohukumiwa na maumbile; na amekwishasema Mwenyezi Mungu (swt) katika Aya iliyotangulia: 'Wala msifanye israfu, hakika Yeye hawapendi wenye kufanya israfu.' Na amesema kabla ya hayo: 'Sema Mola Wangu ameamrisha uadilifu.'

Katika kuvuka kwenda kwenye mpaka wa pande mbili: Upande wa kufurutu na kuzembea, kuna hatari inayoitishia jamii ya kibinadamu kuiweka katika hali ya kuporomoka na kuharibika na kuiondoa katika njia ya wema, kwa kuvunjika nguzo kati ya nguzo za jengo na hatimaye kulibomoa. Ni mara ngapi unadhihiri ufisadi nchi kavu



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 145 11/23/2016 12:37:34 PM

na baharini na unapatikana mzozo unaomalizikia kwenye vita yenye kuangamiza vizazi, yenye kuharibu yaliyotengenezwa, na hakuna chanzo isipokuwa ni ufujaji wa watu na ubadhirifu wao katika jambo la pambo au riziki. Mwanadamu anapovuka mpaka wa uadilifu na njia ya wastani aliyopangiwa, na kwenda katika mwelekeo ambao hatosimama katika mpaka wala hatoogopa kitu, inafaa kisiondolowe kwake kiboko cha malezi na akumbushwe hata yale yaliyo wazi ambayo inahukumu kwayo akili yake. Na katika aina hii ya ukumbusho ni amri ya Mwenyezi Mungu juu ya dharura za maisha kama vie kula, kunywa, mavazi, malazi na kutumia mapambo.

Mtunzi wa kitabu *al-Manar* amesema katika baadhi ya maneno yake – ni uzuri ulioje wa aliyoyasema: 'Hakika anaijua – yaani thamani ya amri ya kuchukua pambo pamoja na wepesi wake na uwazi wake – mwenye kusoma historia ya ummah na mataifa, na akajua kwamba wengi wenye hofu ambao wanaishi katika matatizo na maporini, sawa iwe mtu mmoja mmoja au makundi, wanakimbilia kwenye mapango na mashimo. Na makabila mengi ya wapagani katika baadhi ya visiwa vya bahari na milima ya Afrika wanawake kwa wanaume, wote wanaishi uchi bila ya nguo. Na kwamba Uislamu haujawafikia watu miongoni mwao isipokuwa umewafundisha kuvaa nguo kwa kuwajibisha kwake kujisitiri na kujipamba kwa wajibu wa kisharia. Na walipopindukia baadhi ya wahubiri wa Kikristo wa Ulaya katika kuutuhumu Uislamu ili kuwaweka watu mbali na Uislamu, na kuwapeleka katika mila yao huku Ulaya ikichochea dhidi yao, baadhi ya waadilifu miongoni mwao walijibu wakataja katika jibu lao kwamba hakika kusambaa Uislamu Afrika ni fadhila kwa Ulaya, kwa kusambaza kwao (Waislamu) ustaarabu kwa watu wake, ikiwa ni pamoja na kuwafanya waache kuwa uchi na kuwajibisha kuvaa nguo, kwani hiyo ilikuwa ni sababu iliyopelekea Ulaya kutangaza biashara ya nguo kwao.'



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 146 11/23/2016 12:37:34 PM

Bali nasema: Hakika baadhi ya mataifa ya wapagani wenye ustaarabu, elimu na fani, aghlabu kati yao kulikuwa na maisha ya kutovaa nguo hadi baadhi yao walipoongoka kwa Uislamu, na wakawa wanavaa na wanajipamba, kisha wakawa wanatengeneza nguo na wakaigwa na jirani zao miongoni mwa wapagani."[130]

Na kwa hiyo asili katika mavazi hakika imejaaliwa kwa ajili ya kuhifadhi na kusitiri yale ambayo ni vibaya kuyadhihirisha mbele ya watu. Kama ambavyo ni kuhifadhi na kujikinga na sababu za nje zinazoathiri afya ya mwanadamu, miongoni mwa hali ya kimazingira yenye kubadilika badilika katika joto na baridi, kisha kwa kupita muda ikawa imebeba mazingatio mahususi ya kijamii. Na hapa tutazungumzia kuhusu baadhi ya misingi na mafunzo ya jumla ambayo tunayaona katika maisha ya Maasumini عليهم السلام katika yanayofungamana na upande huu:

## KUTENGANISHA BAINA YA VAZI NA SHAKHSIA:

Miongoni mwa alama za utamaduni usioendelea ni kutengeneza utukufu wa uongo kwa mwanadamu. Katika mtazamo wa watu wenye utamaduni huu, vazi linakuwa ni dalili ya juu ya utu, hivyo mwenye kuvaa aina hii maalumu, anamiliki utu wa hali ya juu. Na kulingana na utamaduni huu aina fulani ya manukato ni dalili ya wema. Bali hata aina fulani ya sigara ambayo anavuta mtu inakuwa ni dalili ya kuwa kwake ni mwenye mafanikio.

Na kama tungefungua macho yetu juu ya maneno ya matangazo yenye kusikilizwa au yenye kuonekana, hakika yanaelezea juu ya mambo haya kwa njia mbalimbali, na hakuna shaka kwamba yana athari isiyokuwa ndogo kwa watu, bali wengi wamekuwa wana-

[130] *al-Mizan Fiy Tafsiril-Qur'an*, Juz. 8, uk. 82.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 147 11/23/2016 12:37:34 PM

tumia ada hizi chini ya fikra za mbadala huo wa uongo. Mtu anavuta sigara ya marlboro kwa mfano, kwa sababu ni sigara ya wenye mafanikio! Hata kama yeye yuko katika daraja la saba katika kufeli na kushindwa, isipokuwa anajumuisha nafsi yake pamoja na jina la wenye kufaulu kwa njia hii kwa kupitia sigara!

Wakati ambapo ilikuwa inapasa mwanadamu ajitume ili awe ni mwenye utu wa juu kwanza katika akili yake na uwezo wake, ambapo "thamani ya kila mtu ni kile anachokifanya vizuri" mara anaanza kufikiri katika njia ya mavazi yake au manukato yake eti ili awe ni mtu muhimu! Vivyo hivyo ukweli umepotea na kuchukua mahala pake utukufu wa uongo.

Na imekuwa - kwa masikitiko - uongo huu ndio kanuni, na yasiyokuwa hayo ni ukiukwaji. Mwananchi mwenye kufika katika idara fulani kuhitajia huduma haiangaliwi kazi yake au vyeti vyake vya kuthibitisha ukamilifu wake, bali unaangaliwa muonekano wake ili kupangiwa muda wa kusubiria. Mavazi na mwonekano wa nje unapokuwa mzuri zaidi basi muda unapungua, na ni kinyume chake mwonekano wake unapokuwa hauvutii katika mtazamo wa mkuu wa idara. Vivyo hivyo mzuri katika jamii anapewa heshima kwa kufumbia macho ambayo yako chini ya mavazi yake miongoni mwa utu wake au fikira na akili. Wakati ambapo mjuzi mwelewa ananyimwa heshima hiyo kama hana mwonekano mzuri. Na ikiwa jamii itageuka kwenda katika ushindani wa kujikwatua na mavazi, hakika uwezo wake unahama kutoka katika uvumbuzi na kwenda kwenye matumizi yasiyo na maana, na huenda kisa kilichonukuliwa kutoka kwa Sheikh Maytham al-Bahraniy ni mfano bora katika mwelekeo huu.

Hiyo ni kwa sababu katika hali ya mwanzo alikuwa amekaa katika kona ya kujitenga na kupuuzwa. Anashughulika na uhakiki wa matawi ya elimu na misingi yake. Wakamwandikia watukufu wa



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 148 11/23/2016 12:37:34 PM

Hilah na Iraki barua juu ya kujitenga kwake na kumlaumu juu ya tabia hizi wakasema: "Ajabu sana kwako, hakika wewe pamoja na umahiri wako katika elimu zote na maarifa, na uerevu wako katika kuhakiki matukio na uvumbuzi mzuri umekaa katika kona za kujitenga na umepiga hema katika kona ya uzembe unaopelekea kuzima vuguvugu la ukamilifu."

Akaandika pembezoni mwa barua yao beti hizi:

"Nilitafuta fani za elimu nikitaka kwazo utukufu,
basi nikapungua na kuwa duni katika yale niliyotukuka kwayo.
Imenibainikia mimi kwamba mema yote ni matawi,
na kwamba mali humo ni asili."

Beti hizi zilipowafikia wakamwandikia:

"Hakika wewe umekosea katika hilo kosa la wazi na hukumu yako katika asili ya mali ni ya ajabu, bali geuza utapatia!"

Akaandika pembezoni mwa barua yao beti hizi nazo ni kutoka kwa washairi wa zamani: "Wameshasema watu bila ya elimu: 'mtu si chochote isipokuwa kwa vidogo vyake viwili.' Nikasema kauli ya mtu mwenye hekima: 'Mtu si chochote isipokuwa kwa dirhamu zake.' Ambaye hana dirhamu, watu hawatomwangalia."

Kisha alipojua kwamba kuwasiliana na kuandikiana peke yake hakukati kiu wala hakuponyi ugonjwa akaenda Iraki kwenda kuwatembelea Maimamu Maasumini عليهم السلام na kusimamisha hoja kwa wenye kumtuhumu. Kisha baada ya kuwasili katika sehemu hizo takatifu, akavaa nguo ngumu za zamani na akajipamba kwa vazi duni lisilo na heshima. Akaingia katika baadhi ya madrasa za Iraki zenye kujaa maulamaa na werevu. Akawasalimia baadhi yao na wakaitikia salamu kwa uzito na dharau. Yeye akakaa – Mwenyezi Mungu amrehemu – katika sehemu ya kuwekea viatu, na hakumwangalia

yeyote miongoni mwao na hawakumtimizia haki yake, na wakati wa majadilino yakotokea baina yao mas'ala magumu yakatatiza ufahamu wao, na zikatetereka nyayo zao. Ndipo akajibu kwa majibu tisa yenye uzuri wa hali ya juu na umakini. Baadhi yao wakamwambia kwa njia ya dharau na kejeli: "Kwa ufakiri wako umekuwa ni mwenye kutafuta elimu!"

Kisha kikaletwa chakula, hawakumkaribisha – Mwenyezi Mungu amrehemu – bali walimpatia kidogo peke yake na wao wakakusanyika mezani. Kilipomalizika kikao hicho akaondoka – Mwenyezi Mungu amrehemu – kisha akarejea siku ya pili kwao na akiwa amevaa mavazi ya kifahari, mazuri, ya utukufu, ya wasaa na kilemba kikubwa na mandhari nzuri. Alipokaribia na kuwasalimia, wakasimama kwa kumheshimu na wakampokea kwa kumkirimu. Na wakazidisha katika kumkirimu na kumfanyia mazuri. Na wakajitahidi katika kumkirimu na kumheshimu, na wakamkalisha mbele ya majilisi hiyo iliyojaa watukufu, wahakiki na wakuu na watu makini. Walipoanza majadiliano na kudurusu akazungumza nao maneno mabaya yasiyo na mwelekeo kiakili wala kisharia, lakini wakayachukulia maneno yake kwa uzuri na kujisalimisha na kutii kwa kumheshimu.

Chakula kilipoletwa wakamkaribisha kwa adabu, Sheikh akatoa vazi lake wakati wa chakula hicho kwa kuwakosoa wajuzi wale na akasema: "Kula ewe vazi langu." Walipoona hali hiyo ya ajabu wakashangaa na kustaajabu na wakamuuliza – Mwenyezi Mungu amrehemu – juu ya maneno hayo, akajibu – Mwenyezi Mungu amrehemu: "Hakika nyinyi mmeleta chakula hiki kizuri kwa ajili ya mavazi yangu ya heshima na sio kwa ajili ya utukufu wa nafsi yangu tukufu, vinginevyo mimi ndio yule wa jana na sikuona ukarimu pamoja na kwamba mimi jana niliwajia kwa vazi la mafakiri na sifa za maulamaa. Na leo nimewajia kwa vazi la wenye kiburi na nimezungumza maneno ya wajinga mkapendelea ujinga badala ya elimu,



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 150 11/23/2016 12:37:34 PM

na utajiri badala ya ufakiri. Na mimi ndio mwenye beti katika asili ya mali na matawi ya ukamilifu, ambazo nilizituma kwenu na nikazipinga kwenu. Na mkazipokea kwa kuzikosoa na mkadai kinyume cha kadhia." Basi jamaa wakakiri makosa kwa kumkosea, na wakamuomba msamaha kwa yaliyotokea kwao kwa kutomheshimu.[131]

Na anaeleza mshairi Hafidh Ibrahim juu ya hali hii katika beti tatu za shairi kwa kusema:

> "Ewe nguo yangu umenifanya baina ya watu,
> juu ya ninayoyatamani na juu ya matarajio yangu.
> Hakika watu wangu wanavutiwa na uzuri wa nguo,
> wala hawapendi isipokuwa kujionyesha.
> Thamani ya mtu kwao iko baina ya nguo,
> nzuri kwa rangi na baina ya viatu."

Na tunaweza kubainisha athari ya kisiasa katika upande huu wa utu vilevile, ambapo ni katika maslahi ya serikali fisadi kutengeneza utukufu wa utu wa uongo katika jamii, kwa sababu inaweza ushindani na kufaulu humo, ikiwa utukufu huo ndio kipimo. Mfano inapokuwa kununua vitu ndio kipimo, ambapo anayemiliki zaidi na anayetoa zaidi, na mwenye kuwa na ekari nyingi zaidi ndiye anayetangulizwa na kuheshimiwa, hakika mwenye kufaulu katika ushindani huu hakuna shaka ni watawala, na vivyo hivyo mwelekeo unapokuwa katika kutia mkazo mandhari kuwa ndio anwani ya utu wenye kuheshimika, hakika uwezekano wa jambo hili kwa watawala ni mkubwa zaidi kuliko wasiokuwa wao, na baada yao ni watu wenye mali.

Hii ni kinyume ikiwa uvumbuzi na elimu ndio kipimo katika kuheshimu utu au imani na uchamungu, kama inavyosema Qur'ani:

---

131 *Sharhu Sheikh Maitham Alaa Miati Kalmati Lil-Imami Ali* عليه السلام, kutoka katika *Raudhwatul-Jannati* cha al-Khunsaariy.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 151 11/23/2016 12:37:34 PM

"Mwenyezi Mungu anawanayanyua daraja walioamini miongoni mwenu na wale waliopewa elimu huwanyanyua daraja nyingi zaidi." Na "Hakika mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni mchamungu wenu zaidi."

Kama ambavyo tunaweza kubainisha athari hii ya kisiasa tunapoangalia katika historia – na hata sasa hivi – ambapo tunakuta kwamba mara nyingi watu walikuwa wanafuata watawala katika vazi lao na maisha yao binafsi kadiri wanavyoweza kupata njia ya kufanya hivyo. Na jambo linaweza kuwa ni la kawaida kwa kuzingatia kwamba ni moja ya athari za utawala juu ya watu, isipokuwa ikibadilika hali hiyo na kuwa utamaduni na dhana ya kijamii na anwani binafsi, inakuwa ni yenye hatari katika kutengeneza utu katika jamii.

Na tusome tamko hili kutoka katika *Murujudh-Dhahabi*.

"Na katika utawala wa Hisham bin Abdul-Maliki alitengeneza hariri na kuvuna Hariri, na watu wote wakafuata katika utawala wake mwelekeo wake na wakazuia yaliyopo mikononi mwao. Hivyo ukapungua ubora na wageni wakakatika na haikuonekana zama ngumu zaidi kuliko zama yake."[132]

Na Sulayman bin Abdil–Maliki alikuwa anavaa nguo nyepesi na nguo nzuri. Na katika zama zake alifanya kazi ya kuuza nguo za urembo Yemen, Kufah na Alexandria, na watu wote wakavaa nguo za urembo joho, shati, suruali, vilemba na kofia. Na alikuwa haingii kwake mtu katika watu wake isipokuwa akiwa amevaa nguo nzuri, na vilevile watumishi wake na wafanya kazi wake na wafuasi wake. Na aliamuru kuvikwa sanda yenye urembo (nzito)."[133]

Na vile vile tunakuta mambo katika zama za Bani Abbasi, Khalifa anakuja na anarefusha kofia na kuwa kama mkonga na watu wanamuiga. Na mwingine anakuja anaipunguza na watu wanafanya

[132] *Murujudh-Dhahabi*, Juz. 3, uk. 217.
[133] Rejea iliyotangulia, Juz. 3, uk. 185.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 152 11/23/2016 12:37:34 PM

hivyo pia. Na al-Mustainu anakuja anaanzisha vazi la kilemba kip-ana (shibiri tatu) watu wanafanya hivyo pia, n.k.

Na mitindo hatari kama tulivyotanguliza ni kubadilika mavazi haya kuwa ni kipimo cha ubora baina ya watu na kwenda kwenye kipaumbele kiasi kwamba watu wanageuka kuwa ni wenye kwenda mbio katika mtindo huu au ule, na unapungua ubora na utoaji wa kijamii kwa ajili ya maslahi ya ushindani huu wa kimandhari kama tulivyoona katika tamko ambalo linazungumzia kuhusu zama za Hisham bin Abdil-Maliki.

Kwa utenganisho huu baina ya utu na mandhari Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wanataka kutia mkazo katika tunayoyaona kupitia aina zao za mavazi (njia – aina – na rangi vilevile), pamoja na kutia mkazo juu ya usafi na kujipamba, isipokuwa sio ili kutengeneza kwa mwanadamu utu asioumiliki, kwani mwenye kuvaa mavazi ya maul-amaa hawi mwanachuoni kwa kuvaa tu mavazi hayo, na wala hawi mwenye kujinyima kwa kuvaa tu nguo zililowekwa viraka. Vivyo hivyo wema sio katika kuvaa nguo nzuri lakini wema ni utulivu na unyenyekevu kama anavyosema Mtume صلى الله عليه وآله وسلم, hakika wao wanataka kwa hilo kutia mkazo katika kutengeneza utu halisi, wenye thama-ni halisi katika dhati yake, kwa kufumbia macho mapambo ya nje, miongoni mwa uzuri au yasiyokuwa hayo. Kama yatapatikana haya pamoja na yale basi ni nuru juu ya nuru, na kama ukipatikana uzuri na mandhari mazuri bila ya utu wenye uelewa au uvumbuzi, basi inafanana na dhahabu katika jeneza!

Na kutokana na haya pia tunafikia kwenye fikra nyingine in-ayokhalifu yale ambayo yanajulikana ndani ya jamii miongoni mwa mafungamano ya kimsingi baina ya mavazi na utu. Ile rai ya ki-makosa ambayo inaona kwamba mwenye kuvua mavazi yake ras-mi basi ameshavua utu wake, na kwamba hatambui haya au yale isipokuwa ndani ya vazi rasmi. Kwa mfano tunayoyakuta katika



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 153 11/23/2016 12:37:34 PM

maisha ya maulamaa na wanafunzi wa elimu ya kidini, na mtazamo wa kimakosa wa watu wa kufungamanisha baina ya jukumu na mwonekano. Mwanachuoni kwa mtazamo wa baadhi hakika anakuwa ni mwanachuoni kweli ikiwa analazimiana na vazi hili maalum, hata kama hamiliki sifa za maulamaa isipokuwa kidogo tu. Na wala hazingatiwi kuwa ni mwanachuoni yule asiyelazimiana na vazi hili, hata kama anamiliki sifa za wanachuoni, bali sisi tunakuta nadharia hii inaendelea kwa mwanachuoni mwenyewe anapokuwa amevaa mavazi yake rasmi anapata heshima zaidi kuliko anapovua vazi hilo kwa muda.

Tunaitakidi kwamba Ahlul-Bayt عليهم السلام walifanya aina zote hizi ili kubainisha kwa watu dharura ya kutia mkazo juu ya uhalisia wa kujinyima, uhalisia wa elimu na uhalisia wa kudhihirisha neema ya Mwenyezi Mungu. Na vivyo hivyo kwa kila uhalisia kulingana na nafasi yake. Na tutaeleza baadhi ya hadithi katika nyanja hii:

Kuhusu Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: Imepokewa kwamba alikuwa anavaa nguo anayopata miongoni mwa shuka na nguo ya kujitanda au shati au joho au nyingineyo. Na alikuwa anavutiwa na nguo za kijani, na vazi lake mara nyingi lilikuwa ni jeupe, na alikuwa na kofia ya hariri anaivaa na kijani chake kinapamba juu ya weupe wa rangi yake. Na alikuwa na kilemba kilichopambwa kwa zafarani, na wakati mwingine alivaa shuka peke yake, na alikuwa na shuka jeusi akalitoa zawadi, Ummu Salama akamwambia: "Naapa kwa baba yangu na mama yangu umefanya nini kwa hilo shuka jeusi?" Akasema: "Nimemvisha." Akasema: "Sijaona kitu katu kizuri kuliko weupe wako katika weusi wake."[134] Na mara nyingi alikuwa anatembea bila ya viatu bila ya kujitanda shuka, kilemba wala kofia kama ilivyo katika habari alipokwenda kumzuru Saad bin Ubadah.[135]

[134] *Al-Mahajatul-Baidhai*, Juz. 4, uk. 140.
[135] Rejea iliyotangulia, Juz. 4, uk. 126.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 154 11/23/2016 12:37:34 PM

Na kuhusu Sajjad عليه السلام, mmoja wa wafuasi wake alimuona akiwa amevaa joho la hariri na koti la hariri na kilemba cha hariri na amejipamba kwa vazi la ghali, akielekea kwenye msikiti wa babu yake Mtume صلى الله عليه وآله وسلم, kama ambavyo mwingine alimuona amevaa kitani na shuka la bluu. Na mmoja wa wafuasi wake alimuona yuko katika hali mbili, katika siku hiyo alikuwa amevaa nguo ya njano na baadaye alimuona amevaa ngumu iliyofumwa kwa hariri. Akamuuliza juu ya hilo akasema kwamba yeye alikuwa ameoa karibuni na siku iliyopita ilikuwa ni siku ya yule mwanamke na alipenda ajipambe kwa ajili yake.

Kama ambavyo anavaa nguo hizo za thamani na nzuri, hakika yeye katika sehemu nyingine anataka kufundisha na kuelekeza athari ya kujipamba sana, na madhara yake kitabia, na athari ya kukosekana uwiano inayoachwa katika utu wa wanyonge, hivyo anaacha kuvaa nguo nzuri. Wakati mmoja alivaa nguo nzuri na za thamani, na akatembea nazo hatua kadhaa kisha akarejea haraka na akamwambia mtumishi wake, nipe nguo zangu za awali, hakika nimeshatembea na nguo hizi kana kwamba mimi sio Ali bin Husein عليه السلام.[136]

Vilevile hakika wao walivaa aina mbalimbali za mavazi na rangi maadamu rangi hiyo na aina hiyo sio alama ya maadui wa dini kama itakavyokuja. Kama ambavyo Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alivaa shuka jeusi, vilevile Amirul-Muminina عليه السلام alitoka kwenda kwenye mkusanyiko huku akiwa amevaa nguo nyeusi, na vilevile ya njano. Amepokea Zurarah amesema: Abu Ja'far alitoka kuswalisha baadhi ya watoto wao huku akiwa amevaa joho la hariri la njano na kilemba cha njano na koti la hariri la njano [137]na vilevile jekundu na la bluu.

Kutoka kwa al-Hikam bin Uyainah amesema: "Nilimuona Abu Ja'far al-Baqir عليه السلام amevaa shuka jekundu, nikamtazama sana,

[136] *Awaalimul-Ulumi* cha Imam Ali bin Husein عليه السلام, uk. 136.
[137] *Makarimul-Akhlaq*.

akasema: 'Ewe Abu Muhammad hakika hili halina ubaya.' Kisha akasoma: 'Sema ni nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amelitoa kwa waja Wake, na mazuri miongoni mwa riziki.'" Na kutoka kwa Sulayman bin Rashid kutoka kwa baba yake amesema: "Nilimuona Ali Abul-Hasan عليه السلام kavaa shuka la bluu."[138]

**1. Kanuni ya kuvaa vazi nadhifu na zuri:**

Vazi ni stara na pambo, na kisha liko katika pande mbili, ni mwonekano wa kijamii, kwani haiwezekani kufikiria stara isipokuwa pamoja na uwepo wa mtu mwingine. Na hali ni hiyo hiyo kuhusiana na pambo. Na kwa sababu ni mwonekano wa kijamii basi unawiana pamoja na mahitaji ya kijamii, wakati ambapo kama utatosheka na upande wa mtu binafsi, mambo yanaweza kubadilika. Kama tutakavyoeleza hayo katika utafiti wa chakula na mlo, ambapo chakula ni jambo la kibinafsi kwa kawaida, wakati ambapo mwonekano ni jambo la kijamii kwa kawaida. Na tunasema kwa kawaida, kwa sababu sisi kama tutatenganisha kati ya vazi na uwepo wa kijamii, tunaweza kusema bila ya anwani iliyotangulia, na tungetanguliza upande wa ugumu na kujinyima, kama yalivyo madhumuni ya baadhi ya hadithi ambazo zinanukuliwa kwamba wao walikuwa wanavaa katika dhahiri vazi laini wakati ambapo wanayoyatanguliza ndani yalikuwa ni mavazi magumu. Na hali ni hiyo hiyo katika Swala na wakati mwingine nyumbani.

Ama kuhusu wanayoyavaa kuwa nadhifu, ni kwa dharura ya kuafikiana na idadi kubwa ya hadithi zinazoamrisha usafi na kujisafisha. Na sisi tunaona kwamba hata katika hali ambazo zinanukuliwa humo, vazi la Maasumu kuwa ni vazi la kawaida hakika hiyo haimanishi kuwa ni chafu, bali hakika sisi tunakuta katika hadithi picha ya kipekee kwa wanaojidai watu wa kujinyima. Ambao nafsi zinapata kinyaa kutokana na hali yao chafu na mavazi yao machafu

[138] Rejea iliyotangulia.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 156 11/23/2016 12:37:34 PM

yenye harufu mbaya. Kama ambavyo sisi tunapoona maneno ya hadithi, tunakuta kwamba zinaunganisha kati ya usafi na kujikwatua katika upande mmoja, na athari zinazotokana na hayo, au kuchukia picha ya kinyume wakati zinapozungumzia mkabala wake miongoni mwa uchafu, na hizi hapa ni baadhi ya hadithi:

a- **Athari za kiibada:**

Kwa kuangalia yale yanayoleta usafi miongoni mwa utakaso, sawa iwe kwa mtu au katika vazi. Ndio maana amri ya Mtume ﷺ ya kuamrisha usafi ilikuwa inakaririwa mara kwa mara, kwa sababu Uislamu umejengwa juu ya usafi, sawa uwe usafi wa nje kama ambavyo sisi tumo humo, au usafi wa ndani. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Jisafisheni kadri muwezavyo; hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri na anapenda uzuri, na ni msafi anapenda usafi." Kama ambavyo mtu anapojitwaharisha na kisha akalala, malaika miongoni mwa malaika anamuombea maghufira, hakika athari hiyo hiyo inakuwepo katika nguo nadhifu. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Ewe Aisha fua nguo hizi mbili je, hujajua kwamba nguo inafanya tasbihi, inapochafuka inakatika tasbihi yake."[139] Na hatuwezi kufahamu namna ya tasbihi ya nguo lakini hadithi inatuwekea wazi uhusiano uliopo baina ya ibada na usafi wa nguo. Hivyo ilikuwa ni miongoni mwa tabia za Manabii kujisafisha.[140]

**b- Athari za kinafsi na za kijamii:**

Mwanadamu anaamiliana (kuathiri na kuthiriwa) pamoja na mazingira yanayomzunguka. Kama ambavyo anahisi utanashati na uchangamfu wakati anapokuwa katika hewa nzuri na mazingira mazuri, vilevile hakika usafi wa nguo unaondoa adha na huzuni kama anavyosema Amirul-Mu'minin عليه السلام, na hili ni jambo linaloonekana

[139] *Mizanul-Hikma*, uk. 10.
[140] *Biharul-An'war*, Juz. 78, uk. 335.

katika uhalisia wa kijamii. Kwa kuongezea katika hilo "Hakika Mwenyezi Mungu anapenda uzuri na kujipamba na anachukia ubaya na kujichafua." "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anapomneemesha mja wake na neema yoyote, anapenda kuona athari zake kwake." Ikasemwa, kwa vipi? Akasema Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Anasafisha nguo zake, anajifukiza manukato na anatengeneza nyumba yake vizuri na anafagia mazingira yake, hadi kwamba, kuwasha taa kabla ya kuzama jua kunazuia ufakiri na kunaongeza riziki."

Kama ambavyo unadhifu na kujikwatua kwa kuzingatia kuwa ni mwonekano wa kijamii kunaathiri athari maalumu katika kudhihirisha sura ya mtu na jamii mbele ya adui, pia kujisafisha na kujikwatua kunamfurahisha rafiki, na "Nguo safi inamvunja adui" kama ilivyopokewa kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام, hiyo ni kwa sababu vazi linadhihirisha utajiri na manukato yanaondoa ubaya. Kwa sababu mwonekano huu una athari katika utu wa mtu, ambapo mtu mchafu hapati heshima kama anavyostahili, na kwa sababu hiyo Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amelaumu aina hii ya watu kwa kusema: "Mja mbaya ni yule mchafu." Na "Wameangamia wachafu."

Na angalizo ni kwamba kadhia hii haifungamani na ufakiri bali inafungamana kwa daraja la kwanza na uchache wa vionjo au mtazamo mbaya au na uvivu, na kwa hiyo Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amefuatilizia kwa maelekezo ya aina hii miongoni mwa hali hizi; kutoka kwa Jabir bin Abdillahi amesema: "Tulimwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم akaona mtu mchafu nywele zake zimetawanyika, akasema: 'Je, huyu hakuwa anaweza kupata kinachoweza kuchana nywele zake?' Na alimuona mtu mwingine amevaa nguo chafu akasema: 'Je huyu hakuwa anaweza kupata maji ya kufua nguo yake?'"[141]

Na hakuna mgongano baina ya fungu hili la hadithi na zile ambazo zinasema kwamba uzuri ni kwa akili na uzuri wa mantiki, utu-

[141] *Mizanul-Hikma*, Juz. 10, uk. 92.

livu na unyenyekevu. Na kila fungu linajadili maudhui maalumu na kuyajumuisha. Hakika uzuri wa sura ni uzuri wa nje na uzuri wa akili ni uzuri wa ndani.

Na inapasa kuashiria kwamba unadhifu na usafi haulazimiani na ubadhirifu kama ambavyo inaeleweka kwa baadhi, na haya ni makusudio ya mshangao wa Mtume ﷺ je, hakuwa anaweza kupata maji? Je, hakuwa anaweza kupata cha kuchania nywele zake? Ambapo inaonyesha urahisi wa kukipata kwake. Kwa kuongezea kwamba kujikwatua ni kwa kutumia vionjo vya hali ya juu katika kusawazisha vazi au umbo la nje, mtu anaweza kutoa mali nyingi katika mavazi yake lakini kwa kukosekana vionjo vyake hawezi kujikwatua. Na mwingine anaweza kuvaa mavazi ya kawaida yasio ya thamani lakini kwa vionjo sahihi yanakuwa ni mazuri na yenye kuvutia.

Baada ya maelezo haya tunarejea katika mwanzo wa maudhui ambapo tulisema kwamba kanuni kwa Ahlul-Bayt عليهم السلام katika tunayoyafahamu katika mas'ala ya mwonekano ni hali ya kijamii, hakika wao walikuwa wanavaa nguo nadhifu na nzuri. Na mavazi hayo yanaweza kuwa ni ya thamani ndogo au kubwa kulingana na utangulizi ambao umeshatangulia kutajwa katika mwanzo wa utafiti, isipokuwa ni kwamba inapatikana katika kanuni hii mambo ya kipekee yanayolazimishwa na mazingira maalumu, yanayobadilisha kanuni hii kwenda kwenye anwani nyingine.

**a- Mazingira yanayoamabatana na nafasi ya uongozi aliyonayo Maasumu:**

Hiyo ni kwa sababu nafasi hii inamlazimisha mtawala kuifunga nafsi yake kwa ada na kanuni maalum hususan kuchunga hali ya kijamii. Na huenda tukapata hilo katika majadiliano ya Amirul- Muuminina pamoja na Alau bin Ziyad al-Harithiy alipomlalamikia ndugu yake Asimu kwa Imamu kwa kusema: "Ewe Amirul Muuminina na-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 159 11/23/2016 12:37:34 PM

kushitakia ndugu yangu Asimu bin Ziyad." Akasema: "Ana nini?" Akasema: "Amevaa joho na ameachana na dunia." Akasema: "Mlete kwangu." Alipokuja akamwambia: "Ewe mwenye kuuwa mbali nafsi yake, umekuongoza uovu, je humhurumii mke wako na watoto wako? Je unadhani Mwenyezi Mungu amekuhalalishia mazuri hali ya kuwa anachukia kuyatumia? Wewe ni dhalili mno kwa Mwenyezi Mungu kuliko hayo!" Akasema: "Ewe Amirul-Mu'minin wewe uko katika vazi gumu na chakula chako ni duni." Akasema: "Ole wako, hakika mimi sio kama wewe, hakika Mwenyezi Mungu amefaradhisha kwa Maimamu waadilifu wakadirie nafsi zao kwa udhaifu wa watu ili asidhurike fakiri kwa ufakiri wake."[142]

Na mtawala wa kisharia – wa uhakika – ni ambaye anaichagulia nafsi yake magumu zaidi. Pamoja na kuwepo mafunzo haya, isipokuwa hakika sisi tunakuta wengi wa watawala wa Kiislamu walikuwa wanayapuuza, ingekuwaje kama yasingekuwepo?

**b- Mazingira yanayoambatana na hali ya kimaada kwa watu wa kawaida:**

Ambapo yanaweza kupita kwa jamii mazingira ya taabu, njaa na ukata, na hapa haiingii akilini kwa mtawala kujipamba (kujikwatua) katika muonekano wake na mavazi yake wakati ambapo watu wote wanakabiliwa na mambo hayo mawili!

**c- Hali za kuongoza na za mafunzo ya kimalezi:**

Umeshapita utajo wake katika maelezo ya hadithi zilizotangulia.

## MAVAZI YENYE KULAUMIWA:

Hatutaorodhesha maneno yote yaliyopo chini ya anwani hii. Katika fikihi mafakihi mara nyingi wanatafiti idadi ya maneno yanayohu-

[142] *Nahjul-Balaghah*, Hekima ya 209.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 160 11/23/2016 12:37:34 PM

siana na anwani hii, kama vile kuvaa dhahabu na hariri kwa mwanaume. Au mwanaume kuvaa mavazi mahususi kwa ajili ya wanawake au kinyume chake, na maneno mengine, sawa iwe katika wakati wa swala au popote. Lakini sisi hapa tutatafiti juu ya maneno mengine nayo ni:

**Vazi la Maadui wa Dini:**

Vazi linaweza kugeuka na kuwa nembo na ufuasi wa mrengo, na wakati huo inahukumiwa kwa hukumu yake. Na linaweza kuwa ni la jumla bila ya kuwa ni nembo. Hakika sisi tunakuta katika hadithi kwamba weusi katika mavazi kwa mfano, huwa haupendwi na haupendelewi, sio kwa sababu unaonyesha huzuni kama ilivyozoeleka sasa hivi, bali ni kwa sababu ulikuwa – wakati huo – ni nembo ya dola ya Bani Abbasi na serikali yao. Kuvaa nguo za rangi hii ilikuwa inamaanisha uungaji mkono wa kisiasa, na kufungamana pamoja nayo. Na kwa sababu hii hakika Maamun baada ya kufariki Imamu Ridha عليه السلام Bani Abbas ili kuwaweka karibu mahasimu wao upya walibadili na kuvaa nembo ya kijani, na vazi la kijani ambalo lilikuwa linajulikana kwamba ni vazi la Alawiyina [143] badala ya rangi nyeusi ambayo ilikuwa ni nembo ya Bani Abbasi, na sisi tunaona hali ya nembo nyeusi tunaposoma katika historia ya wakati huo kwamba Bani Abbasi baada ya Maamun kuacha nguo nyeusi na akachagua kijani wakaona kuwa hilo ni kubwa na wakamwambia abadilishe kwenda katika nyeusi na akafanya hivyo, kama anavyosema al-Mas'udiy katika kitabu chake cha historia *Murujudhahabi*.

Vilevile hakika sisi tunaona pia kwamba katika hukumu ya kuchukia kuvaa pete katika mkono wa kushoto na kupendeza katika mkono wa kulia, Nabii صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa anavaa pete katika mkono wa kulia basi Muawiya akaifanya iwe katika mkono wa kushoto. Na

[143] Pamoja na kuwepo mjadala katika kuwa kijani ni nembo ya Maalawiya.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 161 11/23/2016 12:37:34 PM

watu wakachukua hilo hadi katika utawala wa Safaha al-Abbasiy, akabadilisha hilo na kuwa katika mkono wa kulia, na ikabakia hivyo hadi katika utawala wa Rashidi ambapo kuvaa pete ikawa ni katika mkono wa kushoto na watu wakachukua hilo.[144]

Na tunakuta katika historia ya leo vilevile mfano unaofanana na hayo, ambapo Ataturuk wa Uturuki alichukua hatua kadhaa ndani ya harakati zake za kuwabadilisha Waislamu wawe wa kimagharibi, miongoni mwazo ni kubadilisha herufi za kiarabu na kuwa za kilatini. Na miongoni mwazo ni kuzuia hijabu kwa wanawake na kuwalazimisha wanaume kuvaa mavazi ya kimagharibi (suti na tarabushi) na kuharamisha kilemba.

Hakika vazi linapokuwa ni tangazo la utamaduni wa maadui wa dini, nembo ya nguvu yao na ufuasi wa utamaduni wao na njia yao, inakuwa ni hatari kubwa inayotishia utu wa Mwislamu katika utamdauni wake na kutishia jamii ya Kiislamu kwa kukosekana uhuru wake na ufuasi wa jamii yake kwenye dini yake. Na huenda inakuwa ni sababu ambayo baadhi ya maulamaa wa Kiislamu wameweka mpaka katika zama zilizopita kwa kuharamisha vazi la wazungu, au kuharamisha tai ya shingoni kwa kuwa vazi hili wakati huo lilizingatiwa kuwa ni kujifananisha na makafiri na kushikamana na utamaduni wao na nembo yao. Na hili ni jambo linazunguka katika mzunguko wa nembo, vazi na Mwislamu kujifananisha na asiyekuwa Mwislamu.

**Vazi la Fitina:**

Linalotoka nje ya uzio wa kisharia au rai ya desturi ya mwanadini. Tumeshatangulia kubainisha kwamba jukumu la msingi katika mavazi ni kujisitiri "linasitiri aibu zenu", kisha ni pambo, "Sema nani ameharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amelitoa kwa

[144] *Biharul-An'war*, Juz. 42, Uk. 62.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 162 11/23/2016 12:37:34 PM

waja Wake." Na katika kujisitiri ni kinga kutokana na sababu za kimazingira zinazoudhi afya ya mwandamu, isipokuwa kumekuwepo na kukuza mazingatio ya kijamii ya kimakosa au haja ya binadamu – mume au mke – kwa kuamsha mazingatio ya jinsia nyingine, na hivyo inakuwa mazingatio yake wakati huo ni kuvaa kulingana na raghaba ya wengine. Na inawezekana asivutiwe yeye binafsi na aina hii au na rangi ile, lakini kwa kuchochewa kwake na upande mwingine anaizoesha nafsi yake juu ya vazi hilo. Na unaweza kufikiria ushindani ambao unatokea katika lengo hili. Hakika kila mtu anapotoa juhudi zake katika uchochezi, kwa kiasi au kwa namna nyingine anageuka kuwa mwanamitindo wa mavazi bila ya malipo. Haya na kwa kuongezea katika madhara na uharibifu wa kijamii na ukiukwaji ambao utazalishwa katika mabadiliko ya mwendo wa jamii au baadhi ya makundi yake katika uwiano wa uchochezi huu.

**Vazi la Umaarufu:**

Uislamu unamwangalia Mwislamu kuwa anaishi katika jamii, nao katika mazingatio haya unamtaka awe ni mwanaharakati mwenye kuathiri humo, ambapo inatakiwa kwake awe na uhusiano wa mafungamano pamoja nayo jamii hiyo, ambapo uhusiano wa kiuadui pamoja na jamii au kujitenga nayo kunamzuia kufanya wajibu wake na jukumu lake. Na Uislamu unampa Mwislamu nafasi pana katika nyanja ya mbinu ili kurahisisha harakati wakati ambapo unamtaka kuwa imara katika kufungamana na misingi. Katika mas'ala ya vazi – kwa kuangalia kuwa ni moja ya sababu ya mafungamano – unamwambia: "Vazi bora kwa kila zama ni vazi la watu wake," yaani lililozoeleka katika vazi lao. Kwa sababu kutumia vazi hili lililozoeleka kunafanya kazi yake kuwa nyepesi na rahisi. Wakati ambapo kosa ambalo wanatumbukia humo baadhi ya wafanyakazi hakika ni wao kuwa wanapoteza misingi kwa kutofungamana kwao



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 163 11/23/2016 12:37:34 PM

na jamii wakati wanang'ang'ania, na wanakuwa wagumu katika mambo ya mbinu yasiyo na umuhimu isipokuwa katika upande wa kuwa kwake ni njia na nyenzo.

Tunayoyakuta leo katika kupunguza sana nguo, na ambayo wanayafuata baadhi ya Waislamu, kiasi kwamba mtu anageuza nguo kuwa ni sketi fupi ya kiume, na anageuka mvaaji huyu kuwa ni kichekesho miongoni mwa watu na jambo la fedheha na istihizai, hakika hayo ni makosa katika nyenzo na usahihi wa mbinu, hivyo wanapoteza katika hilo uwezekano wa kuongoa watu, nalo ndio lengo la kimsingi, kwa maslahi ya kupunguza nguo, nalo ni jambo la mustahabu katika makadirio mazuri. Wakati ambapo hadithi iliyotangulia iliyopokewa ndio hakimu juu ya hadithi zilizobakia.

Na inawezana kwa sababu hii ndio maana zimepatikana hadithi zinazolaumu nguo za umaarufu, bali kila inayomfanya atajwe vibaya. Kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu anachukia vazi linalomfanya mtu awe mashuhuri." Na katika hadithi nyingine inaeleza sababu hiyo kwamba inaleta madhila na fedheha: "Yatosha kuwa fedheha kwa mtu kuvaa nguo au kupanda kipando kinachomfanya awe mashuhuri." Na katika hilo pia zinaingia nguo za usufi (mahususi) ambazo wanazivaa wanaojidai kuwa ni watu wa kujinyima ili kuwanasa wajinga na wasiojua miongoni mwa watu. Hiyo inawasukuma kwenye ria, na imeshapita kabla ya hapo riwaya ya Imamu as-Sadiq عليه السلام alipowajadili hao watu na akafedhehesha nia zao.

## MAS'ALA YA KIVITENDO NA UHALISIA:

Kuna baadhi ya maelekezo ya kidini katika hadithi ambayo inafaa kuyaita jina la maelekezo ya kimaisha pamoja na kwamba ni maelekezo ya kidini katika ujumla wake wa kimaisha: "Enyi mlioamini



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 164 11/23/2016 12:37:34 PM

mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume wanapowaita katika yale yanayokupeni uhai." Isipokuwa kuna tofauti katika mahusiano ya maelekezo haya. Amri ya Swala ya usiku kwa mfano inatofautiana na amri ya kutokulala juu ya paa lisilo na uzio. Ambapo amri ya kwanza ni amri halisi ya Mwenyezi Mungu, haina mwingiliano na uzoefu wa kibinadamu kwa karibu au kwa mbali, wakati ambapo amri ya pili inawezekana kuifikia kwa akili na uzoefu wa kibinadamu vilevile.

Pamoja na kwamba kazi ya kimsingi ya ujumbe ni kubainisha upande uliofichikana ambao mwanadamu haufikii kwa akili yake, ila ni kwamba upande mwingine hauko mbali na duara. Kuna idadi ya hadithi zinazofuatia chini ya anwani "adabu na sunnah," na sisi tunaona aina hii ni miongoni mwa hadithi za maudhui yetu, katika jawabu la Imamu al-Kadhim عليه السلام kwa aliyemuuliza je, ni ubadhirifu mtu kuwa na mashati kumi? Alisema: "Hapana, lakini hiyo inasaidia nguo zake kudumu zaidi, lakini ubadhirifu ni kuvaa nguo ya heshima yako katika sehemu chafu." Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Ubadhirifu ni kuifanya nguo ya heshima yako kuwa nguo ya uchafu wako."

Hakika sisi tunakuta hapa kwamba mas'ala yanazungumzia kadhia ya uhalisia kwa nje, hivyo ni wazi kwamba sisi wakati wa kulinganisha baina ya watu wawili, mmoja wao anatumia nguo tatu na anazivaa kwa mzunguko ndani ya mwaka, na mwingine anatumia nguo sita anazivaa kwa mzunguko katika kipindi cha mwaka, hakika kwa wa kwanza tutahitajia zaidi ya nguo sita kwa mwaka kwa kuwa zitakwisha ndani ya muda mfupi kutokana na wingi wa matumizi yake, wakati ambapo wa pili hatahitaji hayo, na hili lina uzoefu kwa watu.

Hivyo wakati huo huo ambao kuna kanuni humo yenye kutawala katika upande huu; isiwe ni katika mavazi ya maadui wa Mwe-

nyezi Mungu na alama zao na isiwe ni katika nguo zinazomfanya mtu kuwa mashuhuri, na iwe ni yenye kusitiri na iwe ni katika vazi la watu wa wakati kwa sababu vazi bora ni vazi la watu wake, kwa kuongezea katika hayo ni kuwe na uwiano wa kivitendo katika kulitumia kwake, na hii ni katika mas'ala ya kimaisha ya jumla ambayo hadithi zinaelekeza kwayo.

Hadi hapa tunamaliza mzunguko huu, baada ya maelezo haya ya hali za Maasumini عليهم السلام katika maisha yao ya kijamii, na moja ya mwonekano wake ulikuwa ni mavazi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 166 11/23/2016 12:37:34 PM

# SEHEMU YA NNE

## CHAKULA NA KINYWAJI

Mwenye kuchunguza maisha ya Maasumini عليهم السلام ataona kwamba wao walichukua msimamo mmoja katika yanayohusiana na chakula na kinywaji. Na msimamo huo ni dhidi ya mtazamo wa shibe na kufurutu. Hiyo ni kwa sababu sura inayojitokeza zaidi katika mtazamo wa kujinyima na kuiacha dunia ni kuchukua msimamo dhidi ya mahitaji ya tumbo na shinikizo lake. Na tofauti baina ya utafiti uliotangulia na ambao tulifikia kusema kwamba asili ilikuwa ni kujikwatua na kudhihirisha neema ya Mwenyezi Mungu, na utafiti wetu huu ambao tunatarajia kusema kinyume chake, tofauti ni kwamba vazi na ambayo yanahusiana nalo miongoni mwa manukato na kujikwatua ni mwonekano wa kijamii, kabla ya kuwa ni jambo la kibinasfi, kwa kuzingatia kwamba uwepo wa Maasumini عليهم السلام ni katika uwanja wa kijamii, na huenda kama lingekuwa ni jambo la kibinafsi msimamo ungekuwa unatofautiana kama tuliyoyataja katika kurasa zilizotangulia.

Wakati ambapo kadhia ya chakula na kinywaji kwa kawaida ni jambo la kibinafsi, wanaojidai kuwa ni watu wa kujinyima walikuwa wanageuza mas'ala na kuyafanya kuwa ni mwonekano wao wa nje wenye kuonyesha hali yao ya kujinyima, wakati ambapo katika uhalisia wao wa ndani wanaachia uroho na matamanio yao kupupia dunia.

Na tunaweza kufahamu msimamo wa mtu katika dunia kupitia kufaulu kwake katika mtihani huu ulio karibu wa kila siku. Baadhi



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 167 11/23/2016 12:37:34 PM

wanaweza kujidhihirisha kwa kujinyima na ibada – kwa mfano – mbele ya watu kupitia mavazi yao, na nyuradi nyingi na kufaulu kutoa picha hii, lakini hawawezi kuendelea katika kuacha chakula kizuri na vinywaji, nalo ni jambo la kibinafsi, ambalo kwa kawaida linafichikana kwa watu. Hivyo tunaweza kusema kwamba msingi mkuu ambao Ahlul-Bayt عليهم السلام wanaufuata ni ule ambao anautoa Amirul-Mu'minin عليه السلام kama mfano katika wasifu wake kupitia kwa rafiki yake: "Alikuwa nje ya mamlaka ya tumbo lake, hivyo hatamani asiyoyapata wala hazidishi anapopata."

Na wala hayo hayamaanishi kwamba wao walikuwa wanaharamisha chakula kizuri au wanajiepusha nacho kwa kukichukia. Katika yaliyopokewa kutoka kwao ni kwamba wao walikuwa wanakula na wanakunywa vitu vizuri – kama itakavyokuja – lakini msingi mkuu ni kwamba wao walikuwa wanaamiliana pamoja na nafsi zao kwa moyo wa kutosheka na wanazingatia kwamba ujumbe wao sio kujaza tumbo. Hakika hawaishi ili wale bali wanakula ambacho kinahifadhi uhai wao kwa jili ya kutekeleza jukumu lao. Na inadhihirika kwamba njia hii ndio mwendelezo wa njia ya Manabii watukufu wa Mwenyezi Mungu ambao walihitimisha uwepo wao katika ujumbe wao, wakati ambapo mafirauni, madikteta na mafisadi walihitimisha maisha yao katika matumbo yao na yaliyo chini yake.

Na kwa kweli ilikuwa inaosha kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwako kuwa ni mfano na ni dalili yako ya kuipuuza dunia na kuibeza, kwa sababu ya wingi wa aibu zake na mabaya yake, kwa kuwa pande zake zilibanwa mbali na yeye hali ikiwa pande zake yeye zimekunjuliwa kwa wengine, na alikatishwa kunyonya kwake na kukatazwa mapambo yake. Na ukipenda (ukiwa ni mfano wa pili) nitakusimulia kuhusu Musa عليه السلام msemeshwa wa Mwenyezi Mungu aliposema: "Eee Mola Wangu kwa kweli mimi ni mhitaji wa kheri yoyote utakayonitunukia." (28: 24) Naapa kwa Mwenyezi Mungu



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 168 11/23/2016 12:37:35 PM

Musa hakuomba isipokuwa mkate ale, kwa kuwa yeye alikuwa anakula mimea ya ardhini kiasi kwamba rangi ya kijani ilikuwa inaonekana kutokana na ulaini wa ngozi ya tumbo lake, kwa sababu ya wembamba wake na uhaba wa nyama yake.

Na ukitaka nitakupa mfano wa tatu wa Nabii Daud عليه السلام Bwana wa Zaburi na msomaji wa watu wa peponi. Alikuwa anatengeneza vikapu kwa makuti ya mitende kwa mkono wake na kuwaomba anaoketi nao: Ni nani kati yenu atanisaidia kuviuza? Na alikuwa anakula mkate wa shairi kutokana na thamani yake.

Na ukitaka nitakusimulia juu ya Isa bin Mariyam عليه السلام, kwa kweli alifanya jiwe ndio mto wake, na alikuwa anavaa nguo ngumu na kula chakula kigumu, kitoweo chake kilikuwa ni njaa, na usiku taa yake ni mwezi. Na makazi yake wakati wa masika ni Mashariki ya ardhi na Magharibi yake. Na matunda yake na maua yake ni mimea ioteshwayo na rdhi kwa ajili ya wanyama. Na hakuwa na mke wa kumvutia, wala mtoto wa kuhuzunisha, wala mali ya kumgeuza mawazo, wala tamaa ya kumdhalilisha. Mnyama wa kipando safarini ni miguu yake na mtumishi wake ni mikono yake.

Na muige Nabii wako mzuri aliye safi صلى الله عليه وآله وسلم kwani kwake yeye kuna mfano kwa mwenye kutaka mfano, na ni ushauri kwa mwenye kutaka ushauri. Na mja mpendwa mno kwa Mwenyezi Mungu, ni yule mwenye kuiga mfano wa Nabii, afuataye nyanyo zake. Alichukua kutoka katika dunia hii kiasi kidogo na wala hakuitupia jicho kwa kiwango kikubwa. Ni mwenye tumbo tupu mno katika watu wa dunia. Alikuwa na tumbo lililo bora mno katika dunia. Alipewa dunia hii na aliikataa, hakuikubali. Na akijua kwamba Mwenyezi Mungu anachukia kitu naye hukichukia, na akikidunisha kitu naye hukidunisha, na akikidogesha kitu naye hukidogesha. Lau kusingekuwa katika sisi ila kupenda kwetu alichokichukia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na kukitukuza alichokidharau Mwenyezi Mungu na Mtume



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 169 11/23/2016 12:37:35 PM

Wake, hilo lingetosha kuwa ni kujiweka mbali na Mwenyezi Mungu na ni kukiuka amri ya Mweneyzi Mungu.

Hakika Mtume ﷺ alikuwa akila chini ya ardhi na anakaa kwa unyenyekevu kama anavyokaa mtumwa. Na alikuwa anashona viatu vyake kwa mkono wake na anatia kiraka nguo zake. Alikuwa anapanda punda asiye na tandiko, na kumpakia mtu nyuma yake. Na ikiwa kuna pazia katika mlango wa nyumba yake yenye picha humo humwambia mmoja wa wke zake: "Ewe fulani – iondoe mbali na mimi, kwa kuwa mimi nikiiangalia nitaikumbuka dunia na mapambo yake."

Akawa anaipa dunia kisogo kwa moyo wake na akafisha kumbukumbu yake katika nafsi yake. Na alipenda mapambo yake yatokomee mbali na macho yake ili asichukue humo vazi la pambo wala asiitakidi kuwa ni mahala pa kuishi, wala asitarajie makazi humo. Akaitoa nje ya mazingatio yake na akaing'oa katika moyo na akaitoa machoni. Na vilevile mwenye kuchukia kitu anachukia kukiangalia na kutajwa mbele yake.

Na kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kulikuwa na kila liwezalo kukujulisha na kukuonya dhidi ya maovu ya dunia na aibu zake, pale aliposhikwa na njaa licha ya nafasi yake mbele ya Mola Wake pamoja na umahususi wake. Na yamewekwa mbali na yeye mapambo ya dunia yake hali akiwa na utukufu mno wa ukaribu. Hivyo basi mwangaliaji na aangalie kwa akili yake. Je, Mwenyezi Mungu amempa heshima kwa hilo au amemdhalilisha? Ikiwa atasema: Amemdhalilisha; basi ajue kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtweza mwingine kwa kumkunjulia dunia na kuikunja mbali na mtu aliye karibu sana na Yeye.

Na amfuate mfuataji Nabii wake na akanyage alipokanyaga na aingie alipoingia, vinginevyo hatonusurika dhidi ya maangam-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 170 11/23/2016 12:37:35 PM

izi. Kwa hakika Mwenyezi Mungu amemfanya Muhammad ﷺ kuwa ni alama ya Kiyama na mbashiri wa pepo na muonyaji dhidi ya adhabu. Aliiaga dunia hali akiwa tumbo tupu, amekwenda akhera akiwa salama. Hakuweka jiwe juu ya jiwe hadi alipofariki na amemwitika mwitaji wa Mola Wake. Ni neema kubwa ilioje ya Mwenyezi Mungu kwetu alipomneesha juu yetu akiwa mtanguliaji tunayemfuata, na ni kiongozi ambaye tunafuata nyayo zake. Wallahi nilishatia viraka kanzu yangu, hadi nikaona aibu kwa viraka vyake na alishaniambia mimi msemaji: Je, huitupi? Nikasema: Niondokee mbele yangu, kwani asubuhi watu watasifia mwendo.[145]

Hakika sisi tunaitakidi kwamba mwanadamu habakii katika maisha yake katika faragha ila ni lazima awe ni mwenye ujumbe. Ikiwa ujumbe huo haukuwa ni kitovu cha dini au jamii hakika kitovu chake kitakuwa ni dhati na matamanio, na kwa hiyo tunaweza kupambanua baina ya aina mbili kati ya watu: Aina inayojitahidi kufanya bidii, kujituma na kupambana – wakati mwingine – ili ipate chakula kitamu, tandiko zuri na mke mzuri. Na aina nyingine inafikiria katika lengo ambalo ameumbwa kwa ajili yake, sawa awe amepata mambo hayo katika njia au hakupata, jambo kwake ni sawsawa: "Sikuumbwa ili nishughulishwe na chakula kizuri kama mnyama aliyefungwa, lengo lake ni malisho yake, au asiyefungwa, kazi yake ni chakula chake, ashibe kutokana na chakula chake na anapuuza ambayo yanatakiwa kwake." Kama anavyosema Amirul-Mu'minin عليه السلام na ulivyo mtazamo wake juu ya yale yanayojaza tumbo lake, na alikuwa anatisisitiza hilo katika sehemu zaidi ya moja. Siku moja alikula katika tende mbaya kisha akanywa maji na akapiga mkono wake juu ya tumbo lake na akasema: "Mwenye kuingiza tumbo lake motoni, basi Mwenyezi Mungu amemuweka mbali." Kisha akasoma shairi kwa

[145] *Nahajul-Balaghah*, Hotuba ya 158.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 171 11/23/2016 12:37:35 PM

kusema: "Vyovyote utakavyolipa tumbo lako na utupu wako haja yake, bado vitaendelea kulaumu."[146]

Na ni wajibu iwe wazi kwamba Maasumini عليهم السلام walikuwa katika wakati huo huo wakiendelea kuwapa watu kwa wingi, lakini wao katika yanayofungamana na nafsi zao wanatosheka na kichache, Imamu Hasan عليه السلام naye ndio mkarimu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام - na wote ni wakarimu – anasoma mashairi maarufu:

"Hakika kipande duni cha mkate kinanishibisha,
na kinywaji cha maji halisi kinanitosha,
na tambara la nguo linanisitiri,
nikiwa hai na nikifa linanitosha kunikafini."[147]

Na yatakuja katika kurasa zijazo maelezo ambayo kayapokea Masuruq juu ya kujinyima kwa Imamu Husein عليه السلام ambaye alikuwa amefunga katika siku ya Arafa, na futari yake ilikuwa ni kikombe cha uji.

Ama Ali bin Husein عليه السلام katika siku ambayo alikuwa anafunga alikuwa anaamuru kondoo achinjwe na kukatwakatwa na kupikwa, na inapofika jioni anapitia karibu na vyungu ili apate harufu ya mchuzi wake hali ya kuwa amefunga, kisha anasema: "Leteni mwiko, ichoteeni familia ya fulani" hadi chungu cha mwisho kisha analetewa mkate na tende na hicho ndio kinakuwa chakula chake cha usiku.[148]

Na vilevile maelezo ambayo yamepokewa kuhusu Imamu Ridha عليه السلام kwamba alikuwa analala kidogo usiku na mwingi wa kufunga. Pamoja na kwamba alikuwa katika nafasi ya uongozi ambapo kulikuwa na vyakula vitamu na vinywaji vingi isipokuwa alikuwa ni

[146] *Safinatul-Bihar*, Juz. 1, uk. 27.
[147] *Biharul-An'war*, Juz. 43, uk. 34.
[148] *Biharul-An'war*, Juz. 46, uk. 72.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 172 11/23/2016 12:37:35 PM

mchache wa kula chakula. Huu ndio mfano ambao tunauona katika maisha ya Ahlul-Bayt عليهم السلام kama msingi mkuu. Na kama mwendelezo wa njia ya wapokezi wa Manabii wa Mwenyezi Mungu عليهم السلام na Mawasii wao. Na haya ndio yanayofuatwa katika yanayohusiana na mas'ala binafsi isipokuwa hakika wao عليهم السلام na kwa kuangalia kwamba wao wako katika sehemu ya kuigwa, kwa hiyo hakika vitendo vyao vinachuma mazingira ya Sunnah na hivyo tumewakuta wao ndio wa mwanzo katika utekelezaji wa madhumuni haya.

Na kama ilivyopita katika utafiti uliotangulia, wao wanafanya baadhi ya vitendo ambavyo havikusudiwi kwa dhati yake bali: **Ni kwa ajili ya sharia:** Na kwa ajili ya kuweka wazi hukumu ya kisharia inayofungamana na mambo ya nje. Hiyo ni kwa sababu wao kama wasingekula kwa mfano chakula hiki au kile kungetokea mkanganyiko juu ya je chakula hiki ni ruhusa kisharia kuliwa au si ruhusa kisharia. Walikuja baadhi ya Maswahaba wa Mtume ﷺ kwake siku moja na haluwa, akala na akasema: "Ni kutokana na nini chakula hiki ewe Abu Abdillah?" Akasema: "Naapa kwa baba yangu na mama yangu, tunaweka samli na asali katika chungu cha udongo na kupika katika moto, kisha tunachemsha kisha tunachukua kiini cha ngano inayosagwa tunakikaanga katika samli na asali, kisha tunakiacha hadi kiive na kuwa kama unavyoona. Akasema ﷺ: "Hakika chakula hiki ni kizuri."[149]

Na vilevile aliletewa Amirul-Mu'minin عليه السلام haluwa akaiweka mbele yake akaangalia uzuri wake na usafi wake, akaingiza kidole chake hadi chini kisha akaimimina na hakuchukua chochote katika haluwa hiyo, na akalamba kidole chake na akasema: "Hakika ni halali nzuri na sio haramu isipokuwa mimi nachukia kuizoesha nafsi yangu mambo ambayo sikuyazoea, iondoeni kwangu." Ikaondolewa.[150]

---

[149] *Safinatul-Bihari*, Juz. 1, uk. 750.
[150] *Makarimul-Akhilaq*, uk. 169.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 173 11/23/2016 12:37:35 PM

Na wanaposimama baadhi ya wanaojitakasa na kuharamisha mazuri ambayo yameteremshwa na Mwenyezi Mungu, na kuzichukia neema Zake, Maasumini عليهم السلام wanawapinga. Na tatizo sio katika kula vizuri hadi wadai ubaya wake bali ni kuwa mtumwa wa tumbo, ambapo lengo lake na kwenda mbio kwake ni kwa ajili ya kula aina hii. Imamu Husein عليه السلام aliona mtu anaikosoa haluwa akasema عليه السلام: “Utomvu wa ngano na utomvu wa tende na samli halisi Mwislamu hawezi kukosoa hili.”[151]

Na hii inafungua mwanya katika maudhui ya vionjo. Baadhi wanafikiri kwamba Maasumini عليهم السلام na waumini walio baada yao hawawezi kufikia vyakula vitamu na vinywaji vizuri, na vilevile hawana shauku navyo, na kwa hiyo wanaharamisha katika nafsi zao chakula hiki na kile. Na wanajiepusha na vitamu, kwa sababu wao hawawezi kwa upande mmoja na kwa sababu hisia za vionjo vyao sio salama. Lakini fikira hii ni makosa ambapo “kama ningetaka ningejua njia ya kuipata asali hii safi na kiini cha ngano hii na uzuri wa hariri hii lakini sitaki yanishinde matamanio yangu au iniongoze tamaa yangu katika kuchagua vyakula,” kama asemavyo Imam. Ukiongezea kwamba wao walikuwa wanaona ni kizuri na kitamu kama ilivyotangulia, lakini wao wanachukia kuzizoesha nafsi zao.

Na katika upande wa kisharia vilevile, na kwa kutoa mfano kamilifu juu ya mafunzo ya Kiislamu tunakuta Maasumini عليهم السلام wanatumia njia zote mbili mbele ya watu. Mmoja wao anaichagulia nafsi yake ugumu na anakubali kufunga, na anapokula anakula chakula duni, wakati ambapo wa pili anachagua wasaa anakula katika vyakula vizuri. Na hiyo ni kwa ajili ya kuwafanyia watu wasaa na kwa ajili ya kuwafahamisha kwamba njia zote mbili kwa mipaka yake ya kisharia zinakubalika katika dini. Na huenda lau kama Maasumini عليهم السلام wangekuwa wanatia mkazo katika njia moja tu tungekuwa ka-

[151] Rejea iliyotangulia.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 174 11/23/2016 12:37:35 PM

tika mkanganyiko kuhusu uhalali wa njia ya pili, na huenda yanay-opokewa katika kufuturu na uzuri wa chakula cha Hasan عليه السلام na kufunga, na uchache wa chakula cha Husein عليه السلام, ni kati ya ambayo yanatuongoza katika ukweli huu.

Imepokewa kutoka kwa Masuruq amesema: "Niliingia siku ya Arafa kwa Imamu Husein عليه السلام nikakuta ana kikombe cha uji na wafuasi wake walikuwa wanasoma Qur'ani wanasubiria wakati wa kufuturu, nikamuuliza mas'ala kadhaa niliyokuwa nayo. Al-ipojibu nikatoka na nikaenda kwa Imamu Hasan عليه السلام, nikaona watu kwake, na kimeandaliwa chakula kizuri, na wao wanakula pamoja naye, nilipoona hivyo nikaathirika na akaniangalia Imamu Hasan na kusema: 'Ewe Masuruq kwa nini hili?' Nikasema: Nimefunga na nimekumbuka kitu, akasema: 'Sema unachofikiria katika akili yako.' Nikasema najikinga kwa Mwenyezi Mungu kuwepo baina yako na baina ya ndugu yako ikhitilafu! Nimeingia kwa Husein nikamuona kuwa amefunga anasubiria kufuturu na nikaingia kwako nimekuona katika hali hii. Imamu aliposikia hivyo akanikumbatia katika kifua chake na akasema: 'Ewe mtoto wa al-Ashrasi je, hujajua kwamba Mwenyezi Mungu ametujaalia kuwa ni vigezo vya ummah? Ameni-jaalia mimi kuwa ni kigezo cha wenye kufuturu na akamjaalia ndugu yangu kuwa ni kigezo cha wenye kufunga ili wawe katika wasaa.'"[152]

Hivyo wewe unaona kuwa Imamu anapitisha njia zote mbili ili watu wawe katika wasaa hata kama wao wanapendelea wakiwa we-nyewe kama tulivyosema, ugumu na kutosheka na chakula duni.

## ATHARI ZA KUVIMBIWA:

Ahlul-Bayt عليهم السلام na hata Manabii na Mitume waliopita kabla yao ka-tika historia, wameelekeza wafuasi wao kula kidogo na kujiepusha

[152] *Muntahal-Amali* cha Sheikh Abbas al-Qummiy, Juz. 1, uk. 34.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 175 11/23/2016 12:37:35 PM

kula sana na kushiba, na sio kutokana na haramu, bali ni kutokana na halali na mubaha. Kwani haramu imeharamishwa kichache chake na kingi chake, Na wao walikuwa ndio wa kwanza katika kutekeleza kama tulivyobainisha awali, na sio katika mlango wa uharamisho wa kisharia, bali ni kwa yale yanayoletwa na kula kidogo miongoni mwa athari katika utu wa mwanadamu katika afya ya kinafsi na kiibada miongoni mwa ambayo hadithi zimeyaita kuwa ni urithi wa njaa na urithi wa shibe na kujaza tumbo.

### 1. Uchache wa harakati na uvivu katika utii:

Kula sana na kunywa sana kunasababisha kuwa mzito na mvivu katika kutekeleza majukumu na utii. Na tunaweza kupata haya kwa uwazi katika sira ya watu katika jamii. Yule mtu ambaye anakula chakula chake kwa wastani au anayekula kidogo anabakia katika hali ya juu ya uchangamfu na harakati, kinyume na yule ambaye anakula sana. Huyo anahisi usingizi na mara nyingi anapatwa na uvivu. Katika hadithi iliyopokewa kutoka kwa Masihi عليه السلام amesema: "Enyi Wana wa Israil msile sana kwani mwenye kula sana anakuwa na usingizi mwingi, na mwenye usingizi mwingi anakuwa ni mchache wa Swala, na mchache wa Swala anaandikwa kuwa ni kati ya wenye kughafilika."

Na kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم amesema: "Jihadharini na kuzidisha chakula, hakika kuzidisha chakula hutia sumu moyo, na kunafanya viungo viwe vizito katika utii na kunatia uziwi azima hivyo inashindwa kusikia mawaidha."[153]

Na kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام amesema: "Katika mazungumzo yaliyotokea baina ya Yahya عليه السلام na Ibilisi, Yahya alimwambia Ibilisi: 'Ni za nini hizi kamba?' Ibilisi akasema: 'Haya ni matamanio ambayo namnasa kwayo mwanadamu.' Akasema: 'Je, na mimi nina

[153] *Mizanul-Hikma*, Juz. 1, uk. 117.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 176 11/23/2016 12:37:35 PM

chochote?' Akasema: Pengine utashiba na nikuzuie kujishughulisha na swala na dhikiri.' Akasema: 'Hakika ni wajibu wangu kwa Mwenyezi Mungu kutolijaza tumbo kwa chakula katu.' Ibilisi akasema: 'Hakika ni wajibu wangu kwa Mwenyezi Mungu nisimpe nasaha mwislamu abadani.'" Kisha akasema Abu Abdillahi عليه السلام: "Hakika ni juu ya Mwenyezi Mungu kwa Ja'far na kizazi cha Ja'far wasijaze matumbo yao kwa chakula abadani, naapa kwa Mwenyezi Mungu ni wajibu wa Ja'far na kizazi cha Ja'far wasitumikie dunia abadani."[154]

## 2. Afya mbaya na maradhi ya mwili:

Matabibu wanatoa nasaha – daima – kuchunga wastani katika mwili na kubakia na afya, kwa kufanya wastani katika kula chakula, na kuacha kula wakati bado unakipenda na kukitamani. Hiyo ni kwa sababu viungo vya mwili huu vina uwezo mdogo katika kupokea vyakula vinavyoingia, tumbo lina uwezo mdogo na damu ina uwezo mdogo wa kunufaika na faida za vyakula vilivyomeng'enywa. Na baadhi wanadhani kwa makosa kwamba kila anapozidisha kula hakika mwili wake unazidi kuwa na nguvu, na huenda anatoa hoja katika hilo kwamba uzito wake umevunja wastani wa kawaida, wakati ambapo hajui kwamba yeye anapandikiza katika mwili wake mabomu ya sumu na ya mafuta yatakayolipuka kidogo kidogo baada ya kufikia umri wa miaka 40 katika hali ya ongezeko la shinikizo la damu, kolesteroli na maradhi mengine ambayo yanaitwa magonjwa yenye kudhoofisha.

Na linaweza kuwa ni jambo la kushangaza kwamba sisi tunakuta mafakiri na watu wenye hali ya wastani kwa kawaida hawaugui kwa kiwango cha maradhi ya wenye ubadhirifu wala kwa aina ya maradhi yao, hiyo ni kwa sababu afya haikai pamoja na kula sana. Na hadithi zimeshaashiria katika upande huu. Kutoka kwa Abu

[154] Rejea iliyotangulia.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 177 11/23/2016 12:37:35 PM

Hasan al-Kadhim عليه السلام amesema: "Kama watu wangepunguza kula basi miili yao ingekuwa na uwiano." Na zimehadharisha kudumu katika shibe na kula sana kwa sababu kunaleta magonjwa. Kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام amesema: "Jihadhari na kudumu katika shibe hakika kunachochea magonjwa na kusababisha maradhi. Na jihadhari na kushiba sana kwani mwenye kulazimiana na hilo maradhi yake yanakuwa mengi."

Na kutoka kwa Imamu Ridhaa عليه السلام ameelezea kwamba kuzidisha chakula hakuna manufaa kwa sababu ya mwili kutoweza kunufaika nacho: "Mwenye kuchukua ziada katika chakula basi hakitomnufaisha, na mwenye kuchua kiasi bila ya ziada humo wala upungufu katika chakula chake kinamnufaisha, na vilevile maji. Njia yake ni kuchukua katika chakula kinacho kutosheleza na uache kula hali yakuwa una hamu na bado ungali unakitamani, hakika hilo lina maslahi katika tumbo lako na mwili wako na utakaso kwa akili yako na wepesi kwa mwili wako."[155] Hebu na tusome anayoyasema tabibu katika nyanja hii:

**Madhra ya kuzidisha aina za vyakula:**

i. **Unene:** Nayo ni maradhi hatari ambayo tunayakuta aghlabu katika watu wa tabaka la matajiri na kwa watu wenye vyeo wazembe. Na unapatikana kutokana na kuzidisha chakula, na hususan kisukari, mafuta na kwa namna maalumu kwa watu ambao wanao utayari wa kurithi. Na unene kwa hakika ni maradhi ya shibe yanayozuia uwezo wa mtu na uchangamfu wake kwa kiasi kikubwa, kama ambavyo unatishia au unashirikiana na baadhi ya maradhi hatari kama vile kuziba mishipa ya moyo, kuziba kwa kifua, ugonjwa wa kisukari na kuzidi shinikizo la damu na kuziba mishipa

[155] *Mizanul-Hikma*, Juz. 1, uk. 133.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 178 11/23/2016 12:37:35 PM

minne, na maradhi yote haya leo yanaenea sana katika jamii ambazo zinaelemea kwenye vyakula na vinywaji vizuri.

ii. **Kuharibika meno:** Nayo pia ni kati ya maradhi yaliyoenea kwa sababu ya kula vitu vitamu hususan ambavyo vinaruhusu kuchokonolewa na vijiti kwa kung'ang'ania kwake katika kinywa.

iii. **Changarawe za figo:** Nayo inatokea kwa wingi kwa wale ambao wanakula sana nyama, maziwa na jibini.

iv. **Mishipa kuwa migumu:** Nao ni ugonjwa hatari unaotokea kwa kiasi kikubwa kwa wale ambao wanatumia kiasi kikubwa cha mafuta ambapo wanapatwa na ongezeko la mafuta kwenye damu.

v. **Nagrasi: "Ugonjwa wa wafalme:** nao ni maumivu ya maungo, yanakuja kwa namna ya kushambulia vikali na hususan katika maungio ya unyayo na kidole gumba. Na yanashuhudiwa kwa wingi kwa wale wanaotumia kiasi kikubwa cha nyama.[156]

**Na Dr. Swabriy al-Qabaani anaona kwamba:**

Udhaifu wa mwili na udhoofu wake hauji tu kutokana na uchache wa chakula, bali unaweza kusababishwa na kuzidisha kula kwa matokeo yale yale. Na maradhi mengi ambayo yanamshambulia mwanadamu bila ya kutarajiwa na katika mikesha ambayo anakesha akiumwa au chini ya shinikizo na jinamizi la kutisha, na mengi kati ya mionekano ya maradhi yanayoonyesha juu ya kukosekana uwiano na wastani katika mwili, mengi kati ya yote haya, sababu yake ni kuzidisha kula.[157]

[156] *Maatwibi Fiyl–Qur'anil-Karim*, uk. 131, Dr. Abdul-Hamid Dabab na Dr. Ahmad Qarqur
[157] *Al-Ghidhaa Laa Dawaai*, uk. 613.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 179 11/23/2016 12:37:35 PM

### 3. Kudumaza kipaji na hekima:

Wakati zinabubujika hekima na vipaji kwa watafuta maarifa na watafiti juu ya ukweli, taa zake zinazimika - kama zipo – kwa wenye kutafuta shibe na wanaotumikia tumbo na wingi wa chakula. Na jambo hapa linashuhudiwa pale linapojaa tumbo, kwani fikira zinallala. Sasa itakuwaje ikiwa wakati wote tumbo limejaa kwa chakula na vinywaji? Je, kutabakia fikra hadi ulale au uamke? Kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema: "Msishibe, itazimwa nuru ya maarifa katika nyoyo zenu."

Na kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام amesema: "Mwenye kuzidisha shibe yake tumbo lake linajaa, na mwenye kujaza tumbo lake, jambo hilo linazuia uerevu."

Na kutoka kwake vilevile: "Uerevu haukai pamoja na shibe."

Na makusudio ya haya kama tulivyotanguliza sio kula vya haramu na vyenye shaka, bali tumbo likijazwa kwa vyakula vya halali moyo unapofuka na kutojali mema.[158] Na historia inanukuu kwamba moja ya matatizo yaliyowapata Waislamu moja ya sababu zake ilikuwa ni kujaza matumbo. Alisema Amru bin Aasi kuwaambia wafuasi wake siku walipohukumu mahakimu wawili: "Mzidishieni Abu Musa al-Ashiariy chakula kizuri, wallahi watu hawajashiba isipokuwa watapoteza akili zao au baadhi yake, na haipiti azma ya mtu aliyelala ameshiba."[159]

### 4. Tumbo kumtawala mtu wake:

Mifano miwili anakutana nayo mtu mwenye kuangalia hadithi na mwenye kufuatilia maisha, mfano wa kigezo unaotakiwa, wa aliye nje ya mamlaka ya tumbo, mwanaharakati mwenye jukumu katika

[158] *Mizanul-Hikma*, Juz. 1, uk. 123.
[159] Sharih ya *Nahjul- Balaghah*, Juz. 19, uk. 186.

maisha yake, ambaye anakula anayoyapata ili aishi. Na tumeshatanguliza katika kutaja kwetu maneno yaliyopokewa kutoka kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام, kilicho karibu ni kwamba kutaja kwake sifa hizo ilikuwa ni katika njia ya kutoa mfano wa kipimo, sifa za muumini zinazotakiwa bila ya kukusudia ulazima, kwamba anakusudia mtu fulani ingawa sifa hizi zinawalenga watu.

Na inaonyesha kwamba idadi ya sharia za Kiislamu zinalenga kulea mfano huu, na mfano unaojitokeza zaidi katika hilo ni Saumu ambayo Mwenyezi Mungu amemuwekea mwanadamu, naye anailipa kulingana na tafsiri ya riwaya. Hakika moja ya malengo muhimu ya Saumu ni kumtoa Mwislamu katika utumwa wa matamanio na kumkomboa na jambo la tumbo na mbinyo wake.

Na mfano mwingine ambao hadithi inauchukia na kuufanya kuwa uko mbali na Mwenyezi Mungu, na mbali na ufahamu wa dini, ni kuzama katika utumwa wa tumbo na chakula, mtu anateketeza anayopata na anatafuta asiyoyapata na ana hamu na kutamani asiyoweza kuyapata. Mfano huu ambao unahitimishwa na juhudi zake, jitihada zake na lengo lake katika maisha kwa kushibisha tumbo lake na kujiburudisha kwa vyakula, unaelezwa na hadithi kuwa ni mnyama katika sura ya mwanadamu. Na katika sira ya baadhi ya watawala wafanya ubadhirifu kuna mfano ulio wazi, huyu hapa Muawiya ambaye ilikubaliwa dua ya Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم juu yake wakati alipomwita akakhalifu amri yake mara tatu, na baina ya kila mara kuna muda, na kila mara Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa anaambiwa kwamba anakula, Mtume akamuombea kwa kusema: "Mwenyezi Mungu asishibishe tumbo lake." Amirul-Muuminina عليه السلام anazungumzia juu yake kwa kusema: "Ama hakika itadhihiri kwenu baada yangu mtu mwenye koo kubwa, mwenye tumbo kubwa, anakula anachokipata na anataka ambayo hawezi kuyapata." Na tunaitakidi kwamba Amirul-Mu'minin عليه السلام alikwishaona alama za mabadiliko



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 181 11/23/2016 12:37:35 PM

hayo ambayo alikadiria kuwa yatatokea katika maisha ya baadhi ya Waislamu na kuwatoa katika hali ya kuwa wanaharakati wapambanaji hadi kuwa wenye kuchupa mipaka waliodhalili kwa matumbo yao, hivyo alielekeza mashambulizi makali katika ubaya wa mifano hii, kwa kuangalia upande wa ushirikiano baina yake na baina ya unyama wa wanyama ambao lengo lao ni matumbo yao, na akakemea juu yake kwa kuelezea lengo la maisha yao baina ya chakula na malazi: "Kama vile mnyama aliyefungwa, lengo lake ni chakula chake, au asiyefungwa shughuli yake ni kutafuta kinachojaza tumbo katika malisho na anapuuzia yanayotakiwa kwake."

Na njia ya kufikia katika lengo hili duni daima ni kutii matakwa ya tumbo, na kutotosheka. Ikitimia hivyo, tumbo linageuka kuwa ni mtawala asiyeshindwa, na wakati huo maamuzi ya mwanadamu katika maisha yake na mafungamano yake na dini yake yanakuwa ndio kituo chake na sio katika akili yake bali ni katika tumbo. Natuache historia izungumze.

Fadhili bin Rabii anataja kwa kusema: "Kadhi Shariku aliingia kwa al-Mahdi siku moja (na Shariku kabla yake alikuwa ameenguliwa na utawala), al-Mahdi akamwambia: 'Ni lazima unikubalie moja kati ya mambo matatu.' Akasema: Na ni yapi hayo ewe kiongozi wa waumini? Akasema: 'Ama uchukue ukadhi au uzungumze na wanangu na uwafundishe au ule chakula kwangu.' Shariku akatafakari kisha akasema: 'Chakula ndio jambo jepesi katika nafsi yangu.' Hivyo akamzuia na akamwagiza mpishi amtengenezee aina ya ubongo uliochanganywa na sukari na asali. Alipomaliza kula msimamizi wa jikoni akamwambia: 'Ewe kiongozi hatofaulu mzee baada ya vyakula hivi abadani.'" Fadhili bin Rabii anasema: "Wallahi Shariku alizungumza nao baada ya hapo na akafundisha watoto wao na akachukua ukadhi kwao, na al-Mahdi alimwandikia ujumbe Jahabadha kuhusu riziki yake (ya Shariku, yaani malipo yake), basi Jahabadha



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 182 11/23/2016 12:37:35 PM

akambana kwa kupunguza malipo na akamwambia: 'Hakika wewe hujauza silaha (hata tukupe malipo makubwa).' Shariku akamwambia: 'Wallahi hakika nimeshauza kikubwa zaidi kuliko silaha, nimeuza dini yangu.'''[160]

Wewe unaona ni kiasi gani tumbo limemtawala Kadhi huyu, na al-Mahdi al-Abbasiy alitarajia hilo alipojaalia kula chakula katika meza yake ndio muamuzi wa nafasi ya ukadhi na kuwafundisha watoto wake. Ama mpishi alithibitisha hayo kwa kauli yake: "Hatofaulu Sheikh baada ya vyakula hivi abadani." Na Shariku hakuwa ni mwenye kughafilika kwa aliyoyafanya, ambapo yeye aliuza kikubwa zaidi kuliko silaha, aliuza dini yake kama alivyosema!

**5. Ugumu wa moyo na mchemko wa matamanio:**

Inaonekana kwamba sababu za udhaifu na sababu za nguvu katika moyo wa mwanadamu ni kama pande za mizani, ikiwa mwanadamu ataelemea upande mmoja utadhoofika upande mwingine kwa kawaida. Na inaonyesha kwamba hekima na matamanio yanakinzana, yote katika mizani, mtu akinywesha moyo wake katika chemchem ya hekima hakika atadhoofisha dauru ya matamanio na udhibiti wake, na kinyume chake anapoelea kwenye matamanio zinazimika katika moyo wake taa za hekima.

Na tumbo kwa sababu ni kati ya visababishi vya kuupa nguvu utashi na njia ya matamanio katika nafsi, kwa hiyo mara nyingi linazalisha ugumu wa moyo, kama ambavyo moto zinapotupiwa humo kuni haushibi na hautosheki, hakika matamanio kwa kawaida hayatosheki mwanadamu anapoyakubalia, kila anapoyapatia yanataka ziada. Na sisi tunakuta katika wosia wa Maasumini عليهم السلام msaada katika kudhibiti matamanio kwa Saumu, kwa sababu ni kinga: "Mwenye kupata kati yenu mahari basi aoe na asiyeweza basi afunge

[160] *Murujudhahabi*, Juz. 3, uk. 320.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 183 11/23/2016 12:37:35 PM

hakika ni kinga." Na sio ajabu sisi tunakuta mafungamano katika sifa za waumini baina ya kuwa nyoyo zao ni laini na macho yao ni yenye kulia, na katika upande mwingine matumbo yao ni mepesi, kwa sababu tumbo kubwa lililojaa linaafikiana na matamanio yenye kuchemka na moyo mgumu, na mara nyingi hauafikiani na moyo laini na unyenyekevu wake.

Na tunahitimisha utafiti huu kwa neno la hekima linalokusanya katika kusifia kutosheka na kula kidogo:

Mmoja wao alimwambia mtoto wake: "Ewe mwanangu izoeshe nafsi yako kuwapendelea wengine, kupiga vita matamanio, na wala usishambulie kama anavyoshambulia mnyama, na wala usiume kama anavyouma mnyama. Wala usile sana chakula kama anavyokula kondoo, wala usile kama anavyokula ngamia. Hakika Mwenyezi Mungu amekujaalia wewe ni mwanadamu, usiifanye nafsi yako kuwa ni mnyama wa kawaida, wala mnyama mkali. Na jihadhari na kukasirika haraka, na ugonjwa wa tumbo, kwani ameshasema mhenga: 'Kama unakula sana basi ihesabie nafsi yako katika wagonjwa.'"

Na Aamash amesema: "Na tumbo siku moja litaangamizwa na matamanio, na jua kwamba shibe inapelekea kuvimbiwa, na kuvimbiwa kunasababisha ugonjwa, na ugonjwa unasababisha mauti, na mwenye kufa kwa mauti haya basi atakufa kifo kibaya. Na katika hali hii atakuwa ameiua nafsi yake, na mwenye kuua nafsi yake analaumiwa zaidi kuliko aliyemuuwa mtu mwingine. Ewe mwanangu Wallahi hajatekeleza haki ya kusujudu na kurukuu mwenye shibe, wala hajanyenyekea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mwenye kushiba sana. Saumu ni afya na huenda ndio sababu umerefuka umri wa Wahindi, na miili ya Waarabu imekuwa na afya.

Mwenyezi Mungu amhifadhi Harithi alipodai kwamba dawa ni kuazimia, na hakika ugonjwa ni kula chakula baada ya chakula



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 184 11/23/2016 12:37:36 PM

(yaani katika hali ya shibe). Ewe mwanangu, kwa nini zimekuwa safi akili za mabedui, na zimekuwa nzuri akili za watawa, pamoja na kukaa sana katika mahekalu, hadi hawajajua maumivu ya maungo wala uvimbe, isipokuwa kwa uchache wa huzuni, na ubaya wa vyakula. Na vipi usipendelee mpangilio unaokukusanyia baina ya afya ya mwili na uerevu wa akili, marejeo mema, ukuruba na maisha ya malaika. Ewe mwanangu, kwa nini kenge amekuwa ni mwenye kiu sana isipokuwa ni kwa sababu anazidisha sana kuvuta hewa. Na kwa nini Mtukufu Mtume ﷺ amesema saumu ni kinga isipokuwa ni kuifanya kuwa ni kizuizi dhidi ya matamanio. Na tambua adabu ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika wao hawamkusudii isipokuwa aliye mfano wako."

"Ewe mwanangu hakika mimi nimefikia miaka tisini na halijapungua jino, wala sijapata ugonjwa, wala sijajua kusumbuliwa na mafua, wala kuumwa macho wala kudondokwa na mkojo. Hakuna sababu ya hayo isipokuwa kupunguza kula. Kama unapenda kuishi basi hii ndio njia ya maisha, na ikiwa unataka mauti basi Mwenyezi Mungu hayaweki mbali isipokuwa kwa mwenye kudhulumu."[161]

## MIFANO KINZANI:

Vitu mara nyingi vinajulikana kwa vinyume vyake, na kwa sababu sisi tumeshataja mwanzo kuhusu maisha ya Maasumini عليهم السلام na kutakasika kwao na utumwa wa tumbo, na kujengea kwao katika mifano mitukufu ambayo ilikuwa nje ya utawala wa tumbo, hivyo Maasumu hatafuti asiyoyapata na wala hazidishi anapopata. Hakika sisi tutataja hapa mifano inayoafikiana na inayokinzana katika sifa hizo, ili zibainike pande za sura kikamilifu. Na utafiti huu hata kama ni kwa ajili ya kuzungumzia Ahlul-Bayt عليهم السلام isipokuwa ilipokuwa

[161] *Sahrhu Nahjul-Balagha*, Juz. 19, uk. 186.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 185 11/23/2016 12:37:36 PM

mifano ambayo tutaielezea imechukua misimamo ya Maasumini عليهم السلام kwa uadui, ilikuwa ni dharura kujua baadhi ya hali zake, ili tujue uko wapi uhalisia wa hawa mbele ya uhalisia wa Ahlul-Bayt عليهم السلام.

**Suleimani bin Abdul-Maliki:**

Watawala dhalimu wamekuwa ni mahususi kwa sifa na alama zinazotofautiana. Kuna baadhi yao wamekuwa ni mahususi kwa sifa hii bila ya ile, na ingawaje zote ni madhambi isipokuwa hakika humo kuna madaraja na mielekeo. Kama ambavyo Abdul-Maliki bin Mar'wan amekuwa ni mahususi kwa ubakhili hadi ameitwa 'tindo' na amezidiwa katika hilo na Abu Mansuri hadi akapewa lakabu ya Dawaniqiy, bakhili mno.

Hakika Suleiman bin Abdul-Maliki amezidi katika wingi wa kula hadi akawasahaulisha watu kumtaja Muawiya mwenye koo pana! Na sisi tunataja kiasi katika hayo juu ya dhima ya historia ambayo imeyanukuu.

Mlo wake wa kila siku ni ratili mia moja za kiiraki, na wakati mwingine wapishi walimwendea na kifaa cha kuchomea mishikaki, na humo kuna kuku waliochomwa na juu yake kuna siagi nzito. Kwa uroho wake na ulafi wake wa kula anaingiza mkono wake katika mdomo wake ili achukue kuku ilihali ni wa moto, na hivyo anamtenganisha.

Na imetajwa kwamba Suleiman alitoka chooni siku moja na njaa yake imezidi akaharakisha kwenda kula chakula, na kabla hajamaliza kula, akaamuru aletewe kilichokuwa tayari katika vilivyochomwa. Akapelekewa kondoo ishirini, akala utumbo wote pamoja na mikate 40, kisha akapelekewa chakula baada ya hapo. Akala pamoja na mchuzi wake kana kwamba alikuwa hajala kitu. Narudia tena ibara kwa mara nyingine: Alipelekewa kondoo 20 akala utumbo



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 186 11/23/2016 12:37:36 PM

wake wote pamoja na mikate 40. Na inasimuliwa kwamba alikuwa anachukua vikapu vya haluwa na anaviweka katika kitanda chake anapoamka ananyoosha mkono wake na haungukii isipokuwa katika kapu, basi anachukua haluwa na kula.[162]

Na huenda sisi hatuamini kila kinachopokewa katika mlo wa Suleiman na mfano wake, ambapo muumini anakula kwa tumbo moja na kafiri anakula kwa matumbo saba; sasa itakuwaje kwa anayekula katika matumbo sabini? Lakini tutasemaje kama vitabu vyote vya historia na fasihi vitaafikiana katika hilo?

Amesema Sharmadal wakili wa Amru bin Aasi: Alikuja Suleiman bin Abdul-Maliki Twaifu, akaingia yeye na Umar bin Abdil-Aziz kwangu, akasema: "Ewe Shamardal, huna cha kunilisha?" Nikasema: Ninaye kondoo mnene sana, akasema: "Mharakishe." Nikamletea kana kwamba ni mafuta kwa unene. Akawa anakula na wala hamkaribishi Umar, hadi haikubaki isipokuwa paja akasema: "Karibu ewe Abu Ja'far!" Akasema: 'Mimi nimefunga.' Basi Suleiman akala na kummalizia. Kisha akasema: 'Ewe Shamardal: Ole wako huna kitu kingine?' Nikasema: Nina kuku sita wakubwa kana kwamba ni vifaranga vya mbuni. Nikamletea akawala kisha akasema: 'Ewe Shamardal: Huna kingine?' Nikasema: Nina togwa kana kwamba ni uji wa dhahabu. Nikamletea akanywa kisha akasema: 'Ewe kijana umemaliza katika chakula chako?'"

Akasema: Ndio. Akasema. Kipi hicho? Akasema: Nina vyungu 30, akasema niletee chungu kimoja kimoja, akavileta na humo kuna mikate, akala katika kila chungu theluthi moja kisha akafuta mikono yake katika tandiko lake na akawaita watu wakaingia na vyombo vikapangwa na akala pamoja na watu.

Je, unasadikisha?

---

[162] *Murujudhahabi*, Juz. 3, uk. 185.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 187 11/23/2016 12:37:36 PM

# DONDOO KUTOKA KATIKA MAFUNZO YA SIRA:

Tunaweza kutoka na natija baada ya kueleza kiasi katika sira ya Maasumini عليهم السلام katika upande huu kwa idadi ya dondoo inayotuangazia njia:

**a- Uelewa wa kiafya katika kula:**

Baadhi wanaelemea katika kula kwa kujaza tumbo kwa anachokipata mezani katika aina za vyakula na aina za vinywaji wakisahau juu ya ukweli unaofungamana na mas'ala hayo kwamba kujaza tumbo sio tu hakutokuwa na faida bali katika hali nyingi kunadhuru. Na inaongezewa katika hayo kwamba aina za chakula ambacho anakila wakati mwingine inakuwa ni pamoja na kuangalia upande wa kiafya, na wakati mwingine ni kwa kutokuwa na angalizo.

Hakika sisi tunaona kuwepo na idadi ya adabu na sunnah za kiafya ambazo wameelekeza Maasumini عليهم السلام, kuna maelekezo ya jumla. Inawezekana kuzingatia kanuni za afya zisizofungamana na wakati au mtu, mfano kauli ya Mtukufu Mtume ﷺ: "Usile ambacho umeshajua madhara yake na wala usipendelee matamanio yako badala ya raha ya mwili wako, na kinga ni kupunguza katika kila kitu, asili ya tiba ni kujidhibiti, (nayo ni kudhibiti midomo miwili na upole wa mikono miwili) na gonjwa baya sana ni kuingiza chakula juu ya chakula. Na jiepushe na dawa maadamu una afya unapohisi ugonjwa uteketeze kwa kinachozuia kabla ya kudhihiri."[163]

Na kauli ya Amirul-Mu'minin عليه السلام: "Mwenye kula chakula katika usafi na akatafuna chakula vizuri na akaacha chakula naye bado

[163] *Al-Mustatwaraf Fiy Kuli Fan Mustatwaraf*, uk. 192.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 188 11/23/2016 12:37:36 PM

anakitamani na hakubana haja kubwa inapokuja, hatougua isipokuwa maradhi ya mauti."[164]

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa kinapokuja chakula chenye mafuta anapunguza kunywa maji, akaambiwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika wewe unaponguza kunywa maji? Akasema: "Hiyo ni mbaya sana katika chakula changu."[165] Na hiyo ni kutokana na athari ya kupunguza mkazo wa kukamua na kumeng'enya katika tumbo.

Na kutokana na mantiki hii ya kiafya imepokewa hadithi kutoka kwa Ahlul-Bayt wake عليهم السلام kwamba: "Sisi ni watu ambao hatuli hadi tuwe na njaa na tunapokula hatushibi." Yaani tunaacha kula kabla hatujashiba. Na kutoka kwao pia kuna mkazo juu ya kwamba nguvu haiji kwa kujaza tumbo kama tulivyosema, wala haiji kwa chakula kitamu bali chakula kigumu kinaweza kuwa na visababisho vya nguvu, na faida za chakula zaidi kuliko inayopatikana katika chakula cha awali, hivyo sio ajabu kukuta kwamba chakula cha jeshi la Waislamu katika vita vingi kilikuwa ni tende na maji ambapo kwa mwenye kufuatilia ataona kwamba ni lazima jeshini kuwe na chakula kingi na cha aina mbalimbali, na tunaweza kunyambua fikra hii kutoka katika maneno ya Amirul-Mu'minin عليه السلام: "Kana kwamba msemaji wenu anasema: Ikiwa hiki ndio chakula cha mtoto wa Abutalib, basi amekwisha dhoofika kupambana na wapambanaji na kupigana na mashujaa. Eee hakika mti wa nchi kavu ni mgumu zaidi, na miti mibichi ya kijani ni laini zaidi, na mimea ya nchi kavu ni migumu na imara na inakawia kunyauka."[166]

Vilevile katika maelezo hakika kuna mkazo juu ya aina maalumu kwa kuzingatia faida yake muhimu katika mwili wa mwanadamu,

---

[164] *Biharul-An'war*, uk. 59.
[165] *Makarimul-Akhlaq*, uk. 146. *Sunanu-Nabiyyi* ﷺ, uk. 178.
[166] *Nahjul-Balaghah*, Barua ya 45.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 189 11/23/2016 12:37:36 PM

kama vile asali ambayo Qur'ani tukufu inaisifia kwamba ni dawa, na yamebainika hayo kwa binadamu baadaye. Au mkazo juu ya chumvi na kuanza nayo na kumaliza kwayo kwa athari inayopatikana katika kuangamiza visababishi vya maradhi. Na sisi hapa hatuko katika kuelezea hadithi zote hizo na kutoa faida zake. Utafiti haukuandaliwa kwa hayo, na inawezekana kurejea vitabu mahususi katika nyanja hii.[167]

Isipokuwa ambayo tunataka kutanabahisha hapa ni kwamba Maasumini عليهم السلام na wao wanajua mahitaji ya binadamu katika chakula. Wameelekeza katika adabu zake, hivyo linamtosheleza mwanadamu tonge linaloupa nguvu mgongo wake, akizidisha anaingamiza nafsi yake. Theluthi ni kwa ajili ya chakula chake, na theluthi ni kwa ajili ya kinywaji chake na theluthi ni kwa ajili ya nafsi yake (kwa ajili ya hewa). Na hivyo inapasa kwa anayetaka kuishi salama kutokana na adha, mwenye afya ashikamane na mafunzo hayo.

## KUJINYIMA NA MAHITAJI YA ZAMA:

Kama ilivyotangulia katika sehemu iliyopita, na tumetaja katika wakati wake kwamba Maasumini عليهم السلام kwa kuzingatia kwamba wao ndio wafikishaji wa yanayotoka kwa Mwenyezi Mungu wana majukumu na maadili, na kwa kuzingatia kwamba wao ni binadamu wanaishi katika jamii wana wajibu, na inaweza kutokea jamii kuwa na mazingira ya kawaida na hivyo wanatekeleza humo mafunzo yao na fikra zao zote. Na inaweza isiwe hivyo na hivyo wanahifadhi msingi wa maadili wakati ambapo wanaachana na mbinu za muonekano, na hiyo haimaanishi kupoteza maadili ya kimsingi kama wanavyodhani baadhi ya watu kimakosa, bali kujitoa muhanga katika mbinu ni kwa ajili ya maslahi ya kimsingi.

[167] Unaweza kurejea kitabu *Ma'a twibi fiyl Qur'an al- Karim*. Na vilevile *al- Athari al-Ham* cha Dr. Baaktiraad: *Awaliyn Danshigahi wa Akhariina Payambar* (cha Kiajemi).



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 190 11/23/2016 12:37:36 PM

Vilevile tumekwishataja mwanzoni kwamba sehemu ya kazi za Maasumu zinahusiana na nyanja ya tablighi na dini, na kwa hivyo kutokana na kwamba wao wanafahamu ulipo uhalali na uharamu, kama ilivyopita, wakati alipoacha Mtume ﷺ kula baadhi ya vyakula mmoja wa Maswahaba akamuuliza: Je unakiharamisha? Na ndivyo ilivyo hali kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام. Ukiongezea katika hayo hakika wao عليهم السلام sio kwamba hawakujua utamu wa vyakula, kama wangetaka wangejua njia, isipokuwa wao walitaka unyenyekevu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kutozoea hayo ili wasiitikie wito wa tumbo. Na kwa hakika walikuwa wanavutiwa na baadhi ya vyakula isipokuwa kuna tofauti iliyo wazi baina ya kuvutiwa na chakula hiki na kutawaliwa na uroho hadi kuwa mtumwa wa tumbo.

Katika yaliyotangulia tunaweza kuoanisha baina ya hadithi ambazo zinaunga mkono kujinyima katika maisha ya kidunia na vyakula vyake na zile hadithi ambazo zinaelezea vyakula vyao kuwa ni kama vyakula vingine, bali huenda zimezidisha maelezo, na aina ambazo zinawavutia. Tusome hadithi ifuatayo: Kutoka kwa Yahya bin Ja'far bin Aasim kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake. Amesema: Nilihiji na pamoja nami kuna kundi katika wafuasi wetu, nikaenda Madina, nikaelekea sehemu tunayofikia, akatupokea kijana wa Abul Hasan Musa bin Ja'far عليه السلام akiwa juu ya punda na chakula. Tukashuka baina ya mitende na akaja na akashuka, na akaleta beseni la maji na sabuni ya kuoshea mikono, akaanza kuosha mikono yake na likazungushwa beseni kuliani kwake hadi akamfikia wa mwisho wetu. Kisha likarejeshwa kwa aliye kushotoni kwake hadi likamwendea wa mwisho wetu, kisha chakula kikaletwa akaanza kwa chumvi kisha akasema:

"Kuleni kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu." Kisha akafuatilizia kwa siki, kisha akaleta nyama ya mkono uliuchomwa, akaniambia: "Kula kwa jina la Mwenyezi



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 191 11/23/2016 12:37:36 PM

Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika chakula hiki anakipenda Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ." Kisha akaleta siki na siagi akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Chakula hiki alikuwa anakipenda Fatma Zahara عليها السلام." Kisha akaleta sakabaji,[168] akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Chakula hiki alikuwa anakipenda Amirul-Muuminina عليه السلام."

Kisha akaleta nyama iliyochemshwa humo kuna biringanya, akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu, hakika chakula hiki alikuwa anakipenda Hasan bin Ali عليه السلام." Kisha akaleta mtindi mchachu umeshaganda akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika chakula hiki alikuwa anakipenda Husein عليه السلام." Kisha akaleta samaki wadogo wa baridi akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika chakula hiki alikuwa anakipenda Ali bin Husein عليه السلام."

Kisha akaleta jibini imejaa chombo akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika chakula hiki alikuwa anakipenda Muhammad bin Ali عليه السلام." Kisha akaletewa *taur* (chombo kilichotengenezwa kwa mawe) humo kuna mayai yaliyokaangwa akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika chakula hiki anakipenda baba yangu Ja'afar عليه السلام." Kisha akaletewa haluwa akasema: "Kula kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Hakika chakula hiki nilikuwa nakipenda."[169]

Hadithi inaonyesha kwamba vyakula hivyo vilikuwa vinawavutia, na haya ni mas'ala ya vionjo (hamu) isipokuwa haimaanishi kuvutiwa daima. Na inadhihirika kwamba kuvutiwa huku hakumzuii

---

[168] Sakabaaji: ni chakula kinachotengenezwa kwa nyama na siki.
[169] *Biharul-An'war*, Juz. 48, uk. 118.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 192 11/23/2016 12:37:36 PM

Maasumu kukiacha kwa ajili ya mwenye kuomba au fakiri, na wala chakula hicho hakimmiliki. Ali bin Husein عليه السلام alikuwa anapenda zabibu. Kijakazi akamletea mkungu wa zabibu akauweka mbele yake. Akaja muombaji akamwamuru ampe, akampa. Kisha akamtuma kijana wake kwa mama wa mtoto wake akamwamuru akaununua kwa muombaji, kisha akamletea akauweka mbele yake akaja muombaji akaomba akamwamuru ampe, basi nikafanya hivyo mara tatu ilipofikia mara ya nne akazila.[170]

Bali huenda tukasema kwamba jambo liko wazi ikiwa linafungamana na kuwakirimu wafuasi na kufafanua hukumu za kisharia. Amepokea Abu Khalid al-Kabiliy amesema: Niliingia kwa Abu Ja'far عليه السلام akaagiza chakula. Nikala chakula ambacho sijawahi kula chakula safi na kizuri kuliko hicho. Tulipomaliza kula akasema: "Umekionaje chakula chetu?" Nikasema: Sijaona chakula kisafi na kizuri kuliko hiki kamwe, lakini mimi nimekumbuka Aya katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu: Hakika mtaulizwa juu ya neema. Abu Ja'far عليه السلام akasema: "Hakika mtaulizwa juu ya ambayo nyinyi mlikuwa na haki juu yake."[171]

## BAINA YA WASTANI NA NJAA YENYE KUDHOOFISHA:

Kuna mipaka miwili katika yanayohusiana na chakula: Kuvimbiwa, na tumeshatangulia kutaja athari zake mbaya katika maisha ya mwanadamu, sawa iwe katika afya yake au nafsi yake au harakati zake, na hadithi zimetilia mkazo juu ya ulazima wa kuepuka kuvimbiwa. Na kuna mpaka mwingine katika upande mwingine nao ni njaa yenye kudhoofisha, nayo kwa nafasi yake haipendezi kwa

170 *Makarimul–Akhlaq*, uk. 174.
171 *Wasailu Shia*, Juz. 16, uk. 445.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 193 11/23/2016 12:37:36 PM

sababu inamalizikia kwenye madhara yaliyotangulia, lakini katika upande mwingine. Hiyo ni kwa sababu aina hii ya njaa inampokonya mwanadamu uwezo wa kujishughulisha, maadamu mwili wake haupati nguvu ya chakula ya kutosha kwa ajili ya kuendesha harakati zake za kivitendo za viungo vyake. Na vilevile kama ambavyo tumbo likijaa, fikra na hekima zinalala, hakika tumbo pia linapohisi njaa na adha ya kukosa kabisa, hakika haliruhusu fikra ije hadi lilale! Na Amirul-Mu'minin عليه السلام anazungumza kwa kubainisha wastani huu wenye sehemu mbili kwa kauli yake juu ya moyo: "Yametegemezwa kwa huyu mwanadamu mambo machache, nayo ni kati ya yanayoshangaza kati ya yaliomo humo: Na huo ni moyo, na hiyo ni kwa sababu una sehemu miongoni mwa hekima na vinyume vyake katika kutofautiana; akiruhusu matarajio basi tamaa inamdhalilisha, na akibanwa na njaa basi unadhoofika, akizidisha shibe anavimbiwa na tumbo. Kila upungufu unamdhuru na kuzidisha pia kuna haribu."[172]

Na kuna yaliyopokewa katika hadithi ambazo zinasifia njaa na zinazingatia kwamba inaleta hekima na kuukanya moyo, na mengineyo. Na pia yaliyopokewa kutoka kwa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم na Maimamu kwamba walikuwa wanapendelea njaa kuliko shibe, hakika inachukuliwa kuwa ni njaa mukabala wa kuvimbiwa na sio njaa yenye kudhoofisha ambayo inamzuia mwanadamu kutekeleza wajibu wake na jukumu lake. Kama ambavyo kuvuka mpaka katika chakula kunalaumiwa kwa sababu ya athari zake mbaya, vilevile kuzembea kabisa pia kunalaumiwa kwa sababu ya athari zake mbaya. Na huenda msomaji anauliza ikiwa mambo yako hivyo, kwa nini hadithi hazikuja katika kulaumu njaa yenye kudhoofisha, kama zilivyokuja katika kulaumu kuvimbiwa na uroho? Na jawabu juu ya hilo kwanza ni kuwepo aina hii ya hadithi, pili hakika maudhui ya balaa ya njaa

[172] *Nahjul-Balaghah*, Hekima ya 108.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 194 11/23/2016 12:37:36 PM

yenye kudhoofisha ni chache kwa watu, wakati ambapo balaa kubwa zaidi ni kupenda chakula na kuzidisha chakula, wakati ambapo kibano cha haja ya kula kinatengeneza msingi wa amani kwa wale ambao wanatumia njaa yenye kudhoofisha, lakini wale wenye kuzidisha katika chakula hawana msingi isipokuwa maradhi na (kisha ni uharibifu wa macho)!

Na mfano huu ni sawa na maana ya hadithi iliyopokewa kutoka kwa Zainul-Abidin عليه السلام: "Hakika mimi siwausii katika dunia kwani mimi najua kwamba nyinyi mnausiana kwayo kheri, lakini mimi nawausieni Akhera." Na hivyo inapasa kuangalia hadithi kwa jicho la wastani, si njaa inayomdhoofisha mtu kufanya shughuli zake na kumzuia kufikiri katika mambo yake kwa maslahi ya kufikiria chakula, wala shibe inayogeuka na kuwa chanzo cha maradhi ya kimwili na kinafsi.

## CHAKULA, ADABU NA SUNNAH:

Pamoja na kwamba mas'ala ya chakula ni kuitikia mahitaji ya mwili na kuutimizia mahitaji yake katika kuondoa njaa na udhaifu unaotokana nayo, isipokuwa Uislamu umekizingira kwa mkusanyiko wa adabu na sunnah, na ukazipa adabu hizi wigo wa kijamii na kiibada. Na tofauti baina ya anayeshikamana na adabu hizi na asiyeshikamana nazo baada ya kushirikiana kwao katika kuitikia mahitaji ya mwili na kuondoa njaa, hakika wa kwanza anajaalia kula chakula ni ibada. Ndiyo, kula chakula ni ibada, na kupanda daraja za kidunia, wakati ambapo mwingine ambaye anafanya kitendo kilekile na anakula chakula kilekile na huenda ni kwa kiasi kilekile, lakini hapati hayo.

Njoo pamoja nami msomaji mpendwa ili ujue adabu na sunnah ambazo walizifanya Maasumini عليهم السلام na walizilingania na huenda



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 195 11/23/2016 12:37:36 PM

kwa kuzijua tutamiliki moja ya sababu za kuzitekeleza katika maisha yetu:

**1. Sunnah za ibada:**

Na tunaanza na nia. Hiyo ni kwa sababu nia ndio kiuganishi cha vitendo kwa ufafanuzi na malengo makubwa ambayo anayabeba mwanadamu. Inachukua nafasi muhimu katika fikira ya kidini hadi imekuwa ni bora kuliko kitendo chenyewe, na hadi imekuwa kwamba kila mtu atalipwa kwa uzito wa kile alichokinuia. Na kwa kuwa iko hivyo basi ni sunnah Mwislamu atie nia hata katika kulala na kula. Kutoka kwa Mtume ﷺ hakika alimwambia Abu Dhar: "Ewe Abu Dhari utie nia katika kila jambo lako hata katika kulala na kula."[173] Yaani hakika wewe unaponuia kula chakula hiki ili upate nguvu unayoielekeza katika ibada ya Mwenyezi Mungu, na kushughulika katika haja za watu, hakika wewe kwa chakula hiki kinachoambatana na nia hii unapata thawabu na malipo, wakati ambapo rafiki yako ambaye anakaa kando yako katika sahani na anakula hali ya kughafilika na nia hii hapati mfano wa malipo yako!

Na imekuja katika riwaya nyingine inayotilia mkazo juu ya mtu kujua anachokula. Na anwani hii inapanuka katika maneno na maana nyingi. Inaweza kuafikiana na kujua uhalali wa chakula hiki na kutokuwa kwake haramu au cha shaka, na kuchunga mwanadamu asiingize katika tumbo lake isipokuwa halali na kilicho kizuri. Na maarifa hayo yanamaanisha kuheshimu neema hii ambayo Mwenyezi Mungu amemneemesha. Hiyo ni kwa sababu kufikiri kidogo katika hatua za kuwa neema hii, iwe ni tunda au chakula, inamfahamisha mwanadamu uwezo wa Mwenyezi Mungu na utukufu Wake ambao amemdhalilishia yeye kila kitu katika maisha yake, Mwenyezi Mungu anasema:

[173] *Safinatul-Bihaari*, Juz. 2, uk. 629.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 196 11/23/2016 12:37:36 PM

فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ إِلَىٰ طَعَامِهِ أَنَّا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ثُمَّ شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا فَأَنْبَتْنَا فِيهَا حَبًّا وَعِنَبًا وَقَضْبًا وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا

**"Hebu na atazame mtu chakula chake, hakika tumeyamimina maji mmiminiko kisha tukapasua ardhi mpasuko tukaotesha humo nafaka. Na zabibu na mboga. Na mizaituni na mitende."**
**(Abasa; 80:24-29).**

Na vilevile nyuradi kama vile *Bismillahi* kwa kuanza, na *Alhamdu* wakati wa kumaliza, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa kinapowekwa chakula mbele yake anasema: "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kijaalie kuwa ni neema yenye kushukuriwa inayoungana na neema za peponi." Na kutoka kwa Amirul- Mu'minina عليه السلام amesema: "Mtajeni Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa kula na wala msizungumze humo, hakika ni neema katika neema za Mwenyezi Mungu. Ni wajibu juu yenu humo kumshukuru na kumhimidi, na amilianeni vizuri na neema kabla ya kuondoka kwake."

Na alimuusia mtoto wake Hasan عليه السلام: "Ewe mwanangu usile tonge moto wala baridi, wala usinywe funda isipokuwa na wewe uwe umesema kabla ya kula na kunywa: 'Eee Mwenyezi Mungu hakika nakuomba katika chakula changu na kinywaji changu salama dhidi ya maradhi yake, na nguvu itakayonisaidia katika kukutii, kukutaja, kukushukuru wewe katika ulichokibakisha katika mwili wangu. Na unishajiishe kwa nguvu yake niweze kukuabudu Wewe na unifahamishe wema wa kujikinga na maasi yako.' Hakika wewe ukifanya hivyo utakuwa umesalimika na shida yake na shari yake."[174]

## 2. Adabu za kijamii:

Pamoja na kwamba kula ni kitendo cha kibinafsi kwa kawaida, isipokuwa kuna nyanja za kijamii. Hiyo ni kwa sababu kimezun-

[174] *Makarimul-Akhlaq*, uk. 143.

gukwa na baadhi ya adabu katika nyanja hii, hivyo hadithi zinaona ni makuruhu harufu zisizopendeza za baadhi ya vyakula kutangulia kufika kwa watu kabla ya chakula kufika. Na hadithi hizi hata kama hazikuharamisha vyakula hivi, isipokuwa Mwislamu anapoangalia katika hadithi hizi anahisi karaha katika hali hii. Na katika yanayosikitisha ni kwamba baadhi ya Waislamu wanahudhuria msikitini, hafla na mikusanyiko mingine bila ya kuchunga mas'ala haya. Hivyo unahudhuria msikitini kwa kutarajia kunusa harufu za manukato na harufu nzuri kwa kuzingatia kwamba ni moja ya uhalisia wa pambo; "Chukueni mapambo yenu wakati wa kwenda msikitini," lakini badala ya hayo unanusa harufu ya kitunguu saumu, kitunguu maji, harufu mbaya na mfano wa hayo. Mtume ﷺ hali kitunguu saumu, sio kwa kukiharamisha bali kwa sababu anaongea na Mfalme. Ameulizwa Imamu as-Sadiq عليه السلام juu ya kula kitunguu saumu akasema: "Sio vibaya kula kiasi lakini ikiwa hivyo basi asiende msikitini."[175]

Na vilevile hakika katika adabu za kijamii ambazo Uislamu unaziamuru ni kujiepusha na yanayodhalilisha utu, kama vile kula sokoni kwa mfano, kwa watu watukufu, na kuzingatia kuwa ni uduni na kwa hakika kula chakula sokoni ingawaje sio haramu katika asili yake isipokuwa inachukiza kutokana na zile athari mbaya za kijamii zinazoachwa na kitendo hicho kwa mwenye kula chakula. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Kula sokoni ni udhalili."

Na mwenye kula akishirikiana na watu wengine hakika ni juu yake kuchunga adabu vilevile, kama vile kutoangalia chakula chao, na kula kilicho mbele yake na wala asifanye vitendo – katika kula kwake – vinavyoudhi waliokaa pamoja naye, kama vile mazoea mabaya yanayotokea kwa baadhi ya watu ya kuteuka, na hivyo mtawaona baada ya kula wanaanza kuteuka, ikiwa ni pamoja na kuwau-

[175] *Makarimul-Akhlaq*, uk. 182.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 198 11/23/2016 12:37:36 PM

dhi waliokaa na kuchukiza. Mtume ﷺ alimkataza Abu Juhaifah juu ya hayo, kutokana na athari mbaya zinazoachwa na kitendo hicho, kwa kuongezea katika athari nyinginezo za kijamii. Kutoka kwa Abu Juhaifah amesema: Nilimwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na mimi nateuka akasema: "Ewe Abu Juhaifah punguza kuteuka kwako hakika watu wenye kushiba sana duniani watakuwa na njaa sana siku ya Kiyama."[176]

### 3. Adabu za maisha:

Kama ilivyo katika upande wa ibada na kijamii, hakika wamependekeza Maasumini عليهم السلام adabu za maisha, nazo ni zile ambazo zinafungamana na namna, na inaweza kuonekana kwa mara ya kwanza kwamba haya sio katika mambo ya Maasumini عليهم السلام bali ni katika mambo ya matabibu, lakini ilipokuwa maelekezo ya Maasumini yanalenga katika wema wa dunia na akhera hivyo walikuwa na maelekezo yanayohusiana na ibada na mengine yanayohusiana na namna ya vitendo vya kidunia katika ambayo yanadhamini usalama wa mwanadamu na afya yake.

Ambayo yataelezwa katika mistari ifuatayo ni katika aina hiyo. Miongoni mwa adabu hizo ni kutilia mkazo kuosha mikono, pamoja na kwamba kitendo hiki leo kimekuwa ni katika mambo ya kawaida kwa watu wengi, isipokuwa kwa kuangalia mazingira ambayo imekuja humo hadithi hii, ambapo jamii ya Kiarabu ilikuwa katika ujahiliya ambao haukuwa unajali kabisa usafi, na ulikuwa unakabiliwa na uhaba wa maji. Imepokewa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anasema: "Mwenye kupenda kuzidisha kheri ya nyumba yake basi anawe wakati kinapoletwa chakula na baada yake, kwani anayeosha mikono yake wakati wa kula na baada ya kula ataishi kadiri atakavyoishi katika wasaa na ataepushwa na ba-

[176] Rejea iliyotangulia, uk. 149.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 199 11/23/2016 12:37:36 PM

laa katika mwili wake." Na kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام kuna riwaya yenye tamko kama hili.

Na miongoni mwa adabu hizi ni kutafuna vizuri, hiyo ni kwa sababu moja ya vinavyosababisha maradhi ni kutotafuna chakula vizuri. Na baadhi ya majarida ya tiba yameandika mwishoni kwamba ambao wanakula mara nyingi mlo wa haraka katika mahoteli mengi yaliyoenea leo hii huko Ulaya, wengi wao ndio wenye kupatwa na maradhi ya tumbo kuliko wengine, hiyo ni kwa sababu kutafuna vizuri kunamaanisha kupunguza kazi ya tumbo katika kumeng'enya chakula. Hiyo ni kwa sababu kinakuja kimeshasagwa na kimeng'enywa na maji maji ya mdomo, wakati ambapo mwenye kula chakula chake kwa haraka hakika hatoi fursa kwa chakula hicho kutulia katika mdomo wake ili kitafunwe au kisangwe.

Na vilevile miongoni mwa adabu ni wastani katika kula, na imeshatangulia kutajwa hayo. Na mwisho ni kuchokonoa meno kwa ajili ya kutoa mabaki ya chakula baina ya meno. Amepokea Imamu as-Sadiq عليه السلام kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema: "Chokoeni meno baada ya kula chakula hakika ni afya kwa kinywa na meno, na inaleta riziki kwa mja." Na inafahamika kwamba mabaki ya chakula, hususan nyama, yakibakia baina ya meno kwa muda hakika wakati huo yanageuka na kuwa ni mazalia ya bakteria na vijidudu vyenye madhara, jambo ambalo linapelekea kupatwa na ugonjwa wa fizi na kuharibika meno. Na tunahitimisha utafiti wetu huu kwa kuelezea hadithi mbili ambazo zinahusu adabu za jumla:

Kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام kutoka kwa baba zake, kutoka kwa Imam Hasan عليه السلام amesema: "Katika meza ya chakula kuna mambo kumi na mbili ambayo ni wajibu kwa kila Mwislamu kuyajua: Manne kati yake ni faradhi na manne kati yake ni sunnah, na manne kati yake ni adabu. Ama yaliyo faradhi: Ni kujua, ridhaa, Bis-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 200 11/23/2016 12:37:36 PM

millahi na kushukuru. Ama ambayo ni sunnah: ni Kunawa[177] kabla ya chakula, kukaa upande wa kushoto, kula kwa vidole vitatu na kulamba vidole. Ama adabu ya kula ni kula kilicho mbele yako, kula tonge dogo, kutafuna vizuri na kutowaangalia watu usoni."[178]

Na kutoka kwa Ibn Umar amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Kinapowekwa chakula mbele ya mtu basi ale kilicho mbele yake na wala asile kilicho mbele ya mwenzake, na wala asile sehemu ya juu hakika sehemu ya juu inaleta baraka. Na wala asiondoke mezani hata kama ameshiba, hakika akifanya hivyo mwenzake ataona aibu na huenda bado anahitajia kula."

[177] Ni sawa iwe kwa maana yake ya kilugha, yaani kunawa au kwa maana ya kiistilahi ya kisharia, na zote mbili zinamaanisha usafi.

[178] Makarimul- Akhlaq, Uk. 141.

# SEHEMU YA TANO

## WATUMISHI NA WATUMWA KATIKA MAISHA YAO G

Wakati mwingine yanajiri mazungumzo juu ya watumishi na watumwa katika maisha ya Ahlul-Bayt عليهم السلام, kwa kuangalia nini faida ya jambo hili, na mara nyingine kwa kuangalia walivyoamiliana na watumishi wao.

Na kuzungumzia masa'ala haya kuna umuhimu sio tu kwa sababu ya kuwa kwake ni moja ya muonekano wa maisha ya kivitendo katika watu wengi, bali ni kwa sababu kuna rai mbili katika kuangalia asili yake. Kuna kundi la watu linaloona kwamba kutumia watumishi ni hali ya ubadhirifu ambayo inampasa muumini ajiepushe nayo, hususan ukizingatia kwamba mtumishi analingana kabisa kiutu na mwenye kutumikiwa, na kufanya kwake kazi za utumishi kunamfanya awe na hadhi ya chini na awe duni kuliko mwenzake. Na yaliyopokewa katika kuwepo watumishi kwa Ahlul-Bayt عليهم السلام hakika inafasiriwa kwamba walikuwa wanataka kuwakomboa wale watumwa ambao wanawanunua sokoni, hivyo walikuwa wanabakia kwa muda chini ya utumishi wao ili kuwalea na kuwaanda kwa ajili ya kuwakomboa. Na kisha hakika matumizi hayo yalikuwa ni hali ya kipekee, haichukui sifa ya kanuni wala haiwezekani kuijengea juu yake.

Ama kundi la pili linaona ni mas'ala ya kawaida kwa kuongezea katika hali ya kipekee ambayo wanaitaja wenye rai ya kwanza ya kuwepo kwa watumwa na mateka na kutumia njia ya kuwakomboa.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 202 11/23/2016 12:37:36 PM

Isipokuwa sisi tunakuta kwamba baadhi ya watumishi wao hawakuwa ni watumwa, bali walikuwa ni watu huru wakati ambapo baadhi yao walikuwa ni watumwa, na baadhi yao walikuwa ni Waarabu, hivyo basi ilikuwaje? Hakika lililothibiti katika historia la kuwepo idadi kadhaa ya watumishi, tunaitakidi kwamba ilikuwa chini ya anwani ifuatayo:

**Ni moja ya njia ya kukomboa na kuacha huru:**

Kama tunavyojua kwamba Uislamu umekuja ukawaraghibisha watu kuwaacha huru watumwa katika wakati ambao soko la kuuza watumwa lilikuwa limeenea, sawa iwe katika njia ya kuwaleta kutoka katika sehemu zisizokuwa chini ya utawala wa Kiislamu au kwa njia ya vita ambazo zilikuwa zinaacha nyuma yake idadi kadhaa ya mateka. Na Ahlul-Bayt عليهم السلام walikuwa wananunua idadi kadhaa katika hawa mateka kwa anwani ya watumishi na kwa ajili ya kuwakomboa, isipokuwa hakika wao walikuwa wanabakia kwa muda chini ya maelekezo ya Maasumini na kutengeneza tabia zao na itikadi zao, kisha wanawaacha huru. Na huenda sisi tukawa tunakuta katika yanayonukuliwa katika kitendo cha Imam as-Sajjad عليه السلام picha kamilifu juu ya mwelekeo huu, hiyo ni kwa sababu alikuwa ananunua watumwa na anawalea kwa muda wa mwaka mzima, na anarekodi makosa yao na matatizo ya vitendo vyao bila ya kuwaadhibu, hadi unapofika mwanzo wa mwaka mwingine ndipo anaanza kuwasomea makosa hayo. Na baada ya kukiri vitendo hivyo ilihali wakisubiria adhabu anawasamehe na anawataka wamuombee maghufira kwa Mwenyezi Mungu kama alivyowasamehe wao baada ya kuwa wamestahili adhabu.[179] Sisi tunakuta kwamba Imamu عليه السلام baada ya kumaliza pamoja nao kozi yake ya malezi ya mwaka mzima anawaacha huru.

[179] Utapata ufafanuzi wa njia hiyo katika kitabu *Binaul-Qaadati fiy Nahji Ahlul- Bait* عليهم السلام cha Mtunzi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 203 11/23/2016 12:37:36 PM

Kando na hawa kulikuwa na idadi ya wanaojitolea kuwatumikia Maasumini عليهم السلام kwa kuzingatia kuwa ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, kama tunavyoshuhudia leo katika hali ya maulamaa wakubwa ambao kuna watu wanaokaa katika nyumba zao kwa ajili ya kuwahudumia kwa kutaka malipo na thawabu au kwa kupenda kunufaika na elimu yao na maarifa yao. Na tutakuta katika kurasa zijazo baadhi yao walikuwa na maandalizi na utayari. Walipochota elimu ya Maimamu wakatingishika, wakastawi na yakamea matunda mema kila kona. Na hivyo tunawakuta watu mfano wa Qanbar mtumishi wa Imamu Ali عليه السلام na msaidizi wake kulingana na msemo wa kileo. Na pia tunamkuta Munjihi Shahidi, mtumishi wa Imam Husein عليه السلام, na Naswir mtumishi mwaminifu, na vivyo hivyo wengine kama itakavyokuja hapo baadaye.

Haya, na kwa kuongezea kwamba sisi tunakuta katika hadithi, maelezo ambayo yanazungumzia juu ya karaha ya mtu mkubwa kuzikabili haja zake ndogo ndogo moja kwa moja. Wakati mwingine ni kwa kuzingatia lililo muhimu na muhimu zaidi, ambapo wakati wa mwanadamu ni finyu, na kwa kuzingitia ongezeko la majukumu yake ya kidini au ya kijamii au ya siasa, msemo wa 'wakati huu' na vipengele vyake unakuwa ni jambo muhimu sana hadi katika daraja ambayo inaweza kukadiriwa mara nyingi kwa kuwaangalia wafanyabiashara wakubwa. Hiyo ni kwa sababu kuchelewa kwa mfanyabiashara katika kazi yake kwa muda wa nusu saa kunampotezea kiasi kikubwa cha mali kinacholingana na ukubwa wa kazi yake, na hali ni hiyo hiyo kulingana na wenye majukumu na mamlaka. Ikiwa wakati wako hautoshi kwa kazi zako zote inapasa kuzigawa kutokana na umuhimu, kama yalivyo makusudio ya hadithi iliyopokewa kutoka kwa Amirul-Muuminina عليه السلام, na angalizo ni kwamba mambo ya maisha na mahitaji yake yanachukua wakati wa kila mwanadamu. Na yanaongezeka na kupungua kulingana na mtu na njia ya maisha



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 204 11/23/2016 12:37:36 PM

yake, na unaweza kutafakari yanachukua muda gani mambo hayo kwa mtu anayemiliki familia kubwa. Na kuwepo kwa watumishi hapa sio kwa maslahi ya uvivu na uzembe bali ni kwa ajili ya maslahi ya mtu kufanya mambo mengine yenye umuhimu zaidi na yenye kuhitajia juhudi zaidi, na ambayo wala hawezi kuyafanya mwingine asiyekuwa yeye.

Na wakati mwingine riwaya hizo zinazungumzia kwa maneno ya karaha ya kijamii na athari mbaya zinazosababishwa na kufanya mambo hayo madogo madogo. Kutoka kwa Muawiya bin Wahab amesema: Aliniona Abu Abdillahi عليه السلام nikiwa nimebeba majani, akasema: "Inachukiza kwa mtu mwenye heshima kubeba kitu duni na kutembea nacho."[180] Na kutoka kwa Abdillahi bin Jabalah amesema: Nilikutana na Abu Hasan عليه السلام nami nimening'iniza samaki mkononi mwangu, akasema: "Zitupe hizo, hakika mimi nachukia mtu mtukufu kubeba kitu duni yeye mwenyewe." Kisha akasema: "Hakika nyinyi ni watu ambao maadui wenu ni wengi, mnafanyiwa uadui na viumbe. Enyi wafuasi wetu, jipambeni kwao hao kwa kile mnachokiweza."[181]

Na inapasa hadithi hizi zichukuliwe kwa kuangalia mazingira ya kijamii yaliyopo. Wakati ambapo mtu kuyafanya mambo hayo yeye binafsi kunamdhalilisha, ndipo hadithi hizi zitumike, na hayo ndio makusudio ya hadithi hizi. Ama ikiwa ada ya kijamii ni watu wenyewe kufanya mambo hayo basi hadithi hizi hazitakuwa ni dharura. Bali huenda kufanya mwenyewe ikawa ndio jambo hasa linalohitajika, ikiwa kunatumikia malengo ya kimaadili, kama vile unyenyekevu na kujiepusha na kiburi au ikiwa makusudio yake ni kuwaelimisha wengine. Kama inavyopokewa kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم, hakika ni kama alivyosema: "Mambo matano sintoyaacha hadi kufa:

---

[180] *Furuul-Kafiy*, Juz. 2, uk. 202.
[181] *Furuul-Kafiy*, Juz. 2, uk. 203.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 205 11/23/2016 12:37:36 PM

Kula pamoja na watumwa, kupanda punda duni, kukamua mbuzi kwa mikono yangu, kuvaa sufi na kuwasalimia watoto, na iwe sunnah baada yangu."[182]

Na zimepokewa hadithi nyingi zinazoonyesha kwamba Nabii ﷺ na Maasumini عليهم السلام walikuwa wakifanya mambo mengi kwa mikono yao. Imepokewa kwamba Mtume ﷺ ukiachana na kukamua mbuzi, alikuwa pia anafunga kamba ngamia, anachinja, n.k, na hiyo ni ili iwe ni sunnah baada yake kama alivyosema.

## KUAMALIANA NA NJIA YA MALEZI:

Hakuna katika rejea zilizopo kwetu ambayo inabainisha kwa namna ya ukamilifu ufafanuzi wa njia ya kuamiliana baina ya Ahlulbayt عليهم السلام na watumishi wao, isipokuwa hadithi zilizopo zinaweza kuweka wazi kwetu njia ya muamala huu na asili yake, kama ambavyo sisi vilevile tunaweza kuona vipengele vya njia hiyo kupitia matokeo yake. Na katika upande wa kwanza tunakutana na hadithi mbalimbali ambazo zinamalizikia katika anwani moja, nayo ni kutilia mkazo utu wa watumishi hao, sawa wale waliokuwa huru au watumwa, Waarabu au wasiokuwa Waarabu, kinyume na mtazamo ulioenea hivi sasa kama ilivyotangulia, ya kwamba mtumishi hana utu na kwamba kuna tofauti kubwa baina yake na anayemtumikia. Sisi tunakuta Ahlul-Bayt عليهم السلام nao ndio viongozi wa fikra ya Uislamu wanawapa watumishi heshima yao ambayo wanastahiki kama binadamu na waumini.

Katika tukio lifuatalo tunaweza kubainisha namna mbili za kuamiliana pamoja na watumishi, namna ile ambayo inadhalilisha utu wao na heshima yao na wala haikubali badala yao wala suluhu yao, na ile nyingine ambayo inamzingatia mtumishi kuwa yuko sawa bali

[182] *Makarimul-Akhlaq*, uk. 100.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 206 11/23/2016 12:37:37 PM

anao utukufu katika hilo joto la ujana na nguvu zake, na kisha anastahiki kuvaa vizuri zaidi  na kupendeza zaidi.

Kutoka kwa Mukhtar at-Tamar amesema kwamba Amirul-Mu'minin عليه السلام alikwenda katika soko la tende akamkuta binti anamlilia muuza tende, akamwambia: "Una nini?" Akasema: "Hakika mimi ni kijakazi, watu wangu wamenituma niwanunulie tende kwa dirhamu moja, nilipowapelekea hawakuridhika nazo, na wakanirudisha. Nikazirejsha lakini muuza tende amekataa kuzipokea." Akasema عليه السلام: "Ewe mtu chukua tende kwake na mrudishie dirhamu zake." Muuza tende akakataa, akaambiwa: "Huyu ni Ali bin Abutalib" ndipo akapokea tende na akarudisha dirhamu kwa binti huyo.

Kisha akaenda katika soko la Karabisi (la nguo) akasimama kwa kijana aliyekuwa na nguo mbili, akasema: "Ewe kijana una nguo mbili kwa dirhamu tano?" Akasema ndio ninazo, akachukua nguo mbili, moja ya dirhamu tatu na nyingine ya dirhamu mbili, kisha akasema: "Ewe Qanbari chukua ambayo ni ya dirhamu tatu." Qanbari akasema: "Wewe unafaa zaidi kuwa nayo, kwani wewe unapanda mimbari na kuwahutubia watu." Imamu akasema: "Wewe ni kijana na una joto la ujana, na mimi naona haya kwa Mola Wangu kujifadhilisha kwako. Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم anasema: 'Wavalisheni mnayovaa na walisheni mnayokula.'"

Na vile vile tunasoma katika sira ya Imamu Ridha عليه السلام kwamba alikuwa anakaa katika meza moja pamoja na watumishi wake na watumwa wake, jambo ambalo linazingatiwa kuwa ni kinyume na mazoea ya kimakosa ya kijamii yanayopelekea ubaguzi dhidi ya hawa. Hadi baadhi ya wafuasi wake, kutokana na mazoea haya wakapendekeza kwamba ajitofautishe nao na kwamba awatenge watumishi na watumwa katika meza, lakini akakataa hilo. Bali huenda Imam عليه السلام aliwaandalia watumishi wake chakula yeye mwenyewe. Na katika habari kutoka kwa Nadir mtumishi anasema: "Abul-Hasan



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 207 11/23/2016 12:37:37 PM

Ridha عليه السلام alikuwa anaweka *Jauzinjiyah* moja juu ya nyingine na kunipatia."[183]

Wakati baadhi ya watu wamezoea kujipamba zaidi na muonekano wa uongo, wamezoea kuwasimamisha watumishi mbele ya wageni wakiangalia chakula pasipokuwa na haja ya wao kusimama. Hakika sisi tunaona Imamu Ridha عليه السلام hakuwa akimzungusha yeyote kati ya watumishi wake au kumtuma katika haja wakati wa kula kwake isipokuwa baada ya kumaliza kula. Na kama anavyonukuuu Yaasir mtumishi: "Alituambia Abul-Hasan عليه السلام: 'Kama nitasimama mbele yenu wakati nyinyi mnakula basi msiache hadi mmalize.' Na alikuwa anapomwita mmoja wetu kisha akaambiwa: 'Wao wanakula' husema: 'Waache hadi wamalize.'"

Kama ambavyo wanatia mkazo katika kujiepusha kuwakalifisha kwa jambo lililo juu ya uwezo wao, hiyo ni kwa sababu mtu huyu kuwa kwake mtumishi haimaanishi kwamba umwangamize kwa kazi kutwa nzima na zilizo juu ya uwezo wake, bali inapasa kumpunguzia, sawa iwe kwa kuangalia nguvu yake katika kutekeleza kikamilifu kazi alizopewa, au kwa kumsaidia katika kuifanikisha. Katika hadithi kutoka kwa al-Baqir عليه السلام amesema: "Mambo manne mwenye kuwa nayo katika waumini Mwenyezi Mungu atamuweka katika daraja za walio juu zaidi, katika vyumba vya juu zaidi, katika sehemu tukufu mno: Ambaye hakumhilikisha mtumwa wake na akamsaidia katika aliyomkalifisha na wala hakumtuma katika ambayo hayawezi."

Na imepokewa kutoka kwa Imamu as-Sadiq عليه السلام kwamba amesema: "Katika sharia ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم imeandikwa kwamba mkiwatumikisha ambao imewamiliki mikono yenu ya kuume katika jambo gumu basi fanyeni pamoja nao. Hakika baba yangu alikuwa anawaamuru, kisha anakuja anaangalia, ikiwa ni jambo gumu

[183] *Biharul-An'war*, Juz. 71, uk. 141. Na *Jauzinjiy* ni aina ya haluwa ambayo inatengenezwa kwa nazi.

anasema: Bismillahi kisha anafanya pamoja nao. Na ikiwa ni jepesi anawaacha."

Yote hayo yalikuwa katika upande wa maelekezo, na kwa kuangalia katika madhumuni ya baadhi ya hadithi zilizopokelewa. Kama ambavyo sisi tunaweza kujua pia kitu katika aina ya kuamiliana kupitia mifano ya wafuasi wao na watumishi wao, ambapo hawa ilikuwa ni kawaida wamalizike na wafutwe kabisa katika kumbukumbu ya historia kama walivyomalizika maelfu mfano wao, kama si hawa kuwa katika duara la Ahlul-Bayt عليهم السلام la kimalezi, na hapa tutaeleza kwa kutaja muhtasari wa baadhi ya hawa na maisha yao na nafasi zao:

## ZAYDI BIN HARITHAH AL-KALBIY:

Kwa malezi ya Mtume ﷺ na uzuri wa upokeaji wake wa malezi hayo alipanda kutoka katika daraja ya mtumwa ambaye anauzwa na kununuliwa na kwenda katika daraja ya mtoto anayemliwaza Mtume ﷺ na kiongozi wa kijeshi ambaye anategemewa. Natuwe pamoja naye kuanzia mwanzo, ambapo Zaydi aliibiwa kwa baba yake Harithah al-Kalbiy katika moja ya vita za Waarabu kisha akaletwa na akauzwa hapo Makkah.

Bibi Khadija binti Khuwaylid عليها السلام alimnunua na akamtoa zawadi kwa Mtume ﷺ baada ya kuoana, na akawa katika milki ya Mtume ﷺ. Na Mtume alipotangaza daawa ya Uislamu, Zaydi akawa ni katika watu wa mwanzo kuamini na kusadikisha ujumbe wake, na aliandamana naye katika mapito hayo magumu hadi alipotoka kwenda Twaifu ili kuwalingania watu wake katika Uislamu alikuwa pamoja naye. Na alikuwa anamhami dhidi ya adha na shari ya watu Thaqif baada ya kukataa daawa yake, na wapumbavu wake wakampiga kwa mawe.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 209 11/23/2016 12:37:37 PM

Alikuwa na imani ya kina juu ya ujumbe, na alikuwa na ufuasi madhubuti kwa Mtume ﷺ, kwani alimuona kwamba ni Nabii na mwongozaji, baba mpole na kaka mlezi, kwa hiyo alijikuta dhati yake na uwepo wake uko pamoja na Mtume. Na mzazi wake alipokuja baada ya kujua kuwa kwake katika miliki ya Mtume na alikuwa ni katika wakuu wa Bani Kalbi, alimuomba Mtume ﷺ amrejeshee mtoto wake Zaydi kwa kumwacha huru au kwa kumuuzia. Mtume ﷺ alisema: "Zaydi yuko huru naaende atakapo." Baba yake akamwambia: "Ewe mwanangu haki iko pamoja na kaumu yako, nasaba yako na ukoo wako." Zaydi akasema: "Sikuwa ni mwenye kumwaacha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ."

Baba yake akajitahidi na akambembeleza kwa upole lakini Zaydi akasema: "Simwachi Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ." Baba yake akasema: "Mimi najiweka mbali na wewe." Zaydi akamwambia: "Hilo ni juu yako. Harithah akasema: "Enyi Makuraishi na Waarabu hakika mimi niko mbali na Zaydi sio mtoto wangu na wala mimi sio baba yake." Hapo Mtume ﷺ akasema: "Enyi Makuraishi Zaydi ni mtoto wangu na mimi ni baba yake." Na hapo akawa anaitwa Zayd bin Muhammad hadi ilipoteremka Aya tukufu:

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَٰكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ

**"Hakuwa Muhammad ni baba wa yeyote kati wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Mitume….." (33:40)**

Hivi ndivyo Zaydi alivyoifadhilisha nasaba ya Mtume na kufuata ujumbe na kuacha nyuma yake ufuasi wake wa kabila ulipopingana, na akawa anapanda daraja pamoja na kwamba katika mwonekano yeye ni mfupi na mweusi sana, na pua yake imebonyea, kama wanavyonukuu wanahistoria.

Na Zaydi akaanza kujitokeza katika uongozi wa baadhi ya vikosi vya Kiislamu hadi ikawadia vita vya Muutah, ambavyo vilikuwa ni kati ya vita muhimu na hatari ambapo Warumi waliamua kuwapiga vita Waislamu kupitia kushambulia mipaka ya Waislamu. Mtume akaamua kuwawahi na akachagua watu kati ya wanaume bora na wenye ikhilasi na kujitolea. Na hapa riwaya zinatofautiana katika kuwapanga viongozi hawa, je aliyetangulia ni Zaydi au Ja'far bin Abutalib na tusome moja wapo:

Nabii ﷺ alipotuma askari kwenda Muutah alimchagua Zayd bin Harithah kuwa kiongozi wao na akamkabidhi bendera na akasema: "Kama Zaydi atauliwa basi kiongozi wenu ni Ja'far bin Abutalib, na akiuliwa Ja'far basi kiongozi wenu ni Abdillahi bin Rawaha al-Answariy," na akanyamaza. Alikuwepo Myahudi mmoja wakati Mtume anaeleza utaratibu huu wa uongozi, hivyo walipoondoka akasema: "Ikiwa Muhammad ni Nabii kama anavyosema basi hawa watatu watauliwa." Akaambiwa: "Kwa nini umesema haya?" Akasema: "Kwa sababu Manabii wa Wana wa Israil walikuwa anapotuma Nabii miongoni mwao kikosi katika jihadi husema: 'Akiuliwa fulani kiongozi ni fualani baada yake' akitaja uongozi wa wawili au mia au pungufu au zaidi, na wote waliotajwa miongoni mwao katika uongozi huuliwa."

Jabir amesema: Ilipofika siku ambayo ilitokea humo vita nyao, Nabii ﷺ alituswalisha Alfajiri kisha akapanda mimbari akasema: "Ndugu zenu wameshakutana na washirikina katika vita." Akawa anasimulia mapigano yao hadi akasema: "Zaydi bin Harithah ameshauliwa na bendera imeanguka." Kisha akasema: "Ameshaichukua Ja'far bin Abutalib na anasonga mbele katika vita." Kisha akasema: "Amekatwa mkono wake wa kulia, ameichukua kwa mkono wake wa kushoto." Kisha akasema: "Umekatwa mkono mwingine na ameikumbatia bendera katika kifua chake." Kisha akasema: "Ja'far



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 211 11/23/2016 12:37:37 PM

bin Abutalib ameshauliwa na bendera imeanguka chini na kisha ameichukua Abdillahi bin Rawaha, na wameshauliwa watu kadha wa kadhaa katika washirikina, na katika Waislamu fulani na fulani." Hadi akataja wote waliouliwa katika Waislamu kwa majina yao, kisha akasema: "Abdillahi bin Rawaha ameshauliwa na bendera imechukuliwa na Khalid bin al-Walidi na Waislamu wanaondoka."[184]

Hivi ndivyo alivyokuwa Zaydi bin al-Harithah ni mfano bora katika watumwa na watumishi. Namna gani anabadilika chini ya malezi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuwa muumini mwenye kufuata, na kuwa kiongozi wa jeshi na kipenzi cha Mtume ﷺ hadi akasema Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Hakika Nabii ﷺ ilipomjia habari ya kifo cha Ja'far bin Abutalib na Zaydi bin Harithah alikuwa anapoingia nyumbani kwake kilio chake kinakuwa kingi zaidi juu yao na anasema: 'Walikuwa wanazungumza na mimi na huku wananiliwaza na wote wameshaondoka.'"

## QANBAR HURIA WA AMIRUL-MUUMININA عليه السلام

Wanahistoria hawakuzingatia kutaja nasaba yake isipokuwa kwa kiasi tu, hakika wao wamesema: Hakika anatoka Mudhar, na huenda ni kutokana na ada ya kughafilika kuwataja watumishi, kwa sababu haitarajiwi kupatikana mtu anayejali nasaba zao, na wala haitarajiwi wao kuwa na athari kubwa au utajo katika historia.

Na huenda ni kwa sababu wao walitosheka na kumnasibisha kwenye jukumu lake na nafasi yake kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام, hivyo linapotajwa jina la Qanbar basi hiyo inatosha kutambulisha heshima yake kwa kujengea juu ya nafasi ambayo alikuwa nayo kwa Amirul-Mu'minin Ali عليه السلام. Na lini mtu ilikuwa inatukuzwa nasaba yake kama amali yake na nafasi yake itaporomoka? Imeelezwa ka-

184 *Biharul-An'war*, Juz. 21, uk. 53.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 212 11/23/2016 12:37:37 PM

tika sifa zake, kwamba Qanbar alikuwa ni maneno ya Ali, anampenda Ali mno, Ali عليه السلام anapotoka, anatoka pamoja naye na upanga. Usiku moja akamuona akasema: "Una nini ewe Qanbar?" Akasema: "Nimekuja ili nitembee nyuma yako ewe Amirul-Mu'minin." Akasema: "Ole wako je, kutokana na watu wa mbinguni umekuja kunilinda au kutokana na watu wa ardhini?" Akasema: "Hapana bali ni kutokana na watu wa ardhini." Akasema عليه السلام: "Hakika watu wa ardhini hawawezi kitu isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, rejea."

Na alikuwa anaandamana na Amirul-Mu'minin عليه السلام katika mizunguko yake ya ukaguzi, ambayo anapitia familia za maskini na wanyonge. Na katika kila makutano alikuwa anajifunza mafunzo katika kuwahudumia kwake watu na kupenda mafakiri kuliko baba wa masikini.

Na alikuwa anapewa kazi na Imamu Ali عليه السلام ya kutekeleza amri zake. Jina lake limepokewa katika ushairi unaonasibishwa kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام:

"Nilipoona jambo ni jambo ovu,
niliwasha moto na kumwita Qanbar."

Na imepokewa kwamba Amirul-Muuminina عليه السلام alikuwa anasema huko Siffin:

"Hakika mimi vita vilipokaribia na kuwadia,
niliharakisha nguo yangu na kumwita Qanbar,
niletee bendera yangu na wala usichelewe kwa tahadhari."

Na hivi ndivyo alivyogeuka na kuwa mkono wa kulia wa Amirul-Mu'minin عليه السلام kiasi kwamba sisi tunakuta jina lake katika sehemu nyingi. Katika hukumu, Amirul-Muuminina عليه السلام anamwita ili kutenganisha baina ya mashahidi na kuchukua kauli zao, na katika ku-



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 213 11/23/2016 12:37:37 PM

peleka chakula kwa mafakiri anakuwa pamoja na Imamu Ali, na katika vita na vivyo hivyo amegeuka mtumishi huyu kijana kuwa mtu kati ya waliotangulia na walio karibu kwa Amirul-Mu'minin عليه السلام, na katika wafuasi wake mahususi, na kwa hiyo al-Hajjaji alipotaka kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa damu ya mtu katika wafuasi wa Abu Turabi aliambiwa: "Hatumjui yeyote aliyekuwa na usuhuba mrefu kwa Abu Turabi kuliko huruia wake Qanbar."

Na inatosha kujua heshima yake na utu wake na hadhi yake kwa kujua mjadala ambao ulitokea baina yake na al-Hajjaji Thaqafiy. Qanbar alipelekwa kwake akamwambia: "Ni nani Abu Turabi?" Qanbar akasema: "Mimi ni huria wa aliyepiga kwa panga mbili na aliyechoma kwa mikuki miwili na akaswali kuelekea katika kibla mbili, na akatoa viapo viwili vya utii, na akahama hijira mbili na hakumkufuru Mwenyezi Mungu hata kwa mpepeso wa jicho.

"Mimi ni huria wa mwema wa Waumini na mrithi wa Manabii, na mbora wa Mawasii na mkuu wa Waislamu na kiongozi wa Waumini na nuru ya wapigana jihadi na kiongozi wa wenye kulia, na pambo la wachamungu, na taa ya wenye kutangulia, na mwanga wa waliopo, na mbora wa wanyenyekevu, na ulimi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mola wa walimwengu, na muumini wa kwanza katika Aali Yasiin mwenye kuungwa mkono na Jibril mwaminifu.

"Na mwenye kunusuriwa na Mikail mwenye nguvu, na mwenye kusifiwa kwa watu wote wa mbinguni, bwana wa Waislamu na waliotangulia, na mwenye kuwauwa wenye kutengua, waasi na waovu, mwenye kuhami utukufu wa Waislamu na mwenye kupiga vita maadui wake wenye chuki, mwenye kuzima moto wa wawashaji, na fahari ya waliotembea kwa miguu katika Makuraishi wote, na wa kwanza aliyekubali na kuitika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 214 11/23/2016 12:37:37 PM

"Amirul-Mu'minin na wasii wa Nabii wake katika ulimwengu, na mwaminifu wake juu ya viumbe na Khalifa wake kwa wote alitumwa kwao, bwana wa Waislamu waliotangulia, mwenye kuwadhalilisha washirikina, na mshale katika shabaha ya Mwenyezi Mungu dhidi ya wanafiki, na ulimi wa neno la wachamungu, mwenye kunusuru dini ya Mwenyezi Mungu na Walii wa Mwenyezi Mungu, ni ulimi wa neno la Mwenyezi Mungu, mnusuru wake katika ardhi Yake na mkoba wa elimu Yake na ngome ya dini Yake.

"Imamu wa wema aliyeridhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Msamehevu, mkarimu, bwana anayekesha usiku. Mtukufu, mtwaharifu, mkarimu, mtoaji shujaa mkarimu, mwenye kusubiri, mwenye kufunga sana, moungozaji, mwenye kutangulia, mwenye kukata vizazi, mwenye kutawanya makundi. Mwangalifu sana, mvumilivu mwenye subira, na mwenye kuthibiti katika vita, na mwenye nguvu zaidi na mwenye kushinda.

"Mtoaji shujaa shupavu, simba shujaa, mwenye msimamo, mwenye azima mwenye hakima, bingwa wa hotuba, mwenye kuhiji sana, mkarimu wa asili, mtukufu wa fadhila, mtukufu wa kabila, mwenye ukoo safi, mtukufu imara, mwenye kutekeleza amana, ni kutoka katika Bani Hashim, mtoto wa Ami wa Nabii ﷺ, Imamu muongozaji mwongofu, mwenye kujiepusha na ufisadi, mdhibiti shujaa, mwepesi simba shujaa.

Ni shujaa wa Badri, mwenyeji wa Makka, Mwislamu halisi, mtawa kutoka katika milima mirefu mwenye kukata vilele vyake, na katika Waarabu ni bawana wao, na katika vita ni simba wao, shujaa na simba mwenye kusonga mbele, na mbalamwezi timilifu, mshindi wa Waumini na mrithi wa Haram mbili, baba wa wajukuu wawili Hasan na Husein. Wallahi Amirul-Mu'minin wa kweli Ali bin Abutalib sala na salamu tukufu na baraka njema na nzuri viwe juu yake." [185]

[185] *Tanqihul-Maqaali*, Juz. 2, uk. 30.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 215 11/23/2016 12:37:37 PM

Al-Hajjaji aliposikia kutoka kwake hayo akamwambia: "Jinasue na dini yake."

Qanbar akasema: "Nikijinasua katika dini yake utanionyesha dini nyingine iliyo bora kuliko hiyo?"

Akasema: "Hakika mimi nitakuuwa. Chagua mauaji gani yanapendeza kwako?"

Akamwambia: "Nimekuachia hilo wewe."

Akasema: "Kwa nini?"

Qanbari akasema: "Kwa sababu wewe hutoniuwa isipokuwa nami nitakuuwa kwa mfano wake, na ameshaniambia Amirul-Mu'minin عليه السلام kwamba mauti yangu yatakuwa ni kuchinjwa kwa dhulma pasipo haki." Basi akaamuru na akachinjwa.

## NA WENGINE NI MASHAHIDI:

Wakati maarifa yasiyo ya kina yanapotilia mkazo juu ya dhahiri ya mambo, utakuta utukufu wote uko katika kunasibiana na kabila na si vinginevyo. Na utukufu wote uko katika utukufu wa baba na mababu, vivyo hivyo kwa kufuata utamaduni huu mtu anakuwa bwana bila ya kujua au kuchangia katika utukufu huu au ni dhalili bila ya kupenda au kuchagua.

Isipokuwa utamaduni wa asili wa Kiislamu unaweka kipimo kingine katika utukufu wa mwanadamu, umuhimu wake na ubora wake. Na umuhimu wa kipimo hiki ni kwamba unaangukia ndani ya duara la uchaguzi wa mwanadamu na kwa uwezo wa mtu mwenyewe, wakati wowote anaweza kuitikia na kisha kupanda daraja ya utukufu. Au anaweza kuacha na kubakia alipo. Kipimo hicho ni misimamo ya mwanadamu, sawa iwe katika upande wa ujumbe na



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 216 11/23/2016 12:37:37 PM

Mtume au katika upande wa jamii na matukio ambayo yanatokea humo, na katika hili watu wote wako sawa, bali kwa matokeo ya misimamo yao wanatofautiana ubora, hivyo Mwarabu ambaye mizizi yake inaingia katika kina cha makabila ya Kiarabu na ambaye ni wa kwanza kwa sifa hii kulingana na utamaduni wa kijuu juu, anakuwa wa pili. Wakati ambapo mtumwa au huria, naye kulingana na utamaduni huo ni duni kwa kawaida, anakuwa wa kwanza.

Na huenda hii ndio sababu ya kuendelea kwa watumishi na watumwa wasiokuwa Waarabu katika ummah wa Kiislamu katika historia yake ya awali. Sisi tunakuta kwamba miongoni mwa hao wasiokuwa Waarabu ni Maulamaa na mafakihi, bali na hata mabingwa miongoni mwa washairi wa lugha ya kiarabu, ambapo nafasi haitoshi kwa ajili ya utafiti wake. Hiyo ni kwa sababu wengi kati ya Waarabu waliona kwamba uarabu wao unatosha katika ubora wao kwa wasiokuwa wao, wakazembea katika kutafuta matukufu wakati ambapo walijitahidi wale wasiokuwa Waarabu kwa juhudi kubwa na hivyo wakatangulia katika nyanja nyingi.[186]

Na hii ndio siri ya maendeleo ambapo hakika mwenye kazi duni nasaba yake haitomnyanyua, kama anavyosema Amirul-Mu'minin عليه السلام. Hivyo muhtasari wa maisha ya mwanadamu ni kazi yake, elimu yake na misimamo yake katika maisha. Na walishajua siri hii baadhi ya wafuasi wa Ahlul-Bayti عليهم السلام wakapanda ngazi ya utukufu na ya milele na wakasonga mbele kwa misimamo yao huru, na wakawa juu ya maelfu ya wanaume walio huru kwa nasaba na watumwa wa misimamo, na tuwe pamoja na maelezo mafupi ya baadhi ya waliokufa shahidi miongoni mwao katika vita vya Karbalaa pamoja na Imamu Husein عليه السلام.

[186] Hilo linathibitishwa na lakabu za Maulamaa na Muhadithina, sawa wawe wale waliotangulia au waliofuata baada yao. Hivyo watunzi wa Sihahi na vitabu vinavyotegemewa na Sunni ni baina ya Bukhari, Nisaburiy, Tirmidhiy. Na upande wa Shia ni Kulainiy, Qummiy na Tusiy, hawa ni mfano tu.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 217 11/23/2016 12:37:37 PM

**Aslamu Mturuki:**

Ibn Umru: Imamu Husein عليه السلام alimnunua baada ya kufariki Imamu Hasan عليه السلام na akampa zawadi mtoto wake Ali as-Sajjad, na baba yake alikuwa ni mturuki. Aslam alikuwa ni mwandishi wa Imamu Husein عليه السلام. Na alikuwa ni wakala wa mahitaji yake, Imamu alipotoka Madina kwenda Makkah, Aslamu alifuatana naye na aliandamana naye hadi akafika Karbala, na alikuwa anaweza kurejea baada ya Imamu Husein عليه السلام kuondoa utiifu juu ya wafuasi wake na akawapa hiyari baina ya kuendelea pamoja naye, na matokeo ya hayo ni kufa shahidi, au kurejea katika maisha yao ya kawaida.

Na alikuwa anaweza kufanya kama walivyofanya wengine miongoni mwa walio huru wa nasaba na watumwa wa misimamo, isipokuwa yeye ambapo alikuwa ni msomi wa Qur'ani, alichukua msimamo wa kunusuru dini na kiongozi wake ni Imamu Husein عليه السلام, akataka ruhusa kwa Imamu, akatoka na kupigana hadi akauwa kundi kubwa la watu kisha akaanguka hali ya kuwa ni shahidi, Husein عليه السلام akamwendea akamuona naye bado yuko hai, Husein akamkumbatia na akaweka shavu lake juu ya shavu lake. Akafungua macho yake akatabasamu na akasema: "Ni nani yuko kama mimi na mjukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ameweka shavu lake juu ya shavu langu?"[187]

Hivi ndivyo mtumwa wa kituruki alivyowatangulia na kuwazidi waungwana wa Kiarabu kwa msimamo wake.

**Sulayman:**

Huria mwingine wa Imamu Husein عليه السلام, mama yake ni kijakazi wa Imamu Husein عليه السلام, jina lake ni Kabshah. Alimnunua kwa dirhamu elfu moja, na alikuwa ni mtumishi katika nyumba ya Ummu Is'haqa,

[187] *Tanqiyhul-Maqaal*, Juz. 1, uk. 152.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 218 11/23/2016 12:37:37 PM

mke wa Imamu عليه السلام. Kijakazi huyo aliolewa na Abu Razin na akamzaa Sulayman, na alikuwa ni mtumishi wa Imamu Husein عليه السلام na akapanda katika hili daraja, akawa ni mjumbe wa Imamu kwenda kwa watukufu wa Basra kisha Kufah. Akabeba barua kutoka kwake kwenda kwao, na baada ya kupeleka barua hizo na kuchukua kiapo cha utii kwa watu wake, usiku wa mwisho alikwenda kwa Mundhiri bin al-Jarud al- Abadiy, isipokuwa mtumwa asiye na msimamo, Mundhir, akamchukua Sulayman mjumbe wa Husein عليه السلام mwenye barua ya Imamu Husein, akamkabidhi kwa Ibn Ziyad, na akaamuru kukatwa shingo yake, akauliwa shahidi. Dua ya kumuombea amani na kumtumia maamkizi imepokewa katika Ziyara tukufu ya an-Nahiyah inayonasibishwa na Imamu Mahdi عليه السلام, na hiyo inatosha kuwa ni fahari kwake na kwa msimamo wake, kuwa ni mjumbe wa Imamu, na ni sehemu ya salamu ya Imamu wa mwisho.[188]

**Munjih:**

Vilevile ni huria mwingine wa Imamu aliyechagua kufa shahidi katika safu ya Imamu Husein عليه السلام baada ya kupigana mapigano ya mashujaa walio huru. Alikufa shahidi katika mapigano ya mwanzo kabla ya Adhuhuri pamoja na Qarib bin Abdillah bin Arqad, naye pia ni huria wa Imamu Husein عليه السلام.[189]

Na historia imeandika misimamo 12 kutoka kwa hawa huria, na walisubiri pamoja na ndugu zao, na wakavumilia katika kumtii Imamu wao hadi wakafa shahidi hapo Karbala. Tunatosheka na kiasi hiki cha maelezo ya shakhisiya hizi ambazo zinazingatiwa katika vigezo vya kimada vya kimakosa kuwa ni za daraja duni la kijamii kwakuwa wananasibishwa katika kundi la watumwa na huria, wakati ambapo kanuni ya Uislamu ni "mwenye kutenda chembe ya

[188] *Tanqiihul-Maqaal*, Juz. 2, uk. 5.
[189] *Tanqiihul-Maqaal*, Juz. 3, uk. 247.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 219 11/23/2016 12:37:37 PM

wema ataiona." Tumekuta ni namna gani watu hawa wametengenezeka chini ya mikono ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, Amirul-Mu'minin na Husein عليه السلام na kuwa ni watu wapya hadi wakawa katika nafasi wanayoionea gele watukufu halisi wa Kiarabu.

Na ilikuwa tunaweza kuelezea wengine, mfano wa Khairan mtumishi ambaye alikuwa ni mmoja wa mawakala wa Imamu al-Kadhim عليه السلام,[190] au Yasir na Nadir watumishi wawili wa Imamu Ridha عليه السلام, isipokuwa tunachelea kurefusha utafiti kwa kuelezea mifano hii kwa ajili ya ushahidi, imetufanya tutosheke na kiasi hiki.

## HITIMISHO

Baada ya kuzunguka katika uwanja mpana wa maisha binafsi ya Ahlul-Bayt عليهم السلام kwa kutaraji kujaza – kadiri ya uwezo wetu - mikono yetu katika hazina ya maisha yao na johari ya sira yao, yamebakia mengi miongoni mwa maudhui ambayo hatujaweza kuyaelezea, kwa kutarajia kuwa tutaafikiwa kufanya hilo siku za baadaye. Kuna sehemu zenye kushirikiana katika maisha ya kisiasa ya Ahlul-Bayt عليهم السلام, na kuna njia ya malezi kwa ajili ya watoto na mengineyo mengi. Isipokuwa sisi tulijaribu katika utafiti huu kutoa picha iliyo wazi juu ya upande huo ulioachwa na makundi ya ufurutu ada na kutweza, kuvuka mpaka na kupuuza, ambapo yote mawili yanapotosha, tukijitahidi kuwa karibu na kadhia nyingi zenye kugusa maisha yetu na mambo yetu.

[190] Rejea *Binaaul-Qaadati Fiy Manhaji Ahlil-Bayt*, cha mtunzi.



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 220 11/23/2016 12:37:37 PM

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
   ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 222 11/23/2016 12:37:37 PM

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 223 11/23/2016 12:37:37 PM

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 224 11/23/2016 12:37:37 PM

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l’Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 225 11/23/2016 12:37:37 PM

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 226 11/23/2016 12:37:37 PM

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 227 11/23/2016 12:37:37 PM

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha– Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli
241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU

242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhia
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitoa Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukosoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo (Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi

## KOPI ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n;amavuko by;ubushiya
4. Shiya na Hadithi
5. Kor'ani Nziranenge



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 229 11/23/2016 12:37:38 PM

6. Kwigisha Mu Buryo Bw'incamake Uka Salat Ikotwa

7. Iduwa ya Kumayili

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique



08_16_Maisha_23_November_2016.indd 230 11/23/2016 12:37:38 PM